

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

KIKAO CHA NNE – TAREHE 14 JUNI, 2011

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 37

Ardhi Iliyotolewa Kujenga Shule ya Msingi Kiraracha

MHE. AUGUSTINO L. MREMA aliuliza:-

Mzee Pauli Sananga Lekule wa Kijiji cha Kiraracha, Kata ya Marangu, Wilaya ya Moshi Vijijini, alitoa ardhi yake ikatumika kujenga shule ya msingi Kiraracha, Marangu miaka 10 iliyopita akiahidiwa na Serikali kupewa eneo jingine kama fidia lakini mpaka sasa hajapewa eneo jingine kama fidia jambo lililomfanya aione Serikali haikumtendea haki.

Je, ni lini Serikali itamlipa haki yake kutokana na makubaliano hayo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa Ndugu Pauli Sananga Lekule wa Kijiji cha Kiraracha, Kata ya Marangu Magharibi, alitoa ardhi yake kwa ajili ya ujenzi wa shule ya msingi Kiraracha, Kata ya Marangu Magharibi kwa ahadi ya kufidiwa eneo lililoko Njia panda. Aidha eneo ambalo Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ilitarajia kumfudia Ndugu Lekule lipo katika mgogoro na kesi bado inaendelea Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa eneo lililopimwa viwanja na kutarajia mlalamikaji lipo katika mgogoro wa kisheria kati ya Halmashauri na wananchi, Serikali inaendelea kufuatilia mwenendo wa kesi na mara shauri litakapomalizika Mahakama mhusika atapewa eneo lake.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za Serikali kuhakikisha shauri hili haliendelei kuchukua muda mrefu, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi imeunda timu kwa ajili ya kufuatilia na kuharakisha shauri hili ili ikiwezekana limalizike nje ya Mahakama ili Ndugu Lekule Sananga aweze kupata haki yake mapema. (*Makofi*)

MHE. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali yafuatayo:-

Kwanza huyu Mzee Pauli Sananga Lekule amekuwa mtu muungwana sana, mkarimu sana. Kwa miaka kumi iliyopita akakubali heka zake nne zichukuliwe na Serikali ya kijiji cha Kiraracha. Hatukuwa na eneo jingine la kujenga shule, miaka kumi imemalizika, watoto wake wamemzingira wanataka urithi, wanataka haki zao.

Sasa Serikali kukaa miaka kumi yule mtu hajapata haki zake na tunamwambia kwa sababu ya kesi iliyoko Mahakama ina uhusiano gani na yeye? Kwanini yeye mwenyewe alikuwa tayari kufidiwa shilingi milioni 40 amalizane na Serikali tumpe haki yake kiwanja tuchukue na shule imeshafika darasa la saba na yeye alikuwa tayari kusema kwamba kama hamtaki kunilipa ondoeni shule yenu nipe ni ardhi yangu?

Sasa kwanini Serikali haitaki kulinda heshima yake ikapatana na yule mwananchi na raia wa kawaida pale kijiji mkampa haki yake milioni 40 ni kitu gani mbele ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba apewe fidia yake tuachane na yeye. Baada ya kusema hayo naomba nimwulize Waziri Serikali itafanya nini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kwanza lazima nitambue hekima aliyonayo mwananchi ule Bwana Pauli, Sananga Lekule ni kweli amekuwa mvumilivu kwa kipindi chote cha miaka kumi na Mheshimiwa Mbunge anatambua migogoro ya ardhi iliyoko Kilimanjaro. Kilimanjaro kuna tatizo la ardhi na maeneo yote yana migogoro.

Lakini katika hili Serikali inayo nia njema ya kumlipa Bwana Lekule kwa sababu kipindi kile toka mwaka 2000 eneo lile lilipopimwa mwaka 2001 wale wananchi walianza mgogoro na ile kesi ilifunguliwa. Mwaka 2003 tukategemea ile kesi ingeweza kwisha lakini ilishindikana kwisha na sisi tukawa tunasubiri maamuzi ya Mahakama kwa kipindi chote hiki kufikia mwaka jana tukawa tumpanga utaratibu mwingine. Tunalo eneo jingine pale Kiraracha la Halmashauri ya Wilaya, lile eneo tumeliombea kibali Wizara ya Ardhi ili tubadilishe matumizi na tayari wameshatukubalia ndiyo makubaliano ya msingi ya kumrudishia ili tuweze kumrudishia ardhi yake. (*Makofi*)

Hatua tuliyofikia sasa huku tukisubiri kesi ile Mahakamani lakini tumeunda Tume kuomba Mahakama ile kesi irudi tuzungumze huku nyumbani ili tuweze kumlipa haki yake ya msingi. Lakini kama itashindikana suala la Mahakama tuna uhakika eneo ambalo tumeshapata kibali cha kubadilisha matumizi ya ardhi kwenye eneo ambalo tumeliombea, bado tuna uhakika wa kumlipa ardhi yake.

Suala la kumlipa milioni 40 Ndugu Pauli Lekule hajawahi kutuandikia barua ya kuomba kulipwa milioni 40, atakapoandika sasa tunaweza tukazungumza kwa nia ya kutaka kumlipa thamani ya ardhi yake ili asiweze kupoteza haki yake ya msingi. (*Makofii*)

Na. 38

Shule za Kata

MHE. PHILIPA J. MTURANO aliuliza:-

Shule nyingi za Kata zilizoanzishwa, licha ta kuwezesha wanafunzi wengi zaidi kujiunga nazo lakini shule hizo zina upungufu mkubwa wa vitendea kazi na walimu wenyе sifa stahiki:-

(a)Je, Serikali ina mpango wa kuzipatia shule hizo walimu wa kutosha wenyе sifa stahiki na vitendea kazi vya kutosha?

(b)Je, Serikali inasema nini juu ya kuwarudishia walimu *Teaching Allowance* hususani kwa walimu wa Shule za Msingi na Sekondari kama motisha kwa watumishi hao ili kuinua ari yao ya kufanya kazi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philipa Maturano, Mbunge wa Vti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, mpango wa kuzipatia Shule za Kata Walimu wenyе sifa stahiki ni bayana na Serikali imejipanga kufanya hivyo kwa kuongeza udahili wa walimu wanafunzi katika Vyuo mbalimbali. Kwa kuendelea na juhudhi hiyo hiyo katika mwaka 2010/2011 jumla ya walimu 9226 wameajiriwa na Serikali na miiongoni mwao wamepangwa katika Shule za Kata. Aidha, Serikali inaendelea kuhamasisha watu binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali kuanzisha Vyuo vya Ualimu ikiwa ni njia mojawapo ya kuongeza udahili wa walimu. Kwa mwaka 2011/2012 jumla ya walimu wanaotarajiwa kuhitimu vyuo mbalimbali nchini ni 19,031 (shahada 12,649 na

stashahada 7,382). Serikali itaendelea kuwaajiri walimu hao kadri wanavyohitimu na kufaulu.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa malengo na mikakati ya mpango wa maendeleo wa Elimu ya Sekondari awamu ya II (MMES II) Serikali imekusudia kuongeza upatikanaji wa vifaa vya kufundisha na kujifunzia katika masoo yote na ngazi zote ifikapo 2013 kwa kupeleka nusu ya fedha za ruzuku ya uendeshaji na fedha kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kununulia vitabu na vifaa vya maabara.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua ukubwa wa kazi ya walimu pamoja na mchango mkubwa unaoutoa kwa jamii na changamoto zinazomzunguka katika kutoa elimu nchini. Serikali imeendelea maslahi, mishahara na stahili za walimu ili kuwapa ari ya kufanya kazi ni azima ya Serikali pia kuboresha posho na maslahi kwa walimu wapya wanaoripoti kazini. Aidha Serikali itaendelea kuboresha maslahi na mishahara ya walimu watumishi wengine kadri uwezo Serikali unavyoruhusu.

MHE. PHILIPA J. MTURANO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kuna walimu ambao wana miaka zaidi mitatu tangu wamehitimu katika vyuo vya Ualimu mpaka sasa hawajaajiriwa. Katika jibu la msingi Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Serikali inaongeza udahili.

Je, hawa ambao wako majumbani na hawajaajiriwa mpaka sasa Serikali inasemaji.

Swali la pili, kwa kuwa Shule hizi za Kata, zinachukua watoto wengi na baadhi yao wanatoka maeneo ya mbali na wengi ni wakike je, Serikali inasemaje kujenga hosteli ili kupunguza mamba ambazo watoto wakike wanazipata wanapokuwa wanahangaika kuhusu masuala ya usafiri?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge kwa sasa hatuna uhakika kama kuna mwalimu yoyote aliyejata mafunzo ya ualimu na yuko mtaani hana ajira. Kwa sababu idadi kubwa ya walimu wote ambao wamehitimu mafunzo ya ualimu iwe ni kwa Diploma na Digrii, tulitoa nafasi na kuwashukuru, tulitoa nafasi mwezi Februari na tukawaajiri 9226 kutokana nakuajiri waliotoka vyuoni lakini pia walioko kwenye soko. Tunaamini wale wote walioomba ndiyo walajiriwa.

Idadi ndogo ya vijana waliomaliza vyuo vya ualimu hawajakamilisha kufaulu masomo ya mtihani kwenye vyuo vyao. Mkakati wa Serikali tunaajiri mwalimu ambaye amehitimu lakini awe amefaulu masomo yote, hiyo ndiyo sifa ya kwanza ya kuajiriwa mwalimu kwa sasa.

Swali la pili la ujenzi wa hostel ni kweli. Serikali ina mpango wa kujenga hostel kwenye shule zetu na moja kati ya mambo yaliyoko kwenye *package* ya MMES ni pamoja na ujenzi wa hestel kwenye shule zetu za sekondari.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote tunamatumaini kwamba ujenzi wa hostel utakuwepo kwenye shule za sekondari lakini tuendelee kushirikiana na kamati zetu zile za Ward C kwenye Kata zetu na Kamati za ujenzi kuratibu mipango hiyo kwenye vijiji vyetu ili tuweze kujenga zile hostel na hatimaye tuokoe mazingira ya watoto wa kike.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja la nyongeza. Serikali inatambua kuwa Walimu ni Jeshi kubwa kama majeshi mengine ambapo walimu wanapambana na adui ujinga.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapunguzia walimu kodi za vifaa vyta ujenzi ili nao wapate makazi bora?

SPIKA: Swali jingine kabisa. Haya Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, nilipokuwa nazungumzia Mpango wa Maendeleo ya Sekondari awamu ya pili nilitamka suala la mabweni.

Lakini jingine ambalo liko kwenye mpango wa MMES kwa fedha ambazo ametenga Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, zile bilioni 59 ni pamoja na kuongeza ujenzi wa nyumba za walimu ili kuwawezesha walimu kuweza kupata makazi bora ili waendelee kufanya kazi kwa ufanasi mkubwa.

Kwenye eneo hili pamoja na malengo mengine ambayo kwa ajili ya kuboresha mazingira ya mwalimu ni pamoja na kukamilisha kuongeza idadi ya vyumba vyta madarasa ili sasa kazi ya ufundishaji iwe rahisi kwa mwalimu kutoa taaluma inayokusudiwa ahsante. (*Makofifi*)

Na. 39

Upatikanaji wa Umeme Vijijini

MHE. JEROME D. BWANAUSI aliuliza:-

Upatikanaji wa umeme vijijini ni kichocheo kikubwa cha Maendeleo ya Wananchi:-

(a) Je, ni lini Serikali itawapelekea umeme wananchi wa vijiji vya Chidya, Chiwata na Mkangaula baada ya maombi yao ya muda mrefu hasa ikizingatiwa kuwa umeme umepita kwenye vijiji hivyo kwa zaidi ya miaka kumi (10) sasa bila kunufaika nao?

(b) Je, ni gharama kiasi gani kitatumika kufikisha umeme katika kila kijiji kilichoanishwa kwenye swali hili?

(c) Je, ni lini Serikali itafikisha umeme kwenye vijiji vya Nanjota, Luatala na Mnavira ambako umeme haujafika kabisa?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, vijiji vya Chidya, Chiwata na Mkangaula vinapitiwa na njia za umeme bila vyenyewe kuwa na huduma ya umeme. Serikali imeagiza *TANESCO* kuanza kazi ya upimaji (*Detailed Survey*) wa njia za umeme msongo wa kilovoti 0.4 na ufungwaji wa *transfoma* ili kubainisha gharama ya kuvipatia umeme vijiji tajwa. Kazi hiyo imepangwa kutekelezwa kwenye Bajeti ya *TANESCO* ya mwaka 2011/2012 ambapo gharama za utekelezaji wa mradi zitawasilishwa kwa wakala wa Nishati Vijijini ili kazi hizo zижumuishwe kwenye mipango na Bajeti ya wakala.

(b) Mheshimiwa Spika, gharama itakayotumika kufikisha umeme kwa kila kijiji kama ilivyoanishwa kwenye swal itafahamika baada ya kukamilika kwa tathimini ya gharama ya utekelezaji wa mradi. (*Makofi*)

(c) Mheshimiwa Spika, kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge, tumeridhia na tutaelekeza kazi ya upimaji wa njia za umeme itakayofanywa kwenye vijiji vilivyoanishwa kwenye kipengele (a) ihusishe pia vijiji vya Luatala, Najota na Mnavira. (*Makofi*)

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri na ya kutia moyo kwa wananchi ambao wamekuwa na kilio cha kupata umeme kwa muda mrefu. Nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Je, Mheshimiwa Waziri atawathibitishia wananchi hawa kwamba kazi hii ya upimaji ambayo ndiyo muhimu sana kabla ya kazi nyingine kufanyika kwamba inafanyika lini? Lakini swal la pili. Je, Mheshimiwa Waziri ameshahakikishiwa na *TANESCO* na Wakala wa Nishati Vijijini kwamba kweli wanazo fedha za utekelezaji wa mradi huu?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ni kweli baada ya kupata swal hili sisi tumeshawaelekeza *TANESCO* na kazi ya kufanya tathimini itaanza katika kipindi hiki kama nilivyo sema na natarijia itakamilika ndani ya miezi mitatu.

Baada ya kukamilika kazi hiyo kitakachofuatia sasa na kwa sababu gharama zitakuwa zimejulikana tutaziwasilisha kwenye Wakala wa Nishati Vijijini ili kama

tulivyosema kwenye jibu la swali la msingi gharama hizo ziingizwe katika Bajeti na Mipango ya Wakala wa Nishati Vijijini.

SPIKA: Sasa namwita Mheshimiwa Kasembe na yeze aseme na pale kwangu itapitia.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja ya nyongeza. Kwa kuwa barabara hii iliyopitia umeme kutoka Mtwara kufika Masasi inapitia katika Vijiji vya Chibite, Nangoo, Nanganga, Chikukwe na Chigugu na njia ya umeme iko tayari.

Je, Mheshimiwa Waziri, wananchi hao wa vijiji hivi nilivyovitaja watapatiwa lini umeme kwa sababu wamekuwa wakiambulia kuwa walinzi wa nguzo za umeme?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri huwezi kurusha umeme itabidi zipite tu.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna dhamira ya kuwafikishia wananchi wengi sana na hasa maeneo ambayo nyaya za umeme zimepita lakini wao wenyewe hawanufaiki.

Lakini, kama ambavyo tumekuwa tukisema, mpango na utaratibu ambao tumejiwekea kama Taifa, tulianza kuunganisha Mikoa, Wilaya na hatimaye maeneo ya vipaumbele kama vile maeneo ya taasisi za elimu, afya, maeneo ambayo yana shughuli kubwa za kiuchumi na lengo kwa kweli ni kufikisha Vijiji vyote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimwahidi Mheshimiwa Mariam Kasembe, kama ambavyo nitaendelea kuahidi wawakilishi katika Majimbo na maeneo mbalimbali ya Tanzania kwamba kwa kadri Mfuko wa Nishati Vijijini unavyoendelea kutanuka, tutaendelea kuwafikia wananchi wengi zaidi katika suala hili la huduma ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Bajeti yetu inakuja, tutaelezea pia hatua ambayo tutakuwa tunapiga katika mwaka huu ujao wa fedha, ni maeneo kiasi gani ambayo tutayafikia baada ya kukamilisha miradi inayoendelea kwa sasa hivi. (*Makofii*)

Na. 40

Upatikanaji wa Hatimiliki za Ardhi za Kimila

MHE. MOSHI S. KAKOSO aliuliza:-

Serikali imehamasisha wakulima kote nchini waachane na kilimo cha jembe la mkono na kuwa na kilimo chenye tija kwa kutumia zana bora zaidi za kilimo. Lakini wakulima wa Jimbo la Mpanda Vijijini ni maskini kwa kuwa rasilimali yao kubwa ni ardhi, lakini ardhi hiyo haijapimwa:-

Je, ni lini Serikali kupitia Waziri husika atafika Jimboni Mpanda kutoa Hati Miliki za kimila kwa wakulima hao ili nao waingie kwenye kilimo chenye tija?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Moshi Seleman Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza Sheria ya Ardhi ya Viji Na. 5 ya mwaka 1999 kwa kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi, kuwapimia ardhi wamiliki halali na kuwapatia Hati Miliki za Ardhi za kimila tangu mwaka 2003.

Halmashauri za Wilaya ikiwemo Bagamoyo, Handeni na Kisarawe zilitekeleza miradi ya majoribio ya utoaji wa Hati Miliki za kimila kwa kushirikiana na Taasisi ya MKURABITA na asasi zisizo za Kiserikali. Hivi sasa Wilaya hizo zinaendelea kutekeleza zoezi hilo wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya za Bariadi, Babati, Manyoni, Namtumbo, Mbozi, Iringa Vijijini na Bunda inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kupanga matumizi ya ardhi, kupima na kutoa Hati Miliki za Ardhi za kimila kwa wananchi kwenye Vijihi vya Wilaya hizo. Zoezi hili linategemewa kukamilika mwishoni wa mwezi huu.

Mheshimiwa Spika, tangu utekelezaji wa miradi ya majoribio ianze katika Wilaya mbalimbali nchini, jumla ya hatimiliki 129,114 zimetolewa. Ili kufanya zoezi hilo kuwa endelevu na kuwezesha kutekelezwa na Wilaya nyingine bila kuitegemea Wizara, zoezi linaloendelea hivi sasa limeshirikisha Maafisa Ardhi na Wapimaji kutoka Wilaya zingine nchini.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kupima ardhi, kutayarisha na kutoa Hati Miliki za kimila ni la Halmashauri ya Kijiji baada ya kupata idhini ya Mkutano Mkuu wa Kijiji. Hatimiliki za kimila huandaliwa na kusajiliwa Kijijini. Hivyo, ni muhimu kwa kila Kijiji kutimiza masharti ya kisheria yatakayowezesha kusajili na kutoa Hati hizo. Masharti hayo ni pamoja na kuandaliwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi, kujenga masjala ya ardhi na kuwa na daftari la ardhi ya Kijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuitikia wito wa Mheshimiwa Mbunge, nitapanga ziara ya kutembelea Jimbo la Mpanda Vijijini mara baada ya Mkutano wa Nne wa Bunge la

Kumi ili pamoja na mambo mengine kuhamasisha viongozi na wananchi wa Jimbo hilo kuanza taratibu za kumilikishwa ardhi kwa mujibu wa kifungu cha 22 - 25 ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999. Aidha, naomba nirudie wito wangu niliotoa tarehe 6 Aprili, 2011 wakati nikijibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, kwamba Halmashauri za Wilaya Daftari la Ardhi ya Kijiji ili kuharakisha utekelezaji wa mpango wa kuwawezesha wananchi kwa kuwapimia ardhi yao pamoja na kuwapatia Hatimiliki za ardhi ya kimila.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo:- Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya imekamilisha taratibu zote za awali kuhusu mpango bora wa matumizi ya ardhi na kuwahamasisha wanavijiji mbalimbali kuijandaa katika mipango bora ya ardhi na kuhakikisha mikutano yote imefanyika na wametekeleza. Ni sababu zipi zinazofanya mpango huu ucheleweshwe kwa makusudi?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, ikiwa wananchi wameishafanya hatua zote hizo/taratibu zote hizo ambazo zinaelekea kwamba wamejiandaa kwa ajili ya kupimiwa ardhi na kuweza kupatiwa Hati. Wizara yangu itawaunga mkono kwa kupeleka Maafisa wa fani zinazohusika ili kushirikiana nao kukamilisha zoezi hilo.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kupima na kuwa na Hati ni jambo moja, na dhamira ya kuwa na Hati ili ziweze kuwasaidia wakulima kupata mikopo na kuongeza tija kwenye kilimo. Serikali inatamka nini kuhusu taasisi za fedha kutokuheshimu Hati za kimila?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, iko dhana kwamba Hatimiliki za kimila hazina hadhi sawa na Hati zitolewazo na chini ya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999. Napenda kurudia tena kama nilivyoeleza wakati nikijibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, mwezi Aprili, kwamba kwa mujibu wa sheria, Hati za ardhi kimila zina hadhi sawa na Hati zitolewazo chini ya Sheria Na. 4 ya mwaka 1999. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi wengi wa maeneo ambayo tayari wamekwishapata Hati hizi za kimila wamepata mikopo. Moja ya maeneo hayo ni Mbozi, wamepata mikopo. Juzi nilikuwa najulishwa kwamba wamefikia karibu shilingi bilioni 16 ya pembejeo na huduma zinginezo.

Mheshimiwa Spika, suala kubwa na hili ningependa nitoe maelekezo kwa Maafisa Ardhi wa Wilaya zote kwamba ni jukumu lao kuwaelimisha wananchi pamoja na kuhamasisha taasisi za fedha kutambua na kuheshimu Hati za Ardhi Kimila.

Mheshimiwa Spika, Hatimiliki za ardhi kimila, tofauti na Hati zinginezo, zenyewe bahati nzuri ni kwamba zina muda mrefu zaidi kuliko hati nyingine hizi.

Kwa hiyo, mimi nashangaa taasisi za fedha ambazo zitaacha kuheshimu Hati ambayo muda wake wala ukomo siyo kesho! Uhai mkubwa zaidi kuliko Hati zitolewazo chini ya Shertia Na. 4 ya mwaka 1999.

Kwa hiyo, ningomba Waheshimiwa Wabunge wote tushirikiane kuhamasisha taasisi za fedha pamoja na kuhakikisha kwamba Maafisa Ardhi wanatimiza wajibu wao kwa kuwaelimisha wananchi umuhimu wa hati hizi. Nashukuru sana.

Na. 41

Uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro

MHE. FREEMAN A. MBOWE aliuliza:-

Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro ni sehemu muhimu sana ya mambo ya utalii Ukanda wa Kaskazini mwa nchi yetu (*Northern Tanzania Tourist Circuit*):-

- (a) Je, ni kampuni gani zimekuwa zikiendesha Uwanja huu tangu ubinafishwe hadi leo, chini ya masharti yapi makuu ya mkataba wa uendeshaji wenye kiasi gani cha uwakezaji kilichofanywa na kampuni hizo kwa kipindi chote hicho?
- (b) Je, nini vyanzo vya mapato vya uwakezaji hao, na ni mapato kiasi gani wamepata kila mwaka katika uhai wa mkataba huo?
- (c) Je, ni nini mapato ya Serikali Kuu kutokana na ukodishwaji wa Uwanja huo, ni kiasi gani imepata kutokana na kodi, ushuru au tozo nytingine za kisheria; na ni kiasi gani cha mapato kimepatikana kwa Halmashauri ya Wilaya ya Hai mwaka kwa mwaka kwa miaka yote hiyo?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Freeman Aikael Mbewe, Mbunge wa Hai, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tangu uendeshwaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (*KIA*) ubinafishwe mwaka 1998, Kiwanja kimekuwa na kikiendeshwa na Kampuni iitwayo *Kilimanjaro Airport Development Company (KADCO)* kampuni ambayo iliingia mkataba na Serikali wa miaka 25 wa kuendesha na kusimamia kiwanja hicho. Masharti makuu yaliyokuwa yametolewa kwa mwekezaji kwa mujibu wa mkataba wa ukodishaji ni:-

- (i) Kuboresha na kuendeleza miundombinu ya kiwanja.

(ii) Kuboresha huduma za usafiri wa anga katika kiwanja hicho na hivyo kukuza utalii na kilimo hususan kilimo cha maua na mboga mboga.

(iii) Kukigeuza kiwanja kutoka chombo kinachoendeshwa kwa hasara kuwa chombo kinachoendeshwa kwa faida.

(iv) Kutafuta wawekezaji katika maeneo mengine ya biashara kama vile mahoteli na hivyo kukifanya kiwanja kuwa lango la utalii katika Kanda ya Kaskazini.

Kwa kipindi cha 1998 hadi 2009, *KADCO* iliwekeza kwenye kiwanja hicho shiliongi bilioni 6. Fedha hizo zilinunua mitambo ya kuimarisha usalama na kukarabati barabara ya kutua na kurukia ndege (*runway*).

(b) Mheshimiwa Spika, vyanzo vikuu vya mapato kwa Kampuni ya *KADCO* ni ada na tozo mbalimbali kutoka kwa watumiaji wa kiwanja kama vile *passenger service charge*, ada ya kutua na kuegesha ndege (*landing and parking charge*) na kodi kwa wapangaji (*rental fee*). Tangu *KADCO* ianzishwe, imepata jumla ya shilingi bilioni 56.94 kutokana na vyanzo hivyo.

Mheshimiwa Spika, nimeorodhesha vyanzo 12, na Mheshimiwa Mbewe nitampatia kwa maandishi kwa sababu idadi ni ndefu.

(c) Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwa *KADCO* imelipa kodi kwa Serikali Kuu zinazofikia shilingi bilioni 3.072 hadi kufikia mwaka 2010. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Hai ilipata mapato (*Service Levy*) kiasi cha shilingi milioni 84.13 hadi mwaka 2010 sawa na wastani wa shilingi milioni 7.01 kila mwaka.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, baada ya majibu ya Waziri, naomba kuuliza maswali yafuatayo ya nyongeza:-

Kwa kuwa suala na tatizo la mkataba wa ukodishaji wa Kiwanja cha *KIA* umekuwa jambo la kudumu katika Bunge kwa maana kwamba ulijadiliwa katika Bunge la Nane, Bunge la Tisa na leo ni Bunge la Kumi, na ulianza kwenye Bunge la Saba. Kwa kuwa timu mbalimbali kwa nyakati tofauti zimekuwa zinalalamika kuhusiana na Uwanja huu wa *KIA*, jambo ambalo lilsababisha mimi mwenyewe nikiwa Mbunge wa Hai katika kipindi cha Bunge la Nane kwenda kuzuru Uwanja ule nikiwa na Waziri aliyejewa anahusika Mheshimiwa Prof. Mark Mwandomsya.

Serikali inatoa tamko gani kuhusu upungufu wa mkataba wa Uwanja huu wa *KIA* ikiwemo ukweli kwamba Uwanja huu unakodishwa kwa shilingi 1000/= kwa mwezi? Swali la pili;

SPIKA: Samahani! Ni shilingi, Dola?

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Dola 1000 kwa mwaka. Swali la pili. Katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri, ameliambia Bunge kwamba Kampuni ya

KADCO iliwekeza shilingi bilioni 6 (sita)kujenga miundombinu ya Uwanja wa *KIA* ikiwemo *runway*, wakati ukweli ni kwamba Serikali ya Tanzania ilikopa Dola milioni 4 kutoka *World Banik* na ikatoa kandarasi kwa Kampuni ya *Fidelis* kujenga *runway* ya *KIA*.

Kwa maana hiyo ni kwamba mwekezaji hakuwekeza chochote katika miundombinu ya Uwanja na ameendelea kumiliki eneo la ardhi la mraba wa square metre 101 na kutoa usumbufu mkubwa kwa wanajiji wangu wanaopakana na Uwanja wa *KIA* kikiwemo Kijiji cha Tibigani, *Sanya Station*, Lundugai na Vijiji vingine vya jirani.

Je, Waziri kwanza atakubali, kukiri kwamba amelidanganya Bunge?

Mkataba huu utaletwa lini ili uweze kupitiwa upya na Serikali inatoa kauli gani? Ahsante!

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Baada ya Serikali kuona kuwa mkataba ulioingwa na wabia mbalimbali wa kuendesha Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro ulikuwa haukidhi haja zile ambazo zilikusudiwa, ilisitisha mkataba huo na kurudisha hisa zote zilizokuwa za wabia hao Serikalini. Hivi tunavyoongea leo, *KADCO* ni kampuni ambayo inamiliikiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati *KADCO* ilipokuwa ni kampuni ambayo ina wabia binafsi, kama alivyoeleza Naibu Waziri, ilipewa majukumu ya kuendeleza uwanja ule.

Hivyo basi, kazi ambazo zilikuwa zinafanyika pale, zilikuwa zinafanyika chini ya *KADCO*. *KADCO* imekuwa inailipa Serikali tozo ambapo baadhi ya tozo hizo zimeingia katika kuboresha Uwanja huo. Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. CHRISTOPHER OLE SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kama Serikali imebaini kwamba mkataba huo haukuwa na tija na uliingwa na watu amba walikuwa na sifa zote, na imeonekana kwamba ulikuwa na upungufu kwa kiwango kikubwa sana.

Je, Serikali inachukua hatua gani kwa watu wanaoingiza nchi katika mikataba isiyokuwa na manufaa ili iwe ni fundisho kwa watu wengine? (*Makofi*)

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, Serikali na nchi inapoingia katika mkataba inaingia kwa nia thabiti ya kuwa mikataba hiyo itatusaidia kushirikiana na wengine kuboresha miundombinu yetu, kuboresha nyanzo vyetu.

Kipindi cha utekelezaji wa mikataba ndipo unapoanza kugundua kuwa wale mliongwa nao kwenye mikataba hawafanyi kazi zile ambazo mlikubaliana mzifanye.

Sasa, suala hapo siyo kuangalia mkataba uliingiwaje, suala ni kurekebisha na kwenda mbele, na hivyo ndivyo tunavyofanya. Mheshimiwa Spika, ahsante sana! (*Makofi*)

Na. 42

Ujenzi wa Reli Ukanda wa Kusini

MHE. MARIAM R. KASEMBE aliuliza:-

Serikali katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 - 2015 iliahidi kuanza ujenzi wa reli Ukanda wa Mtwara, Mchuchuma/Liganga - Mtwara:-

- (a) Je, maandalizi ya Mradi huo yamefikia hatua gani?
- (b) Je, maandalizi yatagharimu fedha kiasi gani?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ujenzi wa reli ya Mchuchuma/Liganga - Mtwara unategemea utekelezaji wa miradi ya Mchuchuma na Liganga ambayo ni mihimili ya Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara. Hivi sasa Shirika la Taifa la Maendeleo (*NDC*) lenye jukumu la kutekeleza miradi hiyo liko kwenye hatua ya majadiliano na mwekezaji kampuni ya *SICHUAN HONGDA Corporation* ambayo ilishinda zabuni mwezi Januari, 2011.

Majadiliano yanatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2011 pamoja na kusainiwa mkataba wa ubia ili kutekeleza miradi hiyo kwa pamoja. Hivyo, maandalizi ya ujenzi wa reli katika Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara unategemewa kuanza mara baada ya kuanza ujenzi wa miradi ya Mchuchuma na Liganga, yaani Januari 2012.

(b) Kutokana na utafiti uliofanywa na *NDC* mwaka 2006, ujenzi wa reli hii utagharimu Dola za Kimarekani bilioni 1.5 (sawa na fedha za Kitanzania shilingi bilioni 2,250/=).

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Spika ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza;

(a) Kwa kuwa utafiti uliofanywa mwaka 2006 ulionesha ghamara halisi zitakazotumika katika ujenzi huo, na tumekuwa tukishuhudia ghamara za vifaa mbalimbali zikipanda siku hadi siku. Je, kwa kuwa ujenzi huu utaanza mwaka 2012 hatuoni kwamba kwa kutumia utafiti huu wa mwaka 2006 tunaweza tukakwama kukamilisha ujenzi huu ipasavyo na hivyo kusababisha ahadi yetu tulioiweka kwenye ilani ya utekelezaji wa Chama cha Mapinduzi kufeli?

(b) Je, ujenzi wa reli hii zitatumika fedha za ndani au kuna wafadhili ambao wameanza kujitokeza kutoa msaada katika kukamilisha ujenzi huu wa reli?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, pamoja na kuyumba kwa uchumi wa dunia upembuzi yakinifu uliofanywa na JIKA mwaka 2006, ulibaini kuwa kiasi cha dola za kimarekani bilioni mbili sawa na pesa za kitanzania trilioni mbili kinaweza kutosha kujenga reli hii kutegemeana na mkandarasi atakayepewa zabuni pamoja na aina ya teknolojia itakayotumika. Kwa mfano kutokana na upembuzi yakinifu uliofanywa mwaka 2009 na kampuni ya Kimarekani *Balington Northen santa-fee* ilibaini kwamba kwa kutumia utaratibu wa AREMA yaani *American Railway Engineering and Maintenance Way Association*, standard zake za Kimarekani kiasi hicho kinaweza kutosha kwa kuwa gharama ya kujenga kilomita moja ni kati ya dola za kimarekani bilioni 2.4 mpaka bilioni bilioni 2.6 yaani trilioni 2.4 mpaka trilioni 2.6, jumla ya urefu wa reli itakayounganisha eneo la Mchuchuma na Liganga ni takribani kilomita 850.

(c) Kwa kuwa kiasi hicho cha trilioni mbili ni kikubwa itakuwa ni vigumu kwa Serikali kutenga fedha za ujenzi kwa kutegemea Bajeti ya ndani. Hivyo Serikali inashirikisha sekta binafsi kwa kutumia mfumo wa *PPP* na hivi sasa kuna utaratibu mwingine wa mfumo wa *PPC* (*Public Private Colaborative*).

MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, mbali na Ilani ya Uchaguzi ya 2010/2015 swali la Mtwara *Corridor* limezungumzwa pia katika ilani iliyopita ya mwaka 2005/2010 na suala hili limechukua muda mrefu sana, na leo kwa mujibu wa majibu ya Waziri mwaka 2012 ndiyo ujenzi wa reli hii utaanza?

Je, Serikali inayo taarifa kwamba kule Angola hivi sasa reli kutoka Benguela mpaka Zambia itakamilika mwaka 2012 huo ambapo Tanzania inatanua Mtwara *Corridor*. Je, ni mapato gani ambayo tunayakosa kwa kila siku kuongea maneno haya lakini utekelezaji hakuna?

Je, Serikali ina tamko gani kuhusu masuala haya? (*Makofî*)

SPIKA: Nilisahau huyu ametokea Angola hivi karibuni.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, sisi tunatambua kwamba reli ya Angola Benguela mpaka Zambia tunatambua inajengwa, na tunatambua

pia kuna upembuzi wa reli ya ukanda wa magharibi inatoka Zambia inakwenda mpaka Kisangani, utaratibu ule unafanywa. Lakini jitihada za Serikali zimefanyika mwekezaji amekuja, kwa Mchuchuma na Liganga na reli itajengwa Mheshimiwa Mnyaa asiwe na wasiwasi hao tutawapita tu. (*Kicheko*)

Na. 43

Mradi wa Majisafi na Salama Jimbo la Kishapu

MHE. MANSOOR SHANIF HIRAN (K.n.y. SULEIMAN C. SULEIMAN)
aliuliza:-

Hatua za michoro ya mradi wa maji ya Ziwa Victoria umekamilika:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza kazi hizo ili wananchi wa Kishapu waweze kupata Majisafi na Salama na kuondoa adha wanayoipata kwa sasa.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Suleiman Chambi Suleiman, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ni mojawapo ya sehemu zitakazofaidika na mradi mkubwa wa maji wa ziwa Victoria. Wizara ya Maji kupitia Mamlaka ya Maji safi na uondoaji Majitaka Mjini Shinyanga (SHUWASA) iliajiri mtalaam mwelekezi *GIBB Africa* kwa ajili ya kupima, kusanifu, kuandaa zabuni na kusimamia utekelezaji wa miradi ya upanuzi na usambazaji wa huduma ya majisafi katika Miji ya Mhunze, Kahama, Ushirombo na Maswa. Mtalaam Mwelekezi huyo amekamilisha usanifu na kuandaa vitabu vya zabuni.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria hadi Mhunze, Makao Makuu ya Wilaya ya Kishapu unaendelea, tangazo la kuwataka Wakandarasi kuleta maombi kwa ajili ya ujenzi wa mradi tayari limeandaliwa na kuwasilishwa Benki ya Dunia ili kupata kibali cha kutangaza (*No Objection*), Mkandarasi anatarajiwa kuajiriwa mwezi Desemba, 2011 na ujenzi kuanza mwezi Februari, 2012.

Mheshimiwa Spika, baada ya utekelezaji wa mradi huo huduma ya majisafi kwa wananchi wa Kishapu na Wilaya nilizozitaja itakuwa imeboreshwa.

MHE. MANSOOR SHANIF HIRAN: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza;

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mhalo imepata tenki la maji ya Ziwa Victoria, kuna ramani zimechorwa za kupeleka maji ya bomba safi kutoka Kata ya Mhalo kupeleka mpaka Ngudu Mjini hususani makao makuu ya Wilaya ya Kwimba.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga huo mradi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba swalii la msingi lilihusu Wilaya ya Kishapu, lakini ni kwamba tunao mpango wa kuendeleza maji yaweze kufika katika Mji wa Ngudu na Mhandisi Mshauri anaendelea na kazi ya usanifu. Kwa hiyo mipango itakapokamilika tutaanza kutekeleza mradi huu.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii mmoja la nyongeza.

Kwa kuwa, kero kubwa kwa wananchi wengi ilikuwa ni ahadi ile iliyotolewa na Serikali katika kuhakikisha kwamba Serikali inasaidiana na wananchi na Benki ya Dunia ili kutatua tatizo la maji katika vijiji vingi kwenye nchi ya Tanzania vikiwemo Vijiji vyangu vya Mkongotema, Maweso na kwingineko; na kwa kuwa mpaka sasa Benki ya Dunia hajaweweza kutoa fedha hizo na wananchi wameishachanga mamilioni ya fedha tayari wakisuburi maji na huu ni mwaka wa tatu; na kwa kuwa mwaka huu wa Bajeti Serikali imeongeza fedha kwa ajili ya Bajeti ya maji.

Je, fedha hizo nazo zitaweza kupelekwa kwenye matatizo niliyoyataja katika vijiji vyangu vya Mkongotema na vile vingine vilivyopo katika Jimbo la Peramihio?

SPIKA: Mimi kwangu ndiyo sisemi maana yake ni shida tu!

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli vijiji vingi vimechangia katika kutekeleza mradi wa Vijiji Kumi na Vijiji hivi sehemu mbalimbali vinatofautiana katika hatua ya utekelezaji, sasa hatuwezi kupeleka fedha kama hatujafikia hatua ambayo fedha zile zitatumika.

Kuna baadhi ya vijiji ambavyo tumeshapeleka fedha na fedha zile zipo hawajazitumia. Sasa tunataka tupeleke fedha wakati wamefikia hatua ambayo wamemwajiri Mkandarasi ili aweze kuanza kuchimba visima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo katika Bajeti hii na katika awamu ya pili ya mradi huu wa *World Bank* tutapeleka fedha mahali ambapo patakuwa tayari usanifu umekamilika.

Na. 44

Matumizi ya Mto Kagera

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA aliuliza:-

Mto Kagera ulioko Wilaya ya Missenyi unao uwezo wa kuleta mabadiliko makubwa kama ukitumika kwa matumizi ya nyumbani au kilimo:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha mto huo unatumika na kuwasaidia wananchi wa Kagera, hasa Kata za Kilimile, Kakunyu ambao wanatumia maji yasiyostahili kwa binadamu?

(b) Je, mpango wa kuleta teknolojia ya Misri umefikia wapi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshana Mbunge wa Nkenge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mto Kagera ni chanzo kikuu cha maji kwa Mkoa wa Kagera ambacho kikitumiwa vizuri kitawanufaisha wananchi wa Mkoa huo na Mikoa jirani kiuchumi na kijamii. Chanzo hicho kwa sasa kinategemewa sana na kiwanda cha sukari cha Kagera katika umwagiliaji wa miwa na kuzalisha sukari.

Serikali kwa kupitia *Nile Equatorial Lakes Subsidiary Action Programme (NELSAP)* imekamilisha utafiti katika mto Kagera eneo la Lusumo kwa ajili ya kuanzisha kituo kitakachozalisha umeme wa Megawati 60 kwa nchi za Tanzania, Rwanda, Burundi na Uganda.

Hatua hiyo itasaidia wananchi wa maeneo hayo zikiwemo Kata za Kilimile na Kakunyu kupata umeme wa uhakika na hivyo kuweza kuanzisha miradi mbalimbali itakayowaletea maendeleo ya kiuchumi na kuongeza kipato.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa maji safi na salama kwa ajili ya Kata za Kilimile na Kakunyu ninaishauri Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi iweke katika mipango yake ya maendeleo miradi ya maji kwa ajili ya vijiji vilivyoko katika Kata hizo ili miradi hiyo itekelezwe chini ya programu ya Maendeleo ya sekta ya Maji iliyoanza tangu mwaka 2006. Kwa njia hiyo, wananchi hao wataweza kupata Majisafi na salama kwa matumizi yao.

(b) Mheshimiwa Spika, teknolojia ya umwagiliaji maji kwenye mashamba inayotumiwa na nchi ya Misri katika matumizi ya maji ya mto *Nile* inaweza kuigwa katika mto Kagera. Teknolojia hiyo ya umwagiliaji wa matone (*drip irrigation*) inatumika sana Misri kwa kuwa nchi hiyo haipati mvua ya kutosha kama ilivyo hapa kwetu. Teknolojia hiyo hutumia maji kidogo na iwapo itatumika katika Bonde la Mto Kagera itapunguza matumizi ya maji na hivyo kutoa fursa kwa watumiaji wengine wa maji kupata maji.

Kwa sasa teknolojia hiyo imeanza kutumika kwa baadhi ya miradi midogomidogo nchini. Wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

kuwahamasisha wakulima wakubwa kutumia teknolojia hiyo ya *drip irrigation* ili kuongeza tija katika kilimo cha umwagiliaji.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika ahsante, ninashukuru sana kwa majibu ya Waziri, ni majibu mazuri sana. Ningependa kuuliza kwamba jambo hili limekuwepo muda mrefu na siyo hilo tu sasa hivi kwa Mkoa wa Kagera na Mikoa jirani kungekuwa hakuna haja tena ya kutafuta chakula wala kupungukiwa na chakula.

Kwa uzuri katika hayo maandishi ya majibu yanaonekana vizuri sana, lakini ningeomba kujuu ni lini wanategemea kuhamasisha wawekezaji wakubwa kuwekeza katika Kilimo kwanza kama tulivyoita wenyewe jina la Kilimo Kwanza kabla ya mambo mengine ili kusudi tuweze kupata chakula cha kutosha.

Ni kweli ameeleza vizuri lakini sioni dalili ya lini hili jambo linaweza likaanza ili kusudi tukomboe wana- Nkenge na mikoa mingine inayotuzunguka.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, miradi na maeneo hayo anayoyaeleza ya Mkoa wa Kagera mimi ninayafahamu vizuri, miradi kama ile ya mto Ngwono, maeneo ya Kyakakera, yote yale kwa bahati mbaya ni maeneo ambayo yanategemea maji yaku- *pump* kwenye mto.

Jiografia ya Kagera kwa ujumla maji yake huwezi kuyapata kwa urahisi kwa *gravity*. Kwa hiyo, Wawekezaji wengi mara nyingi wanakwepa hizo gharama za *pumping*.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo tunachokifanya hivi sasa ni kuendelea kuwahamasisha wawekezaji na hasa katika sukari ili waangalie. Na pale ambapo gharama za uwekezaji zikionekana kwamba mafanikio yanatokea ni mazuri zaidi, *return on investment* Wawekezaji wengi wanapenda kufanya hivyo. Kwa hiyo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Assumpter kwamba mimi mwenyewe nimetembelea kule na baadhi ya Wawekezaji tayari wameanza kutufuata, kwa ajili ya kutaka kuwekeza kwa ajili ya kupanua kilimo hasa cha miwa.

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, nimefurahi kukuona.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Ahsante.

Na. 45

Mradi wa Maji Vijijini na Benki ya Dunia

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA aliuliza:-

Viko vijiji vilivyo kwenye mpango wa kupatiwa maji kupitia mpango wa Benki ya Dunia Wilayani Urambo kikiwemo kijiji cha Ushokola ambacho kilitembelewa na watalaam kutoka Wizarani katika mchakato wa kutekeleza mradi huo:-

(a) Kwa nini kwa muda wa miaka miwili sasa hakuna dalili zozote za kuendeleza mradi huo?

(b) Wananchi wa Ushokola walifungua akaunti Benki na kuchangia Shs. 5,000,000 kama asilimia tano ya mradi husika, fedha ambazo ziko benki tangu Mwezi Machi, 2009.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa kauli ya Serikali katika Bunge lako Tukufu mwezi Februari, 2011 na kuelezea sababu za kucheleva kuanza kutekelezwa kwa programu ndogo ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini. Sababu kubwa ilikuwa ni wakati wautekelezaji wa programu ulipoanza mwaka 2007, watalaam wengi katika Halmashauri za Wilaya hawakuwa na uzoefu wa kutumia mchakato wa kuajiri watalaam washauri kupitia taratibu za Benki za Dunia. Hali hiyo ilisababisha ucheleweshwaji wa utekelezaji wa programu.

Mafunzo tayari yalitolewa kuziwezesha Halmashauri kupata watalaam washauri hao ambaeo wamekwisha na wameanza kazi ya kupima, kusanifu miradi na kuandaa zabuni za ujenzi wa miundombinu ya maji katika Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Spika, tarehe 21 Oktoba, 2009, Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ilimwajiri mtalaam mshauri *Howard Humphrey* ambaye anatafiti vyanzo vya maji, kusanifu miradi na kuandaa zabuni za ujenzi wa miundombinu ya maji.

Tarehe 22 Desemba, 2010, Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ilimwajiri Mkandarasi *PNR Services Ltd* kwa ajili ya kuchimba visima na tayari ameanza kazi ya kuchimba visima vya maji katika kijiji cha Itungu, lengo likiwa ni kuchimba visima katika vijiji vyote kumi na tano kikiwemo kijiji cha Ushokola. Kazi ya uchimbaji visima itakamilika mwishoni mwa mwezi wa Aprili, 2011.

Baada ya kazi hiyo, Halmashauri kuajiri mtalaam mshauri na mkandarasi wa kuchimba visima vya maji ni dalili kuwa utekelezaji wa miradi katika vijiji vilivyoainishwa na Halmashauri ikiwa ni pamoja na kijiji cha Ushokola, umekwishaanza.

(b)Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu, kuwapongeza wananchi wa kijiji cha Ushokola kwa kuchangia jumla ya shilingi milioni 5 kwa ajili ya mradi wao.

Halmashauri imeanza kazi ya kuchimba visima, jambo ambalo ni la matumaini kwa vijiji vyote husika ikiwa ni pamoja na kijiji cha Ushokola. Wananchi wasivunjike moyo bali waendelee kuhifadhi fedha zao vizuri kama sehemu ya mchango wao kwenye mradi na kama sera ya Maji ya mwaka 2002 inavyoolekeza. (*Makofi*)

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuriI ya Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Serikali kwenye jibu la msingi inasema kwamba miradi ya Urambo itakamilika mwezi wa Nne mwaka 2011, leo ni mwezi wa Juni, 2011 hata robo ya visima hivyo haijakamilika.

Mkandarasi anayetamkwa hapa alichimba visima vitatu ambavyo vilioneckana na maji, kikiwepo cha Ushokola, kijiji cha Uhindini na Kijiji cha Songambele ambavyo vimepatikana na maji. Vijiji tisa Visima tisa alivyochimba havikupatikana na maji na visima vingine vitatu kwenye vijiji hivyo hajafika kabisa. (*Makofi*)

(a) Kwa hiyo, ninaomba kujua Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha Miradi ya Wananchi hawa inakamilika kwa sababu baada ya mkandarasi kutokupata maji hakuwahi kurudi mpaka leo? Ninaomba sana Serikali ifuutilie ijue kwa nini visima vingine tisa havikupatikana na maji na mkandarasi hajarudi na hivi vingine vitatu hawajawahi kufika kabisa?

(b) Vijiji vitatu ambavyo visima vilioneckana na maji tangu tarehe 3 mwezi 4 baada ya maji kuoneckana mpaka leo mkandarasi hakuwahi kurudi; ninaomba kujua je, Serikali ina mikakati gani na juhudzi za dhati kuhakikisha kwamba maji yaliyopatikana kwenye vijiji vitatu vikiwemo vya Ushokola, Uhindini na Songambele yanasantabwa kwa Wananchi ili kuwaondolea adha ya maji? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika visima 12 ambavyo walikuwa wamewajiri mkandarasi ni visima vitatu ambavyo vilioneckana vina maji; ni kweli kwamba, mkandarasi yule hajarudi.

Jana Mwenyekiti wa Halmashauri ya Urambo, alikuja ofisini kuelezea habari hii; ni kwamba, kuna tatizo kati ya usanifu kuelekeza kwamba maji yako mahali fulani. Walipokwenda kuchimba ikaoneckana kwamba, hakuna maji na kwa Mkoa wa Tabora kwa sehemu nyingi maji ni tatizo, chini ya ardhi hakuna maji. Japokuwa upatikanaji wa maji umeoneckana ni kidogo kuliko kawaida, mara nyingi tunategemea kwamba, asilimia 70 ya eneo, kwa mfano, katika usanifu huwa tunapata maji, lakini kwa maeneo ambayo walikuwa wamepitia, yameoneckana yana matatizo ya maji. Sasa Wizara yangu itapeleka wataalam kuangalia eneo lote lile na kupima tena kuona ni wapi tunaweza kupata maji ili tuweze kuchukua hatua zinazotakiwa.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya maji yanafanana katika Manispaa ya Tabora. Kweli hali ya maji katika Mkoa wetu hasa Manispaa ya Tabora, kitaalam wanasema ni *semi arid*; kwa nini basi Wizara inang'ang'ania kulipa fedha nyingi kwa makandarasi hawa ambao katika vijiji 12 ni vijiji viwili tu ndiyo vimepatikana na maji; kwa ni nini fedha hizo zisihamie kwenye kutengeneza mabwawa ili kuondokana na tatizo hili?

SPIKA: Visima vinatakiwa halafu na mabwawa labda.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli maeneo mengi, maji chini ya ardhi ni tatizo na kwamba, tuliweza kufikiria kuchimba mabwawa. Katika Programu hii ya Uendelezaji wa Maji ni Halmashauri zenyewe ndiyo zinaamua kwamba, chanzo chao kiwe nini, kwa sasa waliamua kuchimba visima. Sasa kwa sababu waliamua kuchimba visima ilikuwa tuendelee na kuchimba visima, lakini pia tunaweza tukaendelea na Programu ya Kuchimba Mabwawa kama ni sehemu nyingine mbadala. Kwa Manispaa ya Tabora, sisi kama Wizara, tunafikiria tatizo la maji tutalitatua tutakapochukua maji kutoka Ziwa Victoria; Mipango ambayo tunategemea kuanza kuitekeleza mkipitisha Bajeti ya Wizara ya Mwaka 2011/2012.

Na. 46

Wazanzibari Wanaoomba Ajira JWTZ Kupimwa Afya Mara Mbili

MHE. AMINA ANDREW CLEMENT (K.n.y. MHE. MUSSA KHAMIS SILIMA) aliuliza:-

Kuna manung'uniko kuwa Wazanzibari wanaoomba ajira katika Jeshi la Wananchi (JWTZ) hupimwa afya zao kule Zanzibar na wanapofuzu huchanganywa na wale wa Tanzania Bara na kuanza kupimwa upya; wanapopimwa mara ya pili baadhi huachwa kwa visingizio vya upungufu wa afya zao na hivyo wakati mwingine hutetekezwa katika eneo husika bila kurudishwa Zanzibar walikotolewa:-

(a) Je, ni nini kinachosababisha waombaji hao kutoka Zanzibar kupimwa mara mbili na wakati wenzao wa Tanzania Bara hupimwa mara moja tu?

(b) Je, Serikali haioni kuwa waombaji hao walioachwa baada ya kupimwa mara ya pili hawakutendewa haki?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mussa Khamis Silima, Mbunge kuitia Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, waombaji wa kujiunga na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, hupimwa afya zao ili kuhakikisha kuwa, wanaweza kuhimili Mafunzo ya Kijeshi na baadaye waweze kutekeleza majukumu mbalimbali ya kijeshi katika mazingira tofauti.

Mheshimiwa Spika, upimaji wa kina hufanyika katika kituo cha mafunzo ya kijeshi kabla ya kuanza mafunzo. Kwa kuwa upimaji huu ni wa gharama, hufanyika kwa wale tu ambao wamefaulu katika hatua ya awali; wanaonekana kuwa na matatizo ya kiafya hurejeshwa kwa gharama za jeshi hadi makwao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ya utangulizi, ninaomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba, waombaji kutoka Zanzibar pekee ndiyo hupimwa afya mara mbili bila kuhusisha na wenzao kutoka Bara. Utaratibu wa upimaji haubagui bali unafanyika kwa wote kufuatana na utaratibu kama ilivyoelezwa hapo juu.

(b) Mheshimiwa Spika, waombaji walioachwa baada ya kupimwa kwa mara ya pili na kuonekana na matatizo ya kiafya, walitendewa haki kwa kuwa jeshi linahitaji kuwa na wanajeshi wenye afya nzuri, wanaoweza kutekeleza majukumu ya kijeshi kikamilifu. Hii ni kwa manufaa ya jeshi na wahusika pia ikitiliwa maanani kuwa mafunzo ya kijeshi ni magumu na yanahitaji utimamu wa mwili.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa ajira katika Jeshi umebadilika na sasa Jeshi linaajiri vijana ambao wameshapitia Mafunzo ya JKT.

Mheshimiwa Spika, vijana wanaoombwa kujiunga na JKT hutakiwa kuripoti kwenye usaili huku wakiwa na fedha za kuwarudisha makwao endapo hawatofaulu vipimo vya afya. Hili linafanyika kwa kuwa waombaji ni wengi mno na JKT haitoweza kuwalipa wote wanaopaswa kurudi makwao kwa kugundulika kuwa na matatizo ya kiafya.

MHE. AMINA ANDREW CLEMENT: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Zanzibar kuna Hospitali kubwa ya Jeshi Bububu; je, kwa nini Serikali haioni bora kupeleka wataalam huko Zanzibar wakati wa upimaji ili kupunguza gharama za kuleta vijana wengi Dar es Salaam na baadaye kuwarudisha? Ahsante. (*Makofi*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na ushauri wake; ni ushauri mzuri endapo jeshi sasa litaamua kwa makusudi vijana wote wanaotoka upande wa Unguja wawe wanapimwa pale Bububu kabla ya kwenda katika kambi zinazotakiwa. Utaratibu huu hautaweza kufanyika kwa Tanzania nzima, kwa sababu siyo maeneo yote yana Hospitali za Jeshi kama hizo, lakini

ninataka nikubaliane naye kwamba, pengine sasa ni wakati wa kufikiria jambo hili kwa Zanzibar. (*Makofî*)

Na. 47

TRA na Zanzibar Kufanya Kazi Moja Zanzibar

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA aliuliza:-

Kazi ya ukusanyaji mapato Zanzibar hufanywa na *TRA* na *ZRB*; na kuna makubaliano ya pande zote mbili za Muungano kuwa mapato yote yanayokusanywa Zanzibar yatumike katika Serikali ya Tanzania Zanzibar:-

(a) Je, kuna sababu gani ya kuwepo *TRA* Zanzibar wakati *ZRB* inafanya kazi hiyo na ina uwezo kisheria na kiutendaji kama ilivyo *TRA*?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kuwepo kwa Vyombo hivyo ni kuongeza gharama zisizo za lazima?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalî la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, ninapenda kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa ukusanyaji wa mapato Tanzania umegawanyika katika maeneo makuu matatu; mosi, kuna kodi za Muungano; pili, kuna kodi zisizo za Muungano; na tatu, kuna Kodi za Serikali za Mitaa. Mgawanyo huu ni kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 4(3) ya Katiba, inaelezea mgawanyo wa mamlaka za uendeshaji wa Mambo ya Umma ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mambo ya Muungano zikiwemo kodi zinazosimamiwa na *TRA*, zimeorodheshwa katika Nyongeza ya Kwanza ya Katiba. Kwa mujibu wa Katiba, Mambo ya Muungano husimamiwa na Taasisi za Kimuungano.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo ya awali, ninapenda sasa kumjibu Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, swalî lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), kwa Zanzibar ina jukumu la kukusanya kodi zote za Muungano, kufuatana na maelezo ya Ibara ya 138 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikitomwa sambamba na Ibara ya nne aya ya tatu na Nyongeza ya Kwanza ya Katiba hiyo. Kodi nyingine zote ambazo si za Muungano, ikiwemo VAT kwa bidhaa za ndani, ushuru wa stempu, ushuru wa hoteli na kodi mbalimbali kwenye bidhaa za mafuta na kadhalika, hukusanywa na Bodi ya Mapato Zanzibar kwa upande wa Zanzibar. Hii ni kwa mujibu wa Katiba na Sheria zilizopo.

(b) Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni kweli kufanya kazi mahala pamoja kwa Vyombo vyote viwili kunaongeza gharama zisizokuwa za lazima. Kwa kutambua hilo na kwa nia ya kupunguza gharama za ukusanyaji mapato unaofanywa na Vyombo hivi viwili, Serikali ipo katika mchakato wa kuangalia uwezekano wa kuiteua *ZRB* kuwa Wakala wa Kukusanya Kodi zote za Muungano zilizotoka Zanzibar. Ahsante.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri, ningependa kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) *ZRB* ni Chombo ambacho kina uzoefu, uwezo na wataalam wa kutosha katika shughuli za kukusanya mapato kwa upande wa Zanzibar. Je, Serikali itamaliza lini mchakato wake ili Chombo hiki kipewe dhamana kamili ya kukusanya mapato yote kwa upande wa Zanzibar?

(b) Ibara ya 133 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inasema kwamba kutakuwa na Akaunti ya Fedha ya Pamoja kwa Jamhuri ya Muungano; je, akaunti hii imekwishafunguliwa na kama bado ni sababu zippi zinazopelekea kutofunguliwa? Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, *ZRB* Zanzibar ina uwezo na uzoefu wa kukusanya kodi, lakini ni lazima ithibishwe kwamba wana uwezo pia wa kubeba jukumu la kukusanya kodi za Muungano. Siwezi kusema lini litafanywa litamazika, lakini suala hili halitachukua muda, tutaangalia uwezo uliokuwepo na uzoefu ili *ZRB* izikusanye hizi kodi bila matatizo. Hili ni suala la Kikatiba wala halitakuwa na matatizo.

Swali la pili linahusu Ibara ya 133; Ibara hii imeagiza kufunguliwa akaunti ya pamoja kwa ajili ya Serikali ya Muungano na Zanzibar. Ninaomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Akaunti hii bado haijafunguliwa. Sababu ni kwamba, Akaunti hii inatakiwa isimamie na ihifadhi fedha za gharama na mapato ya Muungano, jambo ambalo mchakato wa kukubaliana kutegemeana na ripoti ambayo imetayarishwa na mtaalam mwelekezi haijakamilika. Mara tu Serikali zetu mbili zitakapokubaliana kuhusu gharama na mgawanyo wa mapato ni hapo tu Akaunti hii itafunguliwa na kuanza kutumika. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita na maswali yamekwisha. Nina matangazo ya shughuli za kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa January Makamba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, leo 14 Juni, 2011 watakuwa na kikao saa saba mchana katika Ukumbi Namba 219.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi Chana, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, leo saa saba pia watakuwa na kikao katika Chumba Namba 231. Pia Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omari Kigoda, anaomba

niwatangazie Wajumbe Kamati yake hiyo kwamba, leo saa 7.00 mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati kitakachofanyika Ukumbi wa Pius Msekwa B.

Vilevile nina tangazo la Ofisi kwamba, Waheshimiwa Wabunge, ambao wana vitambulisho nya muda, wavirejeshe mapema iwezekanavyo kabla wataalam hawajaondoka Siku ya Ijumaa ili waweze kupewa vitambulisho vipy. Kwa hiyo, ni muhimu kwa sababu hawa ni wageni, hawatokei hapa; hivyo, kuna siku ya leo Jumanne, Jumatano na Alhamisi, wageni wataondoka Siku ya Ijumaa. Kama wewe una kitambulisho cha muda, basi kakirejeshe kwa Mkurugenzi Msaidizi, Huduma kwa Wabunge, sijui chumba namba ngapi!

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sina matangazo mengine.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, kufuatia kifungu namba 68(7), kinachohitaji niombe Mwongozo wa Spika, ninaomba kuomba Mwongozo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati ninauliza swali langu la msingi kuhusiana na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa KIA, majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na nyongeza ya ufanuzi ya Mheshimiwa Waziri mwenyewe, yalikuwa na upungufu mkubwa. Kwa sababu kwa mujibu ya Kanuni ya 46 ya Kanuni zetu za Bunge, Waziri au Mbunge ye yeyote anapouliza swali lake, anatakiwa kujibwa kikamilifu; na kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(a), majibu hayo yanatakiwa yawe ya ukweli.

Sasa kwa sababu nilisema kauli ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, Kampuni ya KADCO iliwekeza shilingi bilioni sita katika kujenga njia ya kutua ndege katika Uwanja wa Kimataifa wa KIA siyo ya kweli; na akaliambia Bunge kwa mujibu wa kifungu namba 63(4) kwamba, fedha zile zilitolewa na Benki ya Dunia na kujengwa na Kampuni ya Fedelis. Je, Waziri atakubali kulifuta jibu lake hilo ili lisiingie katika Rekodi Rasmi za Bunge kwamba ni kweli mwekezaji aliwekeza fedha hizo? Ninaomba mwongozo wako.

SPIKA: Mheshimiwa Freeman Mboge, ni sahihi ulivyosema. Mwongozo wangu ni kwamba; ni vizuri wewe pia ukaleta maelezo yako binafsi wakati wa *adjourning motion* kueleza wewe unavyojua na kwamba alivyosema Waziri siyo sahihi. Ukifanya hivyo, utatoa nafasi na wengine nao kusema kwamba ni nini. Kwa sababu swali lile wewe umeuliza yeye kajibu, hatuna ushahidi sisi wa kukusaidia kuamua. Tutakusaidia kuamua kama wewe ukaleta maelezo yako wakati wa kuahirisha Bunge au wakati mwingine, kutaka maelezo zaidi baada ya hapo. Kwa hiyo, ndiyo utaratibu. (*Makofi*)

Sasa kitu ambacho ninaomba tukielewe Waheshimiwa Wabunge ni suala la matumizi ya Mwongozo wa Spika. Hivi alivyotumia Mheshimiwa Freeman Mboge, ni sahihi kwamba, hata kama jambo limetokea wakati tunaendelea, sasa kwa wakati mzuri anasimama kuhusu Mwongozo wa Spika kwamba, wakati jambo fulani linatokea

kulikuwa na hiki na hiki ningefanyaje; siyo mnasimama Mwongozo wa Spika, Mwongozo wa Spika, siyo sahihi. (*Makofit*)

Unaacha kitendo kile kinaendelea mpaka mwisho wake, kwa wakati mzuri kama hivi sasa unaona nimefunga shughuli kabla sijaingia kwenye shughuli nyingine, amesimama ameomba Mwongozo wa Spika kwa jambo lililotokea wakati tunafanya shughuli nyingine. Kwa hiyo, hii ni sahihi, siyo wakati nipo hapo Mwongozo wa Spika, halafu wengine wanapiga kelele, hii inaonekana haieleweki.

Sasa kuhusu utaratibu na anasimama mtu, Spika anamwangalia ndiyo anasema kuhusu utaratibu, siyo kuhusu utaratibu, kuhusu utaratibu; utaratibu gani uliovunjwa! Kwa hiyo, hiyo nayo tunaitumia vibaya, wanaotuangalia sura zetu zinaonekana za aibu na sisi tunaitwa Waheshimiwa, mimi sijui kwa nini ninyi wenyewe mnajidharau sana maana mkiwa kama Watu wa Kariakoo mtaonekana kama Watu wa Kariakoo, haya mambo ya Utaratibu na Mwongozo yana taratibu zake.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tusikilizane, Wananchi wanawaangalieni nyote na wanapenda kufuutilia vipindi vyetu, lakini mnavyofanya siku hizi, mimi jana sikuwepo nilikaa kwenye TV, hata sikuwa na hamu ya kuangalia Bunge linavyoendelea. Kwa hiyo, jamani twende kwa utaratibu, tutakuwa na mafunzo kidogo kabla ya kuanza kipindi cha bajeti.

Spika ninapokuwa ninaongea, ninaomba mnisikilize. Tutakuwa na mafunzo tena kuhusu kipindi cha bajeti kupitia vifungu, kwa sababu kama hamlijui eneo hili nalo litaleta aibu mbele ya watu. Ninashukuru, Mheshimiwa Mbowa, unaweza kufanya hivyo, halafu tukipata ukweli basi tutaamua itakavyofaa. Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2011/2012 – 2015/2016

(*Majadiliano yanaendelea*)

SPIKA: Waheshimiwa tukae. Unapofika muda wa kubadilisha magwanda na hawa wanaondoa Siwa, ndiyo maana tunasimama, kwa sababu tunapobadili Siwa hatuwezi kubadilisha tukiwa tumeendelea kukaa. Ndiyo maana ninapoondoka mimi kwenye Kiti kwenda kubadilisha magwanda haya, Siwa inakuja kuwekwa chini au inaondolewa na ndiyo sababu wakati huo tunasimama.

Tunaendelea na mjadala wetu. Leo ndiyo siku ya mwisho, nimewona Mheshimiwa Freeman Mbowa, kaenda wapi tena? Mheshimiwa Gekul, atafuatiwa na Mheshimiwa Kigola.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Niseme kwamba, ni kweli nchi inapokuwa inapanga Mipango lazima iangalie vipaumbele. Pamoja na kuangalia vipaumbele, ni kweli kwamba, nchi ikitaka kuendelea ni lazima iwe na Mipango thabiti.

Nimesoma Mpango huu wa Miaka Mitano wa Maendeleo na kubaini kwamba, Mpango huu umejengwa juu ya Dira ya 2025 na tunachotaka ku-*achieve*. Ukiwaja Mpango huu unaona kwamba, unatuelekeza katika yale masuala matano ambayo yako katika Dira ya Tanzania ya mpaka mwaka 2025. Mpango huu pia unaangalia au unaturudisha, unakuwa kama *speed governor* au kama *road map* ya kutupeleka mwaka 2025. Mpango umezingatia vipengele ambavyo vinatakiwa katika Mipango, umezingatia hatua ya kwanza kabisa kwamba, *we need to plan* na umeangalia Dira ya 2025 inahitaji *to be achieved*. Pia umeangalia rasilimali, vipaumbele, utekelezaji na ufuataliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo na hayo. Nimejaribu kupitia nyaraka mbalimbali, nimejiuliza nchi hii imeanza kupanga leo na ndiyo kitu cha kujiuliza na kukizingatia. Kuna Mipango mingi tumepongo, kuna Dira nyingi katika nchi hii tangu tupate uhuru tumeweza kuzipitia; mfano, baada ya Uhuru tu Dira ilituelekeza kuchapa kazi, kufanya kazi kwa bidii ili kuondokana na umaskini. Miaka ya 1967 tumeingia kwenye Dira. Mkakati wa Azimio la Arusha, tuangalia kipindi hicho tulifanya nini. Azimio la Arusha lilitupeleka katika kuondoa umaskini, kupunguza ujinga, maradhi na vitu kama hivyo. Ukiangalia Mipango ambayo tumeipitia wakati wa Uhuru mpaka leo, tathmini iliyofanyika imeonesha kwamba, Mipango mingi imefeli kutokana na sababu ambazo zimetajwa katika nyaraka mbalimbali; Mipango mingi ya Tanzania imefeli kwa sababu ya hulka ya kutegemea Wahisani. Tunajenga huku tukifikiri kwamba, sisi wenyehe hatuwezi kutekeleza, tunafikiria Wahisani watupatie hizo fedha tuweze kuendeleza kile ambacho tumekipanga. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba, hata huu Mpango wa Miaka Mitano ambao sasa hivi umeletwa katika Bunge hili Tukufu, haujaondokana na fikra hizo za utegemezi. Tumeona katika trilioni 42 ambazo Mpango huu unategemea kuzitumia ili ukamilike, nchi kama nchi pamoja na rasilimali nyingi tulizonazo, inachangia *almost* trilioni 13 tu, tofauti na zile trilioni 42, lakini hatujaangalia ni nini ambacho kimekwamisha Mipango mingi ambayo tulishawahi kupanga. Mimi niseme kwamba, pamoja na kutegemea fedha za Wahisani, lakini kuna tatizo la udhaifu katika utawala; imeelezwa katika nyaraka mbalimbali kwamba, tunapanga Mipango, lakini Serikali haiisimamii ipasavyo. Tunaleta Mipango inapitishwa, ukienda kwenye utekelezaji haieleweki huu Mpango ni nani anakwenda kuusimamia vizuri, kila Mdau amewekwa, Wananchi wamebekwa, sekta binafsi zimebekwa, lakini pia na Wabunge katika Mpango huu wa Miaka Mitano tunaombwa kwamba tuupeleke kwa Wananchi, tukautafsiri kwa Wananchi wauelewe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo kwa sababu kama ni Mpango wa Miaka Mitano wa Wananchi, tulitegemea kwamba, huu Mpango wa Kitaifa unaweza ukawa Wananchi wamehusishwa kuanzia ngazi ya chini mpaka ya juu. Upungufu huu

tumeubaini kwa sababu Mpango wenyewe umeandaliwa kwa miezi sita, Januari mpaka hivi sasa umeletwa kwetu; tujiulize ni Watanzania wangapi wameshirikishwa katika Mpango huu; Wilaya ngapi zimeshiriki; na Wananchi wangapi na wa Kata ngapi wameshiriki katika kuainisha vipaumbele vya Mpango huu. Tumeainisha vipaumbele vitano; tumeanza na miundombinu, ikafuata maji, kilimo, rasilimali watu na vitu kama hivyo, lakini je, tumepita huko na tumefanya *analysis* ya kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kubainisha upungufu huo wa Mpango, sisemi kwamba tusiwe na Mipango, Mipango ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi, lakini Mipango hii, tunapanga kwa ajili ya Watanzania, Watanzania hawa wahuishwe kwa kiasi kikubwa. Tume ya Mipango ikipanga kwa ajili ya Watanzania, kutekeleza itakuwa ni tatizo na ukisoma kwenye hizi nyaraka, kuna mahali wameandika kwamba, *yes we can do*. Mimi ninakubali tunaweza, lakini Serikali imeonesha utashi kiasi gani; *yes we can do ourselves*, siyo kutegemea Wahisani. Kama Serikali inatenga trilioni mbili kwa mwaka ambao tunatakiwa tuwe na trilioni nane kutekeleza Mpango huu, hiyo ya kusema *yes we can do inaonekana wapi? Can we?* Lazima tujiulize.

Niende katika mambo machache, mimi ninapenda kuzungumzia suala la ardhi; katika Mpango huu, ukisoma ukurasa wa 121, kipengele cha ardhi kimetengewa bilioni 141. Nilikuwa ninajiliza Serikali bado haijagundua kwamba hiki kipengele cha ardhi kinatakiwa kutengewa fungu kubwa ili kuhakikisha kwamba migororo mingi ya ardhi inapunga katika nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunapozungumza suala la utulivu katika nchi hii ya Tanzania, lazima tukubali kama Viongozi wa nchi hii kwamba, tatizo la ardhi ni kubwa sana. Migogoro ya ardhi katika Mahakama ni mingi, ugomvi mwingi siyo maandamano ni Watanzania kusogezwa pembedi katika rasilimali ya ardhi wakati wawekezaji wanapewa kipaumbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili niliongee kwa masikitiko zaidi; katika Mkoa wa Manyara, ninashukuru hata Naibu Waziri alizungumza kwamba ni mionganini mwa Mikoa ambayo migogoro ya ardhi ni mingi. Niwape mfano mzuri wa Bonde la Kiru, mpaka leo tunavyoongea, Wananchi wa Kiru wanaishi vichakani sasa ni miezi sita, kama sikosei tangu mwezi wa kwanza au wa pili. Tumesikiliza sana Wawekezaji, wana haki, tunapotaka kuendelea kama Watanzania, tunahitaji Wawekezaji katika nchi yetu; lakini tunapanga vipi vipaumbele vya Wawekezaji na maeneo ambayo wanatakiwa kwenda kuwekeza?

Migogoro ya Wawekezaji na Watanzania ni mikubwa mno. Ninafikiri Serikali imesahau kwamba, kuna *lease* ambazo zimetolewa za mwaka 1999, lakini kuna ongezeko la Wananchi. Miaka hiyo ukimpatia Mwekezaji ekari 600 au 5000 *it was okay*, lakini *tuki-compare population* ya kipindi hicho wakati tunapata Uhuru, Watanzania tulikuwa kama milioni 12, leo tuko zaidi ya milioni 43: Je, Serikali imeangalia vipi kipengele hiki cha ardhi kuhakikisha kwamba migogoro mingi inaepushwa kwa kuwapimia Wananchi maeneo wanayoishi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huu wa Miaka Mitano, niiombe Serikali ifanye utafiti wa kutosha; kuna Watanzania ambao wanaishi katika hizo *lease*, wakiingiza ng'ombe ni ugomvi na Wawekezaji, wakilima ni ugomvi na Wawekezaji, Waziri wa Ardhi anafahamu. Serikali ikae chini imalize hii migogoro, hatupendi Watanzania wapoteze muda kwenda Mahakamani kwa migogoro ya ardhi, inaumiza sana. (*Makofi*)

Nami niliombe Bunge lako Tukufu, hili linapokwenda kutekelezwa, kipaumbele kipelekwe Bonde la Kiru. Nilizungumze kwa umakini kwamba, Watanzania wanahitaji kuishi katika nchi yao, kama inafikia hatua kunakuwa hakuna maelewano baina ya Wawekezaji wa Kiru na Wananchi, ninaomba Serikali iende. Mawaziri watano wamekwenda mpaka leo tunajiuliza nini kimefanyika hatukioni, hebu Serikali iende pale, Wananchi wa Kiru nao ni Watanzania, wanahitaji kuishi, wahalifu wakamatwe wawekwe ndani na Watanzania wajengewe nafasi ya kutulia katika nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshagongewa kengele ya kwanza, ninaomba nizungumzie suala la makazi. Ukisoma Mpango huu, Serikali inasema kwamba, tuna Mpango wa kuleta mashine za kufyatua matofali yanayotumia mchanga na simenti. Mimi nilikuwa ninajiuliza; Serikali ina malengo mazuri lakini hizi bei za mifuko ya simenti kila siku zinapanda; Watanzania wataweza kweli? Tatizo la Watanzania kuishi kwenye nyumba za majani au za tembe siyo matofali, Watanzania wana uwezo wa kufyatua matofali kwa udongo tu na maji wakajenga, lakini ukienda kwenye nondo, bati na simenti ni tatizo. Hawa watu wamepanga Serikali iangalie kama kweli tunahitaji kuondokana na hizi nyumba ambazo tunasema kwamba sasa siyo imara basi nayo Serikali ifanye *intervention*, vifaa vya ujenzi vishuke bei tutawasaidia sana Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimbilie kwenye suala la afya, ni sehemu ambayo ninaipenda sana. Nilipokuwa ninausoma huu Mpango, kuna kipengele kilinifurahisha kwamba, kutakuwa na *construction of 95 maternity waiting homes*. Vyumba ambavyo akina mama wanajisubiria wakati wanakwenda kujifungua. Hili ni jambo zuri, lakini wasiwasi wangu ni kwamba, Serikali inatenga tu trilioni mbili, nyingine zote tunategemea Wahisani. Miongoni mwa Wizara ambazo zime-be affected na fedha za Wahisani ni Wizara ya Afya. Ukiangalia Bajeti ya Wizara ya Afya ya mwaka jana, shilingi bilioni 500, almost asilimia 97, inachangiwa na Wahisani. Je, hili linaweza likatekelezwa kama Serikali inachangia asilimia mbili tu katika Wizara ya Afya? Hivi hii ndoto nzuri ambayo tunaletewa hapa kwamba sasa akina mama wanapokwenda kujifungua hawatatembea tena zile kilomita; akishaona tarehe za kujifungua zimefika anasogea katika hizo nyumba; je, itatekelezwa? Ndoto hii ikitekelezwa tutakuwa tumewasaidia Watanzania

Limenifurahisha suala la bajaji za miguu mitatu. Ukisoma katika Mpango huu, sehemu ya kuhakikisha kunakuwa na hizi pikipiki za miguu mitatu, Serikali imepanga kwa miaka mitano kupeleka pikipiki zisizopungua 2,555 kwenye vituo vyote vya afya. Nilikuwa ninapiga *average* ya utoaji pikipiki hizo; hizi pikipiki mpaka sasa tunaambiwa mwanzoni zilikuja 30, lakini juzijuzi tukaambiwa zimeingia tena 100, nikapiga *average* ya miaka mitano, *of course*, sasa siyo miaka mitano kwa sababu mwaka huu tumpanga

kwa ajili ya ku-review huo Mpango, miaka minne zinatakiwa pikipiki 650 kwa mwaka. Kwa mwaka jana ni 130 tu, tuseme Serikali inaweza au tunawaaminisha tu Watanzania *yes we can do* wakati hatujajipanga ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya yakipewa vipaumbele, kama kweli yalioandikwa katika Mpango huu yatawafikia Watanzania, 2015 tutakuwa tunazungumza mambo mengine, tutahama kwenye vipaumbele vingine siyo hivi. Wasiwasi wangu ...

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Menrad Kigola, Mheshimiwa Mariam Kisangi ajiandae.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kupewa nafasi hii ili niweze kuchangia Mpango wa Miaka Mitano. Kabla sijaingia kwenye mada, ninapenda nitoe shukrani nyingi kwa wote walioshiriki kuandaa Mpango huu, tunauita Mpango wa Kitaifa. *Sentence* ya kusema kwamba ni Mpango wa Kitaifa, mimi binafsi imenifurahisha sana kwa sababu kila mmoja atatakiwa awajibike kwa kufuata Mpango huu wa Kitaifa.

Ninapenda nisisitize kuwa, ninaiomba Serikali kwamba, kwa kuwa huu ni Mpango unaolenga madhumuni makubwa na umeweka vipaumbele kwa undani na kila mmoja inabidi ausome na auelewe ili tuweze kutimiza hii miaka yetu mitano, tunaondokane na hali ngumu ya umaskini. Sasa nilikuwa ninaomba tupate *copy* nyingi sana za Kiswahili, kwa sababu Mpango huu utakwenda katika Wilaya zetu na Kata zetu, wataweza kusoma kila mmoja aelewe tunakwenda wapi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nijikite kwenye vipengele ambavyo vimeoneshwa katika Mpango huu. Tukiangalia kipengele kinachohusiana na masuala ya kilimo; katika Mpango huu masuala ya kilimo yameelezwa kwa undani sana. Sehemu kubwa ya Watanzania wanaishi vijiji na wanategemea kilimo.

Ninashukuru sana katika Mpango huu tumeweza kuelezea kwa undani kuhusiana na kilimo, lakini kuna jambo moja ambalo ninapenda niliongelee, nalo ni kwamba katika Mpango huu kuna mambo yanatakiwa yaoneshwe ili kukiimarisha kilimo. Kwa mfano, ndani ya miaka mitano, Mpango bado haujafafanua ni kiasi gani katika nchi yetu ya Tanzania tutakuwa na viwanda vya mbolea ili kuondokana na tatizo kubwa la upandaji wa bei ya mbolea. Wananchi wengi sana katika vijiji vyetu hivi sasa tunakabiliana na tatizo kubwa la upandaji wa bei kwa upande wa mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mchango wangu, kuhusu kipengele cha Kilimo kwanza, ili tuweze kufikia mahali lengo letu litimie, jana ulisema kuna matrekta yameshaletwa kwa ajili ya kukopesha wakulima na bahari nzuri sana, Wananchi wangu wameanza kunipigia simu wanataka wapate mwongozo unaojieleza vizuri kuhusu

ukopeshwaji wa matrekta ili tuondokane na kilimo cha mkono. Kwa hiyo, ninashukuru sana.

Pili, nilikuwa ninaomba niongelee masuala ya barabara. Katika Mpango wetu wa Miaka Mitano, imeshaoneshwa kabisa kwamba, barabara katika Wilaya kadhaa zitakuwa za kiwango cha lami. Hilo ni suala la msingi kabisa katika maendeleo yetu; ili tuendelee nchi yetu inahitaji kuwa na viwanda vinavyojitosheleza, viwanda vinavyozalisha. Sasa nilikuwa ninajaribu kupitia katika Mpango huu, nimeangalia katika Mkoa wa Iringa, nikajikita moja kwa moja kwenye Wilaya yangu ya Mufindi; Mufindi kuna viwanda vingi sana ambavyo vimejitosheleza katika uzalishaji mali wa kitaifa.

Kwa mfano, ukienda kule, tuna Kiwanda cha Chai ambacho ni kikubwa katika Afrika; tuna Kiwanda cha Karatasi kikubwa sana katika Afrika; tuna Viwanda vya Mbao na Misitu ya kutosha kabisa. Tatizo linalotufanya tusiweze kuzalisha vizuri ni la lami. Tuna barabara moja inayotoka katika Kijiji cha Nyololo, imepita kwenye mashamba ya chai, ninadhani katika Kijiji cha Igowole, ikaenda Kijiji cha Kibao, imekatiza imekwenda mpaka katika Kiwanda cha Mgololo. Hii barabara katika Mpango wa Mkoa, tumeweza kukaa kwenye vikao vyetu vya *RCC* tumejadili na kila anayotoka Mkoa wa Iringa ukimwuliza lazima ataongelea Barabara ya Mufindi kuweka kiwango cha lami. Sasa katika Mpango huu, nimejaribu kuusoma nikaona barabara hiyo haijawekwa na bahati nzuri sana kama sisi Wabunge tumekaa tunaujadili na mimi nikiwa Mbunge ninayetoka kule, lazima niweke kipaumbele katika Barabara ya Mufindi kwani ni muhimu sana kwa uzalishaji wa Kitaifa. (*Makofi*)

Suala la pili, ninaomba niongelee masuala ya Viwanja vya Ndege. Viwanja vya Ndege, Mpango huu umeeleza vizuri kabisa, lakini bado kuna Viwanja vya Ndege ambavyo ni muhimu sana. Kuna Mjumbe mmoja jana alieleza vizuri sana, alisema katika Mpango lazima tuangalie Kitaifa, lakini tunashuka katika Mkoa, tunashuka katika Wilaya. Katika Mkoa wa Iringa sisi tuna viwanda vya ndege viwili. Sasa nimesoma katika Mpango huu kuna Kiwanja cha Ndege cha Nduli, Kiwanja cha Ndege cha Njombe, hakijaguswa kabisa na tusipokiweka kwenye Mpango, maana yake ndani ya miaka mitano hivi viwanja havitashughulikiwa.

Tumetaja Viwanja vya Ndege ambavyo vilikuwa vinapewa pesa, lakini viwanja vyetu hivi vya Iringa na Njombe bado havijawekwa kwenye Mpango. Ninaombu Serikali ivishughulikie viwanja hivi, ione kwamba ni viwanja muhimu na ukizingatia Mkoa wa Iringa ni Mkoa ambaa una neema kubwa; tuna *Ruaha National Park*, tuna kilimo cha maua na sasa hivi tuna Bonde la Mgololo ambapo kilimo cha umwagiliaji kinaendelea. Sasa bila kuwa na Viwanja vya Ndege ambavyo vinajitosheleza, tutawenza kushindwa kusafirisha hata mazao yetu kupeleka nje. (*Makofi*)

Suala la pili, ninaomba nijikite kwenye elimu. Ninashukuru sana kwenye Mpango huu, kipengele cha elimu kimeelezwa vizuri sana. Jana nimesikia kwamba, kila Wilaya tutajaribu kujenga Vyuo vya Ufundu. Vyuo vya Ufundu ni sahihi, vinasaidia sana vijana wetu wale ambaa wanashindwa kufaulu kwenda Vyuo Vikuu, lakini tunapata changamoto kubwa sana ambayo nimeiona katika mwaka huu. Ukiangalia idadi ya

wanafunzi wanaomaliza *Form Four*, wamefeli mtihani; sasa tukisema kwamba kila Wilaya itajenga angalau chuo kimoja bado hakitoshi. Mimi nilikuwa ninapendekeza kuwa, kila Tarafa iwe na Chuo cha Ufundu ili vijana wetu wanaoshindwa kuendelea na masomo ya juu waweze kupata elimu ya ufundu. Sisi Wabunge hili ni tatizo kubwa, kwa sababu tukipita katika Kata zetu, tunapata changamoto kubwa sana, vijana wetu hawana kazi, mpaka sasa hivi wako mitaani. Kwa hiyo hivi vyuo vinasaidia sana kuepusha wimbi kubwa la vijana ambaa wanakaa mitaani bila kazi.

Suala lingine ni la ajira kwa vijana. Taifa letu sasa linaingia changamoto kubwa sana kwa ajili ya vijana na katika Mpango huu bahati nzuri wameeleza kwamba, ajira ya vijana itazingatiwa. Bahati mbaya hawajaeleza tuna vijana wangapi wanamaliza katika Vikuo Vikuu na wangapi tunategemea ifikapo mwaka 2015 watakuwa wameshapata ajira. Hivi sasa changamoto hii inatukabili na ukiangalia vijana wengi wamemaliza vyuo vikuu hawana kazi. Hii ndiyo baadaye itatuletea shida; hawa vijana watashindwa maisha na ili kuwapa maisha ni lazima kila mmoja afanye kazi.

Tukitaka ku-create employment kwa vijana wetu, ni lazima tuimarishe viwanda vyetu vifanye kazi na bahati nzuri Serikali imeanza kuchukua jukumu la kuingiza Wahisani waweze kuanzisha viwanda ili kusaidia vijana wetu wapate ajira. Hii bado haitoshi, inabidi viwanda vinavyokufa vifufuliwe. Serikali ijikite sana kwenye viwanda ili vijiana wetu waweze kuajiriwa.

Mwisho, ninapenda nijikite katika masuala ya maji. Masuala ya maji yanaongelewa sana. Ninashukuru sana, Wizara ya Maji katika Mpango wa *World Bank*, kwenye Jimbo langu la Mufundi Kusini, nimeshachimbiwa visima kumi na huo ni Mpango mzuri ambaa Chama cha Mapinduzi kimeanza kuutekeleza. Kwa hiyo, ninashukuru sana, isipokuwa ninapenda niongezee kwamba, vile visima vimeshachimbwa lakini bado havijawekwa mabomba na hatujui yatawekwa lini. Mpango ni mzuri., nadhani ndanii ya miezi mitatu Wananchi wataanza kupata maji safi na salama.

Kwa kuwa kengele imeshagonga, ninaomba nimalizie kwa kusema kwamba, katika Mpango huu wa Miaka Mitano ili tuweze kufikia mahali pazuri, Viongozi wote; Wabunge na Mawaziri, tuwajibike kwa pamoja. Tuungane pamoja, tushirikiane katika kuutekeleza Mpango wetu tuliojiwekea wenyewe ili ikifika miaka mitano tukianza kupima Mpango wetu tumetekeliza vipi, kila mmoja anakuwa na majibu yake. Tukianza kuoneshana vidole itakuwa siyo sahihi. Mpango huu unamgusa kila mtu na bahati nzuri umeeleza kwamba, huu Mpango utakwenda mpaka vijijini na utamgusa mtu wa chini kabisa.

Tukitaka kupata maisha bora ni lazima wote tufanye kazi, kuanzia Wabunge, Madiwani, matangazo ya vijiji na watu wotem lazima tusimame tufanye kazi. Tukinyoosheana vidole, itafika mwaka 2015 kila mmoja atamwuliza mwenzake, lakini hakuna mtu atakayetoa jibu. Kwa hiyo, ninaomba nisisitize kwamba ni Mpango wa kila mtu. Lengo kubwa ni kuondokana na umaskini na kunyanya uchumi. Kitu kingine ambacho huwa sikipendelei sana, sisi Waafrika tuna tabia ya kuwasifia wenzetu wa nje,

wale wenzetu wa nje wanafanya kazi kubwa sana; kwa nini na sisi tusijitume tufanye kazi kama wale? (*Makofi*)

Ninaona muda umeshafika, tujitume tufanye kazi kama wao, kila mmoja anajua utandawazi umezagaa kila kona, kwa hiyo, lazima tufanye kazi kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni huu. Ninaomba niunge mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa ninaomba nimwite Mheshimiwa Mariam Kisangi na Mheshimiwa Mustapha Akunaay na Engineer Ramo Makani wajiandae.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Mpango huu wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Kwanza, ninapenda nimpongeze Rais wangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuanda Mpango huu. Pia niwapongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Baraza la Mawaziri, pamoja na Tume ya Mipango na Wadau wote walioshiriki katika kuanda Mpango huu wa miaka mitano. Mpango huu umeandaliwa na Wachumi hasa, kiasi kwamba, sisi ambao siyo Wachumi, tumeweza kupata shida sana katika kuusoma. Tumeweza kutumia tu *summary* ambayo tunailewa. Vinginevyo, huu Mpango umeandaliwa kwa utaalam mkubwa kiuchumi; hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu ni Dira na Maendeleo ya Mtanzania kwa kuangalia vipaumbele vilivyowekwa. Vipaumbele ambavyo vimewekwa ni miundombinu, barabara, bandari, reli, rasilimali watu, kilimo na viwanda. Kama haitoshi, Mpango huu unaibua Programu pale panapoonekana inahitajika. Hili ni jambo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia kwa ufupi sana kwa kuwa mengi yamechangiwa na wenzangu wengi waliopita. Nitaanza na suala la miundombinu. Nimeiona katika Mpango, bandari itaboreshwa, itapanuliwa kiasi cha kufikia kukusanya mizigo au kupokea mizigo tani 9.37 milioni. Kwa kweli hii ni faraja, upanuzi wa bandari utaongeza Pato la Taifa na pia utasaidia sana kukuza uchumi. Pamoja na kupanuliwa kwa bandari na uwanja wa ndege wa kimataifa, nina imani katika Mpango huu, Uwanja wa Ndege wa Kitaifa wa Dar es Salaam ni mionganoni mwa viwanja ambavyo vitafanyiwa upanuzi huo mkubwa na hii itasaidia sana katika kuongeza Pato la Taifa na Uchumi wa Taifa utakua kwa kupitia maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia pia katika eneo la kilimo cha chakula na kilimo cha mazao ya biashara. Mpango umezungumzia kilimo cha matunda, mbogamboga na majani, pamoja na uvuvi na ufugaji. Katika suala la kilimo cha matunda na mbogamboga, nina imani Mpango huu utajielekeza kwa wakulima wa mbogamboga katika Mkoa wa Dar es Salaam, ambao wapo katika maeneo ya Pemba Mnazi, Somangira, Kimbiji, Yombo, Chamazi, Mzinga, Chanika, Mbezi na Mbunju, nao wapewe kasma. Matunda na mbogamboga, yanapatikana mengi katika eneo hilo,

iongezwe nguvu kwa wakulima. Nina imani kuwa, Mpango huu utasaidia sana kukuza Pato la Taifa.

Nizungumzie suala la rasilimali watu. Nimeona Mpango unaelekeza jinsi gani utaweza kuongeza Vyuo vya Elimu ya Ufundu Stadi (*VETA*). Kwanza, ninaipongeza Serikali yangu kwa kuweka Chuo cha *VETA* Dar es Salaam, Chang'ombe. Chuo kile ni mkombozi wa vijana wengi nchini Tanzania. Chuo cha *VETA* Dar er Salaam kinakusanya vijana wengi katika mafunzo mbalimbali, ikiwepo udereva ambaao kila baada ya miezi mitatu, kundi la vijana linahitimu na kupata vyeti vya udereva. Mpango huu kama una nia nzuri ya kuweza kuinua vijana kwa kuwapa elimu ya ufundu, basi nipendekeze au nishauri kwamba, katika eneo hilo tusiwasahau ndugu zetu wale mavu. Kuna maeneo ambayo wale mavu nao wanatakiwa wapate elimu ya ufundu. Ninashauri katika shule ambazo ni *inclusive*, zinahudumia wale mavu na ambaao siyo wale mavu, ikiwemo Shule ya Uhuru Mchanganyiko, Wiles Temeke, Sinza, hizo shule zote ziwekewe Vituo ya *VETA* ili na wenzetu wale mavu waweze kufaidika na mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningomba pia nishauri kuwa, Mpango huu uwaelekeze wanafunzi katika elimu ya kujitegemea. Wanafunzi wengi wamekuwa wakidai posho kwa ajili ya mafunzo yao katika Vyuo Vikuu. Kwa kweli hali ya maisha jinsi inavyoendelea, vijana hawa wataendelea kusumbuka, kwa sababu leo wanapata posho ya shilingi elfu tano haiwatashi, wataongezewa itakuwa shilingi 10,000, lakini mwakani 10,000 nayo itakuwa haitoshi watataka 20,000. Tuangalie Mpango ujikite katika kuwawekea vijana hawa elimu ya kujitegemea. Ninasema hivyo kwa sababu tayari tuna upungufu wa walimu katika Shule za Sekondari za Kata. Hali inayonishangaza, kwa mfano, Wilaya ya Temeke, inacho Chuo cha Dufe; kama wanafunzi wa Dufe wataelimishwa vizuri na kupewa vipindi katika Shule za Sekondari zilizopo katika Wilaya yao na baadhi yao wakalipwa posho kidogo, wangeweza kutumia nguvu zao wenye wakichanganya na ile 5,000 ambayo watapewa kule kwenye mkopo au 10,000, basi watu hao wataishi maisha mazuri na wataipenda Serikali yao na nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye afya. Kuna upungufu Madaktari na Manesi katika Hospitali zetu Kuu; Muhimbili, Temeke, Mwananyamala na nyingine nyingi zilizopo katika Tanzania yetu. Tunao Madaktari vyuoni na wanawajibika vizuri sana kwenye mazoezi yao ya vitendo. Sasa kwa nini huu Mpango usiangalie jinsi gani hawa vijana wataongeza kipato chao kwa kujitegemea wenye wakafanye kazi katika hospitali nyingine wapate kipato cha ziada nao waongeze kipato chao badala ya kutegemea tu madeni au mikopo inayokuja?

Ninasema hivyo kwa sababu hii mikopo ambayo vijana wetu wanaidai, itakapokuja kukatwa itawaathiri, wakati huo wako kazini na mishahara nayo wataona haiwatashi; ni vyema Mpango ikajitika katika kuwasaidia vijana, kuwaelimisha juu ya elimu ya kujitegemea kwani ni muhimu katika maisha ya binadamu. Mpango huu ili utekelezeke, lazima watu wafanye kazi katika kuongeza Pato la Taifa. Tufanye kazi, ipo tabia kwenye baadhi ya familia au kaya, kuacha mtu mmoja tu akifanya kazi na wengine wakibaki nyumbani, hayo ndiyo yanayoangusha Pato la Taifa. Mimi ninaomba shime akina mama wenzangu na akina baba, tushirikiane sote kwa pamoja katika kufanya kazi.

Kazi ndiyo itakayoinua Pato la Taifa, siyo kulala, wala kucheza bao au kucheza tu michezo mingine ambayo haizalishi kipato; hizo ni burdani tutazifanya baada ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijikite katika eneo la viwanda. Nimeona Mpango umeelezea vizuri kuhusu kufufuliwa kwa viwanda. Viwanda vingi vitafufuliwa na vijana wengi watapata ajira. Nina imani katika kipindi cha miaka mitano, viwanda vingi ambavyo vipo Mkao wa Dar es Salaam vitafunguliwa. Ukiangalia Barabara ya Mandela yote ina viwanda; *Nyerere Road* ina viwanda; Ubungo ina viwanda; sasa wasiwasi ambao unanipata ni kuhusiana na umeme. Kwa kweli umeme ni tatizo. Tunakiri ni tatizo. Nimeona Mpango unaelekeza kwamba, katika kipindi cha miaka mitano, tunaweza tukapata kama *megawatts* 2,780. Katika maeneo ya umeme, mkakati huu na kuambiwa kwamba umeme utauzwa mpaka nje, ninaona bado. Dar es Salaam peke yake, kwa mtazamo wa karibu, inaweza ikatumia hata *megawatts* 1,000. Sasa kama ni *megawatts* hizi 2,780; je, wenzetu Mikoa mingine watapata nini? Uwekwe Mkakati Maalum kwa Mkao wa Dar es Salaam kuwekewa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninapenda nilizungumzie ni ushirikishwaji katika miradi. Miradi ni lazima iwashirikishe wananchi. Imefika sehemu wananchi wanashindwa kutambua ni miradi gani inawekezwa katika eneo lao. Hii inaleta matatizo na watu kutolewana. Ninasema hivyo kwa mifano, tayari Mkao wa Dar es Salaam tumezungukwa na miradi ya umeme. Juzi kuna wawekezaji wa *SYMBION*, kuna gesi, kuna mambo mengi, lakini bado hatuelewi wananchi wa Dar es Salaam kwamba: Je, wameshirikishwa vipi katika mipango hii? Tufike sehemu Serikali nayo ipate wasaidizi ambao ni wananchi. Wananchi wenyewe waisemee. Wakiwezesha na wakishirikishwa vizuri katika miradi yao, basi hata Serikali itatupunguzia kazi. Sisi wenyewe wananchi ndio tutakuwa tunaoweza kujibu pale ambapo mtu atatugusa kuhusiana na suala hili. Basi na sisi tutakuwa wepesi wa kutoa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kengele ya kwanza imeshagonga, naomba niangalie changamoto ambazo nimeziona katika Mpango. Katika Mpango sikuona uboreshaji katika Sekta ya Michezo na Utamaduni. Michezo inasaidia kuongeza ajira kwa vijana na watu wazima pia.

Tunazo timu zetu za mpira wa miguu *Taifa Stars*, *Young African*, *Simba*, Vijana wa Chini ya Umri wa Miaka 15, timu za *football* za wanawake, *Net ball*; hizo sikuona mkakati wake katika Mpango huu wakati michezo inasaidia kuingiza mapato makubwa sana. Kama tutawapangia mipango mizuri, basi tutakuwa tumekwenda vizuri na itasaidia sana kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa mwenyekiti, pia katika Sekta ya Utamaduni, katika mpango sikuona ni jinsi gani utaendeleza utamaduni wetu, kwa sababu tayari tunao vijana wetu kama *Ze Comedi*, *Five Stars*, Twanga Pepeta, *TMK Wanaume*, Mwasiti, akina *Lady JD*, wengi sana, hawa wanapenda kwenda nchi za wenzetu na wao wakaonyeshe. Vinginevyo tutafanya kazi ya kuwapokea Makhirkiri, tutawapokea sijui nani hawa ambao wanatoka huko wanakuja hapa wanaingiza pesa, wanaondoka na sisi vijana wetu kwa kuwa hawana

uwezo wakiwemo akina Vicky Kamata na miziki yao, hawana uwezo wa kujipeleka wenyewe nje na kwenda kutangaza biashara hizo. Basi tuwawekee mikakati hizi bendi zetu, *OTTU, TMK*, akina Sikinde, akina Msondo, tuwawekee mpango na burudani ni sehemu ya maisha bora. Mwanandamu kisaikolojia ili aweze kuishi vizuri ni lazima apate burudani. Hiyo ni lazima katika maisha ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuangalia eneo la maliasili na utalii. Katika vipaumbele hivi, sikuona eneo ambalo lina-*promote* utalii wetu wa ndani na nje. Tujitahidi katika ku-*promote* utalii wetu wa ndani na wa nje ili tuweze kuongeza pesa za kigeni na kuongeza pato la Taifa na kukuza uchumi wa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi baada ya kusema hayo, naunga mkono Mpango huu kwa asilimia mia moja. Hoja hii ya Mpango wa miaka mitano una nia njema na Taifa letu, lakini watekelezaji ni sisi Waheshimiwa Wabunge na wananchi wetu kwa pamoja. Wananchi wote tuupokee Mpango huu kwa kufanya kazi kwa bidii ili tuweze kufikia malengo hayo. Bila kufanya kazi na bila kutoa tafsiri, mpango huu haufikiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante. Muda ukiisha, hata kama hujamaliza neno, unakaa. Kwa hiyo, ninakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Mustapha Akunaay na niseme Eng. Ramo Makani, ajiandae. Kwa *time* niliyonayo, Mheshimiwa Regia Mtema, pia atafuata.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia mpango wote na kumsikiliza Waziri wa Ofisi ya Rais anayeshughulikia suala hili, nimeona kwanza kulikuwa na tatizo kubwa kwa kutokuwa na mpango maalum katika kupanga mipango ya nchi hii. Kwanza naisifu Serikali kwa kuweza kupanga mipango ya bajeti kwa kipindi chote ambacho hapakuwa na mpango maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu watu wengi wamezungumza maeneo makuu katika vipaumbele vilivyowekwa, mimi nitazungumzia maeneo makuu matatu, nikianza na viwanda. Kauli yetu hapa nchini sasa hivi ni Kilimo Kwanza, badala ya Viwanda Kwanza. Maana yake ni kwamba kilimo tunachofanya sasa hivi ambacho kumbukumbu inaonyesha, asilimia 72 mpaka asilimia 75 ni ukulima wa kuwezesha wananchi waweze kuishi, sio kilimo ambacho kinaleta *surplus*, yaani bakia ya kuweza kusafirisha nje au kuweza kubadilisha mazao hayo kuwa vitu vyatoka viwandani. Sasa hivi Tanzania ni mojawapo ya nchi ambazo zinaunda Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Katika Jumuiya hiyo, kitu kikuu ni sehemu gani nchi imeendelea kiviwanda. Bila kuwa na viwanda ambavyo vitakuwa vinazalisha, nchi itabaki kuwa mlaji wa bidhaa zinazotengenezwa katika nchi nyingine.

Mheshimiwa mwenyekiti, kwa hiyo, katika mpango huu, nimefurahia kuona viwanda vimewekwa. Kwa hiyo, ningesisitiza kwamba viwanda hivyo basi, vitakapokuwa vinawekewa pesa, viwe vinalinganishwa na viwanda vyatoka nchi nyingine kwamba, tunazalisha nini na wenzetu wanazalisha nini, ili tupate nafasi katika

kushindania soko. Historia yetu inaonyesha kwamba wakati wa uongozi wa Mwalimu Nyerere, tulikuwa na viwanda vingi na viwanda hivyo vilijengwa kwa misingi ya kuzingatia kwamba katika miji yetu ni mazao gani yanazalishwa. Kwa hiyo, ni jambo la busara kufufua viwanda hivyo. Kama viwanda hivyo vikifufuliwa, basi la kufuata ni miundombinu imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nahamia kwenye eneo la miundombinu. Ni kilio cha Watanzania wengi kuhusu reli. Reli ni njia moja ambayo ni nzuri kwa kusafirisha mizigo mizito. Kukosekana reli hapa nchini kati ya Dar es Salaam – Kigoma, Dar es Salaam – Mwanza, Tanga – Arusha, ndio imesababisha barabara zetu ziharibike kwa kasi na tunawekeza pesa nyingi. Nimeona katika bajeti ya mwaka huu kwamba, miundombinu ya barabara inachukua kitu kama trilioni 1.5, lakini kama sio waangalifu itakuwa barabara zinajengwa leo na baada ya muda mfupi zimeharibika. Kwa hiyo, ili kuweza kusafirisha mazao hayo ambayo yatatokana na kilimo kwanza, basi kuwe na usafiri wa kuaminika wa kusafirisha mazao hayo kwenda kwenye viwanda ambavyo vitakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miundombinu, jambo lingine ni kuhusu usafiri wa anga. Nchi hii ina matatizo makubwa ya usafiri wa anga kwa kusafirisha mazao ya maua kwenda kwenye soko la dunia kwa kutegemea ndege ya aina moja ya *KLM*, na ndege hiyo inaamua kupanga bei yenewe kwa sababu ya *monopoly*. Iwapo tumeamua kuwekeza katika maua ambayo imeonekana kwamba ni sehemu mojawapo katika biashara ya nje inayoleta fedha za kigeni pamoja na utalii, basi Serikali sasa itazame katika Mpango huu jinsi ya kuwezesha nchi hii iwe na usafiri wa anga wa kuaminika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wetu unategemea ndege kutoka nje. Kwa hiyo, katika hili, Mpango utazame upanuaji wa uwanja wa ndege wa *KIA*, kama ilivyozungumzwa leo asubuhi hapa Bungeni kwamba una matatizo. Basi ukitazamwa katika Mpango huu, ukiwezeshwa basi utasaidia kuinua utalii ambao sasa hivi ni sekta ya kwanza kuleta pesa za kigeni. Lakini yote hayo yanaweza yakafanyika, pesa zitapatikana iwapo misingi mikuu ya utawala bora itafuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii sasa hivi ina matatizo makubwa kwa kukosekana kwa utawala bora. Watu wengi wanashinda Polisi, Mahakamani, wakiacha mazao kwa sababu kesi zao zinachelewa. Mahakama hazipo, hakuna Mahakimu, wasafirishaji wa malori, magari yao yanacheleweshwa njiani, mapolisi wakiwasimamisha, huchukua masaa mengi, kwa hiyo, misingi ya utawala bora ambao tunauhitaji ni ule ambao utasaidia wananchi kupata haki zao kama Katiba itakavyokuwa imeeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia kitabu kizima hiki, sijaona kama kuna eneo lolote limezungumzia juu ya Katiba. Ina maana basi uandishi mpya wa Katiba haujapangiwa mpango na utakuwa hauna bajeti. Sasa dawa au dira ya utawala bora itakuwa ni Katiba ambayo imewekwa imara, kwa sababu kila raia haki yake itakuwa imeelezwa kama ilivyozungumziwa hapa. Kwa mfano ardhi ikielezwa kwenye Katiba umiliki wake na mipaka yake basi hapatakuwa na matatizo ya kuvamia ardhi na kuchomeana mazao katika mahali ambapo wawekezaji wameweka. Utawala bora ni eneo

pana sana. Maana yake ni kutii sheria, ni uongozi, Serikali inavyowaangalia wananchi na pia wananchi wanavyotii sheria inayotungwa na Bunge lao ambalo wao wamelichagua kutokana na sheria ambazo zimekuwa zimewekwa na wananchi ambayo inawaelekeza katika maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango, kitu kikubwa ni kukuza uchumi. Sasa hivi taarifa tulizonazo ni kwamba uchumi unakuwa lakini umasikini haupungui! Sasa tukiwa na viwanda, tukitengeneza miundombinu, kilimo kikaendelezwa, rasilimali ikaendelezwa, iwapo utawala bora haujawekwa inavyostahili, itakuwa tunarudi nyuma na maendeleo hayataendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la viwanda sasa hivi, sisi katika Afrika ya Mashariki, sehemu yetu ya biashara ni ndogo sana, ni asilimia 28 na Kenya ni asilimia 44. Sasa tukiwekeza zaidi katika viwanda, tutaongeza na pato letu ambalo tunategemea katika Mpango huu kwamba mwisho wa Mpango huu itafika dola 3000 kwa mwaka. Nazungumzia *per capita income*, tutaiweza. Lakini hitoria inaonesha kwamba huko nyuma tulikuwa na mipango, lakini kutokana na matokeo mbalimbali ikiwepo kupanda kwa mafuta, vita mbalimbali, mabadiliko ya hali ya hewa, mipango hiyo ilikwama. Sasa katika Mpango huu sijaona mahali kwamba yaktokea mambo kama haya, Serikali itafanya nini ili tusikwame tena kama tuliviyokwama kuanzia mpango wa tatu wa kuanzia mwaka 1975.

Mheshimiwa mwenyekiti, kengele ya mwisho kabisa imelia. Nazungumzia juu ya uwajibikaji. Mpango Miji mizuri imetengenezwa, lakini kwa kukosekana uwajibikaji, Mpango hiyo imekwamishwa. Kwa hiyo, hili eneo la uwajibikaji litazamwe vizuri, ingawaje hata hivyo inaingiliana na ule wa utawala bora, lakini kwa sasa hivi uwajibikaji katika nchi hii umekuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. (*Makofi*)

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Lakini kwa kuwa ninasimama kwa mara ya kwanza Bungeni kutoa mchango kama hivi, nichukue nafasi pia ya kuwashukuru wapiga kura wote wa Jimbo la Tunduru Kaskazini na kwamba kutokana na imani ambayo wameionesha kwangu, basi napenda kuwadhihirishia kwa mara nyingine tena baada ya kuwa nimeshafanya hivyo hapo nyuma kwamba sitawaangusha na watarajie mabadiliko makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda niipongeze Serikali kwa kuja na Mpango huu. Mpango ambao tumeshasema mara nyingi kwamba hii ni *extract* au umetolewa kutoka kwenye dira ya mwaka 2025 na kwa hiyo, sasa tumesogeza karibu zaidi ile *vision* yetu kwa kujipatia nafasi ya kuingalia dira kwa ukaribu zaidi kwa vipindi vyta miaka mitano mitano. Huu ndiyo Mpango wetu wa kwanza wa miaka mitano kwa ile miaka 15 iliyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza pia Serikali kwa kupitia Wizara inayohusika, lakini pia kupitia *POPC* ambayo ni Tume ya Mipango yenyewe kwa kuonesha mfano kwenye nchi hii, kwenye Taifa hili kwamba, kumbe sasa tunatakiwa tuondokane na dhana potofu ya kwamba wanaoweza kufanya mambo vizuri ni watu kutoka nje na kwamba hatuna wataalamu. Mpango huu wote kikamilifu umeandaliwa na watalaamu kutoka Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeusoma Mpango huu kwa vina na vituo, hivyo nataka niseme kwa maneno ya jumla kabisa kwa kuanzia kwamba, Mpango huu ukitekelezwa barabara tutaweza kudhibiti mfumko wa bei, tutaweza kudhibiti kasi ya kushuka kwa thamani ya sarafu yetu (Shilingi ya Tanzania), tutaongeza kwa kasi kubwa na kwa kiwango kikubwa ajira kwa makundi yote ya jamii wakiwemo vijana, akina mama wote walioko vijiji pamoja na mijini. Pia tutaliwezesha Taifa kuongeza soko la ajira, lakini pia kuweza kupambana na changamoto mbalimbali za utandawazi. Tutaweza kulisadia Taifa kuongeza uwezo wa kupokea, nikiwa na maana ya ku-*absorb* vijana wanaomaliza shule katika ngazi za Shule za Msingi pamoja na Sekondari na kwa hiyo, kuanza ku-*address* tatizo kubwa la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niondoe mashaka machache yaliyojitokeza wakati wa mjadala. Kwa jinsi nilivyousoma Mpango huu, kuna suala la kipindi cha mpito cha mwaka mmoja ambacho kimetia mashaka baadhi ya wachangiaji kwamba kwa kuwa kinaangukia ndani ya kipindi chenyewe cha miaka mitano, basi wanahisi kwamba kunaweza kuwa na mashaka kwenye utekelezaji wa Mpango yenyewe. Lakini ninataka nisisitize hapa kwamba suala hili lina uwezekano kabisa wa kuzingatiwa ndani ya Mpango chini ya taaluma yenyewe inayohusiana na mambo ya Mipango na miradi. Maana kabla hujazungumzia mradi unazungumzia Sera, ambapo Sera inazua Mipango, Mipango inazua miradi, miradi inazua shughuli mbalimbali ambazo kwa pamoja zinaunda mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiongeza jambo la kufanya kwenye Mpango, unachotakiwa kufanya ni wanasema unafanya *crushing*, unaongeza *speed* na kwa hiyo, unaongeza *resources*. Bado unaweza katika kipindi kile kile ambacho umekusudia ukatekeleza makusudio yako, kwa hiyo, hakuna mashaka kwamba kuna mipango imetangulia huko nyuma na haikufanikiwa.

Mimi nadhani ni lazima tuwe wakweli, ni mahali gani ambapo mtu anaweza kuweka Mpango mahali popote duniani au nchi yoyote duniani, akaweza kuandaa Mpango halafu akaweza kuutekeleza na kufanikiwa kwa asilimia mia moja? Ukipanga Mpango ukautekeleza, ukafanikiwa kwa kiwango fulani cha asilimia na ukashindwa kwa asilimia fulani, jambo unalotakiwa kufanya ni kuangalia maeneo yapi yamesababisha ukashindwa kwenye maeneo uliyoshindwa halafu ukajipanga sawasawa ili uweze kufanya vizuri zaidi katika mpango ujao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitembea kwenye njia yenye visiki na mawe ukasema unakusudia usijikwae, lakini bahati mbaya ikitokea kwamba umejikwaa, hukatishi safari, unajikwaa, unanyanyuka, unaendelea na safari. Hata kama ikitokea umedondoka chini

kabisa ukaanguka, hulali hapo moja kwa moja, utanyanyuka, utaendelea na safari. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya Tanzania kupitia Mpango huu, imeainisha namna ambavyo tunaweza kupata vyanzo vya mapato vya kutekeleza mradi huu. Katika hili nataka kuondoa mashaka kwamba bajeti ni ndogo, Serikali haijawekeza vya kutosha kwenye Mpango huu. Lakini nataka niwashauri wenzangu wengine wanaosoma Mpango labda wanakuwa hawajapitia ukurasa wa 95 mpaka 172 mahali ambako vyanzo mbalimbali vya kuweza kugharamia mradi huu vimeonyeshwa. Licha ya Serikali yenyewe, lakini pia *private sector* ni mshiriki, lakini pia *PPP* ni mshiriki na wale *development partners* au *DPs* nazo pia zipo. Lakini nataka nisitisize kwamba utaratibu huu hautumiki tu katika nchi yetu, lakini pia nchi nyingi tu zinatumia utaratibu huu wa kushirikisha vyanzo vingine ili kuweza kutekeleza miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi ya hapo nataka nisema tu kwamba hata hivyo vyanzo vingine ambavyo vinatokana na misaada na michango na mikopo haikutokea kwa bahati mbaya imetokana na sifa ya Tanzania. Nchi nyingi duniani zinakosa hiyo fursa kwa sababu ya kukosa sifa ambazo Tanzania inazo. *Strength* zetu au uwezo wetu wa kuweza kuwa na sifa za namna hiyo unatokana na ukweli wa kwamba kwanza tunaaminika, mtu akikukopesha maana yake amekuamini. Kwenye lugha ya Kiingereza wanasema *you are bankable*. (*Makofî*)

Utawala bora tunaouzungumza kwa maneno tu peke yake ambao kwa Kiingereza tungesema kwamba nchi hii ni *governable*, pia unafanya urahisi wa kuweza kuvutia watu wengine kuja kuwekeza. Lakini pia nchi hii kutokana na usalama, amani na utulivu uliopo, yaani *the country is liveable* na yenyewe pia ni sifa ya kutuwezesha kupata misaada hiyo tunayopata. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini yapo maeneo katika Mpango ambayo nakusudia niyaainishe ili yaweze kusaidia katika kuboresha Mpango huu kabla ya utekelezaji wake. Ukurasa wa 52 baada ya kuzungumzia vipaumbele vikuu kwenye miundombinu, umeme ukiwa umetajwa kuwa wa kwanza, sehemu kubwa iliyozungumziwa unahusiana na masuala ya uzalishaji wa umeme au *generation*, lakini pia inazungumzia suala la usafirishaji wa umeme huo (*transmission*), lakini pia ugawaji kwenye maeneo ya mahitaji (*distribution* au *supply*). Bahati mbaya Mpango umeacha kugusa eneo la *consumption*, yaani matumizi yenyewe ndani ya nyumba, ndani ya viwanda na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa nilizonazo upotevu (losses) wa umeme katika nyanja mbalimbali, hatua zote tatu nilizozisema zinachangia kwa kiasi kikubwa upungufu wa kiwango cha umeme tunachokuwanacho kwenye *grid*. Kwa hiyo, hata ukitajiwa takwimu, unakuta kwamba hata kuanzisha *plant* nyingine itakayokupa *megawatt* labda 250 hiyo inafanana na kiwango cha umeme ambao unapotea. Chukua mfano tu wa bomba la maji unaokusudia kupeleka maji mahali, likawa limetoboka halafu kwa nguvu kubwa maji hayo yanapotea, kwa hiyo, nafikiri ni vyema tukapitia pale na kuweza kuangalia namna gani tunaweza tukaziba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele imelia, lakini nimalizie kwa kusema kwamba naipongeza Serikali. Lakini pia kwa kupitia Kamati inayohusika, yaani Kamati ya Fedha na Uchumi, tunatakiwa tuangalie uwiano wa maeneo katika maeneo mbalimbali ya nchi kwenye kutekeleza miradi ya maendeleo au mipango kama hii, na hasa umuhimu wa kuangalia maeneo ambayo tunaweza tukayaita ni *disadvantaged*. Naomba wakati wa kutekeleza Mpango huu na pengine wakati wa kufanya marekebisho kwa sababu niliposema kwamba naunga mkono Mpango huu, nilisema hivi ulivyo lakini baada ya kuzingatia michango mbalimbali iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika kuuboresha, kwa hiyo, utakapokuwa umekamilika baada ya maboresho, wakati wa utekelezaji, ukizingatie dhana ya kuelekea mahali ambako kumebaki nyuma kimaendeleo, yaani ukanda wa Kusini kule Mtwara *Corridor* ni sehemu mojawapo na hasa pale Tunduru. (*Makofî*)

Ukiangalia *grid* ya umeme, inaishia Songea haifiki Tunduru. Ukianzia upande wa pili kutokea Mtwara inaishia Masasi, Tunduru imebaki kama kisiwa. Kwa hiyo, kwa upande wa umeme tulitizame hilo. Lakini naishukuru Serikali, naipongeza kwa upande wa barabara kwa sababu hivi ninavyozungumza ukichanganya na miradi ambayo inaendelea, kinabaki kipande kimoja tu cha barabara ambacho kitakuwa hakijakamilika na chenyewe ni kati ya Mangaka na Tunduru. Lakini Songea - Namtumbo kiwango cha lami mkandarasi yupo *site*, na Namtumbo - Tunduru mkandarasi yuko *site*. Kwa hiyo, kipande kilichobaki cha Tunduru kwenda Mangaka ambacho kwa taarifa zilizopo, lakini nafikiri tutajadili zaidi wakati wa bajeti iko kwenye utaratibu au kwenye hatua ya upembusi yakinifu na *design* zile za mwanzo. Hapa tutapenda kusisitiza juu ya kuongeza kasi na kufanya kazi hiyo ikamilike katika muda ambao ni muafaka ili na penyewe paweze kukamilika na Mtwara *Corridor* iwe Mtwara *Corridor* kweli kweli mtu aweze kutoka kwa baiskeli au bajaji kama tunavyosema mahali pengine na iwezekane hivyo kutoka Mtwara kwenda mpaka Mbambabay.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda nieleze suala la utekelezaji na kwamba ni kweli watekelezaji wako wengi kuanzia mtu binafsi, ngazi ya familia, Kata, Halmashauri, Mkoa mpaka Taifa. Lakini nataka nisisitize zaidi kwenye ngazi ya Halmashauri, niseme kwamba Watendaji kwenye ngazi ya Halmashauri wanatakiwa kwa kweli wapokee fedha za utekelezaji wa miradi hii wakiwa wanatambua kabisa kwamba wao ndiyo watakaowezesha Mpango huu kufanikiwa ama la. Lakini siyo hivyo tu, suala la wataalam litiliwe mkazo, kwa sababu Halmashauri nyingi zinapokea fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika maeneo ambayo hawana wataalam.

Katika hili, pengine niiase Serikali tu kwamba ufile wakati sasa hivi tuseme kwamba kabla hatujapeleka fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi fulani kwenye Halmashauri fulani tujiridhishe kwanza kama wana wataalam wa kutosha kuweza kutekeleza huo mradi, vinginevyo, tupeleke kwenye maeneo ambayo yana wataalam huku yale maeneo ambayo hayana wataalam wa kutosha kutekeleza miradi hiyo yakisubiri mpaka yatakapokuwa na wataalam halafu tuwawezeshe. *World Bank* walifanya hivyo mwaka 2007 na mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda umekeisha naunga mkono hoja.
(*Makofî*)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Regia Mtema na Mheshimiwa January Makamba ajiandae.

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kuhusiana na huu Mpango ulioko mbele yetu. Mimi ninazo hoja chache tu ambazo ningependa waandaaji na wahusika wa Mpango huu wazizingatie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni suala zima la jina lenyewe la Mpango, kwamba Mpango wetu ni wa mwaka 2011/2012 mpaka 2015/2016.

Nilikuwa naomba ufanuzi kwa sababu sielewi. Kwa kifupi, mimi sielewi. Ninatambua kwamba mwaka huu ni mpito, sasa ninahitaji kufafanuliwa ili nijiridhishe. Naomba mtoho hoja baadaye atutafsirie hili ili niweze kuelewa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala zima la watu wenyewe ulemavu. Mpango wenyewe, ukisoma ukurasa wa kwanza mpaka wa 175, watu wenyewe ulemavu hatuj-appear mahali popote. Natambua kabisa kwamba kupanga ni kuchagua, na kupanga vipaumbele siyo jambo rahisi, ni lazima *tu-sacrifice* makundi mengine. (*Makofî*)

Lakini kuna vigezo vya kuweza kupata vipaumbele. Kigezo mojawapo, ni lazima uangalie *minority* kwenye jamii. Jamii ya watu wenyewe ulemavu Tanzania, sisi ni *minority*, lakini Mpango huu umetusahau kabisa. Ingawa kwenye hotuba ya mtoho hoja amejitahidi kutaja watu wenyewe ulemavu na ninaamini ameweka kwa makusudi kama mkakati tu wa kisiasa na ndiyo maana hata hakutamka vizuri, ametuita watu wenyewe mahitaji maalum. Watu wenyewe mahitaji maalum ni *general term*, watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI ni watu wenyewe mahitaji maalum, watu wanaoishi na Kisukari ni watu wenyewe mahitaji maalum, watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu na wenyewe ni watu wenyewe mahitaji maalum. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wenyewe ulemavu tuna jina letu, tunaitwa watu wenyewe ulemavu au jamii ya watu wenyewe ulemavu. Hata takwimu sahihi, mtoho hoja hana, ndiyo maana amesema kwamba Tanzania kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani, wanatumia ile asilimia 10 ya idadi ya watu. Hii takwimu ni ya miaka 30 iliyopita, WHO walikuwa wanakadiria tu, lakini hivi sasa Tanzania tuna Bodi yetu ya *statistics*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Leticia ukiangalia, hapo uko kati ya wanaoongea na mimi. Kwa hiyo, ultakiwa ukae upande mwengine.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani.

MWENYEKITI: Haya ahsante.

MHE. REGIA E. MTEMA: Tanzania tunayo Bodi yetu ya takwimu, hivyo basi, naomba Mpango huu mzuri uingize masuala haya ya watu wenye ulemavu, lakini napendekeza mambo ya muhimu ambayo yanapaswa kufanya kuhusiana na jamii ya watu wenye ulemavu.

La kwanza ni hili la *statistics*, zinatofautiana. Siku Waziri wa Afya akija kutoa hotuba ya afya hapa, atatuletea takwimu tofauti, mtoha hoja wa hoja hii naye ana takwimu zake. Kwa hiyo, ninaomba Mpango huu kwa miaka mitano inayokuja, basi ikajikite kwenda kufanya utafiti wa kujua idadi halisi ya watu wenye ulemavu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile Mpango huu uende kufanya utafiti ya kufahamu ni wenye ulemavu wangapi ambao ni masikini wanaishi Tanzania. Vilevile ikafanye utafiti wa kupata takwimu za kufahamu ni wenye ulemavu wangapi waliopata elimu katika ngazi zote iwe Darasa la Saba, Sekondari, elimu ya juu na hata Elimu ya Ufundji. Vilevile Mpango huu ukafanye utafiti wa kujua ni wenye ulemavu wangapi wako kwenye soko la ajira na wangapi hawako kwenye soko la ajira. Tukishapata takwimu hizi itakuwa rahisi pia kutusaidia hata kwenye mambo mengine ya muhimu sisi jamii ya wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni suala zima la ardhi. Takwimu zinaonyesha kwamba Tanzania ni nchi ya 31 kwa ukubwa duniani. Tuna takribani kilometra za mraba 956,000, lakini bado Tanzania tunatisha kwa migogoro ya ardhi. Lakini vilevile takwimu hizo hizo zinaonyesha kwamba Tanzania tuna hekta milioni 44 zinazofaa kwa kilimo na tunatambua kabisa kwamba asilimia 73 ya Watanzania wanaishi vijijini na wengi wao wanategemea kilimo. Takwimu hizo zinatuambia kwamb asilimia 24 tu ya hekta hizo ambazo zinafa kwa kilimo ndiyo zinazotumika mpaka sasa. Lakini nimejaribu kuitia Mpango huu ambao unajadili masuala ya ardhi, ukisoma kuanzia ukurasa wa 119 mpaka 121 haujaeleza ni kwa namna gani utahakikisha kwamba tunaweza ku-utilize land ambayo haijatumika kwa kilimo. Angalau basi mpaka Mpango huu utakapokwisha tuwe tumefikia asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba Mpango huu ueleze wazi kwamba angalau tutahakikisha asilimia 26 ya *land* yetu inayofaa kwa kilimo iwe imetumika ili tufikie asilimia 50 mpaka mwaka 2016 Mpango huu utakapokuwa umekamilika. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumeondoa migogoro ya ardhi. Vilevile tutakuwa tumepanua kilimo kwa Watanzania na uchumi, hatimaye utakuwa umekua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala zima la mradi wa barabara. Ukisoma kwenye huu Mpango wenyewe ukurasa wa 127 zimetajwa, kuna *road corridors* ya 29 mpaka 36 hazijaweka *length* wala hakuna sehemu ambako wanasema ni kilometra ngapi zitakuwa *constructed au rehabilitated* na ninafahamu kabisa Wizara ya Mheshimiwa Magufuli wao ni wataalam wa kujua takwimu. Sasa nashindwa maana imekuwa *blank*, kuko kweupe, hazijatajwa hizi barabara zina ukubwa gani na ukubwa gani utatengenezwa. Sasa napata wasiwasi: Je, ni kwamba *feasibility study* haijafanyika ya kufahamu barabara hizi zina ukubwa gani au ni *omission* ya bahati mbaya ilifanyika ikasahaaulika kuweka haya?

Lakini mimi ni mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, tumepitisha bajeti ya Wizara ya Ujenzi, wametaja wanafahamu urefu wa barabara hizi, kwa hiyo, naomba wahusika walifuatilie kwa karibu ili liingizwe kwa sababu ni lazima ziwekwe wazi ili nasi tunaotoka kwenye maeneo hayo tujiridhishe kwamba ni kweli mkakati huu utakwenda kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la mradi wa gesi ya asili ambayo inapatikana ukurasa wa 137 wa Mpango wenyewe. Mpango ni mzuri kwamba tunatarajia kuwa *project* ya gesi ya asili ambayo itafanyika kule Dar es Salaam na Mpango wenyewe unatarajia kwamba utaweka *pipe line* za kusambaza gesi kutoka maeneo ya Ubungo mpaka Mikocheni, lakini kwa bahati mbaya mradi huu umetaja nyumba 57 peke yake ndizo ambazo zitakuwa *connected* na gesi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba 57 kwa jiji la Dar es Salaam kwa maeneo ya Mikocheni ni nyumba chache sana na hii *project* ni ya miaka mitano. Labda kama mradi ungesema hizi nyumba 57 ni kwa mwaka mmoja peke yake, kidogo ningelewa. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza basi angalau asilimia 25 ya nyumba za maeneo hayo ziweze kuwa *connected* na gesi hii ili mradi huu uweze kufanikiwa kuliko kuweka nyumba 57 peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa ya kuzungumza. Nianze kwa kutamka moja kwa moja kwamba naunga mkono hoja iliyotolewa na nampongeza Rais wangu kwa *commitment* yake kwa maendeleo na ustawi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze na jambo moja tu la namna tunavyotumia raslimali za umma, kwa sababu namna tunavyopanga na kutumia raslimali za umma, nidhamu katika matumizi ya raslimali hizo ni muhimu sana kwa mafanikio ya Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niende kwenye Mpango wenyewe kwenye hiki kitabu kikubwa ukurasa wa 17 na kwa ruhusa yako naomba nisome paragraph ya kwanza inasema, imeandikwa kwa Kiingereza: “*consolidation the most of the fringe benefit such as housing, transport and allowances into to salaries and wages will be one of the ways of creating an appropriate incentive structure. Sitting and travelling allowances currently create a pervasive, incentive structure and will need to be rationalized or removed.*” Naomba nisome sentensi ya mwisho tena: “*sitting and travelling allowances currently create a pervasive, incentive structure and will need to be rationalized or removed.*” (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hili jambo limezungumzwa sana katika wiki iliyopita na...

MWENYEKITI: Unatakiwa utafsiri sasa.

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA: Kumbe linatoka kwenye Mpango wa Serikali na tafsiri yake ni kwamba Serikali imedhamiria kwenye Mpango wake kwamba hizi posho za vikao na usafiri haziweki mfumo mzuri wa maslahi ya watumishi wa umma, kwa maana hiyo imeona kwamba, aidha, zihuishwe au ziondolewe. Huo ndiyo msimamo wa Serikali. Kwa hiyo, hata kesho mkiusikia unazungumzwa hapa kwa mbwembwe mjue umetoka kwenye Mpango wa Serikali. Hilo la kwanza ambalo nataka kulizungumza ili tuweke *record* sahihi kwamba hili jambo limetoka wapi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nataka nizungumzie suala la nishati ya umeme. Hili bado ni tatizo kubwa na mimi nimesoma huu Mpango na nimefurahishwa na *ambition* ya Serikali ya kuzalisha *megawatt* 2,780 kwa miaka mitano ijayo. Lakini nataka tuwe *realistic* kwa wananchi ili tusitoe matumaini ambayo hatuwezi kuyafikia na wakati tumeweka hii *target*, tukumbuke kwamba katika miaka mitano iliyopita tumepata *megawatt* 145 tu za kwetu. Sasa miradi hii imeorodheshwa na mimi naamini inawezekana kufanyika, lakini ningependa zaidi kuona kila mwaka itakuwa ipi inayoingia kwenye gridi, yaani Mpango uelezee kwamba mwaka ujao ni kiasi hiki na mwaka unaofuatia ni kiasi hiki na kadhalika ili zisiwekwe jumla tu mwaka 2015 ili tuje *progress* kwa kadri tunavyokwenda, kwa sababu suala la umeme kwa kweli ahadi zimekuwa nyingi na mimi ni mwana CCM na Serikali yangu ni ya CCM, lakini ni lazima niseme pale ambapo nadhani tunakuwa na mapungufu.

Kwa hiyo, tuhakikishe kwamba hili tunalitimiza na namna moja ya kufanya hivyo ni kubadilisha tu utamaduni wetu wa kufanya kazi kwa sababu kama itakuwa ni yale yale, basi baada ya miaka mitano matokeo yatakuwa ni yale yale. Tusije tukafikia hiyo miaka mitano tukaanza kusema ah, unajua mwaka ule kulitokea m dororo, mwaka huu kilitokea kile na kadhalika. Ni lazima tu-*deliver megawatt* 2,780 kwa sababu Mpango wote huu bila kupatikana umeme, basi mpango huu ni ndoto. Napenda kwa kweli umeme ungekuwa kitu cha kwanza tukiweke kama kipaumbele kikubwa cha Taifa.

Sasa yapo mambo kadhaa ambayo yanahitajika kufanyika na *of course* Serikali haiwezi kuwekeza kwenye kila *megawatt* na tumeruhusu kuwe na *private sector*, lakini ni lazima tuwekwe mazingira mazuri ya uwekezaji. La kwanza ni *incentives*, yaani inaitwa *tariff structure*. Watu wa *TANESCO* kila siku wanatuambia kwamba: "Sisi kwa kweli hatujidhesi kibiashara kwa sababu bei ya umeme siyo bei ya kibiashara." Ni kweli na Serikali inafahamu hivyo, ndiyo maana Mtwara kuna kampuni ambayo siyo ya Serikali inazalisha umeme, lakini inapata *subsidies* ili iuze umeme kwa bei ambayo ni sawa na ya *TANESCO*. Sasa kama Serikali imeona ni muhimu wale wapate *subsidies* ili wauze umeme bei ambayo ni sawa na ya *TANESCO*, basi tubadilishe utaratibu wa kubadilisha *tariff* ili shirika hili lijiendeshe kibiashara na wawekezaji waje kwa sababu *tariff* siyo tu kwamba inaiumiza *TANESCO* hata uwekezaji kwenye umeme unadumaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni *TANESCO* walitoa *tender* ya kuzalisha umeme *megawatt* 260, yamejitokeza makampuni 18, yamerudisha *tender* matatu na imeshinda kampuni moja na ile moja iliyoshinda *tender* *ime-quote* kwamba *unit* moja Sh.

1,208/= wakati *TANESCO* wanaauza umeme Sh. 157=. Sasa ile Sh. 1,208/= ni gharama halisi ya kuzalisha umeme na faida kidogo. Sasa kama *tariff* yetu hairuhusu uwekezaji, hatutafika popote, maana yake ile kampuni ya Mtwara inazalisha umeme wa gesi na umeme wa gesi ni nafuu, lakini bado tunaipa *subsidies*. Kama ni hivyo, basi tungeipa *subsidies* hata *TANESCO*. Maana yake Kigoma inazalisha umeme kwa gharama kubwa, halafu inakusanya kidogo kwa sababu ya gharama ya kuzalisha umeme.

Kwa hiyo, tuwe *realistic* kama umeme ni huduma, tujue ni huduma moja kwa moja na kama ni biashara, basi tujue ni biashara moja kwa sababu siyo tunaweka *pressure* kwenye Shirika la *TANESCO* lijiendeshe kibiashara, lakini tumeweka utaratibu wa bei ya umeme amba siyo wa kibiashara. Kwa hiyo, hii miradi mafanikio yake yatategemea kwa sababu *assumption* ya huu Mpango ni kwamba umeme ni biashara, lakini hauwezi ku-*assume* kwamba umeme ni biashara wakati mazingira ya sekta yenyewe siyo ya kibiashara.

Sasa miradi imenorodheshwa humu, mingine ni *generation*, lakini kwenye *transmission* na mimi ningependa kweli Serikali iweke kipaumbele kwenye suala la *transmission* kwa sababu umeme uliopotea njiani mwaka jana kutokana na ubovu wa miundombinu ni zaidi ya umeme ulitumika viwandani na sehemu za biashara nchi nzima, yaani *gigawatt hours* 1100. Umeme uliopotea njiani mwaka jana kutokana na ubovu wa njia za usafirishaji ni zaidi ya umeme, ultumika viwandani na sehemu za biashara, nchi nzima kwa mwaka mzima, yaani mwaka jana. Sasa unapozungumzia kuwekeza kwenye kuzalisha umeme, lakini mwingi unapotea barabarani, unakuwa hujafanya kitu. Kwa hiyo, pamoja na miradi hii, tuweke kipaumbele kwenye kurekebisha njia za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni gesi. Tumeona kwenye vyombo vya habari juzi Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani amekwenda kwenye mtambo wa *SYMBION* wa *megawatt* 112 lakini mtambo ule pamoja na kuwa na uwezo huo, lakini ukiuwasha leo unapata *megawatt* 60 na mwezi wa 12 Serikali inaleta mtambo mpya wa *megawatt* 100 lakini hautakuwa na uwezo wa kuzalisha *megawatt* 100, kwa sababu gani? Gesi hakuna.

Sasa huu mradi wa Serikali unaokuja Desemba ulikuwa unajulikana toka miezi 18 iliyopita. Huu mradi wa *SYMBION* umekuwepo miaka minne, imekuwaje hatukufanya maandalizi ya kufikisha Gesi? Sasa unanunua mtambo wa *megawatt* 100 kwa gharama kubwa, lakini hauwezi kuu-*run* kwa sababu huna gesi, sehemu nyininge hii ingekuwa *scandal*. Kwa sababu gesi ipo pale, kwa nini hatukupanga muda mrefu gesi ifike kwenye hii mitambo ambayo tumeinunua? Sasa tunapata haya mambo, lakini tupange tukijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuzungumza ni suala la elimu na vijana. Leo Tanzania tupo milioni 43, lakini watu waliopo shule ni milioni nne, milioni 8.6 wako Shule za Msingi, 1.6 wako Shule za Sekondari na milioni moja wako kwenye Vyuo vya Elimu ya Juu. Sasa kila mwaka vijana wanaomaliza shule ni milioni mbili na robo ya hao ndiyo wanaopata fursa ya kuendelea na masomo, wengine

wanakwenda wapi? Je, kule walikosoma na elimu waliyoipata ina uwezo wa kuwawezesha kuyamudu maisha yao?

Sasa Mpango huu nimeona una *Human Resource Development*, lakini ukiangalia sehemu kubwa ni *input* zaidi, yaani majengo, maabara na kadhalika. Lakini kikubwa ni *output* ya elimu, yaani *learning outcomes*.

Bunge hili lina uwezo wa kutengeneza historia kwamba tuamue sasa kwamba watoto wetu elimu wanayoipata iwawezeshe kuyamudu maisha yao kwa sababu Mpango huu siyo wa Serikali tu, bali ni watu wote, na watu ni lazima wawezeshwe kuwa sehemu ya mpango.

Sasa kama mfumo wetu wa elimu ni kwamba, anayepata *division four* ndiye anayekwenda kufundisha, kwa nini wanaopata *division I* na *II* ndiyo wasiende kuwa Walimu? Kwamba ualimu iwe ni kazi zinazolipa zaidi kuliko kazi zote na ngumu kuipata kuliko kazi zote. Kwa nini tusibadilishe ile *coin* tukaondokana na utaratibu kwamba mtu amekosa kila kitu ndiyo anakwenda kwenye ualimu? *Why?* Kwa sababu sisi bahati tuna *privilege*, tumesoma vizuri kwa sababu tulifundishwa na Walimu wazuri, lakini tunalo kundi kubwa la watu milioni 11 ambao tumeweka utaratibu hawafundishwi na watu ambao ni *the best and brightest* kwenye nchi yetu. Sasa Mpango huu napendekeza tuubadilishe kwamba tujenge kada ya Watanzania vijana ambao wamesomeshwa vizuri. Uwekezaji kwenye elimu ni *software* nzuri, siyo *hardware* kwa maana ya majengo na *infrastructure* ni *software*, *Curriculum Teachers Education*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Serikali hili ni jambo la kuamua tu kwamba elimu ni lazima iwe ni kipaumbele na watoto wetu lazima wasome vizuri ili kukabiliana na mazingira magumu ya dunia ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kwamba mambo yote haya tunayoyazungumza yanategemeana na siasa ya nchi imekaaje, nami sifurahishwi sana na jinsi siasa ya nchi ilivyo sasa na mfano ni humu humu Bungeni kwamba watu hatuvumiliani mpaka mtu amalize kuzungumza, kila mara ni mwongozo na taarifa, halafu hata lugha zinazotoka ni lugha kali. Sasa sisi humu ni viongozi, watu wanaotutazama jinsi tunavyohusiana, tunapandikiza *toxins* katika jamii.

(*Hapa Kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Kengele imelia.

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA: Naomba nimalizie kwa kusema naunga mkono tena hoja, Mpango ni mzuri, tuutekeleze. Ahsante sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Huwezi kumaliza. Nikiendeleza hapo alipoachia Mheshimiwa Mbunge, ninaambiwa nimewataja watu wa Kariakoo kwamba ni watu wa namna gani? Kwa hiyo, kama nimewa—*offend* au nimewaudhi watu wa Kariakoo, wanisamehe. Lakini nilichokuwa nasema ni kwamba ukienda sokoni Kariakoo hakuna utaratibu wa

kuzungumza, kwani kila mtu anazungumza kwa kadri anavyoweza wala huambiwi kaa ama una dakika ngapi, ile ndiyo sababu yangu. Lakini hapa Bungeni tuna utaratibu wa kuzungumza, yaani nani azungumze kwanza, nani asubiriwe, nani asikilizwe, kama una swali la kuuliza pia tuna utaratibu. Kwa hiyo, kama watu wa Kariakoo nimewaudhi, basi wanisamehe lakini nilimaanisha kwamba ukienda Kariakoo sokoni kila mtu anazungumza anavyotaka. Ukitaka kuzungumza kwa sauti sana unaweza, na kadhalika, lakini siyo humu Bungeni hapa ndani tuna utaratibu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nilikuwa na maana hiyo kwamba nani azungumze kwanza, nani asubiri na nani apewe nafasi ya kuzungumza baadaye. Lakini ukiwa pale Kariakoo utaongea kwa kadri unavyotaka na hakuna atakayekuuliza.

Tunaendelea na Mheshimiwa Christina L. Mughwai.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu...

MWENYEKITI: Naomba uhame kwenye hiyo *microphone*, naona inasumbua na kama kuna nyingine inawaka naomba izimwe tafadhali.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kama ulivowasilishwa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yameshazungumzwa na wachangiaji waliotangulia, lakini mimi nitakuwa na machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni kwamba nina wasiiasi wa namna Mpango huu wa Maendeleo wa Miaka Mitano ulivyoletwa, nina wasiiasi na mchanganuo au mkakati au mchakato uliotumika kutengeneza Mpango huu, wakati Mpango huu ni wa kitaifa ambao unatakiwa kutekelezwa na watu katika *level* zote nami nakubaliana na hilo. Wananchi katika ngazi hizo mpaka ngazi ya kaya kama tunavyoambiwa hawakushirikishwa katika kutengeneza Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba vipaumbele vinatofautiana kutoka eneo moja hadi linguine. Labda wananchi wangepewra fursa ya kutengeneza au kushiriki katika kutengeneza Mpango huu pengine vipaumbele vingeongezeka au vingekuja kwa mpangilio ambao ni tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hivyo basi, nilipokuwa nikiupitia Mpango huu wa maendeleo sijaona mahali popote ambapo kuna namna ambayo sasa elimu ya Mpango huu itapelekwa katika ngazi zote ili wananchi wote kama inavyokusudiwa waweze kuutekteleza. Sijaona Tume ya Mipango imetenga fungu gani na wenyewe wamejipanga kiasi gani na wana nguvu kiasi gani ili kupeleka elimu ya Mpango huu kwa wananchi wote na katika *level* zote na hii sasa inanipa shaka kwamba utekelezaji wa Mpango huu utakuwa namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushindwa kuwashirikisha wananchi kumekuwa ni sababu ambayo imepelekeea mipango mingi iliyotangulia kushindwa kutekelezeka kwa sababu wananchi wamekuwa hawa-own au wanajiona siyo sehemu ya huo Mpango, wanaona ni Mpango ulioletwa kutoka juu na wenyewe sasa wanapaswa kuutekeleza.

Kwa hiyo basi, napenda kuishauri Serikali pamoja na kwamba Mpango huu umeshaletwa na nia yake ni nzuri, Tume ya Mpango na Wizara husika wafanye juhudzi za makusudi kupeleka elimu ya Mpango huu kwa wadau wote wanaopaswa kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vipaumbele vya Mpango huu kuna suala zima la kilimo. Nitaliongelea suala la kilimo kwa namna ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano unatuambia kwamba Tanzania ina hekta milioni 44 zinazofaa kwa kilimo, lakini kati ya hizo ni asilimia 24 tu ndiyo inayotumika mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta hiyo hiyo ya kilimo nikirejea changamoto zinazoikabili sekta ya kilimo kama ambavyo imeelezwa katika Mpango huu tunaambiwa kwamba kuna kilimo duni na kilimo duni hiki kimechangiwa na uhaba wa ardhi. Sasa hapa nashangaa kama tuna hekta milioni 44 na zinatumika asilimia 24 tu sasa inakuwaje kilimo duni kichangiwe na uhaba wa ardhi? Hii asilimia 76 ambayo haitumiki ni kwa nini haitumiki? Hapa kuna *contradiction* na ninaomba basi wanaohusika waliangalie hili kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda uhaba wa kilimo unazongumziwa hapa mimi ninavyoona ni kwa jinsi ambavyo tunaitumia ardhi tuliyonayo. Tumekuwa na utaratibu wa kwenda kunyang'anya ardhi ile ile inayotumika na wananchi tunapohitaji kuanzisha miradi mikubwa katika kilimo au katika nyanja nyingine badala ya kutumia ardhi hii ya asilimia 76 ambayo bado haijatumika, tunakwenda kutafuta hiyo hiyo asilimia 24 ambayo wananchi wanaitumia na hapo kunatokea migogoro ya ardhi na tunaanza kusema kwamba ardhi hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ilivyoainishwa katika Mpango huu wa Maendeleo, suala zima la migogoro ya ardhi liangaliwe ili lisitokee, kwani limekuwa ni tatizo sugu katika Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuchangia katika mpango huu wa maendeleo ni sekta ya fedha jinsi inavyoweza kushiriki katika utekelezaji wa mpango huu. Tunajua umuhimu wa sekta ya fedha, tunajua kwamba wananchi wanatakiwa wakope katika taasisi za fedha, lakini sekta au taasisi za fedha zimekuwa zikiwanyonya wakopaji wake. Riba zinazotozwa kwa wakopaji wa taasisi za fedha ni za kinyonyaji na ambazo hazina tija wala manufaa kwa wakopaji wake. Kwa mfano, tunaambiwa kwamba riba za mikopo zinazotozwa na taasisi za fedha ni karibu

wastani wa 14% wakati huohuo riba za amana ni 2%, sasa kukiwa na tofauti kubwa kati ya *lending rate* na *savings rate* inaonesha ni *failure* kubwa katika sekta ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Fedha inalionna hili, Benki Kuu inalionna hili, taasisi za fedha zinatengeneza faida kubwa kutokana na riba kubwa za kinyonyaji ambazo wanawatoza wananchi walio na kipato cha chini, ukiulizia sababu za msingi za riba hizi kubwa, taasisi za fedha wanajitetea kwamba hawana taarifa kamili za wakopaji na kwa hiyo wanaogopa ile *risk* ya kukopesha watu wasio na taariza zao. Hili sio sahihi kwa sababu ukiangalia wale wanaokopa katika taasisi za fedha kwanza ni wafanyakazi walioajiriwa katika sekta rasmi na mfanyakazi hawezi kwenda kukopa benki bila kudhaminiwa na mwajiri wake. Mwajiri anapota dhamana na barua kuidhinisha kwamba huyu ni mfanyakazi wake na akopeshwe, sasa taasisi ya fedha inataka taarifa ipi? Hapo kuna *risk* gani? Naiomba Wizara ya Fedha na Benki Kuu, iwahurumie wafanyakazi na Watanzania wenye kipato kidogo ambao wanaishi kwa mzigoto mikubwa wa madeni kwa sababu hawawezi kuishi bila kukopa japokuwa mikopo hii ina riba kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nichangie eneo langu la mwisho, mpango huu wa maendeleo wa miaka mitano una nia nzuri, lakini wasiwasidhi wangu ni namna utekelezaji wake utakavyokuwa. Kuna tatizo la urasimu katika *system* yote ya utendaji wa Serikali. Tunapozungumzia mazingira mazuri ya biashara au uwekezaji, hivi Tanzania tumejiandaa kweli na mazingira hayo mazuri? Leo hii mtu akitaka kuwekeza au kufanya biashara katika nchi hii anapofika, tuna takwimu au taarifa sahihi za kumpa ni wapi awekeze? Atachukua muda gani kupata majibu anayostahili? Atachukua muda gani *ku-process* leseni yake? Je, vibali vyake atavipata kwa wakati gani? Je, atamkuta ofisa anayehusika ofisini? Kwa mfano, juzijuzi hapa Mheshimiwa Hamad Rashid, alikuwa anasema kuna mwekezaji alipeleka barua ofisi ya Waziri Mkuu ilijibiwa baada ya mwaka mmoja. Hili ni tatizo, tusipojirekebisha katika hili, hayo tunayoyakusudia kwamba sekta binafsi itashiriki katika Mpango huu wa Maendeleo wa Miaka Mitano haitakuwa rahisi kwa sababu ya tatizo la urasimu, hatuko tayari kutoa ushirikiano. Hilo linaambatana na rushwa, ukipewa ushirikiano basi inabidi pia utoe kitu chochote. Lazima Serikali iwe ina mkakati wa makusudi na sielewi sasa itafanya muujiza gani kwa sababu huu ndiyo umekuwa utaratibu wa utendaji, taarifa hazipo wakati zinapotakiwa, majibu hayatolewi wakati yanapotakiwa na pia uamuza haufanyiki wakati unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba baada ya kuchangia hayo machache, kama Serikali inadhamiria kweli kutekeleza Mpango huu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, naomba basi kwanza utekelezaji uwe kama ulivyokusudiwa, ushirikishwaji wa wananchi na wadau wote uwepo ili sisi tusije tukauona huu ni mpango tulioletewa tu na sisi ni wageni katika Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Assumpter Mshama, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jafo na Mheshimiwa Salum Barwany pia ajiendae.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa, napenda kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupongeza Kamati nzima ya mipango.

MWENYEKITI: Fungeni mashine mahali fulani zinaongea.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Kwa kuweza kutuletea Mpango wa Miaka Mitano. Kwa kweli

MWENYEKITI: Mheshimiwa Assumpter hama hiyo mashine.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, nampongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Kamati ya Mipango kwa kutuletea Mpango mzima wa Miaka Mitano wa Maendeleo.

Jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kwamba tunaipongeza Serikali iliyopita au kwa miaka iliyopita kwa kutembea pasipo kuwepo na mkakati au mpango wa kuonesha dira ya wapi unakwenda, kwa kweli hata walipofikia, tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze tu kwa kusema kwamba katika maongezi mengi kumesikika sana ikiongelewa kwamba tangu tupate uhuru miaka 50 hakuna kitu kilichotendeka. Mimi naomba niishauri tu Serikali sasa hebu iandae mpango ule wote, yale matunda yote yaliyopatikana kwa miaka hii yote 50, kuna vijana walizaliwa katika miaka ya 1970 wanaweza wasielewe kwamba Tanzania au Serikali hii ilikuwa inafanya vitu vya maendeleo. Kwa hiyo, ni vyema iandaliwe, isomwe, watu wajue kwamba kweli tulikuwa tunakwenda mbele na wala siyo kusimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona mambo mengi yamefanyika katika miaka 50, hata hili tu la kuwa na Vyama vingi, hata hili tu la wanawake kuwa Bungeni, barabara kutoka hapa mpaka Mtukula, barabara kutoka hapa mpaka Tunduma ni mambo ambayo yanaleta maendeleo na sishangai kwa nini mtu anauliza tutafikaje. Mimi nataka niwaondoe wasiwasi uliojitokeza sasa kwamba tulikuwa tunaweka msingi (*base*) na ukiwa unajenga nyumba ukaweka msingi ukamaliza, unachukua muda mwingi kuliko kupandisha tofali. Kwa hiyo, nachoona sasa tunakwenda kupandisha tofali na kuhakikisha yale tunayoyasema katika miaka mitano, sina wasiwasi kama hayawezি kufikiwa. Mimi ninao uhakika au ninatiwa moyo, hata tusipofika mia kwa mia lakini watu watatuhurumia kwamba lakini walikuwa na mpango labda jambo fulani na jambo fulani halikufikiwa, kwa hiyo mimi nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka niliongelee au nichangie, nataka pia nichangie juu ya ushirikishwaji. Anayesema kwamba wananchi hawajashirikishwa, kwa kweli siwezi kuelewa lakini naweza kufikiri kwamba sisi Wabunge kama tutashiriki jambo hili, sisi ndiyo wawakilishi wa wananchi wetu katika Kata, Matawi mpaka Vitongoji. Kwa hiyo, nina uhakika mimi kuwepo kwangu hapa na

kuchangia, nimemwakilisha mtu wa Kijunja kuwepo mahali hapa kuchangia na kuona mpango unaendeleaje. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, napenda nipongeze mkakati wa kilimo, lakini hebu tuseme, ni kweli mikakati mingi imefanyika lakini naomba tuongezee kutafuta masoko. Kule kwetu Misenyi watu wanalima kahawa, lakini sasa hivi wameiacha kahawa wanaanza kuhangaika kwenye vitu vingine ambavyo hawana ujuzi navyo sana kwa sababu soko la kahawa limekosa mtu wa kulisaidia, kuwapatia namna gani wapate faida katika kahawa. Ukiangalia Uganda, Waganda wanakuja kwetu, wanunuua kahawa yetu, siku moja nilikutana na Mganda nikamuuliza, kwani wewe hizi kahawa unazipeleka wapi? Akikuambia bei ya kilo wanayouza Uganda na ile ni kahawa ni ya Tanzania, unaweza ukashangaa. Sasa nitauliza kwa nini sisi hatufiki kule wanakopeleka hizo kahawa wenzetu wa Uganda? Kwa hiyo, nashauri Bunge lako Tukufu na Tume ya Mipango, unaweza kuhimiza watu walime kwa wingi, lakini wakishalima, je, wanapeleka wapi? Soko liko wapi? Nani wa kuwafikishia soko kule waliko? Kwa hiyo, nashauri katika suala la kilimo tuongezee soko. Mhaya alikuwa anajulikana sana kwa suala la kahawa, sasa hivi hata ukiangalia, ilikuwa inapimwa umaskini uliopo katika kila Mkoa, tumekuta Kagera pamoja na ule umaarufu wake tuko namba nne kutoka chini kwa umaskini, kwa sababu zao letu tulitolizoea limekosa soko matokeo yake watu wanahangaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini na sehemu zingine hali iko hivyo, kuna mahali watu wamesema wana mahindi mengi ndani, wamehimizwa kulima lakini hakuna mkakati wa kutengeneza yale mahindi kuweza kuwalettea faida ya kutosha. Kwa hiyo, nashauri kwenye Mpango huu mzuri basi tukiishahimiza kulima na tulete namna ya kupata masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka kuchangia kwa habari ya vijana, wanawake na uwezesho wa kiuchumi. Ukiangalia vijana wengi katika fikra zao wanawaza nitakapotoka hapa mimi pamoja na digrii yangu au namna yoyote natakiwa kuajiriwa na Serikali. Ni kwa nini wamelelewa hivyo, hawajapata mpango mwengine wa kusaidia na mtu akiwaza nikimaliza Chuo Kikuu au *Masters* yangu nikienda kuomba mkopo anaweza akawa na mawazo ya kwamba afungue kiwanda kidogo, amejifunza *engineering* lakini apate wapi mtaji wa kupata pesa? Kwa hiyo, nashauri kama walivyofanya kwenye wanawake kuwa na Benki ya Wanawake, kwenye dirisha la *TIB*, kwa nini tusiweke nafasi moja ya kusaidia vijana ili wanapomaliza waweze kupata mkopo? (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako vijana akileta *writeup* yake, tukaona kweli hii *writeup* inaweza kuzaa matunda tusiseme hakopesheki, tumpati na atupe vigezo, tubaki na cheti chake, tubaki na *ID* yake ili kusudi tuweze kupata namna gani anaweza kurejesha. Nilikuwa natetea hilo na ninaamini kabisa kwamba tukilifanya hata hawa vijana ambao wana hasira nyingi watarudisha hasira zao chini na wataona kwamba Serikali inawafikiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuchangia pia katika uwekezaji. Tumeongelea uwekezaji wa *private sector* pamoja na Serikali, naomba kusema kwamba hii hali ya mtu kuja kuwekeza kuna vigezo vya mtu kuvutika kuwekeza. Mtu anapokuwa na wazo, zamani watu walipokuwa wanawaza kuja Tanzania, ndiyo maana watu wengine wamesema kwamba aah, Tanzania ni kuingia kiholela, hapana, siasa yetu ilikuwa inaruhusu mtu kuja kuwekeza kwa amani, lakini kwa mtindo tunaokwenda nao wa vijana kukimbizana, maandamano, migomo, sidhani kama inatoa *room* ya kutosha kwa mwekezaji mzuri kuja kuwekeza katika nchi yetu. Mtu anaweza kukataa nakubali kwa sababu hiyo ni *spirit* ikiishaingia ndani ya mtu hamna namna ya kuitoa, lakini hebu tueleze kuna mtu ametolea mfano watu wakitaka kugoma wanaweka vitambaa kwenye mkono, lakini ule mkakati wa kupanga kwamba kesho tunagoma unaanza asubuhi mpaka saa kumi na moja, wanagoma kesho kwa maana hiyo siku hiyo yote hawakufanya kazi yoyote, hawakuingizia pato la Taifa kitu chochote, wana mkakati wa kugoma, kama ni wafanyakazi watakuwa kwenye mikutano wiki nzima, tutagoma, hakuna muda wa kufanya kazi. Nasema wakati wetu ni mzuri lakini kama hautaangalia mazingira ya mwekezaji hawatakuja. Jiulize kisiasa nchi zote zenye vurugu kama wawekezaji wapo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri maandamano, fujo, kule kwetu Kakunyu wamemuua mtu, ni mtu wa tano huyo tangu watu wameanza kuuana, kisa ni ugomvi na huko Babati, hivi mtu akisikia watu wanauawa hana nguvu ya kuwekeza. Naomba kwa kweli tuendelee kuwa na amani, hatukatai kuna upungufu lakini mikakati ya kugoma haiwezi kusaidia kuleta mabadiliko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kutekeleza mpango, kilio changu cha kwanza nawaza namna gani tutatekeleza Mpango huu. Utamaduni wetu wa kutofanya kazi, unakuta mtu anakwenda kazini saa nne, saa tano ikifika anakwenda kutembea kutafuta vitu mjini na ukitembea katika miji yote mikubwa unakuta misururu wa magari haipungui, hujui saa ngapi watu wako kazini na saa ngapi watu wametoka nje. Huwezi kupanga kwamba hapa natoka pointi moja kwenda mahali pengine nisubiri *queue* ipungue, haipunguagi Dar es Salaam, haipunguagi katika miji mikubwa, kwa nini? Kwa sababu watu wanakwenda kazini kama wanavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka kweli kufanya mambo haya tu-*invest* katika *timing*, watu wawe na kadi za kuingia kazini kama *private sector*, hiki tunachoongelea tunakwenda kuchanganya *private sector* na *public*, huyu mtu wa *private sector* ana-*control* vipi kuzalisha kuliko sisi Serikali? Ni kwa sababu masaa ya kazi ya mtu yanaonekana pale, umetoka saa ngapi, umerudi saa ngapi na umetumika masaa mangapi? Hivyo tusione taabu ku-*invest* katika *system* ya kumbana mtu kubaki kazini. Zaidi ya hapo mkakati huu hata ungekuwa unadondosha dhahabu bado hauwezi kutimilika kama watu hawana *spirit* ya kazi. Hakuna mtu anayemuuliza mwenzie ulikuwa wapi, hamna mtu anasema utafika saa ngapi, hakuna mtu anaogopa kutokuwa kazini. Kwa hiyo, mawazo yangu kwa wananchi wa Tanzania, unaweza ukalaumu Serikali uko kitandani, saa nne hujaamka unasema Serikali mbovu, saa sita hujaenda kulima, Serikali mbaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli naumizwa sana na watu kutofanya kazi na ndiyo maana mtu mnaweza mkawa mnapata mshahara mmoja anakushangaa unavyoishi, mtu mchapakazi ataonekana na mzembe ataonekana. Kwa hiyo, sisemi Watanzania wazembe, naomba tuenze na kazi ndiyo twende kwenye mpango mkakati, bila hivyo tutapoteza wakati na hakuna kitakachofanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba Watanzania kweli wamechoka kuona mtu anatenda kosa anahamishiwa mtaa mwingine au Wizara nyingine badala ya kutoka kazini akatupwa nje. Kama kuna watu hawawezi kufanya kazi tuiswalee hao ndiyo wanababisha Serikali yetu ionekane haifai. Naomba kwa kusisitiza, tuisimamie kazi na utendaji bora na utawala bora ndipo tutaweza kutekeleza Mpango Mkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache sitaki kugongewa kengele nyingine, naomba tu nimalize na Mungu awabariki. (*Makofi*)

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii nami kuwa mionganoni mwa watu ambao tunashiriki kujadili mpango huu wa Taifa kwa ajili ya mwaka 2011/2012 hadi mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchache wa fadhila ndugu zangu kama kwanza nisingemshukuru Mheshimiwa Rais. Nyie wote ni mashahidi, Mheshimiwa Rais hapa siku ile wakati analihutubia Bunge kwa mara ya kwanza hili alilizungumza tena alilizungumza kwa umakini kabisa kwa nini tunataka kuhakikisha kwamba inaanizishwa Tume ya Mipango na hii inaonekana ukifuata *reference* kwamba ni kilio cha Watanzania wengi toka muda mrefu. Kwa hiyo, jambo la kwanza, mimi naona kwamba sisi Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ni wawakilishi wa wananchi jambo la kwanza ingebidi tumpigie makofi ya nguvu kabisa Mheshimiwa Rais, kwa kazi kubwa aliyofanya. Ndugu zangu mtu yejote akifanya jambo jema lazima kwanza umshukuru na uweze kuthamini mchango wake, hili ndiyo jambo la kwanza la msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili Mzee wangu Wasira, nakushukuru sana kwa hotuba yako nzuri. Aidha, namshukuru Mwenyekiti wetu wa Kamati pamoja na ushauri mzuri kutoka katika Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu Watanzania sisi tuna bahati mbaya, neno hili nililizungumza siku ya kwanza, bahati mbaya yetu tuliyokuwa nayo tuna tatizo kubwa la kutokujivunia yale mazuri tuliyokuwa nayo, hili ndilo tatizo letu kubwa. Utaona wataalamu wa Kitanzania wameweza kutengeneza mpango mzuri na madhubuti ndani ya miezi sita wengine tunaona kama nongwa, tunashangaa, jamani tunataka nini? Hili ni jambo la kwanza, nasema ni jambo kubwa zaidi sisi Watanzania tuweze kujivunia kwamba kumbe tuna wataalamu wa kutosha wa kututekelezea mipango yetu kwa mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu ukiupitia Mpango huu, nadhani kila mtu ameelezea kwa utashi wake na kuona jinsi gani unaweza kuboreka. Kila mtu anaweza kutoa *reference* hapa kwamba kuna mipango mingapi ambayo ilipita na hivi sasa tuna mpango huu. Kila mtu anaweza kugusa kwao, nimeamini kwamba kila mtu anaguswa na nchi hii. Ndio maana leo tupo hapa, lengo kubwa tukitoka hapa tutakuwa na kitu kizuri na mpango mzuri kwa ajili ya Taifa letu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaingia katika Mpango huu niseme Watanzania tunaweza na wenzangu wamesema. Tanzania hii ukirudia *reference* tena ya miaka mitano nyuma hata ukiangalia katika sekta ya elimu peke yake tumepiga hatua kubwa sana. Hata mtu kama hukubali kutoka shule 1,200 mpaka shule 4,500 sio jambo dogo ndugu zangu hilo. Wapo wenzangu wa Geita kule, mimi nasafiri naenda Geita kutoka Geita kwenda Misungwi barabara ilikuwa hakuna jamani Tanzania hii hii. Daraja la Umoja, wengine wanasema Tanzania hakijafanyika chochote, Daraja la Umoja ni daraja la mfano kwa Tanzania hii, jamani tujivunie kwa mambo yetu. Chuo cha Dodoma sasa hivi kinachukua wanafunzi wengi sana katika Afrika Mashariki na ya Kati, ni chuo cha mfano jamani, Tanzania tujivunie kwa haya na mimi naamini kupitia Mpango huu tunazo dalili tutapata jambo moja la msingi kwelikweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujielekeza zaidi katika Mpango huu hasa katika suala zima la miundombinu na nataka kujikita katika Jiji la Dar es Salaam na Mpango huu umetuonesha vipaumbele mbalimbali hasa katika suala zima la miundombinu. Jiji la Dar es Salaam ndio kitovu cha uchumi wa nchi hii. Aidha, tutake au tusitake hata mchango wake wa mapato ni mkubwa kwelikweli lakini ukija kuuangalia sasa hivi msongamano wa Jiji la Dar es Salaam umekuwa mkubwa kwelikweli. Nashukuru wenzetu wa Mipango wamebainisha kupitia mpango huu kwamba kuna mikakati mbalimbali kwa ajili ya kulikomboa Jiji la Dar es Salaam katika masuala ya msongamano na hasa hasa kuweka vyanzo vizuri vyta uchumi katika suala zima la bandari lazima tujipongeze katika haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana nilipokuwa napitia Mpango huu nilifikiria jambo moja kama kuleta ushauri katika Bunge hili. Katika kikao hiki na katika Tume yetu ya Mipango, kuanzia Mlandizi mpaka Ubungo ni tatizo kubwa sana. Msongamano wa malori umekuwa ni mkubwa kwelikweli. Mtu anaweza akasafiri kutoka Mbeya au Mwanza lakini akishafika maeneo ya pale Mbezi basi tumbo linaanza kumuumaa atatumia hata pengine masaa mawili kwa ajili ya kufika pale Ubungo, lakini Mpango huu jamani unajieleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashauri ndugu zangu wa Tume ya Mipango kwamba katika mpango huu kuna kitu kimoja ambacho kitasaidia sana katika suala la msongamano maeneo ya Dar es Salaam, hasa unapoingia katika Jiji la Dar es Salaam ni kuimarissha barabara inayotoka Mlandizi - Mzenga - Kisarawe unatokea *Airport*. Hili ni jambo muhimu kwelikweli, naomba mlielewe. Barabara hii hata tukiamua kwamba malori yote makubwa ya Tanzania badala ya kupita barabara ya kutoka Ubungo - Mlandizi yapite kule, ni barabara fupi sana, lakini mpango huu

ukiangalia ukurasa 26 - 32 imeonesha kwamba kuna barabara ya kutoka Makofia - Mlandizi mpaka maeneo ya Vikumburu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara nyingine ya kilomita 54 inayotoka Kisarawe - Maneromango. Kuna kipande kidogo cha barabara cha kilomita 42 ambacho hakimo katika Mpango huu na kipande hicho ambacho hakikuwekwa katika mpango huu nini maana yake? Maana yake eneo lile, hilo suala la barabara mbadala litapatikana hata ile kero ya kusema kwamba kuna malori makubwa yanayosababisha msongamano jambo hilo halitatokea tena. Barabara hiyo ni chini ya kilomita 110 kwa nini kama sisi Watanzania tuiseme kwamba jambo hili ni jambo makini na kuliweka katika Mpango wetu wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala zima la kilimo. Sote tunafahamu Mikoa ya ukanda wa Pwani imesahaulika sana katika maendeleo ya kilimo, hili liko wazi na kupitia Mpango huu naomba kushauri yafuatayo. Kwa nini sasa tuiseme kwamba maeneo ya Bonde la Rufiji, Bonde la Mto Ruvu tuhakikishe tunayapa kipaumbele ili mradi Mikoa ya Kanda ya Pwani iweze kuinuka zaidi. Ndugu zangu kama walivyosema wengine na jana nimesikia ndugu zangu wa Kigoma, Mikoa hiyo wakati mwingine inatofautiana katika suala zima la maendeleo. Kupitia Mpango huu lazima kuweka mikakati ya kutosha, jinsi gani tutalipeleka Taifa letu hili liweze kwenda mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni sekta ya maji. Napenda kuishukuru Serikali yetu na Tume ya Mipango kuona kwamba suala la maji ni jambo muhimu kwelikweli. Hata nikiangalia katika suala zima la marekebisho hapa naona hata ndugu yangu Mnyika amezungumzia suala zima la miundombinu ya maji. Napenda kusema jambo moja, uwekezaji wa Serikali unaoweka katika suala zima la kuimarisha maji katika Jiji la Dar es Salaam, ni jambo kubwa sana. Jambo hili ni jambo la kuweka msukumo kila liwezekanalo tuhakikishe kwamba Serikali yetu tunaipongeza na kuweza kuipa nguvu ili jambo hili liweze kufanikiwa ili maeneo yenye shida ya maji sio Dar es Salaam tu na maeneo mengine yote yaweze kupata maji ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Tume ya Mipango, ukipitia kama sikosei ukurasa wa 129 katika jedwali kuna suala zima la kuanzisha *freight station* katika Wilaya ya Kisarawe. Lengo kubwa ni kuondoa, kupunguza msongamano katika bandari yetu ya Dar es Salaam. Lakini Wilaya ya Kisarawe tumesema endapo ikiwepo *freight station* maana yake mizigo yote itakuja Kisarawe. Kwa hiyo, kupitia Mpango huu, naomba sasa tuhakikishe kwamba tunajipanga vizuri kwa suala zima la mpango wa maji katika Wilaya ya Kisarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, napenda kuishauri Serikali, Mpango huu uingize katika ile programu kubwa ya mpango wa maji katika Jiji la Dar es Salaam angalau tuweke maji yanayotoka Mlandizi yapelekwe mpaka katika eneo la Tarafa ya Mzenga ambayo ni chini ya kilomita 32 ambapo tutawezesha eneo lote la

Mzenga kuwa na maji hata tukianzisha ile *Dry Port* katika Jimbo la Kisarawe, tutahakikisha kwamba tuna maji ya kutosha katika eneo la Kisarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu hauwezi kwenda bila kuusimamia. Naomba kusisitiza katika suala zima la usimamizi. Mipango hii tusimuonyeshee mtu kidole, huenda Waziri mpango huu haujakamilika hapana, Mpango huu ni wetu wote. Naomba tuuchukulie sisi Wabunge na Watendaji wa Serikali, tuwe imara kuhakikisha kwamba Mpango huu unakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia ripoti za Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, kuna matumizi mabaya sana katika Halmashauri zetu, hili kama sisi Wabunge tulipangie mipango mizuri zaidi, hata tukiwa na fedha tukizipeleka katika maeneo yetu bila ya kuwa na usimamizi mzuri maana yake tutakuwa tunatwanga maji katika kinu. Lazima tuwe wakali kama Wabunge kwa ajili ya mustakabali wa nchi yetu na Watendaji watuelewe sisi tuna hasira kwelikweli kwa ajili ya nchi yetu, tusifanye masihara hapa hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kabisa Chama cha Mapinduzi ambacho sasa hivi ni Chama Tawala na ambacho mimi nimetoka ni Chama makini zaidi. Nina imani Wabunge wote tulioko humu ndani ya Bunge hili ni Wabunge makini zaidi, naomba tuhakikishe kwamba Mpango huu ndani ya miaka mitano, tunakuwa *frontline* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunafanya *monitoring* ya Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nimesema tuambiwe *the financial communication protocol*. Tuhakikishe kwamba matumizi ya Serikali, Mbunge katika Jimbo lake na Mwenyekiti wake wa Halmashauri wanasi mamia vipi na kwa ukaribu zaidi. Wakati mwingine tunakuja *by surprise* hata Mbunge au Mwenyekiti wa Halmashauri hajui matumizi katika Halmashauri yake ni jinsi gani yanaenda. Huu ndio ubadhirifu wa hali ya juu unatokea. Naomba kwa pamoja kwa kweli tuwe wakali kwa ajili ya mustakabali wa nchi yetu. Mimi nina imani Serikali yetu na sisi sote hakuna hata mmoja anayependa ujisadi. Ndio maana kila mtu humu hana hasira kwa ajili ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, maana Wanasiasa hata ukisema sana unamalizia kwa haya machache. Kwa haya machache, napenda kuwaomba Wabunge wenzangu tusimame kidete kuhakikisha mpango huu unakwenda na kwa asilimia mia moja naunga mkono hoja hii. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Salum Khalifa Barwany, naona kwa muda nilionao hata Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi atafikiwa.

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante labda nifanye marekebisho pia juu ya jina langu hapa, ni Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa hii kuchangia hoja katika mjadala ambaa upo mbele ya Bunge lako Tukufu. Wabunge wenzangu

wamezungumza mengi, lakini la msingi kabisa na la muhimu ambalo limezungumzwa na Wabunge wote ni juu ya mjadala wa Kitaifa. Mpango huu ambao leo upo mbele yetu ni Mpango ambao Watanzania walitarajia katika Bunge lao Tukufu hili tuuzungumzie. Hali ya maisha ya Watanzania kwa ujumla, kusema kweli maisha ya Watanzania ni magumu kwa kiasi kikubwa na kwa matarajio makubwa ya Watanzania wameamua kufanya mabadiliko makubwa katika Bunge hili la Kumi. Asilimia 70 ya Wabunge katika Bunge hili la Tanzania leo ni Wabunge wapya. Wakiwa na matarajio makubwa kuona wanapelekewa maendeleo ndani ya Taifa lao. Hivyo ni vyema tunapotoa na kuchangia hoja hii tukazingatia hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miaka 50 ya uhuru sio kidogo kwa maendeleo ya nchi. Kama kweli Serikali inajipanga vizuri, ikatumia rasilimali zake vizuri, umaskini wa nchi unaweza kuondoka mara moja. Tunaweza tukauondoa umaskini huo kwa kujipanga na kuwa na malengo sahihi ya kwenda katika mafanikio yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango ni mzuri na Watanzania wanatarajia tutapanga vizuri katika hoja hii lakini namna ulivyoletwa ndani ya Bunge letu kasoro ni nyingi, ni namna gani umewashirikisha Watanzania mpaka unafika hapa? Ushirikishwaji katika jambo lolote ni muhimu katika maendeleo ya umma. Kama wananchi wanashirikishwa, wakajua kilichopo, leo tunaweza tukapata michango mikubwa kwa ajili ya jambo ambalo Watanzania wenyewe linawahuhsu katika maana ya ushirikishwaji. Mipango mingi imekuja tangu tumepata uhuru miaka 50 iliyopita, katika awamu mbalimbali, Awamu ya Kwanza imekuja na mipango yake, Awamu ya Pili, Awamu ya Tatu na leo tupo katika Awamu ya Nne. Uzoefu unaonesha kwamba kila Awamu ikimalizika basi inaondoka na mpango wake na hakuna mpango endelevu, hakuna Sera ya Kitaifa ambayo inasema Awamu yoyote itakayokuja ndani ya nchi kutawala nchi yetu basi inatakiwa ifuate utaratibu ambao Serikali ya awali ilikuwa imeufikisha pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tupo katika Mpango huu, naamini Serikali ya Awamu ya Nne itakapotoka na Mheshimiwa Kikwete na Mawaziri wake basi mpango huu utawekwa kabatini, huo ndio uzoefu tuliokuwa nao. Tatizo kubwa ni kwamba hatuna Sera ya Kitaifa katika nchi yetu. Ni vyema sasa tukawa na Sera ya Kitaifa katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna wataalamu wengi katika nchi, tuna Wasomi, tuna Maprofesa, kuna watu wenye uwezo mkubwa, tunawashirikishaje? Ni vyema sasa Taifa letu tukawa na mjadala wa Kitaifa kwa mambo muhimu kama haya. Tujiulize kwa nini mpango huo umekuja leo, baada ya mipango mingine yote kushindikana huko nyuma. Hali ya nchi sio nzuri, Serikali ikaona sasa tunafanyaje ndio umekuja Mpango huu ili Wabunge tuishauri Serikali. Kama ilivyozungumzwa kwamba Mpango huu sio wa Chama, ni wa Serikali, ni wa Kitaifa, hivyo ni vyema Watanzania kwa jumla wangehusishwa. Kama nilivyosema tuna wataalam wengi ambao kwa uwezo na taaluma yao wangeshiriki lakini tunaona kuna uchache wa ushirikishwaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia masuala mengi hapa ya kilimo, umeme lakini suala zima ambalo linaweza likasimamiwa kama ningekuwa mimi natoa

maoni yangu ningesema Umeme Kwanza badala ya Kilimo Kwanza. Umeme kwa dunia ya leo ya teknolojia tuliyokuwa nayo ni muhimu katika maendeleo ya nchi yoyote. Leo umeme usichukuliwe kama ni starehe, umeme sio starehe kama inavyodhaniwa na watu wengi katika nchi yetu. Umeme ni nyenzo muhimu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu na tunaweza tukasema Kilimo Kwanza, lakini je, bidhaa ambazo zinatoka katika kilimo zinakwenda wapi, zinakwenda katika viwanda. Kama viwanda havina umeme basi mafanikio ya kilimo hicho hayawezi kuwaleta tija Watanzania wenyewe. Hivyo, ni vyema tukasema kwamba pamoja na Kilimo Kwanza ambacho tunakizungumzia lakini pia kuna umuhimu wa kusema Umeme Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa tulizonazo juu ya mpango mzima katika eneo la kilimo, kuna mpango umekuja, mpango wa SAGCOT (*Southern Agriculture Corridor of Southern Tanzania*) lakini la kusikitisha mpango huu haukuhusisha Mikoa miwili ya Lindi na Mtwara, hajatajwa katika eneo la Mikoa ya Kusini. Hili linatia mashaka, linatia mashaka kwa sababu kama mpango huu ni kwa ajili ya maendeleo ya kilimo *Southern area* kuitoa Mikoa ya Kusini ya Mtwara na Lindi itafanya Mpango huu usifanikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ya kilimo hakuna zao ambalo linapatikana katika Mikoa ambayo imewekwa katika Mpango wa SAGCOT ambalo halipo katika Mikoa ya Kusini. Historia inatuonesha uchumi ulio sahihi unapatikana katika Mikoa ya Kusini. Leo inapotajwa Mikoa ya Kusini ya Mtwara na Lindi basi tunazungumzia habari ya gesi ya Songosongo na gesi ya Mnazibay kuingizwa katika gridi ya Taifa lakini Mikoa ya Mtwara na Lindi haizungumziwi kwa maendeleo ya Mikoa hiyo, inapozungumziwa ni jinsi gani itachukuliwa gesi kupolekwa katika gridi ya Taifa kwa maendeleo ya Mikoa mingine. Mpango huu tunasema utadumu kwa muda wa vipindi vitatu na tunaanza kipindi cha awali ambacho kinaishia mwaka 2015, kama hautoendelea basi huko mbele inaonekana ni kwa atakayejaliwa katika awamu nyingine lakini tunaona kwamba kama mpango huu haupo kabisa katika maeneo mengine basi itakuwa ni ndoto kuona kwamba kuna mafanikio ambayo yamepatikana katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo katika suala zima la mgawanyo wa rasilimali katika nchi. Kama nchi haijawa makini katika kutenga na kugawa rasilimali zake katika nchi, nchi hiyo inaweza kupoteza amani na utulivu uliokuwepo. Tuna manung'uniko katika maeneo mengi Serikali ione umuhimu wa kuangalia maeneo mengine pamoja na kwamba hazina ya nchi ni moja. Tunashangaa ni vigezo gani ambavyo vinatumika katika nchi kuona kwamba mgawanyo wa rasilimali unaridhiwa na Taifa zima. Kuna maeneo mengine tayari yana maendeleo ya kutosha, maeneo mengine yako nyuma katika sekta mbalimbali, katika sekta za afya, elimu, miundombinu tayari kuna tofauti kubwa ya maeneo, kuna tabaka ndani ya nchi, jambo hili linahatarisha amani na utulivu katika Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasikia katika Kampeni mbalimbali za kuomba kura kwa viongozi wa Serikali, maeneo ambayo yako nyuma kiuchumi Serikali itahakikisha kwamba inaondoa kero. Ndani ya bajeti hatujaona, hivi ni Mikoa mingapi ambayo iko

nyuma kiuchumi katika Taifa letu bajeti hii imehusika nayo kwa kiasi kikubwa. Kuna maeneo mengi tu. Kuna Mikoa kadhaa ambayo iko nyuma lakini bajeti na mpango huu haijaiangalia. Sasa haya ni mambo ambayo tunataka tuyaangalie na kuona ni jinsi gani tunaweza kuhakikisha kwamba mpango huu unawenza kuridhiwa na Watanzania wote la sivyo Watanzania wengine wanaweza wakawa watazamaji juu ya Mpango huu na wengine waone raha kwamba Mpango huu unawaletea tija katika maendeleo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la elimu, wamezungumzia watu ambao ni muhimu kabisa. Mheshimiwa Makamba ametueleza kwa undani kabisa ni vijana wangapi ambao wanamaliza elimu ya msingi, elimu ya sekondari, vyuo vikuu wanakwenda wapi leo? Wanafanywa nini wale? Nafasi ya ajira ni ndogo katika nchi yetu, je, tunawaandalia nini vijana ambao wanamaliza Kidato cha Nne zaidi ya laki tano wanakaa nyumbani wakiwa na umri mdogo! Stadi za shule bado hazzoneshi kwamba wanaweza kuendesha maisha yao kupitia elimu ambayo wamepata. Hii inatufanya tuwe na vijana wengi katika vijiwe ambao tayari hawajui mustakabali wa Taifa lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati muafaka sasa tukatengeneza mjadala wa kitaifa, tukakaa Watanzania wote, tukajifunzia ndani, tukaona je, tunalitoaje Taifa letu. Miaka hamsini ya uhuru si kipindi kidogo, makumi matano hayo, nusu karne hiyo, karne moja Mheshimiwa ina miaka mia moja, miaka hamsini ni nusu karne. Watanzania tunaletea mipango kila siku, mipango isiyofikia mwisho. Tutengeneze mjadala wa kitaifa, tutumie wataalam wetu, tumewasomesha kwa gharama kubwa, tumewasomesha ndani ya umaskini mzito, tuwatumie hawa. Sio kufika mahali kutumia kundi dogo tu la watu eti wakifikiri kwamba wanafikra kuliko Watanzania wote. Si kweli! Tuna wataalam, tuna akina Profesa Lipumba hapa, wataalam wa uchumi, tunawatumiaje katika kujenga uchumi wa taifa letu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike mahali Watanzania sasa tukae tupange mipango yetu, mipango ya dhati kabisa, tuisimamie. Wanasema mpango huu utasimamiwa na kila Mtanzania, kwa namna gani mpango huu utasimamiwa na kila Mtanzania? Wanasisimamiaje Watanzania wote, lazima kuna watu waji-commit juu ya jambo hili si kila mtu anawenza kusimamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisimalize muda wako, haya nafikiri yanatosha sana kwa mchango wangu kwa siku ya leo. Nasema ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii hatimaye na mimi kuchangia katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, kwanza napenda nichukue fursa hii, kuipongeza Timu ya Mkoa wa Mbeya kwa kuchukua Kombe la Taifa kwa kuichapa Mwanza, nilimwambia Highness Kiwia, Mbunge wa Ilemela. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumpongeza na kumshukuru Katibu wa Chama changu, Mheshimiwa Dkt. Slaa, kwa kazi aliyoifanya wakati wa Kampeni za Uchaguzi na kufanikisha kupandisha Wabunge wa CHADEMA kutoka 11 mpaka 48 akiwemo Sugu. Pia nampongeza kwa busara alizochukua katika kushughulikia suala zima la matokeo ya uchaguzi, kwa sababu wote tunafahamu kulikuwa na mushkeli kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba nianze na suala la amani maana naona kila mtu anazungumzia amani. Ukweli ni kwamba kila mtu anajua kule tulikotoka, wote tunazunguka, wengine wanatusema kwamba CHADEMA tunaacha Majimbo yetu tunazunguka kila sehemu, ndiyo tunazunguka na kule kote tunakozunguka tunazona hali za wananchi. Hali za wananchi ni ngumu, wananchi hawana amani matumboni wala vichwani mwao katika suala zima la kufikiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusikae hapa tukasema amani, maandamano utafikiri kama CHADEMA *is a rebel group*. CHADEMA *is not a rebel group*, CHADEMA ni Chama cha Siasa kinachofanya shughuli zake kwa mujibu wa Katiba yakiwemo maandamano. Kwa hiyo, anayetaka kuandamana aandamane tu tuone kama atapata watu labda hilo ndiyo tatizo. Tunatakiwa sasa tuache maneno, tuache porojo maana sisi ndiyo wa kwanza kusema humu ndani hakuna mambo ya kisiasa, humu ndani ni wamoja lakini sisi ndiyo wa kwanza kuleta *interest* za Vyama hata tunapoongelea masuala muhimu kama hili ambalo tunaliongelea hapa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbilinyi, ukijadili hoja utakuwa umetumia muda wako vizuri.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni vizuri tukawa *serious* katika kujadili masuala ya maendeleo. Waziri anayehusika jana alisema mfumuko wa bei ulidhibitiwa kuanzia mwaka 2001 kwa asilimia sita mpaka sasa lakini wote tunajua kwamba kilo ya sukari mwaka 2005 ilikuwa shilingi 400/- sasa hivi ni shilingi 2,000/-, kilo ya nyama ilikuwa shilingi 800/- na sasa hivi ni zaidi ya shilingi 4,000/. Sasa huo mfumuko wa bei uliodhibitiwa kwa asilimia sita sijui ni mfumuko wa bei wa wapi labda Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, imefika wakati sasa humu ndani tuwe wakweli katika suala zima la kuwakilisha wananchi kwa maendeleo yao vinginevyo tutaendelea kufeli kama tulivyofeli wakati wote. Tumefeli katika suala la kilimo, Mwalimu Nyerere miaka thelathini na tano iliyopita ndoto yake ilikuwa ni kilimo cha matrekta leo hii sisi tunakaa na tunajisifu kwamba tumepiga hatua kwenye kilimo kwa *power tillers* ambazo afadhali tungekuwa tunazitengeneza kule kwenye Kiwanda cha Zana za Kilimo Mbeya (ZZK) lakini kiwanda kama cha ZZK kimefungwa kinatumika kama ghala la kuhifadhia bia halafu tunazungumzia Kilimo Kwanza Watanzania tunalima kwa kauli mbiu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema hivi, kama tutaendelea kulima kwa kauli mbiu, tutakuwa na Kilimo Kwanza, Kilimo Pili, Kilimo Tatu tutafika mpaka Kilimo Kumi wakati hali ya mkulima wa Tanzania inazidi kuwa mbaya. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia bei ya mbolea Tanzania, tunashindwa hata kuwapatia wakulima wetu mbolea. Tanzania mbolea inanunuliwa kwa takribani shilingi laki moja kwa mfuko, ukienda Malawi inauzwa chini ya shilingi 10,000/- wao wanatoa wapi mbolea, sisi tunatoa wapi mbolea? Naposema shilingi 10,000 ni shilingi 10,000/- ya Kitanzania. Kama ni hivyo ni afadhali twende Malawi tukanunue mbolea kwa bei ya rejareja ya shilingi 10,000 ili tuje hapa tuuze shilingi 20,000/- tutapata faida kwa asilimia mia moja kuliko hivi tunavyokwenda. Mbolea shilingi laki moja ukienda Malawi chini ya shilingi 10,000/-, ni majirani zetu, tunafahamu, tunafuatilia na ukifuatilia unakuta wote tunatoa mbolea sehemu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia masoko ya mazao ya wakulima, inatisha na inasikitisha. Unatembea katika mabonde ya chai kwa mfano kule Rungwe, wakati unapita barabarani unakuta kuna marundo ya majani yamewekwa chini, unauliza hiki ni nini? Wanasema hiyo ni chai? Unauliza inafanya nini hapo chini? Wanasema wakulima wanavuna chai, wanesubiri gari la kuja kukusanya chai, ikifika saa nne usiku kama hiyo chai haijachukuliwa basi ni chai ya kutupwa, imekula kwa wakulima. Wakulima wanaamua kuchukua hatua ya kujisaidia kwa kujaribu kulima mazao mengine kama mahindi ambayo wanaweza wakauza na kupata fedha kuliko chai ambayo inaozea mabondeni lakini wanaambiwa wakiacha kulima chai na kwenda kulima mahindi watashtakiwa, wanakamatwa na Serikali za Vijiji zinazohusika kwa kuacha kulima chai na wakilima chai, chai ikifika saa nne usiku gari halijaja kuchukua imekwenda. Hivyo hivyo katika maeneo kama ya Kyela wanalima Cocoa, lakini inamsaidia nini mkulima wa Kyela?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kama Uswiss ni maarufu kwa vitu vitatu. Kutengeneza saa, kutengeneza visu na kutengeneza *chocolate*. Hii *chocolate* wanayotengeneza nchi ni ya milima tena milima ya barafu. Si tu hawalimi *cocoa* bali hawalimi hata mchicha lakini wao ndiyo maarufu duniani kwa kutengeneza *chocolate*. Sisi tuna *cocoa* pale Kyela hatuna hata soko na hatujui hata pa kuipeleka ile *cocoa*, wakulima wanalamika kila siku halafu sisi tunaendelea kuleta siasa katika suala la kilimo. Kwa hiyo, ili tuendele, nafikiri taswira ya Mwalimu Nyerere bado inakuja, ili tuhakikishe kwamba kilimo chetu kinaendelea katika kumletea maendeleo mkulima, uchumi uanzie chini, lazima tuijilize, kuliko kuja na kauli mbiu zaidi ni afadhali turudi kwenye kauli mbiu ya Mwalimu Nyerere ya Kilimo cha Kisasa ambaye alikuwa na ndoto ya matrekti. Turudishe viwanda vyetu kama ZZK Mbeya, kwa maendeleo ya mkulima na maendeleo ya mfanyakazi wa Mbeya Mjini ambaye alikuwa anafanya kazi pale kwenye kile kiwanda vinginevyo tutaendelea kupiga *mark time*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye suala la uvuvi. Angalia wavuvi wadogo wadogo, wamepata msaada gani katika maeneo mbalimbali? Juzijuzi nilipita Mbamba Bay, kwa kaka yangu Mheshimiwa Komba, nikiwa napita kandokando ya Ziwa Nyasa kwa gari kwa masaa sita, naliangalia lile Ziwa, naangalia ile *beach* imenyooka kilomita

nne unakuta mchanga safi, unajiuliza hili ni Ziwa au ni Bahari kwa sababu Ziwa Victoria lina shimo limelala hivi, Ziwa Nyasa lina mgongo limenyanyuka kama bahari kitu ambacho ni kivutio tosha kwa ajili ya utalii, ni kupeleka barabara ya lami kule Mbamba Bay, kupeleka umeme, wawekezaji watakwenda wenyeve tukishawawekea miundombinu, watajenga hoteli, hali ya hewa ni nzuri kwa watu kupumzika. Unatembea kandokando ya Ziwa Nyasa kwa muda wa masaa sita unaangalia Ziwani huoni hata mtumbwi, hakuna hata *activities* zozote zinazoendelea, barabarani unapishana na kina mama wamebeba masinia au visahani vya dagaa badala ya kupishana na magari ya *freezer* yaliyobeba samaki na dagaa kwa ajili ya watu wa Nyasa na kwingineko. Haya hatuyatoi vichwani, tumefika kule na wananchi ndiyo wanalamika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda unakwenda, ngoja nirukie kwa vijana kwa sababu hili ni kundi *vulnerable*. Vijana wa Taifa hili hawajafaidika na MKURABITA, MKUKUTA na wala hawajui maana yake nini, hivyo viko kwenye ofisi zetu. Kwa hiyo, labda wale tunaowapa taarifa kwamba njoo ni ofisini kuna hiki na hiki, andika *proposal* ya hivi na hivi, ndio wanaojua MKUKUTA na MKURABITA, ndiyo wanaofaidika lakini vijana wa Mwanjelwa, Mbeya, hawajui MKUKUTA wala MKURABITA, tumeshindwa kuwasaidia vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ndani tunazungumzia Vyuo vya Maendeleo. Vyuo vya Maendeleo vimekwisha, hakuna kitu, kuna magofu tu kule, sio Naliendele, sio Nzovwe hakuna tena vyuo, vyuo havina simu, havina umeme, vile vyenye simu na umeme havina bajeti ya kulipia *bill* za vile vifaa. Kwa hiyo, ili kutuma ujumbe itabidi watu watembee utafikiri wale wanachama wa Al-Qaeda ambao hawatumii simu. Kama unataka kutuma ujumbe unamtuma mtu anatembea kwa mguu au kwa punda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshindwa kuwasaidia vijana katika Taifa hili si tu kwa kubuni mipango, tumeshindwa kuwasaidia vijana hata kwa kuendeleza ile mipango ambayo vijana wamebuni wenyeve ikiwemo sanaa na utamaduni. Bado nchi hii hajatumbwa na sanaa katika kuchangia pato la Taifa. Marekani ambayo tunasema wanatusaidia, takribani asilimia 24 ya uchumi wao unatokana na sanaa na utamaduni na ndiyo maana japokuwa Hollywood ni sehemu ya watu binafsi lakini ukitaka Mmarekani akuchape nenda kachokoze Hollywood kwa sababu anajua asilimia 24 ya uchumi inatoka pale. Sisi tunapiga siasa. Rais anakaa ndani ya Bunge, anasema katika miaka mitano iliyopita nimewasaidia wasanii, wameniomba studio nimewapa, wameniomba nyumba ya kuwekea hiyo studio nimewapa. Waziri anasimama hapa anasema ile nyumba hawajapewa wasanii wamepewa watu ambao wameomba. Sasa inakuwa vipi Serikali inaacha shughuli kubwa inayohusisha kundi kubwa la vijana kama hili inawaachia watu binafsi waiweke mikononi mwao badala ya wao Serikali kuisimamia kupitia vyombo walivyonyavyo kama Wizara ya Utamaduni, kama BASATA, kwa nini wasipewe majukumu ya kuendeleza hii sanaa au la sivyo hii Wizara ifutwe kwa sababu inaonekana kama haina tija, ifutwe tupunguze Wizara. (*Makofi*)

TAARIFA

MWENYEKIDI: Taarifa! Nakuomba Mheshimiwa Mbilinyi ukae.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge ambaye alikuwa amesimama akiongea sio kwamba Wizara ya Utamaduni imekuwa haifanyi kazi zake ipasavyo na kwamba haina mpango wa kuwawezesha wasanii wafanye shughuli mbalimbali za kuendeleza vipaji vyao. Ukweli ni kwamba mikakati ipo, sera zipo na Serikali imejipanga ipasavyo kunyanyua vipaji nya wasanii kwa kuwawezesha kwa kutumia miundombinu mbalimbali na sera mbalimbali ambazo zimekuwa zikiwekwa *from time to time*. Mheshimiwa Mbunge amekuwa akiongelea suala la maombi binafsi ya *NGO* kwa Mheshimiwa Rais na Rais akawajibu wale kuwasaidia sio kwamba hiyo ndiyo mipango halisi ya Serikali lakini Serikali ina mipango yake na mtu yejote anaweza kumwomba Mheshimiwa Rais na akapewa msaada kama vile Mbunge anavyoombwa na wananchi.

MWENYEKITI: Haya!

(*Hapa Mheshimiwa Chuki Abwao alikatiza Kiti*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chiku Abwao siku nyingine usipite katikati yangu na msemaji, lakini Mheshimiwa Mbilinyi endelea.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakataa taarifa yake, pili naomba unifidie muda wangu kwa sababu hiki ni kitu muhimu sana, ndugu yangu pale anakuja hapa kutaka umaarufu wa kisiasa.

MWENYEKITI: Spika akikwambia endelea maana yake hakuna tatizo wewe endelea.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Sijui Baraza jipyaa la Mawaziri limetangazwa lini mpaka yeye aijiibie Wizara inayohusika. Navyojua mimi yeye sio Waziri wala si Naibu Waziri, mimi nafanya kazi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbilinyi sasa kaa. Utaratibu wetu wa kuongea naratibu mimi. Amesema na wala sikusema kitu, maana yake wewe uko sawasawa endelea. Sasa ukianza kumjibu huyo huna sababu, endelea!

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namvunja azma yake ya kutaka umaarufu wa kisiasa, ife hapa.

MWENYEKITI: Hiyo lugha si nzuri, Spika anaposimama, anasikiliza anayeomba taarifa, akikuta kama hakuna sababu, anasema wewe endelea maana uko sahihi lakini sasa ukifanya kumjibu, wewe unatafuta malumbano.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunilinda niendele. Kwa hiyo, naomba kama kweli tunataka kuleta maendeleo na kuondoa hasira kwa vijana, vitu vidogovidogo kama hivi tuviondoe. Unajua vijana wengi

unaposema Dowans, sijui nini, vijana wengi wa mtaani hawaelewi lakini vitu kama hivi vidogovidogo ambavyo wanahusika navyo moja kwa moja tuvishughulikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najua vijana ambaao wamekaa zaidi ya miaka kumi na tano wanasubiri kutoka, wanasubiri kupata nafasi ya kusikika lakini mfumo uliopo, kwa sababu Serikali imeporwa na watu binafsi jukumu la kusimamia na kuendeleza sanaa kama hawa anaowataja Mheshimiwa Mbunge, matokeo yake ndiyo haya. Karibu asilimia tisini ya bajeti ya Wizara iko kwenye uendeshaji, kuna Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, sijui nani Serikali kubwa sana punguzeni hawa watu ili gharama ya mishahara ipungue, hizi hela zipelekwe kwenye miradi mbalimbali kule, hizi hela zipelekwe kwenye ukuzaji wa sanaa kwa sababu sanaa ikitumiwa vyema, utamaduni ukitumiwa vyema kwa maana ya uchongaji, muziki na kila kitu unaweza ukaleta mchango mkubwa sana kwa Taifa hili kwa sababu hapa hata ukimuuliza Waziri wa Fedha, utamaduni unachangia kiasi gani katika pato la Taifa sidhani kama anajua lakini kuna pesa nyingi zinatembea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna siku moja nilikuwa Ubalozi wa Marekani naongea na *Cultural Attaché* wa wakati ule, tukawa tunaongelea masuala ya sanaa Tanzania, wanajua kila kitu wale jamaa, akasema bwana sisi tulikuwa tunaangalia wakati fulani tunaona takribani *cassette empty* laki moja zinaingia kwenye makontena kwa mwezi, lakini wakifutilia *output* wanakuta ni kama 20,000 ndiyo zinazotumika.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Ahsante sana, nitaendelea siku nyingine.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Bunge linarejea

(Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa, tutakaporejea mchana tutakuwa na wasemaji wafuatao. Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mheshimiwa Muhammad Chomboh, Mheshimiwa William Mgimwa na Mheshimiwa Shekifu.

Bahati mbaya tunajaribu kwenda kama mlivyoomba kwa sababu tuko wengi na kwa sababu tunao watu ambaao wanataka kuleta mabadiliko katika mpango huu, kwa hiyo, watapewa nafasi kusudi Waziri aweze kuyasikiliza na kuyatolea maelezo kama yatahitajika.

Sina tangazo lingine, naomba nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji wa Waheshimiwa Wabunge kama wanne, halafu baada ya hapo nitamwita Mheshimiwa Mnyika, awasilishe ile hoja yake ya kuomba kufanya mabadiliko tusikie wote, makaratasi mmepewia. Halafu nitamwita Mheshimiwa Akunaay na yeze pia alikuwa na mapendekozero yaliyoandikwa, atawasilisha. Akishawasilisha, tutakuwa tumewasilisha yale tunayofikiri kwamba yaingie kwenye Mpango. Halafu nitarudi kwenye Kiti hapa, nitamwita mtoe hoja, atajaribu kutoa ufanuzi hapa na pale pamoja na yale mabadiliko, halafu tutakubaliana namna ya kuitisha. Kwa hiyo, sasa hivi tunaingia kwenye Kamati ya Mipango.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mheshimiwa Sara Msafiri Ally!

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mpango ambao ni hoja iliyoko mbele yetu tangu jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kwanza kuishukuru Serikali hasa Tume ya Mipango kwa kuandaa mpango huu vizuri, mpango ambao naamini kabisa una dhamira moja ya kuivusha nchi yetu kutoka kwenye uchumi wa chini na kwenda kwenye uchumi wa kati ambao umelenga kuhakikisha kwamba tunaondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kuishukuru Tume kwa kuandaa mfumo wa utekelezaji wa mpango huu vizuri. Mfumo umelenga kushirikisha sekta ya umma, sekta binafsi, vijana, wanawake, walemaru na umma wa Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu tukiangalia mipango ya nyuma, tutaona kwamba mipango mingi sana ilikwama kwa sababu mingi ililenga kwenye *level* ya Kitaifa, kwa hiyo utakuta kwamba ushirikishwaji wa wananchi moja kwa moja ulikuwa mgumu na miradi mingi iliyoletwa na Serikali ilikufa kwa sababu tu wananchi hawakushirikishwa moja kwa moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii tena kumpongeza sana Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kutekeleza azma yake kwa Watanzania. Aliahidi kwenye hotuba yake ya kwanza ya kufungua Bunge mwaka jana, Novemba 18 kwamba ipo haja ya kurejea utaratibu wetu wa awali wa kuhakikisha kwamba kwenye mipango ya muda mrefu tunakuwa na mipango ya muda mfupi ili kuhakikisha kwamba tunafikia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025. Kwa hiyo, mpango huu ni utekelezaji wa agizo lake na azma yake ambayo alihutubia wananchi kuitia Bunge hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja naomba niende kwenye kipaumbele cha kwanza ambacho kiko katika mpango huu ambacho kinahusu miundombinu. Lakini, naomba nijikite moja kwa moja kwenye sekta ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kipaumbele hiki kuwa cha kwanza kwa sababu tunaamini tangu historia ya hatua ya maendeleo ya binadamu, tunaambiya kwamba binadamu alianza kuhesabika tu kwamba ameanza kupiga hatua ya maendeleo pale tu alipoanza kugundua moto. Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba tukiweza kuimarisha sekta ya nishati hasa umeme, tutakuwa tumeweza kujikita katika kuleta mabadiliko hasa mapinduzi ya kilimo, mapinduzi ya viwanda, ajira ya mtu mmoja mmoja, kuleta amani na utulivu, kupunguza uhalifu wa nchi na kuleta uchumi ambao tunasema uko *stable*. Kwa hiyo, naungana moja kwa moja na Serikali yangu kwa kuona kwamba kipaumbele cha kwanza ambacho tunasema ni *cross-cutting*, kinapita kwenye maendeleo ya aina yoyote ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, napenda kuongelea kuhusu taasisi yenyenye dhamana ambayo tumeipa mamlaka ya kushughulikia umeme, kuzalisha na kusambaza umeme ambayo ni *TANESCO*. Taasisi hii imekuwa ikikumbwa na migogoro mingi. Tumeona kwamba katika shughuli za uzalishaji umeme, taasisi hii ilikuwa inaingiliwa mara kwa mara, kunakuwa na *third party, either* Serikali au sekta yoyote binafsi ambapo tunakuta kwamba tunaingilia watalaan wanaotekeleza shughuli zao za kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea hili kwa sababu utaona kwamba, Wizara ina malengo mengi tu, ina miradi mingi na mikakati mingi ya kuhakikisha kwamba inakomboa nchi yetu kuwa na umeme wa kutosha au nishati ya kutosha. Lakini, utaona kwamba mikataba mingi inayoingiwa kuzalisha umeme, lazima kunakuwa na *third party*. Kwa hiyo, unakuta kwamba watalaan tuliowapa dhamana ya kushughulikia masuala ya umeme wanakuwa pembeni na matokeo yake yanapotoka matatizo *either* ya kutokujibika kuhakikishwa kwamba tunafikia malengo ya kufanikisha kuwepo kwa umeme, inakuwa ngumu kwenye uwajibikaji. Kwa hiyo, naomba kabisa kupitia mpango huu, tuhakikishe kwamba tunaepukana na migogoro hii. Tuwaachie *TANESCO* na tuwaachie na wadau ambao wanataka kuwekeza kwenye suala la nishati. Serikali tujitoe pembeni kwa sababu mamlaka hayo na dhamana hiyo tumeiweka *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona zipo sababu nyingi tu ambazo tunasema kwamba mipango yote inatekelezwa kwa sababu ya kuwa na mtaji. *TANESCO* ni watalaan, *TANESCO* wana mipango mingi ya kuhakikisha umeme unapatikana, lakini tatizo ni mtaji. Mwenye jukumu la kuhakikisha *TANESCO* inapata mtaji ni Serikali. Lakini, vile vile tumefungua milango ya wawekezaji, kama kuna taasisi ina mitaji ya kutosha, waende wakafanye mazungumzo na *TANESCO*, wawekeze, wawakopeshe huo mtaji. Lakini, nachelea kusema kwamba taasisi zingine kwa sababu zina mitaji, zipewe jukumu la kuzalisha umeme. Mwisho wa yote tutakuja kuingia kwenye migogoro mingine kwa sababu hakuna watalaan kwenye hayo maeneo. Tunasikia kwamba mashirika kama *NSSF* yanayohusika na masuala ya mafao, yanataka kuijingiza kwenye masuala ya kuzalisha umeme. Nasema hivi, *NSSF* ichukue mtaji wake, wakaongee na

watalaam ambao ni wadau ambao wanawajibika moja kwa moja na wananchi na Serikali yao, endapo umeme hautapatikana au hali hiyo ikisuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichangie kwenye masuala ya elimu na ajira kwa vijana. Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba kila kijana hawezu kufikia elimu ya Chuo Kikuu. Vijana wengi wataishia kwenye elimu za ufundi stadi ambayo ni VETA. Serikali ya Chama cha Mapinduzi imejitahidi kujenga shule za Kata, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imejitahidi kuweka vyuo ambavyo ni vichache vya VETA. Lakini ukweli utabaki kwamba pamoja na kwamba tuna mkakati wa kuhakikisha elimu inawafikia, lazima tuhakikishe kwamba wanapata utalaam na ujuzi ambao uko VETA. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiangalia kwenye mpango huu kwenye ukurasa wa 145 – 146, utaona kwamba hakuna bajeti iliyotengwa ambayo inaeleza kwamba tutaongeza vyuo vya VETA. Kilichoandikwa pale ni kuhakikisha kwamba tunasaidia kuimarisha vyuo vilivyopo. Vijana tunajua kwamba ni asilimia 60 ambayo ni nguvu kazi ya Taifa, kwa hiyo, tuna wajibu wa kuhakikisha hivi vyuo vinafika kwenye kila Halmashauri ili kuhakikisha vijana wanaomaliza kwenye shule za sekondari wanafaidika na mpango huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni suala la muundo katika kuwafikia vijana. Mpango huu lazima uendane na sera zilizopo kwenye nchi. Sera ya Taifa ya Vijana ya mwaka 2007 inaeleza; kutaundwa Baraza la Vijana, Baraza litakalowakusanya vijana bila kujali itikadi. Huu muundo utaanzia ngazi ya Taifa mpaka ngazi ya Kata. Kama huu muundo ungekuwepo, haya masuala ya mikopo, masuala ya SACCOS tungeweza kuyasimamia kuititia muundo huo ili vijana kule ngazi ya Kata waweze ku-*appeal* kwenye ngazi ya Mkoa na Taifa ili kupata ufanuzi wa utekelezaji wa mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa tunaongea tutahakikisha tunaimarisha vijana, lakini hakuna mfumo sahihi ulioelezwa kwamba vijana watafaidika vipi nchi nzima, au tutabaki kusema kwamba mtu mwenye kisu kikali ndiye atakayekula nyama! Kwamba Mbunge wa eneo lile akiwa *sharp*, vijana wake watafaidika! Kwa hiyo, tuwe na usawa, lazima kuwe na *uniformity*, tuhakikishe kunakuwa na muundo maalum wa kuwafikia vijana wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maoni hayo, nataka nitoe mapendekezo kwamba watalaam waliopo kwenye Idara ya Mipango na Idara mbalimbali wawasadie wananchi hasa Madiwani kutafisiri huu Mpango kwa wananchi wa ngazi ya chini. Mpango umeandikwa kitalaam, mpango ni kitu kingine na mkakati wa utekelezaji ni kitu kingine. Kwa hiyo, lazima tuhakikishe watalaam wanawasaidia wananchi wa ngazi ya chini ili waone wanamiliki huu Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningefurahi sana Madiwani wangu wa Viti Maalum wa Mkao wa Morogoro wawe na uelewa wa pamoja kuhusu huu mpango, wasitofautiane. Madiwani wa Ulanga wawe na uelewa wa pamoja na Madiwani wa Mvomero, Madiwani

wa Morogoro Vijijini, Madiwani wa Morogoro Mjini. Kwa hiyo, nasema kwamba, kuwekwe mkakati maalum ili viongozi wa ngazi ya chini wawe na uelewa wa pamoja, wasije wakatafsiri sivyo! Tumeona hapa Bungeni watu wanavyotofautiana tu, wanaona wengine hawajashirikishwa, wanaona uwakilishi wao hapa hausaidii mpaka wananchi wote tuwe kwenye jumba moja tujadili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, inanipa hofu kwamba kama sisi hatuwezi kuelewa tuwekwe kwenye jumba moja, watu milioni 43, je, Diwani wangu wa Viti Maalum aliyekuwa Kikeo, ana uelewa gani! Kwa hiyo, lazima uwekwe mfumo unaoeleweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile kila mradi uwe na msimamizi wake ili kusaidia uwajibikaji, dakika ya mwisho tujuje tunamkamata nani. Vile vile mradi uwe na muda maalum wa kukamilisha utekelezaji wake, kuwe na *timeframe*. Kama tutakubaliana hapa kila mradi utakaopita baada ya miezi 18, kama ni Kamati za Bunge au kupitia kwa Wabunge wote, ziletwe taarifa, “mradi huu baada ya miezi 18 tulitegemea uwe hatua hii”, ili tuanze kubanana mapema kabla ya kufikia *final*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda niwashukuru vijana wote na nawaomba wote bila itikadi zetu, tuunge mkono Mpango huu. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia kunipa nguvu nikawenza kusimama jioni hii kuchangia mada iliyoko mbele yetu. Lakini pia nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili nami njumuike na wenzangu waliotangulia kuchangia mada hii ambayo imekuja katika kipindi muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutimiza ahadi yake ambayo aliiota wakati alipolihutubia Bunge kwamba anakusudia kuunda Tume hii ya Mpango na ametekeleza ahadi hiyo na hatimaye leo tuko hapa tunajadili mpango huo. Nampongeza pia Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha jana kwa ufasaha kabisa na hatimaye kuanzia jana na leo tumekuwa tukichangia mada hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujikita katika utekelezaji au nitoe muono wangu katika utekelezaji wa mpango huu. Wengi wamechangia, wamejaribu kuboresha, lakini nasema hivi, baada ya hayo yote, kitakachofuatia ni utekelezaji na utekelezaji ndiyo mafanikio ambayo juhudhi yote hiyo iliyotokea au inayoendelea itatupa maslahi au nia halisi hasa iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi, ni wajibu wa kila Mtanzania popote alipo, kuanzia Rais mwenyewe amekwishaonyesha mfano, lakini mpaka mkulima wa kijijini tunapaswa kuwajibika kila mmoja kwa nafasi yake na kila mmoja kwa uwezo wake aliojaliwa na Mwenyezi Mungu ili kutimiza mpango huu kwa maslahi yetu sisi wenyewe. Itakuwa ni ndoto ikiwa katika Mpango kuna kutegeana au ni wa nani au jukumu la nani, hautawenza kufanikiwa. Wenzetu wote tunaowasikia wameendela duniani kote ni kwa ajili

ya ushirikiano na *commitment* na kuweza kujitoa mhanga, hasa kujua kwamba naifanyia nini nchi yangu badala ya kutegemea kwanza nchi yake imfanyie nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango imekwishakuja mingi kama wenzangu waliotangulia walivyoeleza na ni mizuri sana na inaishia *either* katika madawati au watu wengine katika nchi nyingine kutumia mipango yetu na wakafanikiwa. Tatizo hili sugu tunalo Tanzania, tunatakiwa sasa kubadilika na tubadilike kimuono kwamba wakati wa kupanga tu bila utekelezaji haupo, sasa hivi ni utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawapeni falsafa moja ambayo alitoa Kiongozi wa Kwanza wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Marehemu Shehe Abeid Amani Karume. Mheshimiwa yule alitawala kwa miaka nane, lakini alisema hivi: “Tumesoma hatukutambua, tumejifunza tumejua, twendeni”. Nataka mlichukue hilo. *Through theory* hatuna kitu, lakini kwa vitendo tukafanye kinachokusudiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda wa kipindi cha miaka nane alichotawala pale, kuna maendeleo mpaka hivi leo tuna Awamu ya Saba hajawahi kutokea hata Rais mmoja aliyefikia kipindi chake. Tumekwishapanga sana sisi kwenye makaratasi, basi sasa tufanyeni, kwa sababu kwa vitendo ndipo tu tunapoweza kufanya yale tuliyokusudia. Si kwa maneno, wanakuja kuchukua wenzetu makaratasi, tunawatengenezea, hawagharimiki kutafuta Tume ya kutengeneza au kutayarisha mipango, wanakuja kuchukua. Tena cha kushangaza zaidi na sisi tunajisifia, nchi fulani imechukua mpango fulani kutoka hapa kwetu. Leo wanaendelea, hatuna aibu sisi? Inatosha! Ndugu zetu Serikali ambao tumewapa dhamana, sisi tulioko huku, jamani chonde, ni lazima kuwe na *commitment*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna kitu kimoja ambacho nimekiona, vijana wetu ambao wengi sana ndiyo wanategemea mpango huu kwa njia moja au nyingine wautekeleze utekelezaji wake, basi hawana ule muono wa kuwajibika kimtazamo hasa wa kinchi. Ni tofauti na huku nyuma tunakotokea sisi na wengi wenu ninyi Mawaziri mlioko huko mbele, ninyi mliopata matayarisho haya ya kuititia JKT baada ya kumaliza “A” *Level* kabla ya kuingia vyuoni. Mkapata muono na mkajua hasa uzalendo uko wapi. Leo mkajishitukia huko mlipo. Kwa nini mmesahau hivi vitu? Vijana wenu mnategemea nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijana ambao toka anazaliwa ye ye hata kubandika sufuria ya chai inamshinda, amealelewa na *house girl*, amemaliza *A-level*, ameingia *University* hajui hata kufua nguo yake ya ndani, huyo unafikiri anawenza kuitumikia nchi namna gani? Ataandamana, atashawishika kwa kile ambacho anaambiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, turudishe ile na tuwatengeneze vijana wetu kimtazamo, tuwe na mabadiliko ya *mindset* zetu, hatuwezi kutekeleza msimamo huu kama hatukuweza kufanya hivi. Alisema Mheshimiwa Karume kwamba linalowezekana leo lisingoje kesho, tunangoja nini? Twendeni, tutajua huko huko mbele ya safari, hebu

tuchukueni hatua kufanya, kama tumeshindwa tutajua tumeteleza wapi, tuchukue hatua tusiwe tunaishia kwenye makaratasi tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapa tena falsafa nyingine kule kwetu Zanzibar kuna Mji mmoja unaitwa Makunduchi, sisi Wamakunduchi tunasema ‘*kuchupa kwacha*’ maana yake ukiwa uko juu na wewe unataka kuchupa achia nenda chini ukifika utajua nimegaragara, nimetambaa, nimekimbia, lakini unaning’inia na unataka kwenda chini huwezi kufika na huwezi kufanya kitu, twendeni tujiachie tu, tutazame mbele tutakwendaje, tukiishia kwenye makaratasi mpango huu utapita, utakuja mwingine na mwingine na mwingine, kutakuwa hakuna lolote, *story* tu, watakuja wenzetu wachukue, wakatumie, halafu sisi tunajigamba tu wamechukua kutoka kwetu maana yake nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotuponza zaidi sisi Tanzania ni kwa sababu sisi ni matajiri sana, tuna kila kitu. Tunayo ardhi nzuri, bahari, mabonde, maziwa hatuna cha kuhangaika. Wenzetu ambao wanahangaika wana jangwa wanahakikisha wanalitumia wanaligeuza liwe na *fertile* na wanazalisha na kuna hawa wenzetu wa Ulaya wana miezi sita tu ya kuhangaika, miezi sita mingine hawawezi wakalima. Lakini ile rehema aliilotupa Mwenyezi Mungu kila kitu ndiyo kinatulemaza, imekuwa kama mali ya kurithi haina uchungu. Watanzania tunapenda sana starehe, hatutaki kufanya kazi. Leo ukifika barabarani kule Dar es Salaam mitaa yote, kupita Shekilango *Road*, kuanzia Morogoro *Road* mpaka ufikie barabara ya Ali Hassan Mwinyi au Bagamoyo *Road* utakuta pembeni meza za kunywa, watu wanakunywa *full time*, toka Tabata nenda Kinyerezi *all the way* tunalewa tu! Kazi tunafanya saa ngapi? Hatutaki kufanya kazi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nchi gani ninyi mmetembea watu wanafanya namna hii kama siyo Tanzania? Halafu hatuishi kulalamika, nchi hii maskini, Serikali hii itakwendaje? Serikali inaajiri watu kupata mshahara, haiajiri watu kufanya kazi, inawapa kazi watu *just to pay salary*, lakini hatuwajibishi kufanya kazi. Tutaendeleaje? Tufanyeni kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaibana Serikali, Mbunge wa Chama cha Mapinduzi lakini nasikia uchungu sana kuona Serikali ambayo imewekwa na Chama madhubuti, Chama imara, inayumba kwa vitu vya kijinga, jamani tuachenii hii, tuchukue ile misingi ambayo imeweza kutuvusha hapa tulipo. Tumesoma, hatukutambua, tumejifunza tumejua. Kwa kusoma si tunasoma tu hapa? Tunashindana hapa kila mmoja na uelewa wake, hebu twendeni kwenye *field*, si tutaona tulipokosea na tutajisawazisha na tutatekeleza majukumu yetu na mpango huu utafanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali na Watanzania wote tuache kulalamika na tufanye kazi. Hatufanyi kazi, starehe nyingi sana, tunastarehe kiasi cha kushangaza sana halafu tume-*relax*. Vijana wetu ni lazima tuwabadilishe *mindset* zao, ile sheria ya kwamba ni lazima akimaliza *Form Six* kabla hajakwenda Chuo Kikuu waende JKT, wakapate msimamo, wakapate mwelekeo wa nchi inafanyaje, watakuwa na uchungu wa kuweza kufanya kazi. Ndivyo tulivyolelewa na ninyi wengi wenu hapa Mawaziri ndivyo mlivyolelewa. Sijui kwa nini mpango huu ulibadilika. Leo anakuwa

kusimama mtu hapa anasema kwamba, miaka hamsini yote hamna kitu kilichofanyika, nimemaliza Chuo Kikuu tu jana na nimekuwa Mbunge na nimekuwa na gari, Serikali imemsomesha mpaka hapo, bado hajaona kitu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni kosa lenu ninyi kwa sababu ninyi Serikali wenyewe mipango hii hamkumwanda yule na wako wengi sana wako namna ile. Wengi sana wamejaa vyuo vyote, sasa hivi hakuna hata mmoja aliyepita JKT, kwa mpango tuliokuwa nao mnategemea nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti naona nisije nikaharibu mambo. Naunga mkono hoja. (*Kicheko/Makofi*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Spika, ninatumia Kanuni ya 146(1) na (3)(b)

MWENYEKITI: Inasomeka vipi?

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 146(1) inasema: “Mbunge anayeingia kwenye Ukumbi wa Bunge atawajibika kuvala mavazi ambayo ni safi na yenye kukidhi heshima yake, hadhi ya Bunge na utamaduni wa nchi kama ilivyoainishwa na katika Kanuni hii”. Kanuni ya 146(3)(b) inasema: “Kwa Wabunge wanaume:-

(i) Watavaa suti ya Kiafrika au safari ya mikono mirefu au mifupi yenye ukosi au shingo ya mviringo na yenye fulana au bila fulana ndani, ya rangi moja, isiyokuwa na nakshi, pamoja au bila baragashia”.

Mheshimiwa Spika, nimeamua kusimama kwa sababu nimeguswa na Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, jinsi ambavyo ameamua kuvala kwa jioni ya leo. Ukimwangalia utakuta amevaa shati moja juu na chini kavaa suruali ya aina nyingine ambayo ni uvunjifu wa Kanuni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa maana hiyo, naomba mwongozo wako. (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Haya Mheshimiwa tafuta namna ukajirekebishe. Mheshimiwa Machali sipendi kusema usimame tukuone nasema nenda ukajirekebishe. Ndivyo inavyotakiwa, hata mwingine akiona kitu kingine basi anasema. Lakini Machali amesema yeeye anajifunza na anapenda kujifunza. (*Makofi/Kicheko*)

Hapa (Mheshimiwa Moses Machali) alisimama na kutoka Ukumbini

MWENYEKITI: Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mgimwa atafuatiwa na Mheshimiwa Shekifu. Mheshimiwa Mgimwa!

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe. Pili, napenda kumpongeza Waziri kwa kuwasilisha Mpango huu mzuri. Awali ya yote nawapongeza wote walioshiriki kuandaa mpango huu na mimi nina mchango katika maeneo manne.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwanza ni suala la *power generation* yaani umeme kwa mwaka 2015 tumedhamiria kupata megawati 2780, hii ndiyo *target* iliyowekwa ndani ya Mpango. *Target* hii ni nzuri lakini kwa mawazo yangu inabidi tuboreshe. Lengo letu la mwisho siyo *power generation* peke yake, kwa sababu kuna *stage* ya *power generation, transmission* na *distribution*. Tujiulize baada ya kipindi ni Miji midogo mingapi, tuna vijiji vikubwa vingapi ambavyo tayari tutakuwa tumefikisha umeme, siyo kuishia katika *level* ya *power generation* wakati hatuna uhakika tutakuwa tumefikisha kwa walengwa wangapi. Kwa hiyo, *indicators* inabidi tuziboreshe ili mpango huu tuweze kujipima vizuri kama tumewafikishia wananchi au vipi. Hili ni pendeleko langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti jambo la pili, ni suala la *manufacturing Industries*, viwanda vya uzalishaji, nasifu watayarishaji wa mpango huu na Wizara kwamba umelenga katika vipengele muhimu na ni mkakati mzuri umeweka namna ya kuwezesha viwanda hivi vifanye kazi. Kwa maneno yao wanasema *we are building formidable Industrialization* na *export led economic growth*. Wanasema viwanda hivi vitakuwa *agro based industries* na *basic industries*. Haya ni maneno mazito katika masuala ya kuwezesha nchi ianze sasa kuwa *transformed* kwenye uzalishaji kamili badala ya kuwa katika *trade on industrial products and services*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii nina mapendekezo mawili tena juu ya hili. Kwa maoni yangu naona tunatakiwa kuboresha mazingira yatakayotuwezesha kweli kuingia katika *basic industry*. Katika kuboresha huko tunahitaji vile vile kuangalia uwezeshaji wa wawekezaji wa ndani na wawekezaji wa nje, lakini pia tuzingatia kumalizia *regulations* za *PPP* kwa sababu dakika hii *regulations* zile hazijatangazwa au hazijasambazwa. Kwa hiyo, wakati tunaingia katika mpango huu ni lazima hivi vitu vya msingi tuwe tumemaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ni suala la maji. Tunazungumzia mikakati mizuri na naisifu sana mikakati ilivyoelezwa namna tunavyoona tutafanikisha usambazaji wa maji kutoka kwenye miji mpaka *rural areas*. Napendekeza mipango ambayo ilishaamuliwa, mpango huu ni lazima *u-take on board*. Kuna maamuzi kwa mfano, kwamba kila Wilaya kutakuwa na vijiji kumi ambavyo vimeidhinishwa na *World Bank* itatusaidia pamoja na hela za ndani. Mpango huu nikiutazama hauna na kwa hali hiyo tunapofanya bajeti ya mwaka kesho, kuna hatari ya kuruka kutenga fedha kwa ajili ya vijiji hivi kumi kila Wilaya, nasema hivi kwa dhahiri kabisa. Kwa mfano, nikitazama nyumbani ikiwa mpango huu utavichukua hivyo vijiji nitakuwa na uhakika vijiji vyangu katika Jimbo langu la Kalenga Vijijini vya Igangidumu, Isupilo, Lumuli, Mungama, Weru na Itengulinyi vitapata maji kwa sababu tayari vitakuwa ndani ya mpango ambao ulishaidhinishwa. Lakini tukiupitisha huu mpango hivi hivi bila *ku-take on board*

maamuzi mazito ambayo tumeshayafanya huko nyuma kuna hatari ya bajeti mwaka kesho kuruka maamuzi haya ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya nne ni *employment creation*. Mpango umeeleza vizuri kwenye nchi yetu kila mwaka tunakuwa na vijana wapatao laki saba wakiingia katika soko lakini uwezo wa *public sector* ni vijana wasiozidi hamsini elfu. Vilevile kutoka mwaka 2001 mpaka 2007 nchi hii kwa matatizo tumepepunguza umaskini kwa asilimia mbili tu. Yaani kutoka 36 percent 2001 tumefikia 34 percent katika mwaka 2007, hii ni *insignificant* katika haki ya kuweza kuharakisha kupunguza matatizo ya umaskini. Katika hali hii mpango unabainisha kwamba bado tuna *unemployment rate* ya 14.9 au *close to 15 percent* katika nchi. Napendekeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, ni lazima sasa tuboreshe elimu yetu ya sekondari kwa sababu inawezekana hata matatizo ya *unemployment* yanatokana vilevile na *level* ya *quality* ya *output* kutokana na mashule. Kwa hiyo, kwanza tuzingatie kuboresha elimu yetu ya sekondari ili watoto wetu watakapokuwa wanatoka wao wenyewe waweze kuwa tayari kukabiliana na changamoto ndani ya uchumi na namna ya kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naunga mkono hoja ya kujenga Vyuo vya Ufundu. Kwa bahati mbaya Mpango huu haujatamka wazi kwamba utaongeza Vyuo vya ufundi vingapi. Hoja hii ni ya msingi katika kujenga nguvu na uwezo wa vijana wetu wanaotoka mashulenii na watakaokuwa katika harakati za kusaka aidha, nafasi za kuajiriwa au nafasi za kujitegemea wenyewe kwa sababu tutakuwa tumewajengea uwezo. Hili ni lazima wote tuliunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni *Air, Road, Infrastructure* kwa maana ya kuwezesha mawasiliano, tuna maeneo ya uzalishaji ambayo tumeyaa inisha ndani ya Mpango na ili uzalishaji ule uende sambamba kulingana na mpango unavyosema ni lazima tuwe na mawasiliano ya kuaminika. Kwa maana ya *railway line*, barabara na njia za ndege. Kwa mfano, Mkao wa Iringa ni Mkao ambaa kama ilivyo Mikoa minne mikubwa ya *Southern Highland*, ni maalum na ni muhimu katika masuala ya kilimo, misitu, *generation* ya umeme na utalii (Msembe) pamoja na *generation* ya umeme kutoka Liganga na Mchuchuma. Lakini kwa bahati mbaya kama walivyosema wengine, wakati tunatakiwa kuimarisha mawasiliano katika njia za ndege, Kiwanja cha Nduli hakizungumzwi katika Mpango, vile vile Kiwanja cha Njombe hakizungumzwi katika Mpango. Hatuwezi tukaimarisha maendeleo na *taping of resources* katika *area* ile bila kuimarisha mawasiliano haya. Kwa hiyo, naomba katika Mpango huu hivi viwanja viwili viingizwe ili viweze ku-facilitate uwezekano wa *transportation* kwa njia ya *air transport*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine, kuna barabara ambayo inatoka Iringa Mjini, Kalenga mpaka Mbuga za Wanyama, Msembe, mbuga ile ni maarufu sana kwa utalii na sasa hivi inailetea nchi pesa nyingi. Lakini kwa bahati mbaya Mpango huu umeeleza tu kwamba barabara ile imeorodheshwa pamoja na barabara

zitakazotengenezwa. Lakini bahati mbaya ni kwamba tofauti na barabara zingine zilizoainishwa sehemu zingine Mpango umekuwa ukisema kila barabara itatengenezwa kwa kilomita ngapi, lakini barabara hii imetamkwa tu kwamba itatengenezwa, haisemi itatengenezwa kwa kilomita ngapi. Kwa hiyo, ni vizuri kuainisha barabara hii ya Iringa, Kalenga mpaka Mbuga za Wanyama, Msembe ambayo inatuletea fedha nyingi za utalii katika nchi hii. Naomba iainishwe itatengenezwa kwa kiwango gani cha urefu kama zilivyoainishwa barabara zingine zinazoelekea katika maeneo mazito ya utekelezaji wa uchumi katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niseme naunga mkono Mpango huu nikiomba kwamba haya niliyoyapendekeza Waziri anayehusika afikirie namna ya kuuboresha Mpango huu.

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa nimwite msemaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa Shekifu Daffa.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mungu na kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya mwisho. Naamini mengi sana yamekwishachangiwa pengine si vizuri pia nisiposhukuru na kuwapongeza wale wote ambao kwa kweli wamechangia vizuri katika kujadili au kuwasilisha Mpango huu. Kwanza, napenda kumshukuru sana Rais wetu kwa kutekeleza azma yake. Lakini pia kwa jinsi alivyotoa taarifa yake tulipokuwa pale *St. Gasper* na alivyochambua Mpango huu inaonekana ana uelewa wa kutosha na anaelewa kinachotakiwa kuiendesha nchi yetu ifike katika malengo tarajiwaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru Waziri Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, kwa kweli ameuchambua Mpango na jana ametupa maelezo ya kutosha. Mtu ambaye hataki kuelewa ni kwamba hataki tu kuelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutafakari mambo kuna aina mbili, kuna muono na kutafakari kwa hisia hasi na mwingine anaweza kutafakari kwa hisia chanya. Kwa mfumo wetu wa kisiasa, sishangai kwa wale ambao wana mtazamo hasi hata kama wanaona ukweli. Ni kawaida na ndio mchezo unavyotaka. Lakini kwa sisi ambao tunaamini lazima tuwe na mtazamo chanya na ni kweli kwamba Serikali yetu inafanya mambo mema na Mpango huu ni dhahiri utatuvusha katika hatua tunayohitajika kwenda. Sasa nitajikita kwa utaratibu tofauti hasa kwa sababu namalizia kujadili Mpango huu utaendaje ili uweze kupata mafanikio. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waasisi wa nchi hii wamesema ili tuweze kufanikiwa tunahitaji mambo manne; watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Nikijikita katika mchangi huu, watu wengi na wachangiaji wengi wamezungumza asilimia zaidi ya 60 ya Mpango huu utachangiwa na wananchi pamoja na *private sector* yaani watu binafsi kuititia *PPP* au *PPO*. Naamini tunahitaji kutoa elimu ya kutosha ili wananchi waelewe maana ya Mpango huu na jinsi wao watakavyochangia kwa kuibua miradi katika maeneo yao. Miradi ambayo italeta muafaka katika maendeleo yao. Hakuna asiyejua kwamba

katika vipaumbele viliviyotamkwa katika Mpango huu kwa mtu mwenye kuelewa, bila umeme huwezi kuendeleza nchi hii wala huwezi kuleta maendeleo wala kutekeleza Mpango. Vile vile bila Miundombinu, maji, reli na barabara nchi haiwezekani kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mtu anapobisha kwamba hatukuandaa vizuri unataka tuanzie wapi? Maana vipingamizi vyetu nya maendeleo kwa leo hakuna asiyejua kwamba tunalo tatizo la umeme na umeme umerudisha sana maendeleo ya nchi yetu. Hakuna asiyejua kwamba tunahitaji barabara, hakuna asiyejua matatizo ya Reli ya kati, Reli ya TAZARA, Reli ya kwenda Tanga na Arusha, sote tunajua. Sasa ukisema tupange vingine, tupangeje? Huko ni kudhoofisha fikra sahihi za kuiongoza nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naamini Mpango huu utapaswa kutengewa fedha nyangi kwa ajili ya kuelimisha wananchi ili waukulali Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwa haraka haraka, tukija katika ardhi, tatizo kubwa la Mpango ili utekelezeke ni ardhi. Ardhi ni rasilimali ambayo ni muhimu sana. Hivi leo ukimwita mwekezaji yoyote kitu cha kwanza atakuuliza ardhi iko wapi? Upo upungufu mkubwa ambao lazima tuuandae ili kutoa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna *land bank*, leo hujui kama tunataka kulima miwa ni maeneo gani yamewekwa kwa ajili hiyo na kwa ukubwa wa kiasi gani cha ardhi. Kwa hiyo, tunategemea wakulima wadogo wadogo, lakini naamini tukiaboresha hawa na tukichanganya na wakulima wakubwa nchi hii itaondoka katika hali iliyopo na tutaleta uzalishaji wa kutosha katika kilimo. Kwa hiyo, tunahitaji kabisa kuangalia sheria za msingi zinazohusu ardhi. Wawekezaji wengi wana dhamira tofauti na tabia za Watanzania. Kwa bahati mbaya au bahati nzuri sana Watanzania wameandaliwa kisiasa na wameiva, hawataki kuonewa na mazingira ya nchi yetu yanataka hivyo. Kwa hiyo, ni vizuri wawekezaji wakaambiwa, wakaandaliwa na maeneo yakaandaliwa bila kuondoa hadhi ya wananchi wetu na naamini inawezekana. Sasa kwa kufuata sheria na taratibu mbalimbali nina uhakika tutafanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni siasa safi. Nina woga sana katika mazingira ya siasa iliyoko sasa kama tutafanikiwa katika mipango yetu. Wakati sisi tunazungumzia Mpango sahihi na tunaamini ni njia pekee ya kutuvusha hapa tulipo, wengine wanadai tunazungumzia mambo ambayo hayana msingi. Tunasimamishana humu Bungeni tunauliza. Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa kwa heshima sana alisema hivi maandamano ya kila siku yanatusaidia nini? Mmoja akasema wenzetu katika nchi ndogo sana wao badala ya kufanya maandamano mchana wanafanya usiku ili wasisumbue mwelekeo wa kuleta maendeleo. Sisi tunakwenda kuwabembeleza vijana wagome na kwenda kuwaasa wafanye maasi. Tusipoliangalia hili, naogopa sana kwamba, msingi wa siasa yetu hii na mpango huu hautafanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niingie kwenye hili la mwisho ambalo ni uongozi bora. Nasema Serikali iwasimamie. Hawa watu wanaozunguka na kuleta fujo wadhibitiwe. Huo ni ukweli, ni lazima waambiwe, sasa tumefanya uchaguzi umekwisha, Kikwete ndiye Rais, CCM ndio Mtawala na wala si vinginevyo. Hatua zichukuliwe, utawala wa sheria uwepo. Tumefika mahali tumeyumbisha hata Mahakama. Nchi

isipokuwa na vyombo vinavyosimamia haki kwa sababu unaweza tu kufanya jambo ambalo linakiuka misingi ya sheria kwa sababu kuna tatizo la siasa na liko tatizo pia la uongozi ambao pengine ni kuangalia au ni kuleta fujo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo ambayo nimeomba ili tuweke msingi mzuri katika utekelezaji wa Mpango huu ni hayo matatu, watu waandaliwe, sheria sahihi za kulinda ardhi yetu na kupanga maeneo sahihi ya uwekezaji ziandaliwe. Siasa safi za watu kuelewana na kuvumiliana ziwepo, uongozi bora wa kudhibiti maendeleo yaliyopatikana uwepo. Kila mtu ajue kwamba iko Serikali na yule anayeleta fyokofyoko, ashughulikiwe kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine nijielekeze kidogo kwenye Mpango hasa kwa upande wa kilimo. Mpango huu umeandaliwa vizuri na liko eneo ambalo naomba kwa kweli litahusu sana eneo la uwakilishi wangu. Wakulima wadogo wadogo wa mboga pamoja na matunda na hili lilitamkwa wakati Rais alipokuwa anawasilisha mpango huu kwamba ili tuweze kupata mnyumbuliko wa haraka wa kupata fedha za kigeni, ni kuanzisha mpango huu wa mazao ya mboga mboga, maua pamoja na vile vitu ambavyo vinahitajika katika soko. Ninachoamini ni kwamba, tunahitaji maeneo madogo madogo kama Lushoto yaangaliwe katika utaratibu, kwa sababu uko ukosefu wa ardhi, basi ardhi iandaliwe, ipimwe, wananchi wapate hati miliki za asili na waweze kupewa mikopo ili wapate maendeleo. Kwa kufanya hivyo, ndio tutawavusha katika mpango huu. Naomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. Wakorofii wadhibitiwe. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, wale tuliotaka wachangie kwa jumla jumla wameshamalizika, sasa nitaomba Mheshimiwa Mnyika ataanza kuzungumza yale yaliyozunguka hoja yake ya kuleta marekebisho. Halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Mbewe, ye ye pia hakupata nafasi ya kuzungumza kabla, kwa hiyo, ataeleza yale mazingira ya hoja yake. Nimewapa dakika 15 kila mtu ili tuweze kuelewa maudhui ya hoja yao. Halafu Mheshimiwa Akunaay atapewa dakika 10 kwa sababu alipata nafasi ya kuongea. Kwa heshima aanze Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Wadogo siku zote wataonewa tu.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kupendekeza mabadiliko ya msingi kwenye mpango huu wa maendeleo ya miaka mitano. Eneo la kwanza la msingi ambalo lilikuwa linapendekeza kufanya marekebisho au nyongeza ni kifungu namba 2.3.4 kinachozungumzia *Human Capital Development and Social Services*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sura hii ya 2.3.4 mipango mingi ya kutayarisha watalaam wetu katika Taifa imezungumzwa, ni mipango mizuri tu. Lakini ningependa kuzungumzia jambo moja la msingi sana ambalo ningeomba sana Mheshimiwa Waziri na Serikali ione umuhimu wa kuliingiza katika Mpango huu. Tanzania ni sehemu ya utandawazi na kwa kuwa katika sehemu ya utandawazi hatuwezi tukapuuza

yanayoendelea katika nchi nyingine kama kweli tunataka kuwa na ushindani wa Kimataifa, kama tunataka kuwa washindani katika soko la ajira, washindani katika uwekezaji, washindani katika *regional integration* ambazo tumekusudia na tumeingia ni lazima Taifa liandae watalaan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mpango mzuri tu wa kuandaan watalaan wa ndani, lakini ni dhahiri kwamba katika Mataifa mengine wana maeneo mengine ambayo wamebobe na ni lazima kama nchi kama Taifa tujifunze kuiga kwa wenzetu. Mwanafalsafa mmoja wa Kichina alisema unaweza kushindwa kuvumbua lakini usishindwe kuiga. Kwa hiyo, kama tunashindwa kuvumbua katika maeneo mengine tusiwe wazito kuiga kwa wenzetu kwani Mataifa yote makubwa duniani yanafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, ninacholenga kukisema ni kwamba, tuna maeneo ya msingi sana katika Taifa hili ambayo yanaweza kuwa chanzo kikubwa cha kukuza uchumi na yanaweza kuwa chanzo kikubwa cha kukuza ajira, lakini bado hatujawahi na hatujawea kuyafanya kazi kwa kina ili sekta hizo zikawa na tija kwa Taifa letu. Mataifa yote ya Asia ya Kati na Mashariki na Mashariki ya Mbali yalifanya mkakati wa makusudi kabisa ya ku-*identify* vijana wake, wakawapeleka katika Mataifa makubwa ya nchi za Magharibi kwenda kujifunza mambo fulani fulani *strategically*. Mataifa kama *China, Korea, Vietnam, Japan* kwa nyakati tofauti yalipeleka watalaan au vijana wao kwenda kuwasomesha katika *specialist training* na vile vile wakafanya *attachment*. Walivyorudi kwenye Mataifa yao walikuwa ni nyenzo muhimu sana ya ku-*transform* mifumo yao ya kiuchumi, ya kifedha na leo Mataifa hayo dunia nzima inawa-*admire*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna maeneo machache ambayo napendekeza Serikali ione umuhimu sana wa kuyafikiria, kama uvuvi wa bahari. Tunapokuwa tunajadili mpango wa leo tutajadili mambo mbalimbali yanayohusu maendeleo yetu ya leo. Tutajadili changamoto zinazotukabili leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni lazima Bunge lako lielewe kwamba tuna kazi ya kuandaan kizazi cha kesho. Kwa hiyo, tunavyokwenda kujitahidi kupanga mipango ya kufikiria kuvuna mwaka huu lazima tufikirie vile vile tunaandaa vipi kizazi cha kesho, kuvuna miaka 20 na 30 ijayo. Pendekezo langu nikianza na sekta mbalimbali ambazo ni sekta muhimu sana na uvuvi wa bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi wa bahari kuu bado hatujauona kama ni fursa nzuri sana ya maendeleo. Tu- *identify* vijana kwenye shule zetu mapema kabisa tuwapeleke kwenye Mataifa yaliyobobe na ambayo yana uzoefu wa kazi hizi wajifunze mkakati wa makusudi kabisa kuhusu suala la uvuvi wa bahari, ikiwezekana tuwa-*attach* katika Mataifa hayo na makampuni makubwa duniani wajifunze chini ya *sponsorship* ya Serikali hatimaye warejee Tanzania waje wasaidie kuleta *new idea* katika kukuza uchumi wa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *mining*, tunajaribu kufanya *gas exploration*. Tunategemea Mungu akipenda siku za usoni tutakuwa na mafuta. Tumeliandaaje Taifa?

Tulikwenda kwenye *privatization*, tulipokwenda kwenye *privatization* hatukuijiandaa, matokeo yake tumejikuta tunayumba, tumejikuta tunategemea Makampuni makubwa ya Kimataifa yaje yatusaidie sisi kurekebisha uchumi wetu. Hatukuandaa vijana wetu na wenyewe hatukuijiandaa vyakutoshaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vema tujifunze kwa makosa tuliyofanya nyuma ili tuone mbele tunafanya katika kulisaidia Taifa. *Section ya petroleum, section ya gas*, hayo ni maeneo ambayo *training* yake huwezi ukaifanya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa hali ya sasa na huwezi kuifanya katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Lakini pengine siku za baadaye tuwaandae vijana wetu mapema, vijana wabichi, tuwapeleke Mataifa makubwa tuwa-*attach* kwenye *multinational companies* zinazofanya *gas and petroleum exploration* ili hatimaye watakaporudi nchini kwanza watakuwa chachu ya ile *investment*, wanawenza wakawa wabia wa kizalendo katika makampuni hayo kwa sababu wana utalaam huo na vile vile hata kama wataajiriwa na Makampuni hayo makubwa ya Kimataifa wakifanya kazi ndani ya Tanzania watakuwa jicho la Taifa kujua wawekezaji hao wa Kimataifa wanafanya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo katika *mining sector* maeneo muhimu kama *gold mining* tunalamika ni kwa sababu vijana wetu wengi na watalaam wetu wengi wanapewa zile ajira ambazo hazichungulii kule ndani kabisa kuna nini. Ni vema ndugu zangu tuliandae Taifa, *gas* na *petroleum* ni *industry* kubwa sana. Tusijidanganye, Watanzania hatuna ujuzi nayo. Watakuja wageni hapa tutashindwa kuwadhibiti. Tufanye mapema tuandae vijana wetu tusifikirie leo na kesho, tufifikirie miaka 10 mpaka 20 hatutakuwepo kwenye Bunge hili, watoto wetu watatushukuru kwamba tuliwaandalia Taifa lenye watalaam wazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningeomba liingizwe, nina *focus* hapo hapo kwenye *training* kwa sababu kama hatutaingia gharama kufundisha watu wetu na kama hatutafundisha watu wetu *strategically* tutabaki tunalamika. Tutabaki tunawanung'unikia nchi za jirani, tutabaki tunawanung'unia Mataifa makubwa yenye kuleta *multinational* katika nchi hii. Hatuna uwezo wa kudhibiti *multinational*. Enzi za zamani ambako unasema Makampuni makubwa ya Kimataifa yazuwe yasiingie Tanzania, katika utandawazi huwezi kuwazuia. Kama huwezi kuyazuia basi unakula nao sahani moja. Unaandaa watu wako, wanaingia ndani, wanakuwa ni sehemu ya kuwadhibiti hao *multinationals*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo linaweza kuwa chachu kubwa sana ya Taifa tuna *potential* kubwa sana Tanzania ambayo ni *tourism* (utalii). Kwa bahati mbaya sana bado tumejikita sana kwenye kufikiria utalii wa wanyama, utalii wa mlima, utalii wa baharini, lakini utalii ni sekta ambayo ni *multi-sectoral in itself* na ina mambo mengi mno. Juzi nilimsikia ndugu yangu Mheshimiwa Hamad Rashid akizungumza habari ya *Maldives*, mambo ya *sea shores*, mambo ya *Caribbean*, hebu tujiulize leo tumeandaa vipi vijana wetu ku-*invest* katika *tourism*? Tuna *strategic plan* gani katika *tourism*? Inaweza ikawa siyo sehemu maalum ya mpango lakini haya ni mambo ya msingi. Kama Taifa tuache kufikiria leo, tufifikirie kesho na tufifikirie kesho kutwa. Kama

hatukuijandaa kwa makusudi kupitia mipango kama hii hakika siku za usoni zitafika, tutalalamika, tutanung'unika na bado tutakuwa hatujalitendea sana Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nizungumze, huu Mpango ni wa Kitaifa na nimesikia michango ya Waheshimiwa Wabunge wengi wakizungumza kwamba huu mpango unawagusaje katika maeneo yao, lakini niseme tatizo moja kubwa sana, tumelifanya Taifa letu halifikiri, tumejiweka katika utamaduni ambaao tunatengeneza *a consumption economy*, yaani uchumi ambaao unatafunu tu. Matokeo yake unakuta Wilaya nzima inatengeneza bajeti ya mwaka, Wilaya ina Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi, Mwenyekiti wa Halmashauri, Wakuu wa Idara lakini hakuna mpango wowote wa Wilaya wa kuhakikisha angalau basi Wilaya inatengeneza ajira elfu moja kwa mwaka, hakuna, wanasubiri hela itoke TAMISEMI, pesa itoke Serikali kuu wapelekewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima katika mipango yetu, pamoja na mpango wa kutoka juu kwenda chini, lazima tuwe na mipango ya kutoka chini, ni lazima Viongozi wetu katika Mikoa, katika ngazi za Wilaya tuwa-task, tuwajibishe hawa, lazima wawe na mipango ya ndani ya kufufua uchumi, lazima kuwepo kuna *some kind of stimulation* ya *economy from the bottom* ili waanze kuangalia maeneo ambayo wanafikiri wana *comparative advantage*, waweze kuyafanya kazi *ku-invite investors* katika maeneo yao badala ya kusubiri kila kitu kitoke juu na Serikali Kuu itoe maelekezo mahususi *particularly* TAMISEMI itoe maelekezo mahususi kwamba katika ngazi za Halmashauri kuwepo utaratibu wa kuandaa mpango mkakati wa kufufua uchumi na kutoa ajira kwa vijana wetu kwa sababu ni dhahiri kwamba hatuwezi wote tukatoa ajira kuanzia ngazi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niyazungumze hayo yanatosha. Kwa sasa nijikite kwenye hicho kifungu kwa sababu ni jambo la msingi mno kwamba katika *planning* yoyote duniani ni kweli watu wanaweza kuzungumzia *vision 2025*, lakini watu makini zaidi kwenye *planning* *wana-plan 50-75 years*, lakini niombe kuwasilisha nikiamini kwamba mchango wangu utapewa fursa ya kuingizwa katika Mpango kwani kwa kweli pamoja na Mpango kujikita sana katika mipango ya ndani, tujikite katika mipango ya dunia, *we are part of the global village* na kwa sababu ni sehemu ya *global village* tuangalie vilevile wenzetu nje wanachezaje na sisi kama hatuwezi *ku-innovate* basi tujifunze angalau kuiga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, katika hilo ni sekta mbili nyingine muhimu za kufanya *specialised training, international finance* na *ICT*. Masuala ya fedha duniani ni *industry* kubwa na pesa zinahama Mataifa mbalimbali usiku na mchana, ni Watanzania wachache sana wanajua kwamba tuna mabenki katika Taifa ambayo yakifunga biashara hapa fedha inalala Johannesburg, asubuhi inarudishwa hapa, usiku imesha—*trade internationally*. Lakini haya ni mambo ya utandawazi huwezi ukayazuia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana, sasa nimwite Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii ya kuwasilisha mapendekezo ya mabadiliko ya kwenye Mpango kwa mujibu wa Kanuni ya 57 na Kanuni ya 58 ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba yetu, Ibara ya 63, Bunge ndiyo chombo kikuu kwa niaba ya wananchi chenyé wajibu wa kuishauri na kuisimamia Serikali na katika kutekeleza wajibu huu, Ibara ndogo ya (3) inatamka kwamba, kazi mojawapo ni kujadili na kuitisha mipango ya muda mfupi na muda mrefu na huu ndiyo wajibu tulionao mbele hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza kwenye maeneo mahususi ambayo nimewasilisha mabadiliko ambayo nitaomba yazingatiwe kwa mujibu wa Kanuni ya 57 na 58 kwenye hoja iliyo mbele yetu. Kwanza ni eneo ambalo liko ukurasa wa 117 wa nyaraka hii wa mpango wa miaka mitano. Hili ni eneo linalohusu miradi ya maji, sababu ya kuwasilisha mabadiliko haya ni kwamba huko nyuma kumekuwepo na miradi ya maji ikiwemo miradi mbalimbali katika Jimbo ambalo wamenituma kuwawakilisha la Ubungo. Miradi ambayo ilihuisha ulazaji wa mabomba ambayo yanajulikana zaidi kama mabomba ya Wachina, lakini pamoja na mabomba kuwekwa kwa muda mrefu, wananchi wa maeneo mengi sana ukienda King'ong'o, Mbezi, Mavurunza, Makoka na kwingineko. Serikali imetumia pesa nyingi sana ikiwa kiasi kikubwa ni mkopo kutoka Benki ya Dunia, lakini maji hayatoki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa kuna mpango ambao unalenga kuchangia katika kurekebisha kasoro zilizotokea kipindi cha nyuma, lakini mpango wenye kama ukiachwa kama ulivyo utarudia kasoro za kipindi cha nyuma na kasoro kubwa iliyoko kwenye mpango huu ni kwamba ukitazama kwenye hilo jedwali la miradi hii ya maji ya Ruvu juu, Ruvu chini pamoja na ujenzi wa mabwawa Kidunda na visima Kimbiji na Mpera ambayo yangeorgeza vilevile uzalishaji wa maji Dar es Salaam, yamegawanywa rasilimali zake katika kipindi cha miaka mitano. Kwa hiyo, ukianza utekelezaji mpaka utakapokamilika, kitakachotokea ni kama kinachoendelea sasa Ubungo, mradi wa mabomba wa Benki ya Dunia umewekwa, maji hayafiki, mabomba yameanza kuharibika, miundombinu imeanza kuharibiwa kwelikweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nafahamu, ndani ya Baraza la Mawaziri, ndani ya Serikali, baada ya mijadala ya umma na sisi kule Ubungo tulifanya kongamano la wananchi la maji, Serikali ikaamua kwamba miradi hii ya Ruvu juu, Ruvu chini, ujenzi wa bwawa Kidunda na visima vya Kimbiji, Mpera ikamilike kwa ukamilifu wake ifikapo mwaka 2013 na Serikali kwa maana ya Rais akatoa kauli, Waziri wa Maji akatoa kauli hadharani, sasa kilichopo kwenye mpango, kinapingana na Kauli ya Waziri na Rais ya kumaliza miradi hii ifikapo mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu ya mabadiliko kwenye kifungu hiki ili kurekebisha hii hali, rasilimali zilizotengwa hapa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na mwaka wa fedha 2015/2016 zipunguzwe bila kuathiri jumla, zirudishwe nyuma kwenye miaka mitatu ya kwanza na nimewaeleza kwenye mapendekezo ambayo

Wabunge mnayo nakala yake, kiwango cha pesa kinachopaswa kuhamishwa ili miradi ikamilike kwa wakati kuepusha hasara kama iliyoko hivi sasa kutokana na mradi wa mabomba ya Wachina na ili kutimiza kauli ya Rais na Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinyume cha mapendekezo haya ni kutengeneza bomu lingine la wakati la kutumia rasilimali nyingi sana, lakini mradi ukachukua miaka mingi kukamilika, miundombinu ikaanza kuharibiwa kabla hata maji kuanza kupatikana. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge hii ni kauli ya Mheshimiwa Rais, Waziri na Wabunge. Humu kuna Wabunge wa Majimbo mbalimbali ili si kwa ajili ya Jimbo la Ubungo tu, kuna Wabunge wa Mkuranga, Kigamboni, Wabunge wote wa Dar es Salaam na Wabunge wa maeneo mbalimbali ambao wanaamini katika usimamiaji wa kauli hizi kwa ukamilifu wake. Kwenye eneo hili nitaomba niishie hapa nihamie eneo lingine la mabadiliko ninayoyapendekeza. Hili lilikuwa linahusu ukurasa wa 147 kifungu cha A.1.4 ambacho kinahusiana na Kifungu cha 3.4.4 cha Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili liko ukurasa wa 127 ambaao ni kifungu cha A1.2.2 ambacho kinatokana na Kifungu cha 3.4.1.1 cha kuhusiana na kupunguza foleni Dar es Salaam. Kwa mujibu wa Mpango huu, yale mapendekezo ambayo wadau wamekuwa wakiyatoa na tumekuwa tukiyatoa kwa muda mrefu kwamba ili kupunguza foleni Dar es Salaam, lazima kuwekeza sana kwenye barabara za pembezoni. Humu kuna barabara zimeingizwa, mapendekezo yale yamekubalika, barabara ya kutoka Goba mpaka Mbezi, Mbezi Malambo Mawili mpaka Kinyerezi, Changanyikeni kwenda Chuo Kikuu kuititia Msewe na nyinginezo. Kabla sijasema pendekezo mahususi ambalo liko hapa kuhusiana na hii barabara nyingine, niombe tu katika kutekeleza Mpango huu ili jambo liharakishwe kwa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa litalikumba jiji la Dar es Salaam wakati wa utekelezaji wa mradi wa mabasi yaendayo kasi utakapoanza. Barabara ya Morogoro itakapoanza kutengenezewa njia maalum ya mradi wa mabasi yaendayo kasi, foleni ambayo itakuwepo kwenye barabara ya Morogoro, itakuwa ni foleni ya kihistoria kwa sababu barabara ni nyembamba lakini kutaanza *construction pale*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maamuzi ya kujenga barabara za kuchuja magari, barabara ya kutoka *External* kuititia Kilungule mpaka Kimara na nyinginezo inabidi yaharakishwe, naelewa kwamba hizi barabara zote zimeshafanyiwa upembuzi yakinifu, nipendekeze katika utekelezaji tathmini ya fidia ufanyike haraka ili zoezi lifanyike haraka kabla ya kuanza kwa ujenzi wa mabasi yaendayo kasi. Lakini kuna hoja mahususi iko hapa mbele ya barabara hii ambayo naomba iingizwe kwenye *schedule*, barabara ya kutoka Kimara kwenda Mavurunza mpaka Bonyokwa mpaka Segerea. Hii barabara ni muhimu iingizwe kwenye *schedule* hii niliyoisema ya barabara, katika ukurasa wa 127, kuna orodha ya barabara na hii barabara haipo, iingizwe kwa sababu ni ahadi ya Rais ya tarehe 24 Mei 2010 alivyokwenda kutembelea Mavurunza na alisema kwamba barabara hii ndani ya miaka mitano itajengwa kwa kiwango cha lami ili kupunguza foleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa isipokuwepo kwenye mpango wa miaka mitano maana yake ni kwamba hii ahadi itakuwa ni ahadi hewa. Sasa ninachosema tu hapa ni kwamba, wengine wanachambua, wanasema ahadi zote za ujumla za Rais zinafikia takriban trillioni 95, sasa hizi za hapa jumla ni trillioni kama 42 *plus*. Sasa ili kupunguza ule mzigzo wa lawama kwamba kuna ahadi nyingi ambazo haziko kwenye Mpango, naomba kutoa pendekezo hapa kwa mabadiliko kwamba barabara hii ya kutoka Kimara kuititia Bonyokwa mpaka Segerea ambayo itaunganisha Majimbo haya mawili na kupunguza foleni iingizwe kwenye hii orodha kama ambavyo nimewasilisha kwenye jedwali la mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni suala la nishati, Kifungu cha 3.4.1, kuna mambo mengi ambayo tungeweza kuzungumza kuhusu nishati, lakini hapa kuna pendekezo mahususi sana kwenye ukurasa wa 135, kwenye ile miradi ya umeme. Kuna mradi mmoja ambao Mheshimiwa Rais aliuzungumza Bungeni na baadaye aliuzungumza alipotembelea Wizara na baadaye kukatangazwa kuundwa Kamati ya kushughulikia mradi huo, mradi wa *Stigler's Gorge*, lakini mradi huu pamoja na kutangazwa kwamba ndani ya miaka hii mitano utekelezaji wake unaanza, mradi huu kwenye miradi ya umeme inayozungumzwa haupo kwenye orodha ya miradi. Kwa hiyo, mabadiliko ninayoyapendekeza hapa ni kwamba, kwa ajili ya uzalishaji mwingi wa umeme wa Taifa letu na huu ni mradi mkubwa sana utekelezaji wa mradi huu, maandalizi yake ya kirasilimali na kifedha uingizwe ndani ya mpango huu wa miaka mitano ili tuweze kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni ukurasa wa 112, mabadiliko mahususi yanahusiana na uzalishaji, *manufacturing* ya Kifungu 3.4.3, lakini hapa narejea kifungu 1.12, kwanza nashukuru kwamba *concept* ya *Special Economic Zone* imeingizwa kwenye Mpango. Nitaomba tu katika utekelezaji wake huko nyuma tumewahi kuwa na mipango ya kuanzisha viwanda, tukiondoa hivi viwanda ambavyo vina motisha maalum na Ubungo ni moja kati ya maeneo ambayo yalikuwa *industrial area* yaani ukizungumza kuhusu viwanda vya Dar es Salaam unazungumza *UFI*, uzalishaji wa Zana za Kilimo, unazungumza Ubungo Maziwa, uzalishaji wa maziwa, Ubungo *Garment*, Urafiki na kadhalika lakini viwanda vile vingi vimefungwa, vingine vinafanya biashara tofauti, hatimaye watu wanakosa ajira. Sasa wakati tunafufua vile viwanda tumeanzisha mkakati mwagine wa maeneo maalum ya viwanda likiwemo hili la Benjamin Mkapa *Special Economic Zone* lililopo pale Mabibo na kule kuna viwanda vinakusudiwa kuanzishwa. Sasa naomba, vitakapoanzishwa vichangie kwenye ajira lakini tufufue viwanda vile vile vilivyokufa ndani ya Jimbo la Ubungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa kuna hoja mahususi sana ambayo naomba izingatiwe ni sehemu ya 1.1.2 ambapo ndani ya Mpango huu inakusudiwa kama sehemu ya Benjamin William Mkapa *Special Economic Zone* kujenga bomba maalum la mtaro kutoka eneo la viwanda kupeleka kwenye mabwawa ya kumwaga uchafu yaliyoko pale Mabibo yanaitwa Mabibo *oxidization ponds*. Sasa naomba hili pendekezo lizingatiwe, hii hoja ni hoja hatari sana. Kwa sababu kwa mtu anayefahamu jiografia ya Dar es Salaam, mabwawa yale ya Mabibo yameshazusha zogo sana kutokana na uchafuzi wa mazingira usio wa kawaida. Sasa hii ni *waste* ya kawaida tu imezusha zogo, fikiria uwe na eneo la viwanda lenye viwanda zaidi ya kumi, halafu *industrial sewage* ijengewe

bomba lipeleke kwenye mabwawa ambayo yako katikati ya *community* ya watu ni janga litakalokuja kutokea baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa hoja yangu ninayopendekeza hapa ni kwamba, mabadiliko yafanyike kwenye hiki kifungu na nimeandika *text* ya Kiingereza sitasoma kwa Kiingereza iingie kwenye rekodi rasmi kwa sababu ni nyaraka rasmi, lakini hoja yangu ni kwamba huu mtaro wa maji machafu uelekezwe, uungane na *sewage system* inayo-service viwanda badala ya kupelekwa Mabibo *oxidization ponds* na kwa kiwango cha pesa kilichotengwa *technicalities*, tutazungumza baadaye, ni jambo ambalo linawezekana ili kupusha hiyo hatari ya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kwenyewe kuna uchafuzi mkubwa wa mazingira kwenye mto unaoitwa Mto Ubungo pale eneo la Kisiwani kutokana na uchafu wa majitaka kutoka Hosteli za Mabibo kuishia njiani na kumwagwa mtoni badala ya kumwagwa kwenye mabwawa kwa sababu ya huo udhaifu wa mtandao wa *sewage system*. Kwa sasa kama hali iko hivyo, je, itakuwaje kama *industrial waste* ikienda kuelekezwa kwenye eneo kama hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nimalizie rekebisho lililoko kwenye ukurasa wa 146, linahusu kifungu cha...

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, iingie kwenye kumbukumbu rasmi kwa sababu nimeshawasilisha kuhusu Chuo cha Butiama ambacho kipo kwenye hotuba ya Waziri kwamba kitajengwa Chuo cha Butiama, lakini kwenye Mpango wa miaka mitano hakipo. Kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba hicho Chuo nacho kiingizwe kwenye Mpango pamoja na maelezo mengine ambayo nimeyatoa lakini kutokana na Kanuni...

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MHE. MUSTAPH B. AKUNAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hoja inaletwa chini ya Kanuni ya 57(1)(c), hoja inahusu Utawala Bora. Katika ukurasa wa 39 mpango umezungumzia mafanikio yaliyofanywa katika kuboresha taasisi zinahusika na Utawala Bora, lakini katika mustakabali au mkakati wa mpango katika ukurasa wa 49 mpaka 50 mambo ambayo yanahusu jinsi ya kuboresha zaidi taasisi hizo haikuwekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu ukipitishwa unakuwa ni mkataba baina ya wananchi na Serikali yao kwa miaka mitano ijayo. Kwa ajili hiyo, mipango yoyote ya bajeti itakuwa inatazama mpango huo, sasa kitu kikubwa ambacho hakikutazamwa pamoja na nia nzuri ya Mpango kwa kutamka Utawala Bora, lakini kitu kikubwa ambacho kinatawala Utawala Bora hakikutamkwa na kitu hicho ni Katiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshaanza mchakato wa kuandika upya Katiba kwa kuleta Bungeni Muswada wa mchakato huo, lakini ningependeza zaidi au ingefaa zaidi kwa wananchi wake, Serikali ingeweka katika Mpango huu jinsi gani gharama hizo zitapatikana au zionyeshwe wakati wa kupanga mipango ya kila mwaka kwa kipindi chote wakati mchakato wa kuandika Katiba utakapokuwa unafanywa. Sasa hivi mategemeo ya Watanzania wengi ni kwamba, hali yao au haki zao na uhuru wao wa kutoa mawazo au kukuza demokrasia ni kuandika Katiba upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwekezaji, katika Mpango imeandikwa kwamba, mazingira ya kufanya biashara yataboreshwa yaani kwa lugha iliyotumika ni *ku-create condusive environment of doing business*, nayo hiyo ni sehemu itakayohusu kumiliki ardhi na utumikaji wa maliasili zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa japo Katiba haitakuwa imewekwa katika hali yake na hajjawekewa, Bajeti itaendelea, kutakuwa na migogoro mingi. Sasa hivi kuna Waheshimiwa Wabunge wanalamika wakiona kwamba kuna maandamano, kumbe maandamano ni sehemu ya haki za Kikatiba. (*Makofi*)

Kwa hiyo, yote hayo ili kuzuia kusiwe tena na malalamiko juu ya pesa zimekosekana za mchakato wa kuangalia Katiba hiyo iwe pia ni sehemu ya mpango huu. Kuna usemi wa watu wachache kwamba Katiba siyo kipaumbele cha nchi, kipaumbele ni maji, kilimo, lakini kumbe haki ya raia ndiyo kipaumbele kuliko mambo hayo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kutokana na hali hiyo, nimeona kwamba urekebishwe mpango katika ukurasa wa 50 kwa kuongeza maneno katika sehemu ya mkakati au sehemu ya *intervention*, liandikwe neno *national constitution output* yaani matokeo iwe ni *new constitution*. Kwa sababu asubuhi nilizungumzia kwa kirefu naomba nisitumie muda mwingi naishia hapo. Ahsante Mwenyekiti. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Tume hii ya Mipango kwa kuandaa mpango huu, ila nionyeshe masikitiko yangu kwa lugha iliyotumika kuandaa mpango huu wa maendeleo wa miaka mitano. Mpango huu umeandaliwa kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania ni ukweli usiopingika kuwa Watanzania wengi lugha hii ya Kiingereza hawaielewi hivyo basi tungeomba kama kweli tunataka utekelezaji wa mpango huu uwahusishe Watanzania wote tuombe kitolewe kitabu kingine kwa lugha yetu ya Taifa (Kiswahili).

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuwa mpango huu umesahau jambo muhimu sana ambalo nchi yetu imeanza mchakato wake. Mpango huu ultakiwa kuonyesha kwa uzito mkubwa suala la Katiba mpya na tujue utagharimu kiasi gani kukamilisha mchakato huo wa marekebisho ya Katiba, hivyo basi Waziri tunamwomba atupe maelezo ya kina juu ya suala hili la Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umaskini bado, ni tatizo kubwa sana katika nchi yetu hasa kule vijijini hali ni mbaya, ndugu zetu wanaokaa vijijini hata mlo moja kwa siku unakuwa wa shida. Mpango huu umeelekeza vipi kuondoa umaskini huu kwa watu wetu kule vijijini kwa kuwa uchumi wa Taifa unakuwa, ingependeza zaidi kama uchumi wa Watanzania wale wa kawaida uchumi wao ungekuwa kwa pamoja na wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nchi yetu ina tatizo la utawala bora, tunaona Watanzania wanavyonyimwa haki, mahakama zetu bado hazitendi haki kwa watu ambao hawana haki, haki inatolewa kwa wenye fedha, polisi nako ndiyo kubaya zaidi, wananchi wamekuwa wakibambikwa kesi ambazo hazina ushahidi na kufanya familia za watu hawa kuishi kwa shida sana, mpango huu utambue suala la utawala bora ni muhimu sana katika kuleta maendeleo ya nchi yetu, hii itaondoa ule muda unaopotea kwa kukaa magerezani kwa kesi za uongo na muda huo kutumika kwa kufanya kazi za jamii kwa faida ya familia na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nishati bado ni tatizo kubwa ambalo linaendelea kuwa kikwazo kwa Taifa letu la Tanzania, hakuna nchi yoyote ambayo inaweza kuendelea bila umeme, nchi yetu imekuwa kwenye mgao wa umeme kwa muda mrefu na hii imechangia ukuwaji wa umaskini katika nchi yetu. Tuelewe vijana na akinamama wengi wamejajiri katika sekta binafsi na shughuli wanazofanya nyangi zinatumia nishati ya umeme. Hivyo basi tatizo hili la mgao liwaathiri sana Watanzania. Tumechoka kusikia kila siku miradi inayotajwa kuwa inatekelezwa bila mafanikio yoyote. Tunaitaka sasa Wizara husika kutekeleza miradi hiyo ili tuondokane na mgao wa umeme katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la huduma za jamii ningependa kuzungumzia suala la maji, nchi yetu tunakaribia kuadhimisha miaka hamsini ya Uhuru bado Watanzania hawajui au hawajapata maji safi na salama, leo Watanzania wanapata maradhi kwa kunywa maji yasiyo safi na si salama, hii ni aibu kwa Taifa, mpango umeonyesha kuwa utaondoa tatizo hili kwa miaka mine, hivi mipango hii ni ya kweli au tumeandika tu ili kuwapa moyo wananchi waendelee kuishi kwa matumaini. Naomba tuwe na mipango ambayo itatekelezeka kwa wananchi wetu, tunahitaji maji kwa watu wote na hasa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kutoa machache, pia naomba yale yote yaliyoandikwa katika mpango huu yatekelezwe, yasiishie kwenye kitabu tu, tunajua muda na fedha vimetumika kuandaa mpango huu wa maendeleo wa miaka mitano ya Taifa hivyo basi ni muhimu matunda yake yaonekane kwa kuondoa umaskini kwa wananchi wetu wa kawaida na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa 58 hadi 59 ni kuhusu kilimo, mifugo na uvuvi. Utekelezaji ni kwa Serikali , wananchi, sekta binafsi

na washirika katika maendeleo (*development partners*). Mpango haujaeleza kwa uwazi ni kwa namna gani sekta binafsi itawezeshwa kushiriki kikamilifu katika kutekeleza mpango huu. Kwa mfano, katika sekta ya kilimo (mazao, mifugo na uvuvi) ukurasa 58 – 59. Kwenye *strategic interventions* zilizoainishwa kwa asilimia kubwa zitakazotekelezwa na Serikali .

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya sekta binafsi hayaoneshwi wazi kwa kuwa lengo kuu la kukuza uchumi na kupunguza umaskini hususani kwa wakulima, wafugaji na wavuvi ni kuwaongeza thamani mazao na mifugo yao. Ili mazao na mifugo viweze kuongezewa thamani ni lazima kuwepo na viwanda vya kutosha vya kusindika mazao hayo. Hali ilivyo sasa hatuna viwanda vya kutosha, vilivyokuwepo vilibinafsishwa na havifanyi kazi, mfano, viwanda vya kusindika nyama vya *Tanganyika Packers* vya Shinyanga, Mbeya na Dar es Salaam. Wakati Serikali kila wakati inahimiza wafugaji wavune au kupunguza mifugo, sasa kama hakuna viwanda wavezaje kuvuna hiyo mifugo ili waweze kupata bei nzuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi unaosemwa siyo viwanda bali ni machinjio (Ruvu, Shinyanga na Dodoma). Je, bila kiwanda cha kusindika nyama na kuuza na kusafirisha nyama nje ya nchi tunaweza kuinua uchumi? Je, tunaweza kutoka katika umaskini? Kwa kuwa sekta binafsi bado haina uwezo wa kutosha wa kuwekeza katika viwanda vya kusindika mazao, napendekeza Serikali ijenge viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na mifugo na baadaye viwanda hivyo viendeshwe kwa utaratibu wa ubia kati ta Serikali na sekta binafsi. Vilevile Serikali ihakikishe viwanda vilivyobinafsishwa vinafanya kazi zilizotarajiwaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uvuvi kazi zimechanganywa na zilizoonyeshwa ni za mifugo. Je, hii Bajeti ipo sahihi? Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amesaini mpango huu. Je, kuna uwezekano wa kubadilishwa? Na kama upo ni kwa nini mlikimbiza mpango huu kwa Mheshimiwa Rais? *Intervention* ya 5 na 6 katika ukurasa wa 107, *Activity/project* inasema; (5) *regulatory framework of the livestock sector* na (6) *gender mainstreaming in the livestock Industry*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu ya umwagiliaji; mpango wa maendeleo wa miaka mitano (*FYDP*) ukurasa 59 unaonesha kuwa umwagiliaji unapanuka kutoka hekta 330,000 ilivyo sasa hadi kufikia hekta 1,000,000 (2015/2016). Kwenye mpango kunaonesha kuna hekta 330,0000 lakini kwenye matumizi hakuoneshi chanzo cha fedha cha kuendesha mradi huu. Je, pesa za kuendesha huo mradi zimetoka wapi ikiwa hata malipo kwa watumishi hayaonekani kwa mwaka 2009/2010 (ukurasa 220 matumizi ya Serikali ya watumishi ya umma).

Mheshimiwa Mwenyekiti, umwagiliaji ni tija yenye kuleta maendeleo ya kilimo, hivyo kuna haja kuwekeza zaidi kwenye umwagiliaji ili kupambana na tatizo la chakula kwa kuwekeza zaidi, kwani hekta zilizotengwa/tarajiwaa ni ndogo kwa kilimo (1,000,000 – 2015/2016) na pesa zilizotengwa bado ni ndogo kwa miradi mikubwa ambayo imepewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa sekta ya umwagiliaji ingeboreshwa kusingekuwa na haja na kuongeza utegemezi kutoka mazao ya nje kama vile ngano (Rejea Bajeti ya Mheshimiwa Mkulo ukurasa wa 76) kuagizwa nje. Wakati nchi ina utajiri wa kutosha wa kuwa na ardhi nzuri yenye rutuba, mito mingi, maziwa makubwa na madogo, kujenga mabwawa na malambo, maji ardhini na kukinga maji ya mvua na wataalamu ambao Serikali ingeweka juhudi zaidi hili suala lingeisha. Tuwekeze kwenye umwagiliaji kwanza; tatizo ni nini? Hatuwezi kuzalisha ngano ya kutosha? Je, rasilimali watu wasingepata ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafuteni utaratibu mwengine wa kupanga huu mpango ili uwe wa tija kwa nchi. Kutoingizwa kwa mpango wa miaka mitano ya maendeleo (*FYDP*) ikiwa Serikali imehusisha MKUKUTA II pekee kama nyenzo kuu ya kuliwezesha Taifa kufikia dira ya maendeleo ya Taifa 2025, ni wapi ulipo mpango wa miaka mitano (*FYDP*) ambao Mheshimiwa Rais ameidhinisha kuwa wa manufaa zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushindwa kwa Serikali kuwekeza kwenye rasilimali watu, kwani ni sehemu ndogo ya mpango na Bajeti imeelekezwa kwenye elimu na afya ambazo zina msingi mkubwa kwa maendeleo ya Taifa lolote, ukizingatia asilimia mbili zimepelekwa *VETA* sehemu ambayo inaajiri au kujajiri wenyewe kwa kuzalisha wataalamu wasiotegemezi na asilimia nne kwenda Bodi ya Mikopo ambayo ingeweza kujiendesha yenye? Hivyo napendekeza kuongeza au mpango wa kuongeza ujenzi wa vyuo vya *VETA* kujengwa kila Wilaya nchini na kila mkoa kuwa na vyuo vinavyotoa Elimu ya Juu (Vyuo Vikuu) ili kupunguza vijana wanaokosa fursa ya kujunga katika vyuo vingine kwa ajili ya uchache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala yaliyoanishwa ni ya kawaida tu ambayo hakuna tofauti na hali ilivyo sasa ambapo ufutiliaji wa utekelezaji wa majukumu kutokutekelezwa ipasavyo. Mfano, utekelezaji wa programu za maji, afya, miundombinu, kilimo, elimu na kadhalika. Napendekeza Wizara ya TAMISEMI na Wizara husika zisimamie kikamilifu bila kutegeea kuwa programu hiyo ni ya TAMISEMI au Wizara. Kila Wizara iwajibike kufuatalia, sio kupokea taarifa kwa maandishi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. RASHID ALI OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima ya Bunge lako tukufu, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu awali ya yote kwa kuniwezesha kuchangia kwa njia hii ya maandishi kuhusu mpango huu wa maendeleo wa miaka mitano (2011/2012 – 2015/2016).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Kikwete kwa kutangaza rasmi mpango huu wa Kitaifa ambao umebuniwa na Watanzania wenyewe bila wataalam tok Toka nje ya nchi. Pia napenda kusema tujipongeze sisi wenyewe tunaweza!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu maelezo yake yanaeleweka vizuri sana na umesheheni vipaombele vinavyojaa mwelekeo wa kuleta maendeleo ya Taifa letu hasa

ukizingatia mpango umeelekeza kupambana na changamoto kubwa ya kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa 48 hadi 70 umeeleza juu ya mkakati wa mpango huu katika maeneo muhimu. Maeneo hayo ni pamoja na utawala bora, ardhi, nyumba na makazi. miundombinu, nishati, reli, barabara na bandari, *TEHAMA*, kilimo, uvuvi, mifugo na viwanda. Ni mpango rasmi unaoelekeza maendeleo muhimu ya kukuza uchumi wa Taifa letu, lakini changamoto kubwa ni uimara wa usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ijenge mkakati rasmi juu ya suala zima la usimamizi wa utendaji katika ngazi zote kuanzia Taifa hadi vijijini. Mpango huu umeandaliwa vizuri baada ya kuchambua na kunusuru malengo yake, inaonekana sasa Serikali kama ndio msimamizi wa mpango huu wa miaka mitano wa maendeleo. Kwa hiyo, nashauri Serikali mambo yafuatayo, Serikali ione haya kuwabana na kuwachukulia hatua wale wote watakaoonekana kukwamisha mpango huu katika kutekeleza mpango, aidha, kwa uzembe au ubadhilifu na ni katika sekta zote kwenye utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi ndio wadau muhimu katika kushiriki kwenye shughuli nzima za maendeleo yao, kwa hiyo, kuna haja ya kushirikishwa ndani ya mpango tangu mwanzo hadi mwisho katika kutekeleza azma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naunga mkono hoja hii, Watanzania tunaweza.

MHE. NAOMI A. M. KAIHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kutoa mchango wangu kuhusu mpango huu wa maendeleo. Naomba nitambue umuhimu wa mpango huu kwa Taifa letu la Tanzania. Kwa kutambua ukweli wa faida za mpango makini kwa vile kinyume chake ni kupanga kushindwa. Mfano, mpango huu ulikiuka taratibu za uwazi (*transparency*) na ushirikishi. Badala ya kutekeleza mambo inayoyatamka na kuandika kwa vitendo inafanya kinyume chake. Katika kusoma na kutafakari mpango huu, nimeona nitoe mchango kwenye maeneo yafuatayo, kwanza maeneo ya kipaumbele ni rasilimali watu, viwanda, kilimo na ustawi wa jamii na huduma za jamiii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali watu ni muhimu sana kwa maendeleo ya watu wenyewe na nchi. Lakini mpango uwasisitize kuongeza udahili wa wanafunzi wa vyuo vya juu, badala ya kujenga misingi imara kuanzia shule za awali na msingi na zitoe elimu bora au elimu muafaka, kiasi kwamba wanafunzi wanapofika huko juu wanakuwa hawana msingi mzuri wa elimu. Huko vyuoni wanazingatia zaidi kusoma” *literacy* badala ya elimu/taarifa/maarifa na ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango ungeweza kuweka msisitizo zaidi katika kuweka fedha kwa ajili ya kutengeneza mitaala inayoendana na mazingira yao. Mfano, nchi inategemea kilimo lakini vyuo vya kilimo ni vichache sana au sawa sawa na hakuna kwani hata vilivyokuwepo vimeshakufa kifo cha mende. Vyuo vya Uvuvi navyo ni

vilevile lakini bayo zaidi mpango haujazingatia kuwa na wataalamu Vyuo vya Madini utaona kuwa nchi ina rasilimali kubwa ya madini ambayo yangetosha kabisa katika kuiondoa nchi katika dimbwi la umaskini mkubwa ili kupata wataalamu wa kuingia katika migodi ambayo sasa imedhibitiwa na wageni tu hivyo wanajifanya watakacho na kutuobia mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango pia haujazingatia kuweka fedha kwa ajili ya kuwabakiza (*rentantion*) wataalam tokna ndani na nje. Tunapaswa pia kuweka fedha kwa ajili ya kuwavutia kwa makusudi wataalamu walioko nje na waliokimbia nchi kwa kutafuta *green pasture* (maisha bora) huko nchi za wenzetu. Nchini tunazungumzia uhaba wa wataalamu kuwa ni wachache na hivyo kuruhusu wawekezaji kuleta wafanyakazi wao kwa kisingizio. Pendekazo ni kuona kuwa mpango unaliangalia hili kwa kuona kuwa vijana wengi tulionao ambao wamemaliza vyuo lakini hawajapatiwa ajira Serikali ni huenda kwa vile kama nivyoelezea huko mwanzo kuwa hawapati elimu inayoendana na mazingira yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia zaidi juu ya viwanda kwa kifupi ni kuwa fungu la *Nkaka Coal Mine*, Mchuchuma fedha iwekwe wazi na kuomba umeme. Mimi niko kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara, tumeona kuwa Shirika la *NDC* ikiwezesha vizuri kama ilivyoomba itaweza kutoa umeme katika mwaka mmoja kuanzia *megawatt 600* hii ni zaidi ya pesa tunazowapa wawekezaji. Sasa sioni kwa nini tukazanie kuwapa wawekezaji wakati wataalamu wetu wenyewe wanawenza kututoa katika utegemezi tuzinduke, tuachane na ujisadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwajibikaji ni mdogo sana kwa vile uadibishaji wa watendaji na viongozi katika ngazi zote. Jambo linalotakiwa katika mpango ingefaa kuwa utawala bora kwa kuzingatia kupongeza au kukaripia. Lakini katika mpango huu haijaonyesha fedha kiasi gani zitapatikana kutohana na mpango wa kuwatoza faini kuwafilisi wale wote ambao wanabainika kuwa kwa njia fulani fulani wameliingiza Taifa katika gharama zisizohitajika. Inabidi mkakati huu juu ya suala la kufilisi mafisadi ungepewa kipaumbele ili kukomesha ujisadi. Kwa mtindo huu tungeweza kujenga uwajibikaji na kulinda rasilimali za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo kwenye mpango limetungiwa ngonjera tu. Nasema hivi kwa vile katika mpango huu sijaona utaratibu mahsuswa wa utekelezaji hadi kufikia kule chini kwa wananchi hasa kwa kuwafikia wanawake ambao hawana fursa ya kufikia mikopo hiyo. Kilimo kiwe ni kipenyo cha kuondoa umaskini kwa wanawake lakini kwa kuwawekea miundombinu safi kwa kutumia (*civil society*) Mashirika yasiyo ya Kiserikali ambayo yana uwezo wa kuwafikia kama vile mashirika ya dini ambayo watu wengi wanashiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashukuru iwapo maoni yangu yatazingatiwa katika kuboresha mpango huu. Naomba kuwasilisha.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Lamadi (Mwanza) – Bariadi (Simiyu) – Mwanduya (Kisesa) – Mwanhuzi – Sibitu –

Nduguti – Iguguti – Iguguno – Singida – Mbulu – Babati – Arusha. Barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami kwa kuwa inatoa fursa kubwa kiuchumi na shughuli za jamii inaunganisha mkoa wa Mara, Mwanza, Simiyu, Singida na Arusha. Maeneo yenye rasilimali nyingi kama samaki, pamba, madini, mifugo, viazi na vitunguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii iingizwe katika mpango wa maendeleo ya miaka mitano (2011/2012 – 2015/2016).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja za mpango huu kuwa mwaka 2011/2012 uwe ni muda wa mpito na utekelezaji wa mpango uwe 2012/2013 na vipaumbele vya mpango na mapendekezo ya rasilimali zinazohitajika kwa utekelezaji wa mpango. Kuna mtaalam alisema naomba kutopanga na kupanga kufeli, nami naipongea sana Serikali kukubali kutofeli na ndio maana imetuletea mpango. Hivyo ni wajibu wetu kuunga mkono na kuboresha pale inapobidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri maeneo ya changamoto kuanzia ukurasa wa 10. Kwanza nipongeze kwa kuzijua changamoto hizi maana kujua tatizo ni mwanzo wa kutatua tatizo.

(i) Ukuaji wa uchumi ni mdogo, nashauri tutenge maeneo ya masoko kila kata, kila kijiji ili kuongeza mizunguko ya fedha vijijini.

(ii) Wizara ishirikiane na Wizara zingine na sekta binafsi kuongeza fursa za shughuli za uchumi na biashara na tunaposema biashara rasmi za Kimataifa tuanze na biashara za ndani *automatically* zitaenda Kimataifa. Mfano, mazao tuna soko la *EAC* lakini tuanze na masomo yetu vijijini Ilula - nyanya, Njombe - viazi masoko yawe rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu mzuri sana nashauri uwe *adopted* (uhaulishwe) kila halmashauri (*Local Government Authorities*) ili twende pamoja. Kila Idara ichukue eneo lake na iweke mikakati hii ya Idara katika utekelezaji. Nipongeze mpango huu kujikita katika Wizara, wakala na *LGA'S* na ushirikishaji wa *PPP*. Pamoja na mfumo mzuri sana wa utekelezaji aidha suala la muda (*frame work*) lazima lizingatiwe na tathmini ifanyike katika muda uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya tunaweza (*can do spirit*) ni nzuri lakini lazima ianze chini ili Bajeti yetu ya Taifa isiwe tegemezi, ni muhimu kutafakari kuanzia chini yaani *LGA* zisiwe tegemezi/vijiji visiwe tegemezi/mkoa usiwe tegemezi na baadae Taifa. Hivyo suala zima la kuongeza masoko na *export* ni lazima litiliwe mkazo mahsusii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vijana, nipongeze sana mpango huu kutambua kundi hili la vijana kwanza kabisa wanahitaji elimu. Stadi za maisha hivyo vyuo vya ufundi lazima vitiliwe mkazo na kusambazwa nchi nzima kama tulivyosema sekondari kila kata hivyo kila wilaya itenye eneo na sisi Ludewa tumejenga eneo Shaurimoyo. Aidha, taasisi za fedha zipunguze sana riba hususan katika mikopo midogo ya vijana na

wanawake kwani riba ya mfanyabishara inafanana kabisa na mlemavu na mjane, makundi haya yaangaliwe sana na mabenki yetu mara wanapoomba leseni za biashara. Nipongeze sasa suala la kila mtaa/kila kijiji kiwe na mpango huu na hata kila kaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango iwe na uhusiano wa karibu na maafisa mipango Wilayani na katika wakala za Serikali. Aidha, Tume ipewe uwezo wa kifedha (*non tax revenue*) na wataalamu zaidi. Mipango iliyopangwa ipewe kipaumbele, yapo maeneo muhimu sana nchini ambayo sote tunakiri ni muhimu, bado haijachukua nafasi. Mfano, Mchuchuma na Liganga. Maeneo mengi nyeti yametajwa hivyo maeneo hayo yawekewe *strategic working plan*, mfano, Mchuchuma na Liganga ufanyiwe *monitoring and evaluation*, mfano viwanda vya chama vitatumia madini ya chuma kutoka Mchuchuma na Liganga. Aidha, Serikali iweke *database* ya wadau wa kushirikiana nao katika kila sekta *PPP*. Mfano, wadau na taasisi za kilimo/Mchuchuma na Liganga na vigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi ya haraka ni muhimu sana katika suala zima la mpango. Naunga mkono hoja.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mchango wangu kuhusu mpango wa maendeleo kama ifuatavyo; kilimo kwa kuwa sekta hii ndiyo yenyenye ajira nyingi kwa vijana na wananchi wengi vijijini. Ili kutekeleza mpango huu kwa ufanisi zaidi nashauri Serikali itoe matrekta kwa wananchi bure ili walimiwe mashamba yote pamoja na yale ambayo hushindwa kulima kwa kukosa uwezo wa kutosha. Serikali itoe matrekta katika kila kijiji ili tuongeze uzalishaji kwa ajili ya matumizi yetu majumbani na pia kuongeza mauzo kwa ajili ya matumizi ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo Serikali itatoa *stimulus package* kwa wakulima, hakika mpango huu utaleta tija kwa kutoa ajira na kuboresha maisha ya Watanzania wote. "Kupanga ni kuchagua," Mwalimu Julius K. Nyerere.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mpango mzuri wa maendeleo wa miaka mitano sijaona mpango kabambe wa ujenzi wa barabara ya kutoka Lamadi (Mwanza) – Bariadi (Simiyu) – Mwandoya (Kisesa) – Mwanhuzi (Meatu) kisha inagawanyika kulia na kushoto ambazo ni Mbulu – Babati hadi Arusha na Sibiti – Nduguti – Iguguno hadi Singida. Barabara hizi tatu zinazogawanyika Mwanhuzi (Meatu) ni muhimu sana kwa maendeleo ya mikoa ya Mwanza, Simiyu, Shinyanga, Singida, Manyara, Arusha na mikoa inayopakana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri kuangalia uwezekana wa kuingiza ujenzi wa barabara hizi kwenye mpango huu mahiri sana wenye lengo la kuwaondoa Watanzania kwenye umaskini. Naomba kuwasilisha.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wadogo (*peasant*) wapate bei nzuri ya mazao yao. Mpango ni mzuri kwa mambo yote yaliyobaki, pembejeo, wagani na kadhalika. Lakini bei za mazao yao ndogo Bukoba tunalima

kahawa. Bei ya kahawa katika soko la dunia ni nzuri. Kati ya soko la dunia na mkulima, kuna milongo mrefu na gharama nyingi ambazo hupunguza fedha anazozipata mkulima. Mamlaka za mazao, vyama vya ushirika, kodi na tuzo mbalimbali na kadhalika, milongo hii ipunguzwe ili mkulima apate bei nzuri. Wakulima waheshimiwe ili tuongeze uzalishaji na hivyo tuboreshe uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wakubwa wazidi kuhamasishwa na kuhimizwa kuboresha kilimo kikubwa (*estates*) kwani kinasaidia sana uchumi wetu. Hata mtu anayeajiriwa katika mashamba haya, anaweza kupata ujira mkubwa kuliko kipato anachowezza kupata akilima mweyewe kilimo kidogo (*peasant*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ndio msingi wa maendeleo wa Taifa lolote. Serikali inafanya vizuri katika sekta ya elimu, shule na vyuo vinaongezeka, walimu na vifaa vinaongezeka. Lakini tuongeze jitihada walimu waboreshewe maslahi, hasa wale waliopo vijijini katika shule za msingi na sekondari, mishahara iongezwe na pia wajengewe nyumba za kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishati ya umeme ni muhimu sana kwa maendeleo. Serikali na *REA* inafanya vizuri katika umeme. Tuna matatizo ya upungufu wa umeme kwa sababu tunauhitaji na kuutumia sana. Tuongeze jitihada kuuzalisha na kuusambaza. Hivi sasa Bukoba tuna mradi mkubwa wa kupeleka umeme katika vijiji vingi katika kata kumi za Kemondo, Katerero, Ibwere, Buterembuzi, Rubala, Izimbya, Mupajwala, Nyakibimbili, Kaibanja na Katoro. Kisichokuwepo ni kuwawezesha wananchi waingize umeme katika nyumba zao, kuna mpango mahsus kusaidia hili.

Wananchi wengi hawana uwezo wa kugharamia kuingiza umeme majumbani na katika shughuli zao. Umeme unafika juu ya nyumba, lakini watu hawana uwezo wa kuingiza ndani kama tulivyofanya kuanzisha *REA*, tuanzishe mpango wa kuwasaidia watu waingize umeme katika makazi na shughuli zao ili tuchochee maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango ni mzuri, lakini hauna kipaumbele cha kuongeza mapato ya Taifa. Tusipange tu kutumia, tupange pia namna ya kuongeza mapato. Wigo wa kodi ni mdogo, na vyanzo vingine ni haba mpango ujikite katika fursa za kuongeza mapato. Mipango yote iliyoinishwa inahitaji fedha nyingi sana tuziongeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tishio la amani na pasipo na amani hapawezi kuwepo na maendeleo. Kuna watu ambao kazi yao ni kuchochea ghasia na kuhatarisha amani. Mpango uonyeshe namna gani amani isimamie ili mchakato wa maendeleo usikwamishwe na ukosefu wa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ABDALLA HAJI ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuanzisha mpango huu wa miaka mitano. Mpango huu kama utatekelezwa ipasavyo unaweza kutupeleka pahali pazuri kimaendeleo. Naishauri

Serikali juu ya uwajibikaji wa utekelezaji kwa usimamizi madhubuti, kwani hiki ndio kilio cha wananchi wengi juu ya usimamizi na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwe makini juu ya utekelezaji wa mpango huu, miongoni mwa mambo ambayo yanatusaidia ni kuangalia rasilimali tulizonazo nchini ikiwemo bahari. Bahari ina rasilimali ya kutosha ikiwa itaratibiwa ipasavyo. Baharini kuna samaki wa kutosha ambao wanaweza kuchangia Pato la Taifa na kupunguza makali ya ajira kwa vijana. Naishauri Serikali kuwatafuta wawekezaji wa uhakika kuweza kujenga viwanda vya samaki hapa nchini. Wawekezaji hao wawe wale ambao wanapewa leseni ya kuvua bahari kuu kwa kutozwa pesa kidogo wakati wanachokivua ni kingi sana. Mfano, meli iliyokamatwa mwaka jana ni mfano wa hayo. Hivyo Serikali isiruhusu makampuni kuvua na kuondoka, bali wajenge viwanda vyao nchini ili waweze kulipatia faida Taifa ikiwemo kupata ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo chetu kimekuwa cha msimu kutokana na upatikanaji wa mvua. Hatuwezi kuendelea kwa kusubiri mvua ambazo hazina uhakika wa kunyesha kwa wakati. Hivyo naishauri Serikali pamoja na kipaumbele cha Kilimo Kwanza lakini bila maji hatufanikiwi. Hivyo Serikali iwekeze katika upatikanaji wa maji na hasa hasa katika uhifadhi wa maji ya mvua yatakayowasaidia wakulima katika kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele vya mpango vyote vinahitaji mchango mkubwa na wa dhati wa wahandisi tena katika ngazi zote za shahada na utaalamu (*professional, technician level*, na *vocational level* yaani *engineer* (mhandisi), *technician* (fundi mchundo) na *artisan* (fundi stadi)).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufundishaji na uboreshaji wa hudmua unatakiwa kutiliwa maamuzi katika ngazi zote za vyuo vikuu, vyuo vya ufundi na vyuo vya ufundi stadi. Kwa kifupi chuo kikuu na *Technical and Vocational Education Training (TVET)*. Wataalamu hawa watoshe kwa idadi na umakini. Kwa upande wa idadi, Tanzania inao wahandisi 10,200 hadi sasa. Hawa ni wachache na hawatoshi kukidhi haja ya mahitaji ya wahandisi ya nchi katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 34 katika mpango unataja idadi ya wahandisi na wasanifu majengo (*Architects*) 88,000 kuwa ndio lengo la mwaka 2015. Kutokana na idadi iliyoko hivi sasa, uwiano wa wahandisi na wasanifu majengo ni 1:20 (wahandisi wakiwa ndio wengi). Idadi ya 88,000 kama takwimu itakuwa sahihi ikiwa itahusisha wataalamu wa ngazi ya kati (*technicians*). Hata hivyo, iangaliwe upya maana kwa kutumia idadi ya watu (*population*) ya Watanzania, lengo hilo la mwaka 2015 linaweza kuifanya Tanzania ikawa na uwiano sawa na Japan, Uingereza na kadhalika (*engineer: number of people*). Ni lengo kubwa sana, kwa hiyo idadi hiyo ijumuise *technician* ambao wameachwa/wamesahaulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahandisi kufanya kazi kwa kuwasaidia/kushirikiana na *technician* na *artisans* kwa uwiano wa 1:5:25 (*by ILO*) bila kada ya kati, utekelezaji wa miradi ya miundombinu ambayo ni kipaumbele namba moja utakuwa ndoto. Kada ya kati haipo kwa wahandisi pekee. Hata wale wataalamu wa sekta za afya, kilimo, mifugo na kadhalika wanahitaji sana kada ya kati. Kada ya kati itaboreshw sambamba na ile ya awali (*vocational*) kwa mafanikio zaidi. Kwa hiyo, hata katika Bajeti (*allocation*) kada ya kati (*technical education*) isinyimwe gawio kama ilivyo sasa. *Skill development Level* ilianzishwa ikichangiwa zaidi na zaidi na viwanda na migodi na kadhalika katika jitihada za kujiwezesha, wakilenga kupata wafanyakazi katika kada hizi za kati. Kada za kati ndizo ambazo zinazalisha ajira rasmi na isiyo rasmi, kumudu soko la ajira na hata Jumuiya ya Afrika ya Mashariki soko la pamoja na kadhalika, kada hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekerezo langu ni vema kwa manufaa ya nchi hii mgawanyo wa 6% *Development Levy* uwe hivi; *higher education* 3%, *technical education* 1% na *vocational education* 2% badala ya *higher education* 4%, *technical education* 0% na *vocational education* 2%.

Kada ya kati ina uwezo mkubwa zaidi wa kupokea (*absorb*) wahitimu wa shule za msingi na sekondari; hivyo kuondoa vijana mtaani. Mpango uoneshe wazi umuhimu wa kada ya kati katika kila sekta ya kipaumbele na hivyo kuonyesha dira kwa ajili ya Bajeti.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na kupongeza mpango uliowasilishwa mbele ya Bunge lako tukufu kuwa mpango huu umeandaliwa vizuri na utabadili hali ya Watanzania kiuchumi, kijamii na kufikia dhana ya mpango huu ni kuhakikisha kuwa wananchi wengi wa Tanzania wananaufaika na maendeleo yatakayopatikana kutokana na mambo yalioyoko kwenye mpango kama yatakelezwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia maeneo niliyodhamiria naomba niwaombe wadau wote wa mpango huu ambao kwa kweli ni Watanzania wote wabadilike kifikra, na kiutamaduni hasa katika kuthamiji kazi na kuchapa kazi kwa saa za kutosha, tukiamini kuwa neema itapatikana katika nchi hii ikiwa kila mmoja wetu atakuwa na dhamira ya dhati ya kuleta maendeleo na kuutekeleza mpango katika maeneno yanayomhusu kwa nafasi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele vilivyoaninishwa katika mpango naunga mkono na katika vipaumbele hivyo nina mchango ufuatao, kilimo kinakuwa kwa asilimia 4.2% na ni tegemeo la Watanzania wapatao 74% na mchango wa kilimo kwenye pato la Taifa ni 25.3% ya *GDP*. Hii ni changamoto kubwa kwetu sote kuwa eneo linalotegemewa na Watanzania wengi linatoa mchango mdogo katika pato la Taifa, lakini pia ukuaji wake unasuasua na kwa maana nyingine ipo nguvu kazi inayokaa bila kuzalisha, mpango lazima uone changamoto hiyo ili nguvu kazi hiyo iweze kuzalisha. Lakini pia tutazame kwa nini mchango wa kilimo kwa Taifa unakuwa mdogo sana?

Changamoto zingine zinazoikibili sekta ya kilimo ni pamoja na zifuatazo, kwanza, miundombinu duni ya kusaidia kilimo, leo Watanzania wanajishughulisha na

kilimo asilimia zaidi ya 70% wanatumia zana duni za kilimo kama jembe la mkono. Hapa mapinduzi katika kilimo yanaweza kupatikana, ushauri mpango utazame kwa makini ili kuona Watanzania wanaojihusisha na kilimo wanawezeshwa ili wajikomboe na wakomboe Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya mazao ya kilimo siyo za kuaminika hivyo imekuwa ni tatizo kubwa kabisa na ni lazima lipatiwe ufumbuzi. Kupatikana kwa masoko ya kuaminika katika kuimarisha kilimo, nashauri mpango kuwa na mtazamo mpana wa kuangalia namna wakulima watakavyonufaika na kilimo ili pia wanaojihusisha na kilimo wabaki na matumaini ya kazi zao. Hakuna chombo cha kifedha kinachotoa huduma za uhakika kwa wakulima ili waweza kupata mikopo na huduma zingine za kifedha ili kuboresha na kuleta mapinduzi ya kweli katika kilimo, hii ni pamoja na mafunzo yaani gharama za mafunzo kwa mkulima.

Kuhusu kununua zana za kilimo kama matrektu na malori kwa ajili ya kuwahudumia wakulima, maendeleo yasiyotosheleza ya utafiti katika kilimo, tafiti bado hazitoshelezi wingi wa wanaojihusisha katika kilimo hivyo lazima sehemu zinazotoa huduma za kitafiti ziongezeke. Katika kilimo ni kushughulikia kwa kina matatizo yote yanayohusu kilimo kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu mibovu. Kuhusu umeme maandalizi yaliyoainishwa kuwa yataweza kuzalisha umeme wa kutosha ili kufikia *mw* 2780 amba o utaweza kugawanya kwa kupitia njia za umeme zilizoainishwa kupeleka maeneo yaliyolengwa. Nashauri kuwa kwa vile umeme ni muundombinu unaochochea kwa haraka, maendeleo ya watu na nchi, mkakati wa kueneza uzingatie sana maeneo yaliyo nyuma kimaendeleo kama vile jimbo la Nkasi Kusini na uweze pia kufika kama Tanganyika ili kuweza kuvutia wawekezaji kujenga viwanda vya minofu ya samaki ambayo itasaidia sana na vile vile ikaongeza ajira. Ziwa Tanganyika lina rasilimali ambazo zinaweza kuwakomboa wananchi maskini sana mpaka sasa wilaya zingine zinakuwa hazina umeme kumbe maendeleo yanaweza kwenda taratibu na tunaweza kuachana kimaendeleo na inaweza kuleta shida hata ya utangamano wa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango miundombinu ya barabara imeainishwa vizuri namna itakavyoshughulikiwa kumbe ushauri unaotolewa wa hapa ni kugawa rasilimali kwa usawa na kwamba barabara kama za Wilaya ya Nkasi, Wilaya ya Mpakanji kamwe haziwezi kuleta matarajio katika mpango huu. Barabara zinazoenda katika mipaka na maeneo yenye *strategic* katika uchumi Ziwa Tanganyika ni muhimu kwa uchumi lakini halijaunganishwa na barabara nzuri ili samaki, dagaa wanaozalishwa kule mazao hayo yawafikie walaji ili kuimarisha afya pamoja na kuongeza pato la mmoja mmoja. Tume ya Mipango izitambue barabara za Sumbawanga - Kasanga izitambue barabara ya Nkana - Kala izitambue barabara ya Kitosi - Wampembe izitambue na kuziweka kwenye mpango barabara zote zinazoenda kwenye rasilimali hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja vya ndege katika mpango yameainishwa maeneo yatakayoshughulikia lakini sijaona kiwanja cha ndege cha Sumbawanga, huu siyo mgawanyo wa rasilimali za Taifa kwa usawa. Usafiri wa majini katika kupitia

mpango suaona eneo la kuongeza meli ya usafiri katika Ziwa Tanganyika kama ilivyoahidiwa na Rais wetu wakati wa uchaguzi, nashauri meli mpya inunuliwe ili pia wananchi waendelee kuwa na imani kwa viongozi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya awali na msingi imepangwa vizuri lakini unapokuja kwenye sekondari changamoto zinaanza kuongezeka kama ukosefu wa madarasa, walimu, vilevile vifaa vya kufundishia lakini mpango umezingatia kuondoa kero hizo. Elimu ya juu inatakiwa kugawanywa kwa usawa. Katika mikoa ya Rukwa, Katavi, Kigoma hazina shule za juu za kutosha kama vile *high schools* na vyuo vikuu. Tujenge Chuo Kikuu kwenye mikoa hiyo ili tuweze kuwa na mgawanyo unaolingana kila eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya afya yameoneshwa mambo mengi ikiwa ni pamoja na kuainisha changamoto na umependekeza kutoa suluhisho kwa kila changamoto. Nashauri mgawanyo wa usawa uwepo katika afya, mpango lazima uweke mkazo kuanzia maeneo yanayokuwa na shida katika huduma za afya na hasa vijijini, wilaya za pembezoni kama vile Nkasi na hasa katika jimbo la Nkasi Kusini, mfano mama mjamzito aliyeshindwa kujifungua katika kata ya Kala kilometra 152 kutoka makao makuu ya wilaya ambapo hakuna barabara ya uhakika yuko hatarini zaidi kuliko maeneo yenye miundombinu ya usafiri zaidi. Kumbe vituo vya afya vichache nilivyoainishwa vizingatie ugumu wa wananchi kufikia huduma za rufaa ili kuokoa maisha yao. Lazima mgawanyo uzingatie hali halisi ya kijiografia, miundombinu ya barabara na zaidi ya hao kiwango cha umaskini katika maeneo mbalimbali. Kadhalika hospitali za wilaya chache zitakazojengwa kipaumbele kiwe ni hali ya utoaji huduma ulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi yametajwa na kuweka mipango mizuri lakini yapo maeneo yaliyosahaulika sana nayo ni yale ya Mji wa Namanyere hauna kabisa maji miaka 22 ya umri wake wananchi wamepata maji kwenye mfumo rasmi kwa chini ya 16%, hii ni hatari na aibu kwa wasimamizi wa maendeleo.

Naomba na kushauri tuongeze Mji wa Namanyere kuwa na mkakati wa suluhishi mfano lipo andiko la mradi wa maji ambaou ungeweza kutoa suluhisho la msingi na la kudumu kwa Mji wa Namanyere na kwa vijiji zaidi ya 12 vya Kate, Ntalamila, Chonga, Isale, Kitosi, Ntemba, Msilihofu, Ifundwa, Mtapenda, Mkangale, Kipundu na Isunta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia kuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, maeleo yaliyomo katika kitabu cha mpango huu, ni mazuri sana. Vipaumbele vya mpango huu kama nishati ya umeme, usalama wa chakula miundombinu, ukosefu na ajira na mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nishati ya umeme, wimbo wa ukosefu wa umeme umechosha katika masikio ya Watanzania, vyanzo vya umeme ni vingi, katika jimbo langu la Ileje upo mkaa wa mawe ambaou Mwenyezi Mungu alitupatia tangu zama

nyingi zilizopita. Mchuchuma kule Ludewa na sehemu zingine, tunaotoka maeneo haya tutaenda kuwaambia wapinge kwa kuwa katika mpango huu rasilimali hizi za mkaa zitatumika, ni vema utekelezaji ukawapo au kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa upatikanaji wa mbolea kipitia kwa mawakala liangaliwe upya kwa lengo la kuboresha na kurahisisha upatikanaji wa mbolea. Tufikiriwe pia uwezekano wa kujenga kiwanda kipywa cha mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miundombinu napongeza kuwepo kwa upunguzaji wa msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Kuna wilaya zingine hazina hata barabara moja ya lami, nashauri na kuomba wilaya hizi zipewe kipaumbele katika ujenzi wa barabara. Kama maeneo ambayo Halmashauri hazina vyanzo vya fedha vya kutosha kutengenezea barabara mfano, wilaya ya Ileje ni yenyе milima na mvua nyingi na kufanya barabara nyingi kutakiwa kufanyiwa matengenezo angalau mara mbili kwa mwaka. Nashauri maeneo ya aina hiyo barabara zake zichukuliwe na mkoa. Mfano, barabara ya Ibaba-Katengele hadi Isoko hospitali, barabara ya kutoka Luswisi – Ndapwa Sapanda hadi Mbalizi Mbeya. Hizi zinapaswa kuwa chini ya meneja wa mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mfumuko wa bei, umakini katika sekta ya fedha ni muhimu ili kupunguza mfumuko wa bei. Tuzuie bidhaa zetu kununuliwa kwa dola. Tubadilishe utamaduni wa kufanya kazi, tupunguze muda wa kupumzika. Serikali iangalie upya utamaduni wake wa watu wake na namna ya kufanya kazi.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuwapongeza kwa juhudi kubwa zilizofanyika katika kuandaa mpango huu. Pamoja na pongezi na kwa lengo la kuongeze msisitizo, suala la vipaumbele katika shughuli za viwanda na biashara, ni muhimu sana lipewe jicho la karibu. Nchi zilizoendelea, pamoja na kuwa na tatizo la *global warning* zimeshindwa kabisa kuondoa viwanda na badala yake hutoa msukumo kwetu wa kulinda mazingira na kutosaidia katika maeneo hayo ya viwanda kwani ndio wao hupata soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo langu kuu ninalolitolea msisitizo ni juu ya mradi wa Liganga, Mchuchuma na Ngaka, pia reli yake. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Mnyaa na pia niwaunge mkono kwa kuchagua vipaumbele vichache kwanza ili kuongeza pato la Taifa. Mradi huu ni mkombozi kwa Taifa letu. Juzi tulivyoenda Angola tulitembelea bandari ya Lobito iliyopo jimbo la Banguela, tumeona kazi kubwa sana. Hakika kupanga ni kuchagua. Reli ile na bandari ikikamiliika itatoa ajira kubwa kwa watu wa Angola, na pia pato lao litaongezeka sana. Lakini wakati huo huo nina imani Zambia kutegemea tena Bandar ya Dar es Salaam kuna reli yetu ya *TAZARA* huenda ikawa *bye bye*. Maana waliteta wakesema; “Afadhali bwana tuachane na hao Watanzania, kwanza migomo kila siku.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Waziri wetu wa Uchukuzi na pia wa viwanda na biashara wawatembelee wenzetu wa Angola eneo hilo na pia *NDC*. Mpango umetajwa

kwa kiasi miradi hii ya Liganga, Mchuchuma na Ngeka, naomba ipewe uzito mkubwa na pesa za kutosha ziwekezwe kwenye Bajeti zetu tu kwanza ni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili tuombe msongamano wa kuboresha Dar es Salaam. Hiyo itewezekana tu kwa kuandaa maeneo mengine ya biashara na hivi kuwezesha kupata sehemu za uwekezaji *EPZA/SEZ* tukianzia na Bagamoyo ipewe pesa za kutosha, pia wananchi walioachia maeneo yao walipwe fidia zao ili kuondoa manung'unico. Bajeti iliyotengwa ni kidogo sana, tafadhalii kama ambayo ilijitokeza wakati wa kujadili Bajeti yetu, ni vema hizo ziongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu nchi yetu imepiga hatua kubwa katika kutoa elimu na sasa tuna watu wengi wa kufanya kazi, ikiwemo kutengeneza ajira zao na kuajjiri wenzao. Lakini hiyo itawezekana tu pale *SIDO* itakapowezeshwa kuondoa mitaa ya biashara/kazi ikiwemo viwanda vidogo. Lakini pia mitaa hiyo itasaidia kuzitambua rasmi shughuli na hivyo kuziandikisha na kuwezesha kulipa kodi. Wajasiriamali nao wataweza kuendelezwa na wao wenye kwa walimu wanategemeana, lakini pia hata kukopeshana pesa na bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Wamachinga wengi wanafanya biashara za watu ikiwemo za wageni bila kulipa kodi na hakuna njia nyepesi ya kuwapata. Amepanga mfanyakiaishara mmoja, lakini ndani kuna biashara chungu mbovu hivyo basi ni muhimu sana Wizara ya Viwanda na Biashara ipewe kipaumbele ili kuwezesha biashara na ajira zinazopatikana kulipa kodi stahiki kufuatia uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali kwenye barabara na kilimo ama sivyo itakuwa ni sawa na kuotesha mazao na yakikomaa kutokuvuna. Kwa suala la ajira, hasa kwa vijana, pamoja na kuwezesha kulipa mikopo yao, hivi suala la utambulisho wa Taifa umefikia wapi? Kwa nini hatuoni kuwa wanaolipa kodi ni wachache tu ikilinganishwa na watu wanaostahili kulipa kodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hali ya kutokuwa na kitambulisho cha Taifa kinakosesha kutathmini uhalsia wa watu wetu, kwani kuwepo kwa kitambulusho hiki kinaweza kuwa *direct linked tax payers ID* na hiyo pia kuwa ni kigezo cha kudai huduma kama za kiafya, elimu na kadhalika. Vitambulisho vya Taifa ni kikwazo kikubwa. Nchi nyingi zinazo vitambulisho vyake, hata zilizotoka kupigana hivi karibuni, kuna nini? Hivi tutaingia katika *interpretation* na hizo *free movements* wakati hatufahamiani?

Sasa hivi umemtufautisha mtu wa Kenya na Tanzania au Uganda na Tanzania, kwa macho tu? Watu wanakuja, wanasingizia kuoa na wanachukua ardhi, hata hiyo Sheria ya Ardhi haina nguvu peke yake, ni vyema hili jambo lipewe uzito maana inakuwa kana kwamba hata hao wanaoshughulikia vitambulisho wao sio raia. Aidha, hawaoni umuhimu wake au wanahofia pia hawatafaidika au watajulikana kuwa sio raia wa Tanzania na wapo katika nafasi nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunawapokea wakimbizi na kuwakaribisha nchini, wakati Watanzania hatuna vitambulisho, Katiba inawakataza kugombea nyadhifa fulani fulani, hivi umewatofautisha vipi? Jamani tusingojee mpaka waseme wa upande wa pili, hili ni suala muhimu sana kimkakati, kwanza Taifa na Taifa ni watu na rasilimali zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya *SADC* kuhusu *Mtware Corridor* ipo *very slow*, wakazi wa Nyasa - Tanzania ni maskini, biashara na Malawi ifunguliwe. Naunga mkono hoja.

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuendelea kuonyesha dhamira yake ya kuleta maendeleo ya haraka kupitia mpango huu. Aidha, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Stephen Wasira, kwa kuwasilisha mpango huu na Tume ya Mipango kwa matayarisho ya mpango wenyewe. Mpango huu ni utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Tanzania (*TDV*) 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu utakuwa na matokeo yenyе tija iwapo utasimamiwa na kutekeleza vizuri na wahusika wote. Utekelezaji wake utahitaji nidhamu ya hali ya juu na kujituma. Kwa upande wa elimu, Serikali imefanya vizuri sana ukiondoa mapungufu machache, kupitia MMEM na MMES. Hata hivyo kuna umuhimu wa haraka kupatiwa elimu ya kidato cha tano na sita, vinginevyo tatarudia tatizo la mrundikano wa wahitimu wa darasa la saba kama ilivyokuwa mwaka 2004. Kwa bahati mbaya sana hakuna mpango wa maendeleo wa elimu ya juu na vyuo yaani MMEJU. Juhudi za makusudi zifanywe ili kuanzisha mpango huu na kipaumbele kikiwa masomo ya sayansi, teknolojia (ufundi) na *ICT (skilled labour force)* na mitaala (*curriculum*) katika ngazi zote za elimu iangaliwe ili wahitimu wawe na uwezo wa kumudu maisha yao na kutatua kero za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu afya ili kutekeleza mpango wa MMAM na baadhi ya malengo ya milenia (*MDGs*) kuna haja ya kuongeza kasi ya ujenzi wa zahanati. Vituo vya afya, hospitali na kusomesha wataalamu wa kutosha wa ngazi zote za upatikanaji wa dawa. Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Mloganzila (*MUHAS*) uharakishwe kwa kuwaondoa wavamizi wa eneo ukizingatia ya kwamba *South Korea* tayari wapo kusaidia ujenzi wa chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miundombinu Tanzania ina bahati ya kuzungukwa na nchi nane na bandari tatu. Fursa hii itumike vizuri kwa kuimarisha reli, barabara na bandari zetu pamoja na mkongo wa mawasiliano wa Taifa. Kuimarisha reli inayobeba mizigo mingi zaidi utapunguza idadi ya malori barabarani na kufanya barabara zetu zidumu kwa mda mrefu zaidi. Juhudi za makusudi zifanywe kupunguza msongamano Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na kutatua reli ya ubungo.

Pia barabara zinazokwenda makao makuu ya wilaya zijengwe kwa kiwango cha lami kama ilivyoahidiwa Iringa – Kilolo kwa kuzingatia uwezo mkubwa wa kilimo cha mazao, matunda na mboga mboga katika Wilaya za Kilolo, Mufindi na Njombe; viwanja vya ndege Iringa na Njombe vipewe kipaumbele cha kupanuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania wanategemea kilimo kwa maisha yao. Wakulima wengi wameelewa umuhimu wa kutumia mbolea kwa kilimo; lakini mbolea haitoshi. Napongeza jitihada za Serikali

sikivu ya CCM ya kuanza kujenga viwanda vya mbolea nchini; jambo ambalo litapunguza gharama ya mbolea kwa wananchi na matumizi ya vocha yatakuwa si ya lazama. Aidha, uanzishwaji Benki ya Kilimo uharakishwe ili uongeze ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji wa kutosha katika utafiti (*1% GDP*) utaleta msukumo mkubwa wa maendeleo nchini, katika mwaka 2010/2011 Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 30 kwa utafiti, lakini ni kiasi cha shilingi bilioni 5.2 tu ndicho kilichopatikana. Serikali iainishe vizuri utafiti katika mpango huu.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imetengeneza Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa miaka mitano (2011/2012 hadi 2015/2016) ijayo kuanzia sasa na kwa kuwa mpango huu ndiyo mwongozo wa Bajeti zote za Serikali kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi katika kitabu cha mpango chini ya kifungu cha 2.3.4 *Human Development and Social Services* kiwekwe kifungu kipyta kitakachotoa utaratibu kwa Serikali kwa kila mwaka kuwa na programu ya *Strategic Special Training and Attachment Program* katika nchi mahsus ambazo ni mabingwa katika sekta za uvuvi katika bahari kuu, mafuta, gesi, madini na utalii wa kisasa.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hoja na pia nachukua fursa hii kumpongeza Rais Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kutimiza ahadi yake aliyoitao tarehe 18 Novemba, 2010 alipolizindua Bunge hili Tukufu kuwa angeunda Tume ya Mipango, jambo ambalo kalitimiza kwa kumteua Dkt. Philip Mpango kuwa Katibu wa Tume na wajumbe wengine na mpango ukafanyiwa na kuzinduliwa na Rais mwenyewe. Ninaipongeza pia Kamati ya Fedha na Uchumi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda kwa kuupitia mpango na kutoa ushauri. Aidha, nampongeza pia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, mahusiano na Uratibu kwa uwasilishaji wake mahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia nianze kwa kusema kwamba Taifa linapotaka maendeleo ni vema likawa na mipangilio ya namna ya utekelezaji wa masuala mbalimbali yanayohitaji usimamizi maalum. Taifa linapokuwa halina mipango yake ya maendeleo linafanana na mtu anayejenga nyumba yake bila kuwa na ramani ya nyumba anayojenga. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hatua hii nzuri na muhimu katika historia ya Taifa letu. Pamoja na uzuri wa mpango uliletwa mbele yetu, iko haja ya sisi Wabunge na Watanzania kubadili tabia zetu na kuondokana na mazoea ya siku za nyuma ambapo Taifa letu liliwahi kuwa na mipango mizuri ya maendeleo viwanda vilijengwa, mashirika ya umma yalianzishwa, mabenki yakaanzishwa, lakini cha kushangaza ni kwamba mashirika yote haya na viwanda vilikufa kwa wafanyakazi kukosa uzalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tena tunaporejea tena katika utaratibu wa kuwa na Mpango wa Maendeleo wa Taifa linakabiliwa na matatizo lukuki ikiwa ni pamoja na Shirika la Reli, Shirika la Ndege, Meli, *TANESCO* yako katika hali mbaya wakati katika Mataifa ya wenzetu bandari na mashirika niliyotaja hapo juu ndiyo sekta kiongozi katika ukuaji wa uchumi na Mataifa husika. Katika hali kama hii turejee msemo wa wahenga

usemao kutenda kosa si kosa kosa ni kurudia kosa. Tulikosea kuvunja Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977 iliyokuwa imeundwa mwaka 1967 lakini tumeifufua tena baada ya kubaini kuwa tulitenda kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuingiza ubia na wawekezaji katika rasilimali za Taifa hasa madini kupitia Shirika la NDC huu ni mwanzo mzuri. Sasa ni wakati kwa Serikali kuendelea na utaratibu pia wa kimakusudi wa kutumia teknolojia ikibidi toka Mataifa mengine kwani nchi kama India upo utaratibu wa Serikali kuzinunua teknolojia toka nje na kuziingiza nchini ama kwa kuwalipa pesa wataalam waliobobea katika fani mbalimbali na kuzifanya zao. India iliweza kununua teknolojia ya *nuclear* toka Urusi pia teknolojia ya vifaa vyta utafiti wa anga za juu na kurusha *satelite* angani pia Urusi zilipoyumba kiuchumi ilikuwa tayari kwa *cryogenic engines* kwa India jambo lililopingwa vikali na Marekani iliyojitelea kuisaidia Urusi kurekebisha uchumi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siri nyingine ni kuchukua hatua madhubuti ya kuwasomesha Watanzania wenyе vipaji vyta kisayansi katika Mataifa yenye teknolojia hizo za hali ya juu na wahitimu na kufanya kazi kwa vitendo huko nje wanarejea nchini na kuleta teknolojia hapa nchini. Katika hali hii pia zipo sababu za msingi za kuwatumbia vizuri Watanzania walioko nchi za nje kuleta mawazo mapya. Kimsingi Watanzania wanaweza isipokuwa mfumo wetu unatakiwa uendelee kurekebishwa na kuwapa fursa Watanzania kuonyesha vipaji vyao. Tatizo sisi kwa sisi tunashindwa pindi ikitokea kufanya kazi na watu wa nje tumefanya vizuri mbona? Angalia NBC ilipobinafsishwa wafanyakazi wakawa ni wale wale na wengine wakastaa fishwa, baada ya kulipwa haki zao benki inafanya maajabu, angalia CRDB chini ya Dkt. Charles Kimei, NSSF ya Dkt. Ramadhani Dau nimewataja kwa uchache.

Sasa angalia pia TRA ilipopewa nguvu inakusanya mapato kisasa kabisa baada ya kufanyiwa marekebisheso. Kama ikiwezekana TRA, CRDB na NSSF kwa nini isiwezekane TRL, ATCL hatua zichukuliwe za kuwapunguza watumishi katika mashirika haya kwa kuwalipa haki zao watumishi wasiokuwa na lazima na wale watakobakia walipwe vizuri ili wayaone mashirika haya ni yao, waone haya kuyaua na badala yake wajitume kujenga. Inawezekana tutimize wajibu wetu.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia Mpango huu wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa njia ya maandishi. Mpango huu iwapo utatekelezwa kwa vitendo na kwa ufanisi na uwajibikaji na sio kwa maneno tu kubakia vitabuni, utaleta mafanikio makubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanikiwa kuiwezesha reli ya kati kufanya kazi, itakuwa ni hatua moja ya muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Reli ni kiungo muhimu katika sekta ya usafirishaji wa hitaji linalotegemewa na Mikoa mingi na hata nchi jirani ambazo hazina bandari, kwa kusafirisha shehena kubwa za mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango umepangika lakini wasiwasi wangu ni juu ya ufanisi katika utekelezaji kwani uzoefu unaonesha kuna uzembe, ubadhirifu na matamanio binafsi kwa Watendaji wetu hasa wale wa ngazi za Wizara na Taasisi za Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongozi kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kubuni Mpango huu. Mpango huu utatoa dira ya maendeleo katika nchi yetu. *Logic* itumike zaidi kuliko ushabiki katika utekelezaji wa Mpango huu. Msemo wa vijana, bora kuzaliwa mbwa Ulaya kuliko kuzaliwa binadamu Tanzania. Tukiamua tunaweza, sasa tuamue. Umaskini wa kifikra ni hatari na mbaya zaidi kuliko umaskini wa uchumi. Watanzania ni mabingwa kupanga mipango kinadharia lakini utekelezaji wake kivitendo ni *zero*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Mpango huu, hatuna budi kuchukua tahadhari na hatua kali juu ya watu watakaochochea au kuwatia hamasa baadhi ya watu wasifanye kazi au kuwazuia raia wasitekeleze azma ya Mpango huu. Wachukuliwe hatua kali mfano kuhukumiwa vifungo, kufukuzwa kazi, kulipishwa faini pamoja na kuzuiwa hata mishahara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu vifuatavyo vinahitajika katika kutekeleza Mpango huu:-

- (a) Uzalendo na moyo wa dhati wa kuipenda nchi.
- (b) Moyo wa upendo na huruma kwa nchi yetu na wananchi wake.
- (c) Moyo wa kuweka mbele maslahi ya Taifa badala ya ubinafsi, chuki, tamaa ya utajiri, tamaa ya madaraka, roho mbaya na kadhalika.
- (d) Ari ya umoja na mshikamano wa Kitaifa.
- (e) Ari ya kujitoa mhanga kwa kufanya kazi kufa na kupona ili kutetea maslahi ya Taifa letu.
- (f) Kuchagua viongozi wenye dira na maono mbalimbali ya kimaendeleo na si wale wanaoliwazia Taifa hili maovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu kwa kiasi kikubwa utajikita katika vipengele vya kilimo, uwekezaji katika madini, elimu ya ufundi/biashara pamoja na suala la miundombini. Kwanza, bila shaka kilimo bado kitaendelea kushikilia nafasi ya kwanza kumuinua raia maskini wa Tanzania. Mpango huu umelitambua hilo na kusisitiza wazi kuwa bila chakula cha kutosha hatuwezi kupata fikra za kimapinduzi katika nchi

yetu. Tukila na kushiba, tutafikiri zaidi lakini na tahadhari iwepo ya kutosinzia katika fikra.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu uhakikishe unatekeleza yafuatayo katika kilimo:-

- (a) Mkulima anawezeshwaje kukabiliana na changamoto ya mafuriko, ukame, viwavi, mmomonyoko wa udongo, mbegu bora, pembejeo za kazi, mbolea ili aweze kunufaika na nguvu anazozitumia katika sekta hii ya kilimo.
- (b) Mkulima wa Tanzania anawezeshwaje ili baada ya miaka mitano hiyo aweze kujitegemea na kutoa ajira kwa Watanzania wengine.
- (c) Mkulima wa Tanzania atawezeshwaje ili apate soko la uhakika la mazao yake ya chakula/biashara. Hivyo mkulima apate kujuu umuhimu wa kuchangia pato la Taifa kutokana na mazao anayozalisha.
- (d) Mkulima wa Tanzania atawezeshwaje ili aweze kufikiria namna ya kuanzisha viwanda vidogovidogo vya mazao anayozalisha katika vikundi mfano kwanda cha mikate, kiwanda cha juisi, kiwanda cha mvinyo n.k.
- (e) Mkulima atawezeshwaje ili aweze kumiliki ardhi yake mwenyewe iliaweze kuitumia ardhi hiyo kukopea zana za kilimo, mbegu, mbolea n.k.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabenki yawakopeshe wakulima kwa masharti nafuu kwani kwa kufanya hivyo uchumi utakua kwa kiasi kikubwa. Ifahamike wazi kuwa uchumi haukui kwa sababu asilimia 90 ya Watanzania hawakopesheki. Haya yote yatawezekana endapo benki na taasisi nyingine za kifedha zitatanguliza uzalendo kuliko maslahi binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya madini ilete tija kwa Mtanzania wa kawaida. Moja ya matatizo yanayoikabili nchi yetu ni rasilimali na utajiri tulionao kuporwa na wageni kwa mwamvuli wa uwekezaji. Naishauri Serikali ihakikishe kuwa ili sekta ya madini iwanufaishe wananchi yafuatayo yazingatiwe:-

- (a) Mikataba yote mibovu isiyo na manufaa katika nchi yetu irekebishwe.
- (b) Wananchi walipwe fidia halali kwa maeneo yao wanayoyatoa kwa mwekezaji.
- (c) Serikali ihakikishe kuwa inawaendeleza wachimbaji wadogowadogo kwa kuwapatia eneo lao la uchimbaji pamoja na nyenzo za kufanyia kazi.
- (d) Sehemu zote zenye migodi hususani wanavijiji wanaozunguka migodi hiyo wapewe ajira.

(e) Ahadi zinazotolewa na wawekezaji zitekelezwe kwa muda muafaka. Ahadi kama vile maji, umeme, elimu, afya na barabara itekelezwe na ionekane *physically*, kuliko kuwa ya kufikirika.

(f) Kwa kila hatua inayochukuliwa kuhusu mwekezaji na Serikali ni muhimu wananchi wahuishwe.

(g) Wawekezaji wasiwanyanyase wananchi kwa visingizio vyta uwekezaji na muhimu zaidi wafuate sheria na taratibu za nchi bila kuonesha vitendo vyta ubaguzi, rushwa n.k.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila shaka elimu ya ufundi katika kipindi hiki cha Sayansi na Teknolojia, itakuwa ni nyenzo muhimu sana kwa kuwakomboa vijana wengi wasio na ajira. Natolea mfano nchi ya China ambayo sasa inatisha kwa kukua kiuchumi, kwa kiwango kikubwa elimu yako imeegemea katika fani ya ufundi. Manufaa ya elimu ya ufundi katika China yanaonekana wazi, utengenezaji wa vifaa vyta kieletroniki, samani za majumbani, maua, vifaa vyta michezo na watoto ambavyo vina soko dunia nzima na hivyo kuchangia pato kubwa sana la fedha za kigeni katika nchi hiyo. Kwa uhakika zaidi Mpango huu uhakikishe kuwa unatilia sana mkazo wa elimu ya VETA na uhakikishe kuwa kila Wilaya inakuwa na Chuo cha VETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifahamike wazi kuwa mhitimu wa VETA, akihitimu anaingia moja kwa moja kuzalisha ikiwa ana nyenzo za kazi lakini mhitimu wa mfumo rasmi mfano Sekondari na *Universities* akihitimu anasubiri ajira huku akiambiwa uzoefu wa miaka mitano au zaidi na akiajiriwa anasubiri kulipwa mshahara zaidi badala ya kuzalisha. Kwa mantiki hiyo, kama hatutabadilika na kuwekeza zaidi kwenye elimu ya ufundi, kwa hakika elimu yetu itaendelea kuandaa walalamikaji badala ya wazalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na elimu ya VETA pia biashara itiliwe mkazo. Elimu ya biashara ikiwezekana ifundishwe katika ngazi zote za elimu. Mpango huu uhakikishe kuwa unawaandaa wahitimu wetu kujajiri katika biashara kwani fursa nyingi za uchumi zitakuwa zimefunguliwa na hivyo tusitegemee zaidi elimu ya ufundi, pia elimu ya biashara inaweza kutoa nafasi kubwa kwa wasomi kujihusisha na biashara na hivyo kuweza kuchangia kwa kiasi kikubwa pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kuwa tukiamua tutaweza, tuamue sasa. Kwa heshima na taadhima, naunga mkono hoja ya Mpango wa Maendeleo.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuipongeza Serikali kwa hatua ya kuratibu na kuandaa na kuwasilisha Bungeni Mpango huu wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongozi hizo, naomba kutoa ushauri wa kuboresha Mpango huu. Kutokana na ukweli kuwa viwango vyta maendeleo kati ya sehemu moja ya nchi na nyingine kutofautiana, ipo haja sasa ya kuwa na mpango

mahsusini wa kuzisaidia jamii zilizo nyuma au pembezoni kuinua kiwango chao cha maendeleo ili waweze kumudu ushindani wa ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umefika wakati sasa wa kutenganisha mipango ya ufugaji kutoka mipango ya kilimo ili kuainisha zaidi mahitaji mahsusini ya mfugaji na kuziwekea utaratibu wake ili kumwondoa mfugaji wa asili kutoka ufugaji wenye tija ndogo na kumfikisha katika ufugaji wa kisasa wenye miundombinu stahiki na kuongeza tija. Mpango huu ni lazima ubainishe hatua zitakazomwezesha mfugaji wapi pa kupata mbegu bora tofauti na aina ya mifugo aliyonayo sasa, maeneo ya malisho, maji na soko la uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, Dr. Philip I. Mpango, Katibu Mtendaji, Tume ya Mipango, Watendaji wa Ofisi ya Rais, kwa kuandaa rasimu ya Mpango tajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasimu hii ni nzuri sana kwa vile imezingatia vipaumbele muhimu kwa wananchi wote kwa lengo la kuleta maendeleo kwa jamii nzima ya Watanzania, kwa vile changamoto zilizoainishwa zimetafutiwa ufumbuzi wake na jinsi ya kugharamia miradi mbalimbali ya kiuchumi, hata hivyo, nina ushauri kama ifuatavyo:-

- (a) Mchakato wa kurekebisha sheria na taratibu mbalimbali uanzwe mapema ili kuwezesha Mpango kutekelezeka kama ilivyopangwa.
- (b) Maeneo yaye mafupi na sasa vitendo vishike kasi katika utekelezaji wa Mpango.
- (c) Pamoja na kwamba Mpango utatekelezwa na wawekezaji mbalimbali wa ndani na nje, nashauri Serikali iwe na sehemu kubwa ya asilimia katika miradi ya “*Public Utilities*” kama umeme, maji, miundombinu n.k ili Serikali iwe na uzito katika kutoa maamuzi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Mpango imefafanuliwa kuwa mikopo itatumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo tu si vinginevyo. Napongeza kuhusu ufanuzi huu kwa vile kwa kufanya hivyo mikopo husika itakuwa na tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika sana kubaini kuwa ndani ya Mpango umetambua umuhimu wa kuwezesha makundi hatarishi na yasiyojiweza kama watoto, wanawake, watu wenye ulemavu n.k. Nashauri makundi haya yachanganuliwe kinagaubaga (*streamlined*) kwa vile kila kundi lina changamoto zinazozidiana. Hivyo changamoto hizo tofautitofauti zitasaidia kubuni mikakati ya kuzitatua na kupanga rasilimali kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kuwa endapo mpango huu ukitekelezeka kama ilivyopangwa na kila mwananchi akatekeleza wajibu wake, uchumi na maisha ya Watanzania yatakuwa bora ndani ya miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nchi ikitaka kuendelea lazima iwe na vipaumbele, nimeridhishwa sana na vipaumbele vilivyoelekezwa katika kipindi hiki cha miaka mitano, nishati, maji, miundombinu, afya, pamoja na kilimo na uboreshaji wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu na ushauri tupunguze kusema sana, tuelekeze nguvu zetu kwenye matendo. Wataalamu wasaidiwe ili waweze kutekeleza yale ambayo yapo kwenye Mpango na ikionekana mtaalamu kashindwa kutimiza wajibu wake, asihamishwe ila aondolewe kwenye nafasi hii ili dhana nzima ya uwajibikaji iwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana mipango hii ya maendeleo iwe endelevu na iwe inaangalia dhana ya kitaifa badala ya haya maendeleo kuwa yanaelekezwa katika maeneo yaleyale mfano kuna baadhi ya maeneo katika Wilaya ya Mufindi – Mufindi Kaskazini, katika Kata ya Ihanu, Mdaburo, Mpanga Tazala, Ifwagi, Sadani, Ikweha, hakuna maji ya aina yoyote pamoja na umeme lakini kuna uzalishaji mkubwa sana wa chai, mbao, mahindi, maharage na matunda. Pia tatizo la miundombinu mpaka inakuwa taabu kusafirisha malighafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mpango huu wa Maendeleo ya Miaka Mitano.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Tume ya Mipango kwa ubunifu wake juu ya mikakati sahihi ya kutekeleza Dira ya Taifa ya 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uhusiano na Uratibu na uongozi wa Tume ya Mipango kwa kusimamia kwa ukamilifu maandalizi ya Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha maoni juu ya maeneo kadhaa ya mpango huu:-

(a) Mpango umeandaliwa kwa vizuri na malengo yanatupa matumaini kuwa kero nyingi zinazokabili jamii yetu zitapata ufumbuzi.

(b) Tuhakikishe kuwa kiasi cha 35% ya bajeti ya Taifa inawekezwa kwenye miradi ya maendeleo hata kama itabidi tupunguze matumizi ya kawaida.

(c) Uwekaji wa miundombinu kwa ajili ya mahitaji ya watu wenye ulemavu na makundi mengine yenye mahitaji maalum uzingatiwe na kutekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha fedha zilizotengwa kwa ajili ya kukuza ushirika (*SACCOS, SACCAS* na *VICOBA*) ni kidogo sana ikizingatiwa kwa muda mrefu ushirika hakupewa kipaumbele kinachostahili. Nashauri kuwa utazamwe uwezekano wa kuongeza fedha kwenye eneo hili kuwezesha wajasiriamali wajitegemee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe Benki ya Maendeleo ya Kilimo inaanza kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *DART*, imeoneshwa kuwa Awamu ya I na II ya mradi huu itatekelezwa kwa pamoja. Je, hii inawezekana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *decongestion of cities*, inaelekea kuwa msongamano unaonekana Dar es Salaam pekee lakini Miji ya Arusha, Mbeya na Mwanza una matatizo makubwa, hivyo mpango wa kuyanasua uwekwe.

Mheshimiwa Rais alipokuwa kwenye kampeni ya Uchaguzi Mkuu mwaka 2010 aliahidi kuwa barabara za Halmashauri ya Arusha zitaboreshwa ili zipitike miaka mitano. Pia aliahidi kuwa barabara ya lami itajengwa Ngaramtoni - Sambasha (km.12.5).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutimiza ahadi hizo, naomba barabara zifuatazo ziingie kwenye mpango:-

- (i) Ngaramtoni – Sambash;
- (ii) Ngulelo – Bangata – Nkoaranga – Maji ya Chai;
- (iii) Arusha – Bwawani – (*Nelson Mandela IST*);
- (iv) Sekei – Olgilai – Ngiresi; na
- (v) Mianzini – Ilboru – Oldonyosapule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuitia Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ilitenga ardhi hekta 5,000 kwenye Kata ya Bwawani kwa ajili ya ujenzi wa Taasisi ya Nelson Mandela (*Main Campus*). Naomba Mpango huu uoneshe nia ya kuendeleza ardhi hiyo kwa kuweka ujenzi wa miundombinu ya barabara, umeme na maji kwenda kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango haujatambua umuhimu wa michezo kama chanzo cha ajira na afya. Ujenzi wa viwanja uwe sehemu ya Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha, naunga mkono hoja.

MHE. MANSOOR S. HIRAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa Mpango mzuri wa kuharakisha maendeleo kwa kupanga vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu, naomba nishauri kwenye kipaumbele hiki, Serikali itujengee barabara ya lami kutoka Magu – Ngudu – Hungumarwa. Barabara hii itaunganisha Majimbo matatu na itaboresha uchumi wa wananchi wa Jimbo la Magu/Sumve/Kwimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kilimo Kwanza, ni mpango mzuri sana. Nashauri Wizara ya Ardhi ingeagizwa ianzishe mpango wa kupima mashamba kila Wilaya hususani waanzie hata hekari mia tano kila Wilaya, ziwe tayari zimelipwa fidia na mwekezaji wa ndani au wa nje wakija wanapata mashamba tayari kuliko utaratibu wa sasa hivi wa mwekezaji kwenda kijijini na kuomba maeneo, huu ni usumbufu na inavunja moyo wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri matrekta yaliyotolewa na Serikali ambayo yako SUMA – JKT, yasambazwe kwenye Halmashauri zote ili wakulima wanunulie kwenye Halmashauri zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha maji ni muhimu sana ukizingatia tabia nchi ilivyobadilika. Nashauri bomba la maji ya Ziwa Victoria kutoka tanki la Mhalo yasambazwe na kupelekwa Mji wa Ngudu amba ni Makao Makuu ya Jimbo la Kwimba. Ngudu wana mgao wa maji, wananchi wanapata maji mara mbili kwa wiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa asilimia 85% ya mapato ya ushuru tunategemea bandari ya Dar es Salaam, kwa hiyo, hii bandari ni moyo wa nchi yetu. Nashauri bandari hii miundombinu yake iboreshwe haraka sana, pia miundombinu ya kupokea mafuta hapo bandarini inatakiwa iboreshwe, hii inachangia kupanda kwa bei ya mafuta. Mwisho, naunga mkono hoja hii.

MHE. MBAROUK SALIM ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuwepo hapa leo hii kujadili Mpango huu wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niipongeze Tume ya Mipango kwa kuweza kuandaa Mpango huu amba unatoa mwelekeo wa Taifa letu kwa miaka mitano 2011/12 – 2015/16. Historia inaonesha kuwa huu sio Mpango wa kwanza kwa Tanzania, bali kuna mipango mingi iliyopangwa hapo nyuma tokea Uhuru wa Nchi hii lakini utekelezaji wake unakuwa mbovu au hauridhishi, hii ni dhahiri kuwa kupanga tunaweza lakini utekelezaji inakuwa ni tatizo. Hivyo, kama hatukujipanga vizuri katika sekta zote basi na utekelezaji wa Mpango huu pia utakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, Mpango huu unatajwa kuwa ni wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini katika maandiko mengi au yote ni ya upande mmoja, yaani Tanganyika. Huu ni utata na zaidi uko kwenye uwasilishaji wa Mpango nje ya nchi kwa kusema kuwa ni Mpango wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini kumbe ni Mpango wa Tanganyika. Hili lingewekwa wazi ili kupunguza utofauti wa maendeleo utakaopatikana. Nashauri suala hili liwekwe wazi ili kuweka sawa Mpango huu kwa jamii yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huu nilitegemea katika moja ya vipaumbele ni kuondoa kero za Muungano ambazo ni utata mkubwa wa maendeleo kwa pande zote. Mpango unaweza ukawa mzuri lakini kama kuna migongano na mivutano, utekelezaji wake pia ukawa na vikwazo. Nahisi tungeondosha kasoro na kero zilizopo ili tuweze kwenda vizuri hapo baadaye na kwa sababu nilizozitaja hapo juu Mpango wenyewe pia unaweza kuwa kero baina ya pande hizi za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu unahitaji mikakati mikali ya utekelezaji ambayo ndani ya Mpango wenyewe haijaainishwa au haiko wazi. Nashauri Tume ya Mipango iweke mikakati iliyo wazi na thabiti ili tuweze kufanikisha utekelezaji wa Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango unaonesha utegemezi zaidi wa rasilimali (fedha) za kutekelezea Mpango wenyewe. Hii ni hatari na inawezekana tukamaliza mwaka au kipindi cha Mpango na tukawa tumefanya mambo machache sana. Nashauri Tume ya Mipango iweze kuratibu vianzio vya fedha vya ndani ili tuweze kulazimisha kuwa na fedha nyingi za ndani kwa ajili ya utekelezaji. Mpango ni wetu kama Watanzania na hivyo ni budi kulazimisha uwezo wetu kwa njia yoyote ile na tuachane na kutegemea zaidi misaada na mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu utekelezaji wake uwe wazi na ueleweke kwa Watanzania wote, lakini pia na Bunge linatakiwa liweze kusimamia Mpango huu kwa niaba ya Watanzania. Hivyo nashauri mipango ya mwaka mmoja mmoja iletwe Bungeni ili ijadiliwe na kuitishwa na Bunge kabla ya utekelezaji, hii ni kukidhi ile dhana ya usimamizi wa pamoja wa Mpango huu, hivyo, ni lazima ushirikishwaji wa wadau wakiwemo Wabunge katika ngazi mbalimbali za Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru kwa kuweza kuchangia hoja hii.

MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano. Umeandaliwa vizuri na unazingatia vipaumbele muhimu kama kilimo, miundombinu kwenye upande wa elimu na afya, Mpango unatumia lugha ya kulinda mafanikio yaliyokwishapatikana katika sekta hizo mbili (*grandfathering the two sectors*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu ni kwamba hatujafikia kiwango cha kuridhisha cha mafanikio katika elimu na afya. Kwa upande wa elimu bado kiwango cha elimu kiko chini kutokana na uhaba wa Walimu, tatizo la vitabu, hatuna Walimu wa Sayansi katika shule zetu za msingi na sekondari, upungufu wa maktaba na maabara. Kwenye afya, utekelezaji wa mpango wa MMAM mfano kujenga Zahanati kila Kijiji na Kituo cha Afya Kila Kata bado ni tatizo kutokana na uhaba wa fedha. Kwahiyo bado elimu na afya ni vipaumbele muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naunga mkono suala la kupunguza utegemezi (*dependence*) kwa wafadhili. Tutafanya hivyo kwa ku-*promote exports* na kwa hiyo ni muhimu kujenga viwanda, *industrial base*. Ni muhimu pia kukaribisha *Foreign Direct Investments (FDI)*. Kwa hiyo, suala la kuwa na mazingira mazuri kwa wawekezaji ni muhimu. Bado kuna *Redtape*, ucheleweshaji wa leseni na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la kuzingatia katika utekelezaji ni ukusanyaji wa mapato, *TRA* ina uwezo wa kukusanya zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali za Mitaa zijengewe uwezo wa kukusanya mapato. Fedha zikishakusanya basi tusimamie vizuri matumizi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango ni mzuri la muhimu sasa ni kuandaa mikakati ya utekelezaji. Serikalini tuna tatizo la kigugumizi cha kufanya maamuzi (*procrastination*) wakati wa *implementation* kunatakiwa kufanyike *Implementation decisions*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *comparative advantages* nyingi kama bandari, maliasili, utalii, amani, kwa nini tusiwe makini tuka-exploit hizo *comparative advantages*. Wakati tuna hizo *comparative advantages* pia tuna udhaifu (*weaknesses*) ambazo inabidi tupambane nazo. Bado elimu ya watu wetu ni ndogo (*not well developed Human Resource*) ili tuwe *competitive*. Rushwa (*corruption*) bado ni kikwazo katika utekelezaji mzuri wa mipango. Hatuko makini (*Lack of Seriousness and commitment*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, msisitizo au *focus* on *SAGCOT* unanifanya niwe na wasiwasi kwamba Mikoa mingine kama Kagera tunaweza tukasahaulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora bado ni tatizo. Pia tuwe makini na suala la ajira kwa vijana na akina mama. Tu-*support* Benki ya akina mama. *Let us exploit the informal sector* kupitia MKURABITA na mipango mingine. *Whether we like it or not* bado kilimo ndio uti wa mgongo. Viwanda vitazalisha zana za kilimo, *we need to mechanise agriculture* katika harakati za kufikia malengo ya Dira ya 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitakia kila la kheri Serikali yetu na Watanzania kwa ujumla.

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa Mpango huu wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mpango huu umegusa sehemu zote muhimu za maendeleo ya kila Mtanzania, kwa hiyo, kama Mpango huu utasimamiwa vizuri basi tutafikia malengo.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango huu nazungumzia kuhusu uvuvi. Watanzania tunazo rasilimali nyingi tu ambazo Mungu ametubariki. Miongoni mwa rasilimali hizo ni

Bahari ambayo zimo mali nyingi na zikisimamiwa ipasavyo inaweza kuondoa umasikini na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tufikie malengo ya Mpango huu sehemu ya uvuvi ni kuwawezesha wavuvi wadogowadogo kwa kuwapatia zana za uvuvi za kisasa ambazo zitawezesha kuvua kwa utaalamu. Wataweza kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa, watapata mapato makubwa ya kuweza kumudu maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wetu wadogowadogo hawafikii malengo kutokana na kukosa mambo muhimu katika kazi yao. Hivyo mimi nashauri Serikali iwapatie elimu ya kazi yao ambayo itawezesha kufanya kazi yao kiutaalamu. Wapatiwe vyombo vya uvuvi ambavyo vina mahitaji yote ambavyo vina uwezo wa kufika umbali mkubwa wa bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiacha uvuvi sasa nazungumzia ufugaji, Tanzania ni nchi ambayo ina mifugo mingi sana hasahaha mifugo ya ng'ombe. Katika Mpango huu wa Miaka Mitano ufugaji unataka kusimamiwa vizuri na kama halitosimamiwa vizuri basi tija yake ni ndogo sana. Leo utakuta wananchi wengi wa Tanzania ufugaji wao ni kukusanya makundi makubwa makubwa ya ng'ombe amba wanamshinda katika huduma mbalimbali kama dawa za kuogeshea, sindano za kinga za maradhi mbalimbali na machunga bora.

Watanzania wengi wanaona fahari kuwa na wanyama wengi lakini yeye mwenyewe akiwa na maisha duni hata nyumba ya kukaa hana. Wanyama wanakosa sehemu za machunga na kuharibu mazingira na wanasababisha jangwa kutokana na kuwa wengi. Hivyo, inahitajika kusimamiwa vizuri na kutolewa taaluma endelevu ili wafugaji wanufaika na wanyama wao. Ushauri wangu wawepo wataalamu wa mifugo, wawe karibu na wafugaji ili kuwapa ushauri mzuri katika ufugaji ili mifugo yao ikuze maisha yao na pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia mchango wangu kwa kuunga mkono hoja, lakini naomba usimamizi madhubuti na uwajibikaji juu ya Mpango huu.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba Mpango wa Miaka Mitano uliozinduliwa na Mheshimiwa Rais tarehe 7/6/2011, nathubutu kusema kwamba haukuzingatia hata kidogo katika kuandaa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 utekelezaji wa Mpango unakadirwa kugharimu trilioni 8.277/= ukilinganisha na Bajeti ya Maendeleo ya Shilingi trilioni 4.295. Utekelezaji wa Mpango haumo kabisa katika bajeti ya Waziri. Kutokana na uchambuzi huu, inaonesha wazi kwamba hakuna uratibu kati ya Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango. Katika hali hii, ni dhahiri kwamba Mpango wa miaka mitano uliozinduliwa na Mheshimiwa Rais hauwezi kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano umeweka lengo la kukua kwa uchumi kwa asilimia 8 – 10. Wakati huohuo lengo la bajeti ni

uchumi kukua kwa asilimia 6 kwa mwaka 2011 na asilimia 7.2 mwaka 2012, malengo ya Serikali ni yapi hasa? Ni kwamba uchumi ukuwe kwa asilimia 6 – 7 au ukuwe kwa asilimia 8 -10?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kasi ya kupanda kwa bei za bidhaa na huduma, hili limeelezwa kwamba linasababishwa na kuongezeka kwa bei za mafuta katika soko la dunia na pia kutopatikana kwa umeme wa uhakika na kusababisha kuathirika kwa uzalishaji na upungufu wa chakula nchini na nchi jirani. Hata hivyo, mfumuko wa bei mwaka 2010 unaelezwa kuwa ni asilimia tano tu vilevile Waziri ameeleza kuwa baada ya msukosuko wa uchumi duniani bei ya mafuta ilishuka hadi dola za kimarekani 40 kwa pipa. Kwa sasa bei ya mafuta katika soko la dunia imefikia takribani Dola 120 kwa pipa ambayo ni mara tatu ya bei iliyokuwepo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za hali ya uchumi wa Taifa zinaonesha kuwa mfumuko wa bei mwaka 2008 wakati wa mtikisiko wa uchumi duniani na bei za chini za mafuta zilikuwa ni asilimia 10.3 ukaongezeka na kuwa asilimia 12.3 mwaka 2009 na kupungua na kufikia asilimia tano mwaka 2010. Waziri ana maelezo gani kuhusu kitendawili cha takwimu za mfumuko wa bei?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei za mafuta zikiwa chini mfumuko wa bei unakuwa juu na bei za mafuta zikipanda mfumuko wa bei unateremka. Je, takwimu za mfumuko wa bei ni ukweli zinapita katika ongezeko la gharama za maisha? Ni ukweli usiopingika kwamba Tanzania bado inakabiliwa na udhaifu mkubwa wa takwimu na kwahiyu kuathiri uibuaji wa Sera na Mipango ya Maendeleo. Bila ya kuwa na takwimu sahihi hatuwezi kupanga na kusimamia maendeleo yetu kikamilifu.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Taifa lolote lile ndio dira ya maendeleo na ndipo Taifa linapoweka vipaumbele na hivyo kuvitekeleza. Kwa bahati mbaya sana Tanzania imekuwa na utaratibu mbovu wa kuwa na vipaumbele vingi sana hivyo kushindwa kuvitekeleza na pia vipaumbele hivyo kwa kiasi kikubwa kutegemea wahisani toka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna nchi yoyote duniani iliyoendelea kwa kutokuipa elimu kipaumbele. Ni jambo la kusikitisha kuona katika vipaumbele vitano, elimu wala afya haipo. Ni kwa namna gani tutapata wataalam kama hatuwekezi katika elimu? Nashauri elimu iwe moja ya vipaumbele vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo na ufugaji ni uti wa mgongo wa Taifa letu huku asilimia zaidi ya 80 wakitegemea kilimo. Pamoja na kukipa kipaumbele kilimo bado eneo la mifugo na mazao yake hayapewi kipaumbele. Kwa mfano, ni jambo la kusikitisha kuona wawekezaji hususani wa migodini kama Geita Gold Mines, Barricks kununua nyama na maziwa kutoka nje ya nchi kwa wafanyakazi wake huku Tanzania ikiwa na mifugo lukuki. Ni kwa nini Mpango huu hauoneshi ujenzi wa Kiwanda cha Nyama wala usindikaji wa maziwa katika maeneo yenye migodi ili mazao ya mifugo yetu yaweweze kupata soko la ndani na nje pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imejaliwa rasilimali nyingi ikiwa ni pamoja na bahari ambapo tumekuwa na bandari nyingi kubwa ikiwa ni ile ya Dar es Salaam. Ni kwa kiasi gani bandari hii inabeba uchumi wa nchi hasa tukizingatia kuwa nchi yetu inazungukwa na nchi sita (6) zisizo na bandari. Hii ni fursa kubwa sana kwa nchi yetu kuongeza pato la Taifa. Nchi kama Singapore inategemea sana bandari yake na imekuwa na pato kubwa la Taifa kutokana na bandari tu. Inasikitisha kuona fedha iliyotengwa kwa ajili ya kupanua bandari zetu hususani ile ya Dar es Salaam ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Wizara ya Ujenzi hususani miundombinu imepewa kipaumbele lakini bado tatizo la msongamano Dar es Salaam linapunguza sana pato la Taifa. Barabara za juu (*flyovers*) ni muhimu sana lakini katika Mpango haioneshi kama barabara hizi zitakuwa tayari ifikapo mwaka 2016. Jiji la Dar es Salaam lina wakazi zaidi ya milioni nne, ambapo wataalam wanassema Jiji linapokuwa na watu milioni mbili inapaswa kuwa na *flyovers*, hivyo tangu miaka ya 1990 tulipaswa kuwa nazo. Nashauri wakati hili linashughulikiwa, barabara za pembezoni zitengenezwe ili kupunguza msongamano.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kumpongeza Waziri kwa kuwasilisha vizuri Mpango huu wa Maendeleo ya Miaka Mitano ili kufikia malengo ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini kwa Watanzania wote hapo nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, sasa napenda kutoa mchango wangu katika kutekeleza Mpango huu ili tupate mafanikio tuliyokusudia kwa faida ya Watanzania wote popote pale walipo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Watanzania wengi ambao ndio wenye wajibu wa kuutekeleza Mpango huu ni vijana, ambao ndio nguvu kazi inayotegemewa katika nyanja tofauti za harakati zao za maisha na kutafuta elimu, kwa maoni yangu ni kwamba lazima tubadilike kimtaalamu na mwelekeo wa uwajibikaji katika kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vyote vilivyokuwemo katika Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwaanda vijana wetu ili wawe na fikra za uwajibikaji katika kujenga nchi hii, ni vyema basi ile Sheria ya Vijana kwenda JKT na JKU kwa mafunzo kabla ya kujiunga na Vyuo au hata kuajiriwa basi itekelezwe ili tupate vijana wenye maadili mema na uzalendo kwa madhumuni makuu ya uwajibikaji katika dhamana wanazopewa sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, kwa Mpango huu wa Miaka Mitano. Pia niwapongeze na watu wote wa Tume ya Mipango kwa kazi nzuri waliyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu umekuja kwa wakati muafaka kabisa kwa Taifa letu. Nikiangalia katika vipaumbele, ni hakika Tume imefanya utafiti wa kutosha kabisa. Tukianza na miundombinu ilivyoainishwa, ni hakika pato la Taifa litaongezeka sana. Nachoomba ni kwamba hii miundombinu ya umeme, barabara iimarishe katika vijiji kwa sababu zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wanaishi vijijini. Tukiimarisha upatikanaji wa umeme na barabara za lami vijijini, nina uhakika uzalishaji utaongezeka sana kuliko ilivyo hivi sasa. Hivyo nakumbusha tu kuwa utekelezaji wa miradi hii iangalie vijijini na mijini. Kwa kuwa na umeme, vijana wataweza kujajiri katika shughuli za uzalishaji mfano viwanda vidogo vitaanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipengele cha pili ambapo ni Viwanda, kipaumbele hiki ni muhimu sana. Ili wananchi waweze kushiriki vizuri katika uzalishaji viwandani, ni vizuri Tume hii iangalie namna ya kutoa elimu hasa kwa wananchi namna ya uendeshaji wa viwanda hivi, elimu ya uanzishaji wa viwanda hivi. Kwa mawazo yangu, nashauri *SIDO* ipeleke elimu vijijini ambako ndiko kuliko na wananchi wengi. Wananchi hawa wakipata ujuzi huu, nina uhakika itaongeza tija katika uzalishaji katika viwanda vidogovidogo mwisho wa siku itachangia katika pato la kila kaya na hatimaye itachangia katika kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitimisha kwa kuupongeza Mpango huu, nisisitize tu kwamba katika utekelezaji wa Mpango huu kipaumbele kiwe katika kuvifika vijiji. Programu zote zilenge katika kutoa huduma vijijini maana zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania maskini wako vijijini. Tukielekeza nguvu vijijini, nina uhakika tutaguswa Watanzania walio wengi matokeo yake itakuwa mafanikio na maisha bora kwa Watanzania walio wengi. Hivyo basi miradi ya umeme na viwanda vidogovidogo vielekezwe vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuleta Mpango huu katika muda muafaka. Mpango huu ni mzuri kama utakuwa na utekelezaji mzuri. Watanzania ni mabingwa wa kuandaa mipango isiyi na utekelezaji. Hivyo, tunaomba ipewe kipaumbele ili iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia katika sekta ya kilimo. Kilimo bado hakijapewa msukumo mkubwa. Ili tuendelee, tunahitaji kuwawezesha wakulima wadogo wadogo ambao ndio wengi katika nchi hii, unapowawezesha wananchi walio wengi, umepandisha uchumi wa nchi. Wawezeshwe vipi? Wakopeshwe matrekta na Serikali, watafutiwe masoko ya uhakika na kuwa na mpango endelevu wa kujenga viwanda vyakusindika mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uvuvi haijafanyiwa kazi kwani tuna rasilimali kubwa ya maziwa ya Nyasa, Tanganyika, Rukwa, Victoria na Bahari ya Hindi lakini sehemu zote hizi hazijafanyiwa kazi. Endapo wavuvi wadogowadogo wakiwezesha na Serikali wakaanza kuvua uvuvi wa kisasa, wananchi wangkuza uchumi wao na kukuza uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kukuza uchumi kama nishati ya umeme haijapatikana, maendeleo yoyote yale yanahitaji nishati ya umeme. Tunapozungumzia nishati hii ilenge na vijijini kwani nishati hii ikiishia mijini bado hatutakuwa tumewasaidia, walio wengi wanaishi vijijini hivyo nishati ikifika vijijini wakulima watasindika mazao yao na kuyaongeza thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kwenda mbele bila miundombinu kwa kuboresha barabara zinazounganisha Mkoa hadi Mkoa, Wilaya hadi Wilaya, zижengwe kwa kiwango cha lami. Reli iboreshwe, huwezi kuwa na maendeleo bila reli, ni mhimili mkubwa wa uchumi katika nchi. Hivyo, tunaomba Mpango huu ujielekeze zaidi katika reli sambamba na ujenzi wa bandari katika maziwa na upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Mpango huu uangalie uwiano wa mgawanyo wa rasilimali, tusipoangalia Mpango unaweza kuwanufaisha zaidi wale ambao wamepiga hatua. Ni vizuri ikaangaliwa Mikoa ambayo iko nyuma kimaendeleo ikapewa kipaumbele ili iweze kunyanyuka. Vinginevyo tunaweza tukaandaa Mpango usiwasaki die sana wale ambao Mikoa yao iko chini kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini yote mazuri hayawezi kufaulu kama Watanzania hawatafanya kazi. Lazima tuandae utaratibu utakaombana Mtanzania ye yote mwenye uwezo wa kufanya kazi kufanya kazi. Nchi haiwezi kwenda mbele bila kufanya kazi, tuna wananchi walio wengi wanaishi vijijini na mijini hawafanyi kazi. Naunga mkono hoja.

MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Tume ya Mipango kwa kazi nzuri inayofanya na iliyofanya ya kutengeneza mpango huu. Mpango huu unaweka umuhimu katika mambo *specific* ya kusaidia kukuza uchumi wetu. Mpango huu unatuelekeza kwenye sera zetu ambazo zinajitofautisha na sera zilizopita na kuweka msisitizo katika maeneo ambayo naunga mkono kwanza, kuondokana na kupanga kutokana na mahitaji ambayo nayo yanatokana na *resources* zilizopo na kupanga kutokana na *opportunity* tulizonazo. *Opportunities* za kukuza uchumi katika nchi yetu ni nyingi iwapo tutaweka sera zitakazosaidia *opportunities* hizo kuzipata na kutumika kusaidia uchumi mfano, nafasi za uvuvi katika bahari kuu, ni kwa kiasi gani nchi na wananchi wananaufaika. Je, mazingira ya uvuvi wa bahari kama yanamfanya mwananchi aweze kujiingiza? Sera basi zielekeze namna ya kuweka *environment* nzuri ya kusaidia utekelezaji wa uvuvi wa bahari kuu uchangie uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuweka msisitizo juu ya ukuaji wa uchumi kama tukifaidika na utoaji wa huduma za kijamii na kuweka msisitizo wa rasilimali watu wapate ujuzi unaofaa ili rasilimali watu hao wasaidie uchumi kwa kuitia soko la ajira watu wenye ujuzi na elimu wanasaidia kuboresha huduma. Ziko nchi nyingi zimeweza kukuza uchumi wao kutokana na utoaji huduma tu, huduma bora zilizotukuka zinazotolewa na walioelimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, umuhimu wa kushirikisha sekta binafsi katika kukuza uchumi. Tanzania imepiga hatua kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji, lakini nionavyo mimi wengi wanaonufaika ni wawekezaji wa nje, kwa kupata *tax exemptions* nydingi na wengine hudiriki kuza uwekezaji wao anapofikia muda wa kulipa kodi. Nchi nydinge za wenzetu katika kuwasaidia watu wake wameamua kwa makusudi kutaka uwekezaji katika maeneo fulani nchini lazima mzawa awe mshiriki na mbia lazima amshirikishe mzawa. Ni kwa kiasi gani na sisi tunaweza kufaidika kwa njia hii? Ni vema tuangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kuweka msisitizo na mkazo katika ubora wa utekelezaji wa miradi yetu na shughuli zetu mbalimbali katika utekelezaji wa mikakati tuliojiwekea. Mipango tunayoipanga ni mizuri na hata namna ya kubuni mipango ya utekelezaji wake unawekwa vizuri. Tatizo lipo katika utekelezaji, usimamizi na ufuatiliaji. Kazi nzuri ya kubuni mipango hii lazima iende sambamba na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vipaumbe vya Mpango, nakubaliana na maeneo yote yaliyoainishwa umeme, bandari, reli, barabara, viwanja vya ndege, usafiri wa anga na matumizi ya *ICT*, madini, sekta ya uzalishaji, kilimo, maji na mazingira na rasilimali watu. Katika eneo la kilimo yafuatayo yafanyike:-

- (a) Tuongeze kusaidia/kuboresha *deep sea fishing* na *fish processing* ifanyike nyumbani.
- (b) Tuweke msisitizo juu ya *ku-process products* zetu nyumbani na kupeleka nje *finished products* mfano, korosho zilizobanguliwa, pamba iliyotengenezwa nyuzi na vitambaa na hata nguo (*finished products*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme na maji. Uganda imetumia maji ya Ziwa Victoria kupata umeme kwa kutengeneza *Dam*, je sisi hatuwezi? Hata kama tutatumia maji ya ziwa Tanganyika. Maporomoko mengi ya maji ambayo yanawenza kutupatia umeme bado hatujayawekea mkakati, tutumie uwekezaji kwa njia ya *PPP*. Matumizi ya takataka zinazosalishwa majumbani na vijijini hutoa umeme unaoweza kusaidia maeneo kadhaa kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwajibikaji, Mipango mizuri, fedha zitatafutwa, HR (*Professionalism*) itapatikana ila bila uwajibikaji kwa watekelezaji wa Mpango huu katika maeneo ya vipaumbele itakuwa ni hadithi tu. Uzembe wa kazi, *poor management of time*, ufisadi na *poor followup*. Msisitizo uwekwe, wazembe waachwe, *few committed* wawe *motivated* ili kuongeza *productivity*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono Mpango huu wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili pamoja na Mpango huu kuzungumzia kwa kina suala la miundombinu kama barabara na viwanja vyta ndege lakini mashaka yangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiboresha viwanja vyta ndege kama tulivyoahidi katika Mpango huu, vitatusaidia kuongeza mapato, lakini Mpango huu haujaaeleza tutanunua ndege ngapi? Zipo nchi maskini kama Jamaica, Rwanda na hata Trinidad na Tobago zina mashirika ya ndege, sisi shirika letu linasuasua. Nadhani sambamba na kuboresha viwanja vyta ndege, tulimarishe pia Shirika letu la Ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ni kiungo muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yoyote. Mpango huu kama utatekelezwa na barabara zikatengenezwa na kuwa na *network* nchi nzima, nina imani tutapata mafanikio. Barabara ya *Great North*, Babati – Kondoa – Dodoma – Iringa kama itatengenezwa kwa kiwango cha lami kama Mpango unavyoonesha, ni imani yangu tutafika pale tunapopahitaji, lakini kama kutakuwa na ubinafsi katika utekelezaji bado hatutafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo ni moja ya eneo ambalo katika Mpango huu halikuguswa hata kidogo. Michezo ni sehemu muhimu sana kama sehemu ya ajira kwa vijana na ni moja ya maeneo yanayoweza kuitangaza nchi yetu kwa kiwango kikubwa. Ni imani yangu kama Mpango huu utajielekeza pia katika michezo kama soka, riadha n.k. Ni imani yangu tutakuwa tumeongeza soko la ajira kwa vijana na pia kuboresha viwanja vyta michezo ili viwe na tija kwa Taifa letu.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la nchi yetu sio mipango bali ni utekelezaji wa mipango yenye. Kama mipango yote inayopangwa katika nchi yetu ingetekelezwa basi nchi yetu ingekuwa imeshapiga hatua kubwa ya maendeleo. Ipo haja ya makundi Mpango huu wa Miaka Mitano sasa uwepo mkakati maalum wa utekelezaji haidhuru mpango huu umeshaanza na dosari mapema ya kukosa fedha za utekelezaji wake katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wake 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, navyoona mimi eneo la kwanza litakalokuza upatikanaji wa fedha haraka na kusaidia sehemu nyingine ziweze kukuwa kiuchumi ni bandari. Bandari yetu au nchi yetu kwa ujumla imebahatika kuwa na nchi karibu sita ambazo kama huduma yetu itakuwa ni yenye ufanisi tunaweza kuwashudumia kwa kupitia bandari zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa bandari zetu na hasa bandari ya Dar es Salaam ina urasimu mkubwa na kwa utaratibu huo nchi zitakimbia bandari yetu. Hivi sasa huduma inayotolewa na bandari zetu haikidhi matakwa ya wateja husika. Kufanyike mabadiliko makubwa ya kimuundo na utendaji katika bandari zetu. Katika hili la bandari na miradi mingine itakayosimamiwa na Serikali ipo haja Menejimenti ikapewa kazi kwa mkataba, wanaposhindwa wawe wamejiachisha kazi wenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa reli ya uhakika na yenyewe uwezo mkubwa wa kutoa huduma, ni suala la msingi katika kujenga uchumi imara. Shirika la reli ni bovu badala ya kuchangia pato katika Mfuko Mkuu wa Serikali, shirika lenyewe linabidi lipate ruzuku kutoka Serikalini. Shirika hilo liwezeshe na Menejimenti pia nayo iajiriwe kwa mkataba maalum, wakashindwa wawe wamejifukuzisha kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii unaweza ukakuza uchumi wetu kwani nchi yetu ina vivutio vingi vya utalii. Ipo haja Serikali igharamie zaidi katika kuutangaza utalii ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila ya kuwa na Shirika la Ndege, ukuaji wa utalii utakuwa kwa kasi ndogo sana. Kwa hiyo, ipo haja ya kuundwa upya Shirika la Ndege na Menejimenti itakayoundwa ikishindwa kazi baada ya kuwepo mkataba maalum wafukuzwe kazi na pale itakapogundulika wamelitia hasara Taifa kwa makusudi wapelekwe kwenye vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme ndio nishati ya msingi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yoyote. Juhudi za kupatikana nishati hiyo yaende sambamba na uimarishaji wa huduma kwenye bandari zetu. Mipango mingine kiutekelezaji itafuata baada ya kuwepo miundombinu na kuimarika bandari zetu.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri husika, Katibu Mtendaji wa Tume, Ndugu Phillip Mpango na Watendaji wote wa Tume ya Mipango kwa kazi nzuri sana ya uandaaji wa Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imeonesha nia ya kuendeleza kilimo cha kisasa kwa kuzingatia kuwa kilimo ni sekta mama na ni kiungo muhimu, nashauri Kambi za Jeshi la Kujenga Taifa zitumike katika kilimo cha umwagiliaji na kambi hizo ziwe darasa kwa kilimo cha kisasa kwa vijiji vinavyozunguka makambi hayo. Mabwawa makubwa yatakayotumika kwa umwagiliaji yatutumiwa na wananchi wa maeneo hayo kwa kuwa kwa sasa hakuna vijana wengi katika makambi hayo. Vijana wanaozurura bila kazi maalum na wale wanaofanya biashara za kuuza maji, karanga n.k mijini wapelekwe katika makambi hayo kuendeleza kilimo na watengewe posho kidogo kwa ajili ya familia zao. Naamini pamoja na wakulima wadogowadogo, wawekezaji katika kilimo, JKT pia ikitumika vizuri ina uwezo wa kuongeza uzalishaji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango yetu ni mizuri sana tena sana, tatizo ni Watendaji. Naiomba Serikali Mtendaji atakayeonekana kutotimiza wajibu wake ipasavyo aachie ngazi. Mpango huu mzuri tunaousifia hautatekelezeka iwapo Watendaji wetu hawatabadilika kufanya kazi kwa kasi inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tufikie malengo yetu, Watendaji wabovu wasionewe haya. Suala la barabara, makandarasi walioonesha kutoamilisha kazi zao ipasavyo wasipate nafasi tena ya kutupotezea fedha zetu katika kipindi hiki. Serikali iwe makini katika mikataba mbalimbali na wawekezaji ili isitokee kupoteza rasilimali za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme, pamoja na juhudi kubwa ya Serikali ya kuzalisha MW 2780 za umeme, kuna haja ya kuondoa kodi kwenye vifaa hasa vya umeme wa jua na *Bio gas* ili wananchi wa vijiji ni waweze kutumia umeme huo usiohitaji kulipia *bill* kila mwezi. Wananchi wanashindwa kutumia nishati hiyo kwa sababu ya ughali wa vifaa vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu, nashauri vijana waliomaliza Darasa la Saba na wale wanaomaliza Kidato cha Nne, wasiachwe wakizurura hovyo mitaani. Wapelekwe kwenye Vyuo vya Ufundu ili wakajifunze taaluma mbalimbali kama vile kilimo cha kisasa, ufundi stadi, ufugaji n.k. Hili linawezekana na vijana ni nguvukazi kubwa inayozurura tu mitaani bila kuwa na mwelekeo. Wanaomaliza Vyuo Vikuu na kukosa kazi, vyeti vyao vya vyuo vitumike kama dhamana ili wakopeshwe vifaa au fedha kwa ajili ya kuanzisha miradi ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri utalii wa ndani na wa nje utiliwe mkazo kwa kuwahamasisha wananchi kutembelea hifadhi zetu na pia maeneo ya makumbusho. Watanzania hawana mazoea ya kutembelea makumbusho na kufanya utalii wa ndani kiasi cha Mtanzania kutokuwa na uwezo wa kueleza rasilimali nyingi za nchi nje ya Tanzania. Mali za nchi kama vile misitu inakatwa hovyo bila usimamizi wa kutosha kwa Serikali. Pia uvuvi, meli za kigeni zidhibitiwe katika bahari na maziwa ili kuhakikisha tunakusanya mapato ya kutosha kutokana na uvuvi, misitu, wanyamapori na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulibinafsisha viwanda baada ya Serikali kujiondoa katika suala la uzalishaji katika viwanda vilivyobinafsishwa. Nashauri, viwanda vilivyobinafsishwa kwa watu binafsi na havizalishi virudishwe Serikalini na kuuzwa upya ili viwanda hivyo vizalishe kwa nia ya kuchangia pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuwapongeza sana Tume ya Mpango kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

MHE. AGNESS E. HOKORORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja kwa sababu pamoja na mambo mengine Mpango huu umetambua changamoto kubwa niliyonayo kwa vijana wetu hasa walio vijiji ambalo ni ukosefu wa *skills* zitakazowawezesha kujajiri au kushiriki shughuli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika kuona Mpango huu sambamba na kupanua Vyuo vya Ufundu (*VETA*) pia umetoa kipaumbele kwa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (*FDC's*) ambavyo viro 55 nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli Mpango utatekelezwa kama ilivyo (ukurasa wa 69) tukiboresha Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Wananchi na kuongeza idadi ya Wanachuo, basi tutakuwa tumewawezesha mamia ya vijana wa kike na kiume hasa wa vijiji. Ushauri wangu ni kwamba vijana hawa tuwaweke kwenye kozi ndefu za miaka

miwili kwa mafunzo ya Uashi, Useremala, Magari ili tatizo ambalo mpango huu umebainisha katika (ukurasa 46) la kukosekana kwa ajira kwa vijana hatimaye limalizwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Vyuo vya VETA sawa, lakini tukumbuke kuwa VETA inachukua vijana waliohitimu Kidato cha Nne tena wanaofaulu mtihani wa usaili, *FDC*'s zinachukua vijana waliomaliza Darasa la Saba, ambao ni wengi nchini karibu vijana 500 kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usawa wa jinsia. Nimefurahi Mpango huu katika (ukurasa 41) umetambua kutokuwepo kwa usawa wa jinsia katika nyanja za kiuchumi na kijamii ambalo bado ni tatizo katika maendeleo ya kiuchumi ambapo 90% ya wanawake wanaishi vijijini wanajishughulisha na kilimo na ufugaji. Kutokuwa na usawa wa jinsia inasababisha umaskini mkubwa katika familia nydingi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu ni kwamba kila sekta/mradi ambao tutautekeleza katika Mpango huu, ni muhimu kuingiza masuala ya jinsia (*gender mainstreaming*) ugawaji wa rasilimali uzingatie usawa wa jinsia katika maamuzi, utekelezaji na matokeo ya miradi hasa katika sekta za kilimo, ufugaji, viwanda, maji, afya na elimu, iwepo fursa sawa kwa wanawake na ushiriki wa wananchi wote kwa ujumla kama inavyoiezwa katika (ukurasa 50) wa Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa rasilimali watu, mpango huu umetambua tatizo la rasilimali watu, ni dhahiri kuwa ni tatizo kubwa linalorudisha nyuma ufanisi katika huduma za jamii hususani afya. Matatizo yanayoikumba sekta ya afya ni pamoja na kutokuwa na rasilimali watu ya kutosha ndio maana hospitali haziwezi kutoa huduma zake kwa ufasaha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu ni kwamba katika utekelezaji wa Mpango huu, Serikali ikubali kuchukua idadi kubwa ya wanawake pamoja na kuwaimarisha katika vyuo husika kama Udaktari, Uuguzi, ni vema wanawake wengi wakapewa mafunzo ya afya ya msingi hususani vijijini ili jukumu la uboreshaji wa afya uanzie katika ngazi ya kaya/familia. Hii itapunguza gharama kubwa inayotumika katika kutibu magonjwa ambayo yakielimishwa vizuri, inawezekana kabisa ikawa kinga badala ya tiba kama ilivyooneshwa katika (ukurasa 70), wote tunatambua ule usemi usemao “kinga ni bora kuliko tiba.”

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa kuwa suala la kuitia upya vyano vya mapato nchini (*Tax structure*) na mfumo wa matumizi ya kawaida (*Recurrent expenditure*) katika Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Serikali za Mitaa ni jambo la msingi sana linalolenga kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani, kudhibiti mianya ya ukwepajji kodi lakini pia kuepuka matumizi yasiyo ya lazima na kudhibiti ufujaji wa fedha za Umma. Lengo kuu ni kupata fedha za kutekeleza Mpango huu.

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa iundwe Tume kuitia mfumo wa mapato na matumizi nchini?

(b) Kwa nini kazi ya kupitia upya mfumo wa mapato na matumizi haujatengewa fedha katika Mpango huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, utekelezaji wa Mpango huu unategemea sana ukuaji wa sekta binafsi na ili sekta binafsi ikue lazima kuwepo na uhakika wa upatikanaji wa mikopo (*Access to loans*) ambalo ni tatizo kubwa sana hapa nchini:-

(a) Serikali haioni kuwa kutenga bilioni 100 kwa kipindi cha miaka mitano katika benki ya *TIB* ni kupiga danadana (*ratorace or backward movement*)?

(b) Je, Serikali kutenga bilioni 100 katika Benki ya Kilimo (*TADB*) ni kutokuwa makini katika maamuzi yetu?

(c) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa kupitia mapato yetu ya ndani kwa kipindi cha miaka mitano tupeleke Shilingi 500 bilioni (*Tanzania Agricultural Development Bank*) ili kuwezesha uwekezaji nchini?

(d) Ahadi ya Mheshimiwa Rais ni kupeleka Shilingi 400 bilioni kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2010/2011 – 2013/2014 kwa kupelekwa 100 bilioni kwa mwaka, kwa kuwa hivi sasa zimepelekwa Shilingi bilioni 50 tu. Je, bilioni 50zilizobaki zitapelekwa *TIB* kabla mwaka wa fedha haujakwisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kwa kuwa ujenzi wa barabara ya Lamadi – Bariadi – Kisesa – Mwandoya – Mwanhuzi – Singida – Arusha (kupitia Babati) ni ya muhimu sana inaunganisha Mkoa wa Mara, Mwanza, Simiyu, Singida na Arusha na wananchi wa maeneo haya wanazalisha pamba, madini, samaki, mahindi, mifugo, karanga na vitunguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali itakubaliana nami kuwa barabara hii iingizwe kwenye Mpango huu wa miaka mitano ya mwanzo ili kupunguza fursa ya uchumi na kijamii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara za Lamadi-Bariadi-Mwandoya-Mwanhuzi-Mbulu-Babati-Arusha na Lamadi-Bariadi-Mwandoya-Mwanhuzi-Sibiti-Nduguti-Iguguno ni muhimu na naomba zijengwe. Naomba kuwasilisha.

MHE. UMMY A. MWALIMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja ilioletwa mbele yetu na Mheshimiwa Wasira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhishwa na jinsi Mpango huu, pamoja na mengineyo ulivyoainisha kuwa mojawapo ya changamoto tulizonazo kama nchi na jamii katika kujiletea maendeleo yetu ni kutokuwepo kwa usawa wa jinsia katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa. (Ukurasa 41 wa Mpango).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na hoja kuwa kuingiza jinsia (*Gender mainstreaming*) katika Mpango huu utakuwa ni mkakati sahihi (*strategy*) ya kufanikisha (ku-promote) fursa sawa kati ya wanaume na wanawake. Hii ni muhimu sana kwa nchi yetu kwa sababu kuna takwimu na ushahidi wa kutosha kuwa wanawake na wanaume wana fursa tofauti (zisizowiana) hasa katika kumiliki mali, nyenzo za uzalishaji na pia wanafanya majukumu tofauti katika maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa (*Vision 2025*) kuwa usawa wa jinsia na uwezeshwaji wa wanawake ni mojawapo ya mkakati wa kufikia maisha bora kwa Watanzania. Ningependa kuweka msisitizo kuwa Mpango huu pia utamke katika *Chapter three (On strategic interventions)* kuwa kuingiza masuala ya jinsia (*Gender mainstreaming*) ni lazima liwe sharti la Sera na miradi au mipango itakayopangiwa fedha na kutekelezwa chini ya Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa vipaumbele vyote vilivyoainishwa (yaani Ardhi, Nyumba na Makazi, Sayansi na Teknolojia, Kilimo, Viwanda, Maji, Elimu na Afya ni lazima kuainishwe ni kwa jinsi gani masuala ya jinsia yanazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, ningependa kupendekeza yafuatayo hasa tutakapoingia kwenye hatua ya utekelezaji:-

Kwanza, kuwepo na viashiria maalum (*Special Indicators*) vya kufuutilia usawa wa jinsia katika utekelezaji wa kila kipaumbele kilichoainishwa.

Pili, kuwepo kwa kitengo au focal person ndani ya Tume ya Mipango ambaye atakuwa na jukumu la kila siku kushughulikia, kusaidia na kufuutilia uingizwaji wa jinsi (*Gender mainstreaming*) katika utekelezaji wa Mpango. Kitengo hiki pia kitumike kushauri na kuzielekeza Wizara, Idara na Halmashauri zote nchini jinsi ya kutengeneza viashiria muafaka (*appropriate indicators*) za kupima matokeo ya jinsi utekelezaji ulivyozingatia masuala ya jinsia hasa katika kutambua fursa za ajira na maendeleo ya Rasilimali watu kati ya wanawake na wanaume.

Tatu, uwepo wa *Gender Audits* kwa kila kipaumbele kilichoainishwa. Naunga mkono hoja.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kutoka maeneo yafuatayo:-

Kwanza ni elimu. Ni kweli kwamba Mpango umetilia maanani katika kukuza rasilimali watu katika maeneo ya Elimu ya Msingi, Sekondari, Elimu ya Juu na VETA. Maoni yangu katika hili ni kwamba, badala ya kuvuka ngazi moja ya elimu ambayo ni elimu ya awali (*Pre- Primary Education*), Mpango huu uzingatie uanzishwaji wa Elimu ya awali kwa shule za Serikali kuliko ilivyo sasa ambapo kila mzazi anajitegemea kutafuta shule ya awali katika sekta binafsi na ni wachache hasa wa mijini ambaa ndio hupata fursa hii ya kusomesha watoto wao katika shule hizo. Watoto ambaa hawakupata

mafunzo ya awali inawawia vigumu pindi wanapoanza darasa la kwanza kulinganisha na wale ambao wameipata. Katika hili, walimu wawe ni wale waliostaafu na hasa wanawake maana wanaonesha uwezo mkubwa katika kulea watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika elimu ni kuhusu uanzishwaji na upanuaji wa Vyuo Vikuu katika maeneo kadhaa. Suala hili ni geni lakini ningependa kutoa angalizo kwamba kwa kipindi hiki “*Transition period*” tunapokuwa tunasubiri kupata Wahadhiri wa kuwafundisha wanafunzi ambao nina imani watadahiliwa kwa wingi, ni mkakati gani umefanywa ili kuwafundisha hao ambao tunawategemea kuwa wataalam wetu ifikapo 2015? Hii idadi kubwa ya wanafunzi na hivyo Vyuo Vikuu vinavyotegemewa kuanzishwa, vitahudumiwa na wataalam kutoka wapi na wanafunzi watafundishwa na Wahadhiri wapi wakati kwa sasa kuna upungufu mkubwa wa Wahadhiri hasa katika ngazi za Wahadhiri wenyewe (*Dvs*), Wahadhiri Waandamizi – *Senior Lectures* na kuendelea? Serikali katika Mpango huu imejipanga vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kushauri Serikali, ili kuondokana na tatizo la uhaba wa walimu katika shule za sekondari hususan za kidato cha tano na sita, badala ya kutoa tu ajira na kuongeza udahili katika vyuo vya juu kwa wanafunzi wanaochukua Shahada ya Elimu, ni vizuri sasa Serikali ikaingia mkataba wa lazima na wanafunzi wote wanaomaliza Shahada hizo kutoka vyuo vikuu binafsi na vya umma wanaopata mkopo toka Bodi ya Mikopo, kwamba ni lazima wanafunzi hao wanapomaliza wakafundishe katika sekondari za Serikali kwa miaka mitatu au minne bila kuondoka na wasipofanya hivyo wawe tayari kurudisha mkopo kwa mkupuo na hatua zingine zichukuliwe. Kwa kufanya hivyo, Bodi ya Mkopo itakuwa na nafasi nzuri ya kuweza kukusanya au kurudisha fedha za mkopo kwa urahisi maana tayari itakuwa inawafahamu watumishi wake na mahali walipo. Hii itasaidia kutoa fursa ya kupata fedha ili kuongeza idadi ya wengine wenye kuhitaji mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kuhusu Katiba mpya ya nchi na mchakato wake katika Mpango huu kwa bahati mbaya haujaingizwa. Najiuliza ni vipi Katiba mpya itaanzzishwa bila kuwa na mpango na bajeti ya kuanzishwa kwake? Hili nalo linatakiwa litiliwe mkazo na liongezwe katika Mpango wa miaka mitano ili muda huu tunapojiandaa na mchakato wa kuandaa Katiba mpya tuwe tayari na bajeti yake na iwe imewekwa kama kipaumbele kati ya hivyo vingine vilivyoainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nathubutu kusema kuwa ni mpango mzuri sana iwapo utatekelezwa ni mpango wa ukombozi wa Mtanzania katika maisha bora. Mipango yote iliyotajwa tuwaeleweshe Watanzania wote washiriki kikamilifu kwa pamoja tufanye kazi kwa bidii, tuuheshimu muda, sababu Serikali pekee haiwezi bila kuwashirikisha wananchi. Leo wananchi na wafanyakazi walio wengi hawajui wajibu wao. Kila Mtanzania kwa nafasi yake ajitume kwa bidii kama ni mkulima au mfanyakazi lazima ajitambue na wajibu wake. Kuhusu viongozi kuanzia ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya, Kata na Vijiji tushiriki kwa pamoja kuunga mkono Mpango huu kwa vitendo na sio kwa maneno tu. Miaka mitano si mingi

tusipoutekeleza Mpango huu, Watanzania hawataielewa tena Serikali yao na kupoteza imani kwa Taifa lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kama Mbunge wa Jimbo la Nyang'hwale wananchi wa Jimboni kwangu kwa hali ya umaskini walionayo kupitia Mpango huu hususan wakulima tunaona kuwa kweli iwapo tutatekeleza basi ukombozi wa maisha bora kwa kila Mtanzania ndoto itakuwa imekamilika. Katika utekelezaji Serikali itoe taarifa ya kiwango cha fedha zote zinazotolewa sehemu husika katika *Notice Board*. Sehemu husika ili wananchi waelewe na kuwatia moyo zaidi wa kuunga mkono Mpango huu. Kwa kufanya hivyo kutazuia ufujaji wa pesa kiholela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Mpango huu kwani ni muhimu sana kwa Taifa letu.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *agenda* kubwa kwa Mpango huu ni ukuaji wa Uchumi na kuondoa au kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kutayarisha Mpango huu japo umekuja umechelewa. Umechelewa kwa sababu nchi yetu ina rasilimali nyingi ambazo zingetumika vizuri kwa miaka mingi ya nyumba, uchumi wetu ungeshakua sana. Mpango huu hauna miujiza ya ziada kwa kuwa rasilimali ni zile zile, nguvu kazi (*Human Resource*) ni le ile na watunga mikakati ni Watanzania wale wale. Hii ni sawa na *Self Assessment* na kuja na mikakati mipyta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati inayowekwa na Mpango huu umeboreshwa sana, mbinu mpya imewekwa na hivyo tunaona sasa mwanga wa kupambana na umaskini, ujinga na maradhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango ni dira na hivyo ni lazima watekelezaji wa Mpango wafuate dira kwa utekelezaji makini na sahihi. Mipango yetu mingi ni mizuri lakini utekelezaji umekuwa tatizo kubwa. Naomba utendaji kazi wa watumishi wa umma utazamwe upya kwa sababu uwajibikaji ni hafifu mno. Pia uaminifu ni tatizo kwa watekelezaji na uhuru wa kupita kiasi, kutojali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango uainishe wazi yafuatayo:-

- (a) Watekelezaji wa kila eneo husika.
- (b) Adhabu itakayoendana na kutotekeleza au kutowajibika na uaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu utafanikiwa kwa kuwa:-

- (a) Nchi yetu ina rasilimali za kutosha.

(b) *Geographical positioning* – Bandari zetu, Reli, Bahari, Maziwa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Mpango huu uangalie sana tofauti kubwa iliyoko baina ya jamii za Kitanzania. Tumetofautiana sana kimaendeleo mkoa hadi mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Manyara uligawanyika toka Mkoa wa Arusha. Mkoa huu hadi tukaribie kama Arusha tuna njia ndefu. Arusha inaunganisha Wilaya zake zote kwa barabara za lami. Arusha-Longido, Arusha-Karatu, Arusha-Monduli, Arusha-Arumeru, zote ni lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija Manyara Barabara za Babati-Mbulu, Babati-Hanang, Babati-Kiteto, Babati-Simanjiro na Babati vijiji zote ni za vumbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwa Mpango huu uzingatie “vipaumbele vya vipaumbele”. Ukitazama Mkoa wa Manyara una fursa nyingi sana ambazo ni uzalishaji wa mazao tunaongoza na uzalishaji wa mazao yatokanayo na mifugo na kuwa na mifugo mingi tunaongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Viwanda vya Nyama na Mazao viro Arusha, wakati mifugo mingi iko Simanjiro, Kiteto na Hanang.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mpango huu uzingatie kukuza uchumi wa Manyara, kuongeza ajira ya vijana wa Manyara kwa kuanzisha viwanda Manyara ambako kuna uzalishaji zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu ujumuushe pia kujenga viwanja vya kisasa vya michezo ya Riadha Mkoani Manyara ambako kuna *Potential* kubwa ya kuwepo kwa wanariadha bora. Michezo katika mpango huu haijapewa umuhimu unaopaswa. Wachezaji riadha walioweka Tanzania kwenye ramani ya dunia walitoka Manyara na hivyo naiomba Serikali iweke michezo kuwa sehemu ya Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango ni mzuri sana, ila nashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, badala ya kuelekea Dar es Salaam kutoka eneo la Mlandizi hadi Ubungo linakabiliwa na msongamano mkubwa wa malori, gari ndogo na mabasi ya abiria. Katika Mpango huu napendekeza ijengwe barabara mbadala inayoanzia Mlandizi-Mzenga hadi Kisarawe. Hii itasaidia malori yote ya mizigo kupitia barabara ya Mlandizi-Mzenga-Kisarawe hadi Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ujenzi wa bandari kavu ya Kisarawe ambayo imeainishwa katika Mpango huu ni muhimu sana. Nakazia pia ujenzi wa barabara tajwa hapo awali, itaongeza ufanisi wa kitendaji katika bandari kavu ya Kisarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Mikoa ya Ukanda wa Pwani imekuwa nyuma kwa kipindi kirefu katika maendeleo ya kiujumla. Napendekeza katika Mpango huu kuipa kipaumbele kwa kuiwezesha Mikoa ya Ukanda wa Pwani. Matumizi ya Mabonde ya Mto Ruvu na Mto Rufiji yatasaidia sana maendeleo ya kilimo na ukuzaji wa maendeleo katika Mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ushirikishaji wa vijana na wanawake katika utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu inayotarajiwa kutekelezwa ndani ya Mpango huu. Hii itasaidia vijana na akinamama kupata ajira ambayo itasaidia kukuza uchumi sambamba na utekelezwaji wa mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, naomba suala zima la usimamizi lipewe kipaumbele. Tuache kufanya kazi kimazoea. Watendaji, viongozi wa siasa na wanajamii, sote kwa pamoja kushiriki ipasavyo katika kufanikisha Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, kubuni mipango mbalimbali ya kuongeza pato la Taifa tukikazia mapato ya ndani. Tuendelee kubuni vyanzo mbalimbali vyta mapato na kudhibiti mianya ya ukwepaji kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. SAID MUSSA ZUBEIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Pili, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuamua kwa makusudi kuanzisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa maslahi ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mpango umekamilika na kama tutaufuata kama ulivyo na kujitolea kufanya kazi kwa moyo mmoja kila mtu kwa sekta yake na kuwajibika ipasavyo nchi itabadilika na maisha mazuri kwa kila Mtanzania yataonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango umekamilika, kasoro ndogo ndogo za kibinadamu haziachi kuwemo ili kila zitakapojitokeza tuwe tayari kuzirekebisha kwa manufaa ya umma. Kwa upande wangu nilihisi tuwe na vipaumbele ndani ya vipaumbele hivi vilivyokuwemo kwenye Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kawaida kwa mwenye njaa, kipaumbele chake cha kwanza ni kutafuta chakula ila chakula kikiwa mezani huja mawazo mapya ya kipi cha kuanza kati ya chai au mkate. Kama hajatia kitu tumboni kwa muda mrefu basi kipaumbele cha mwanzo huwa ni chai kabla ya mkate ili alainishe koo na kushtua tumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, basi mawazo yangu yanahisi kipaumbele cha mwanzo kabisa ni umeme wa uhakika, pili, rasilimali watu yaani elimu na mengine yafuate kama yalivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kusitiza kuwa ni lazima tufunge mkanda wa kujituma kwa hali na mali ili tufikie malengo, vinginevyo mipango mizuri hii itabakia kwenye makabrasha na kufungiwa makabatini na mwisho wake kuwa historia kwa watoto wetu na wajukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa nia yake safi na ya dhati kabisa ya kutaka tuondokane na hali tuliyonayo, tushirikiane nae na tumuunge mkono kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naunga mkono hoja.

MHE. EUGEN E. MWAPOSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuja na wazo hili la Mpango wa maendeleo kwa kipindi cha miaka mitano. Nampongeza kipekee Waziri na Idara ya Mipango kwa kazi nzuri waliyoifanya pamoja na kutumia muda mfupi wa maandalizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya jambo zuri kuona kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuwa na mpango utakaokuwa kama dira ya Serikali katika utekelezaji wa mambo yaliyoainishwa katika mpango huu kwa kipindi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga ni jambo moja lakini kutekeleza nako ni jambo lingine na ndilo muhimu zaidi maana ndilo linalotoa matokeo baada ya kipindi kwisha na kufanyiwa tathmini ya mafanikio. Nchi yetu wakati mwingi imekuwa na mipango mingi mizuri lakini utekelezaji umekuwa kikwazo kikubwa cha mafanikio ya mipango hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuhakikisha kwamba inasimamia Mpango ili uweze kutekelezeka vizuri. Natambua mara nyingine mipango mizuri hukwama kwa sababu ya kifedha haswa ukizingatia kuwa Serikali inapanga lakini mfadhlili wa mipango hiyo kwa sehemu kubwa ni nchi au taasisi au wadau toka nchi za nje. Hivyo, wasipotimiza ahadi zao bado mipango yetu itabakia bila kutekelezwa. Kwa sababu hiyo naishauri Serikali kufanya juhudhi kubwa za kukusanya mapato yake ya ndani na kubuni vyanzo vipyta vya mapato ili kuendelea kupunguza au kumaliza kabisa utegemezi wa bajeti ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu una vipaumbele vyake vitano (5). Vipaumbele hivi ukivitazama ndizo kero kubwa kwa wananchi wa Tanzania. Vikitekelezwa hata kwa asilimia 50 vitakuwa vimemtoa Mtanzania katika kero kubwa. Lakini naishauri Serikali baada ya Mpango huu kupitishwa na Bunge lako Tukufu basi Mpango huu ushike chini kwa watendaji na wananchi kwa kutumia semina au majukwaa ya wanasiaya ili kuwaelimisha wananchi ili wajipange katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo lililojitokeza nchini siku hizi za karibuni, wananchi wamekuwa na tabia ya kulaumu mno na kulalamika kuwa Serikali haifanyi hiki au kile, wameshindwa kujua kuwa Serikali ndio wao na wanatakiwa wachukue mpango

huo waufanye wakwao, wachape kazi kwa bidii ili kuongeza vipato vyao na kupata maisha bora ambayo kwa ujumla wao ndio tunasema pato la Taifa kwa jumla limekuwa na kugusa maisha halisi ya mwananchi. Bila wananchi wa Tanzania haswa vijana kubadili tabia na kuamua kufanya kazi ni vigumu sana kubadili sura ya nchi haswa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ianze kuchukua jukumu la kuwafundisha vijana katika shule za sekondari na vyuoni kuwa wajiandae zaidi kujiajiri badala ya kupoteza muda mwingi kutafuta kazi ambazo imekuwa vigumu kupatikana. Tukiwatayarisha na kuhakikisha wanapata fursa za kupata mikopo katika taasisi zetu za fedha basi tutapunguza tatizo kubwa la ajira na pato la Taifa litaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. FENELLA E. MUKANGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Mpango huu. Nashauri pamoja na vipaumbele vilivyowekwa ambavyo nakubaliana navyo kabisa. Ni muhimu suala la “habari” na vijana” lijitokeze kwa kuonesha umuhimu wake kwa dhati katika Mpango. Wahusika waainishwe, wawezeshwe na wasikilizwe, pia wawajibike kuleta na kusimamia matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Habari 2.3.3 – *Supporting Infrastructure (Under science, technology and Innovation – page 31-32)*. Nashauri “ICT” isiwekwe in a general sense ibebe umuhimu wa habari kama kiungo muhimu katika hiyo communication technology au mkonga kwa maana ya information kama rasilimali inapewa umuhimu wake kwa maana ya kuweka mpango madhubuti wa kuhakikisha tunaendelea kujenga jamii yenye uelewa chanya wa misingi na maadili ya habari. Pia mpango wa kuwezesha Serikali to communicate between self and its people, effectively and efficiently.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuhakikishe katika Mpango *information support forms* zinapewa umuhimu wake na zinapangiwa mikakati. *Information support forms* kwa maana ya *information resources* (Rasilimali za habari) *information sources, services, systems*. *Page 142 to 143 to be coordinate in collaboration with HVUM – for Information support forms to be harnessed. And ensure consistent development of information literate Tanzanians. With capacities to manage the information explosion and the challenges of daily changing technologies and the rising expectations of our young population.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikumbushe tu kwamba *British Council Library, USIS* na *USAID* iliyopo sasa haipo kwa bahati mbaya. Ni mpango wa makusudi wa kuwekea *support forms* za Serikali zao. Kujengea *infor capacities* zao na sisi tunapata, kubwa ni wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Habari vijana, katika hili *support form* za habari vijana wetu watapata kazi na ni sehemu kubwa pia ya *empowerment* kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya *the decision we make are as good as the information they are based on*. Hii iko *live* katika settings zetu. Sasa au kwa kiasi gani maamuzi yetu ya maendeleo na mipango kama viongozi na *decision makers* kwa ujumla yanafanyika *based on, timely, accurate and appropriate information for development?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zote zilizoendelea zina utamaduni wa kujenga watu waelewa wa habari na kujituma na kuanzia na kujenga utamaduni wa kujisomea na kusimamia Utaifa na uzalendo wao. Sisi hatutaweza kutumia hizi *ICT* kama hatutakuwa na utamaduni wa kujisomea. Mipango ipeleke dhana ya kujisomea nchi nzima. Magazeti ni *sensational news*, ni matokeo sana sana ya ukosaji ufahamu mpana wa nini habari ya kumjenga mwananchi na nini udaku, uzushi au uchochezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *bookshops, novels* na vitabu mbalimbali vyatoto vyenye kujenga tangu utoto dhana ya kusoma ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa 69 wa Mpango unazungumzia (*Education and skills level*). Nashauri kuwe na mkakati wa kutoa *information experts/officers responsible for managing and developing infor support forms at all levels*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia katika Mpango suala la *employment creation* lipangwe kama *youth empowerment* kwa mfano, katika *page 178* (A.1.8) hayo yapo ndani ya sekta ya vijana. Sasa masuala ya *employment creation* ni masuala ambayo kila sekta au Wizara na sekta binafsi na *informal sector* watabeba kama jukumu kuu ikiwemo Wizara ya Kazi na Ajira. Wizara ya Vijana kama jukumu lake la kusimamia na kubuni mikakati ya maendeleo ya vijana itasimamia hilo kuhakikisha *employment creation* walengwa wakuu ni vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kusema hayo bado Mpango na mikakati ni kwa namna gani hii inaweza kufanyika, bado haijaka vizuri katika Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie vijana, michezo, utamaduni (Sanaa mbalimbali). Mipango ibuniwe na ile ya vijana waliyonayo hasa kupitia sanaa ya utamaduni iwezeshwe ili tuhakikishe vipaji mbalimbali vinakuzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujenge uwezo wa vijana kuboresha kazi zao kwa kupitia Mpango na kuona uwezo wa sekta binafsi kubeba masuala ya *theatre arts*. Pia Serikali iweke miundombinu ya kuhakikisha tuna Mpango wa kuwa na viwanja vyatya michezo (Wizara, TAMISEMI, Elimu, *Non Government, Private et cetera*).

Katika *employment creation*, ningeweza kutoa ushauri kila Wizara na sekta muhimu au vile vipaumbele vyatya Kitaifa viweke kigezo cha angalizo la vijana, kuhakikisha maendeleo ya vijana ndani ya sekta zao au vipaumbele vyao vinatekelezeka. Sasa hii inawezekana na Wizara inaweza kuhakikisha inasimamia nafasi ya vijana ndani ya Wizara husika (sijui kama hii inawezekana). Nadhani kukiwa na *political will* ya dhati inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango ubebe:-

(a) Mikakati iliyopo ya kuwawezesha vijana wa ngazi zote kuweza kujajiri, nashauri labda kuwe na mkakati wenyewe kuwatayarisha kujajiri na kuajiri wenzao (*Youth Empowerment*).

(b) Mpango wa kuona ujasiriamali (sio pesa mfukoni tu). Pesa iwe pia ya kuwawezesha kujitambua, kuwa na tabia, mwenendo na hulka ya kujituma na kuthubutu kufanya kazi kwa malengo. Vituo vya vijana visivyoratibiwa viangaliwe (Hili Wizara ya Vijana inalishughulikia).

(c) *Work hard and smart* na kupenda kazi na kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango na mikakati ipewe *resources* za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Vijana mpaka sasa ni muhimu uwe na pesa za kutosha za kuweza kufikia mahitaji ya vijana na ngazi mbalimbali kwa shughuli za ujasiriamali lakini pia za *youth empowerment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa utekelezaji wa Baraza la Vijana *in line with African Youth Charter*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu michezo. Pia haikujitokeza katika Mpango, ni namna gani tutaoa kipaumbele kuhakikisha tunakuza vipaji mbalimbali, kutoa uwezekano wa kutumia njia tofauti – muundo kadhalika wa michezo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa *Community Sports* nchini pia upatiwe mtazamo wa karibu. Hii ni kutokea kila Kijiji, Kata na kadhalika na itatoa nafasi ya ajira, vijana imara, watiifu, mshikamano na amani.

Changamoto nyingi za michezo utatuzi wake upewe mpango unaoelewaka. (sijui kama hii *plan* iliwafikia watendaji wa Wizara katika hilo au Vyama vya Michezo. Ainisheni mipango ibebe hayo ya sera ya maendeleo ya michezo na wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia utamaduni. Yale ya msingi hasa yaendanayo na vijana wetu na maadili ya Taifa ikiwemo kuendeleza amani ni muhimu yajengewe mikakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, MKUKUTA II umebeba michezo na Utamaduni, *please contact the responsible* watendaji *to provide the priorities for the next five years*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango utoe kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Ilani ya CCM na ahadi za Rais. Hizo *small prints* zibebe hayo zaidi. *So far*, naona imebeba kwa kiasi kikubwa lakini tutenge pesa kwa hayo.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika mambo yafuatayo:-

Kwanza, wazo la Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ni zuri na sahihi kwa nchi yetu ambayo inakabiliwa na changamoto nyingi. Lakini, kama wachangiaji wengi walivyoonyesha, Mpango una mapungufu katika maeneo mbalimbali, mfano ugharimiaji wa mpango (ugharimiaji mkubwa ni wa mashirika au nchi za nje), tatizo la ubainifu na uhakikifu wa mpango, uthabiti wa viashiria vya malengo na utekelezaji wa Mpango wenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu ni kwamba, Tume izingatie maoni ya Kamati ya Fedha, msemaji wa Upinzani na wachangiaji wengine ili tupate Mpango wa Taifa ulio bainifu, pangifu na hakikifu. Napenda kusisitiza, kama wengine walivyositisiza, kuwa Mpango utangazwe kama Mpango wa Taifa bila kuingiza ushabiki wa vyama kwa sababu vyote vimeshiriki katika kuuandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya angalizo hilo, naomba nitoe maoni katika mambo yafuatayo:-

Nitaanza na utamaduni wa mazoea ambao umekuwa kikwazo katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika miaka 10-20 iliyopita. Utamaduni huu wa mazoea unahusisha mambo yafuatayo:-

Usanii (kutofanya mambo kwa makini), ufisadi, uzembe wa makusudi na ubinagsi. Je, Serikali imejipangaje ili misingi ya umakini, uchapakazi, uadilifu na uzalendo itawale katika utekelezaji wa mpango huu? Nauliza swali hili kwa sababu bila kujipanga sawasawa katika jambo hili, mafanikio ya mpango yatakuwa chini ya malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni jambo halikuzungumziwa kabisa na Mpango. Hili linahusu nafasi ya Lugha katika maendeleo. Naomba jambo hili tulitafakari kwa makini. Napenda kusisitiza kuwa hakuna nchi ambayo imeendelea kwa kutumia Lugha ya kukopa. Nchi zote ambazo zinaendelea mfano, China, Japan, Malaysia na kadhalika zimetumia Lugha zao ambazo zinasemwa na raia wao. Hata nchi ndogo sana kama Iceland (yenye idadi ya watu 250,000 tu!). Nchi hizi pia hutumia Lugha za kigeni (Kiingereza, na kadhalika) katika shughuli maalum. Hapa Tanzania utumiaji wa Kiswahili kufundishia Shule za msingi hadi vyuo vikuu utarahishisha utoaji wa elimu na uelewa na uhawilishaji wa Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kusema kuwa, tusipuuze Kiswahili, tukipe hadhi yake. Hii haimaanishi kuwa Lugha nyingine hazihitajiki, zinahitajika; zifundishwe vizuri ili ziweze kutumika katika Nyanja husika. Nashukuru.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kupongeza watendaji wote walioandaa Mpango huu wa Maendeleo kwa Miaka Mitano 2011/12 – 2015/16. Kwa kuwa Mpango huu umetokana na dira ya miaka ya 2025 na mpaka sasa hii dira imemaliza miaka kumi. Tunaitaka Serikali ieleze Bunge hili

ndani ya miaka kumi ya *vision 2025* kwenye yale malengo matano tumefanikiwa kwa kiasi gani? Ni muhimu sana kuwa na utaratibu wa kutathmini mipango tunayojipangia ili tuweze kujua na kuwaeleza Watanzania tumefanikiwa wapi, tumeshindwa wapi na tunakwendaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango umeeleza kwamba kilimo kinaajiri zaidi ya asilimia 74 ya Watanzania kwa kutambua kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa Watanzania wote wa vijiji na hata wa mijini. Ni vizuri Mpango ukazingatia sana sana azma ya kujenga miundombinu ya ukusanyaji maji kwa ajili ya umwagiliaji, kilimo cha kutegemea mvua hakina uhakika. Mvua zinanyesha mpaka zinaleta mafuriko na uharibifu mkubwa, lakini baada ya hapo, mazao ya wakulima yanateketea mashambani, wananchi wanakosa maji ya matumizi majumbani, vilio vinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina mifugo mingi sana lakini inachangia kidogo sana kwenye pato la Taifa, 4.6%. Hii inatokana na kutokuwepo na mpango mahususi wa kuwainua wafugaji. Wafugaji wengi bado wanafuga kienyeji vijijini na hata mazao ya mifugo ile bado soko siyo la uhakika. Maziwa mengi yanamwagwa huko vijijini, mifugo inakuufa kila leo kwa kukosa matibabu ya uhakika. Pamoja na Mpango kuwa na machinjo matatu ya kisasa, suala la soko la maziwa ya ng'ombe, mbuzi, mayai na kadhalika bado ni tatizo. Ili Taifa lifaidike na ufugaji lazima kuwa na wataalam wa kutosha, waende vijijini sio wa sasa ambao wanakaa mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo ya ngozi za wanyama wetu yamekuwa yana shaka kila panapotokea *financial crises*, hii ni kwa sababu ndani ya nchi hatuna mpango mahususi wa kutumia ngozi yetu kutengeneza bidhaa mbalimbali. Viwanda vyetu vya ngozi viro, lakini haviendelezwi na vingine vimekufa kabisa. Tunategemea kuinua uchumi wa nchi za wenzetu China, Thailand, South Africa, Uarabuni na kadhalika kwa kununua makontena lukuki ya viatu, mabegi, pochi za akinamama, bangili na kadhalika huku ngozi zetu zikioza huko vijijini na mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima katika kutekelezaji wa Mpango huu Serikali ihalalishe mali au malighafi zinazopatikana ndani ya nchi yetu zinatumika, kuziongezea thamani na kuziwa nje ya nchi ili kulinda shilingi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasumba ya Taifa hili ya kuagiza kila kitu nje hata maua, *tooth pick, cotton buds*, ni aibu kwa Taifa. Hivi kweli kwa kutumia mbao zetu za Sao Hill na Mufindi hatuwezi kuwapa vijana ajira ya kutengeneza *tooth pick* zikasambazwa madukani na hata kuuzwa nje? Hata masuala madogo yanatushinda? Masuala yasiyohitaji utsalamu wowote wala kuwa darasani? Wakati huo huo vijana mamilioni hawana kipato chochote hata elfu moja (1,000/=) kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli huu ni Mpango waTaifa zima na kila mmoja anatakiwa kushiriki lakini wapo viongozi au watendaji wa Serikali ambao tunategemea waongoze au waelekeze utekelezaji. Tanzania tuna unafuu wa kuwa na mipango mizuri lakini kwa kukosa watendaji waadilifu na waaminifu tumekuwa tunashindwa kutekeleza na kufanikiwa. Ili kuwa *realistic* ni vizuri Serikali ikaweka sheria au kanuni

zitakazowabana watendaji wabovu, wasiokuwa wazalendo, wenyewe uchu, wabinafsi na adhabu kali kwa wote watakaokiuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Taifa letu kuwa na misitu, eneo kubwa sana lakini pato la mazao la misitu kwa uchumi wa Taifa ni mdogo sana kutokana na changamoto zilizolezwa *page 22* ya Mpango huu. Kikubwa na cha msingi ni lazima Serikali kutoa nishati mbadala au mkaa kwa matumizi ya kupikia. Nishati ya uhakika inahitajika ambapo wananchi wengi wanamudu! Vinginevyo uhalisia wa eneo linalolezwa kuwa na misitu hapa nchini siyo kweli kwani misitu mingi imebaki vichaka, miti imekwisha. Usafirishaji haramu wa mbaao, magogo na nyara za Serikali ni tatizo kubwa. Watendaji wa misitu na wanyamaporu wanashiriki kwenye wizi huo lakini hakuna hatua zinazochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. NASSIB S. OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali kwa kutayarisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2011/2012 – 2015/2016, naukubali Mpango huu. Ukiupitia Mpango huu, haukujikita katika mambo ya muungano au mambo yanayowahusu Wazanzibari. Moja, katika maeneo ambayo yanaweza kupunguza umaskini visiwani ni kuendeleza bahari kuu na uvuvi mdogo mdogo. Uvuvi wa bahari kuu utasaidia kujenga Viwanda vya Samaki hivyo kusaidia kutoa ajira kwa wananchi pamoja na kulilettea Taifa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi mdogo mdogo utawagusa moja kwa moja wananchi na hivyo kuongeza kipato chao. Ili itimie azma hii Serikali isaidie kupatikana kwa mikopo midogo midogo ili uwasaadie wavuvi kununua zana za uvuvi. Pia teknolojia za kiwango kidogo kama ukaushaji samaki kwa kutumia *Solar*. Utengenezaji wa boti za uvuvi, utengenezaji wa nyavu na vifaa vingine *locally*.

MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielekeze mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu kilimo. Asilimia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo, mifugo na uvuvi kama shughuli za uchumi na maisha yao ya kila siku. Kisiasa tukidhamiria kuwaahidi wananchi maisha bora kwa kila Mtanzania bila kuwa na mikakati madhubuti katika eneo la kilimo, dhamira hiyo haitatimia. Natambua kilimo ni moja ya vipaumbele vitano, lakini napenda kuweka msisitizo katika sehemu zifuatazo:-

- (a) Tuwekeze zaidi katika elimu kwa mkulima hususan walioko vijijini.
- (b) Tujikite katika kuweka mazingira wezeshi ambapo mkulima atawezza kupata pembejeo.
- (c) Nia njema ya Serikali ya kutoa pembejeo za ruzuku ichukuliwe kama ni mpango wa mpito ambao hatimaye utakufa.

(d) Kuwa na mikakati ambayo wananchi wanaoishi katika maeneo yaliyo kame watalima mazao yanayostahimili ukame na waweze kuwa na akiba. Suala la Serikali kutoa chakula cha njaa limefanya baadhi ya wananchi kubweteka na kuona kwamba chakula cha njaa ni haki yao.

(e) Umwagiliaji unaweza kuleta mageuzi katika kilimo na mifugo endapo maji ya mvua yatavunwa, mabwawa kuchimbwa na maji hayo kuhifadhiwa.

(f) Pamoja na kwamba Tanzania ina eneo kubwa la Bahari ya Hindi, mapato yatokanayo na uvuvi ni mengi kutoka maji baridi kuliko yale ya baharini. Tukitaka kuimarisha sekta ya uvuvi ni lazima tukubali kuwekeza katika *deep sea fishing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Uwanja wa Ndege wa Songwe, ukiacha Uwanja wa Mtwara, Mikoa yote iliyoko Kusini mwa reli ya kati haina uwanja wa ndege wa Kimataifa. Wananchi waishio Nyanda za Juu Kusini walifurahishwa na uamuzi wa Serikali wa kujenga Uwanja wa Songwe. Mategemeo ulikuwa ukamilike kabla ya mwaka 2007, lakini mwaka 2011 mradi huo unaingizwa katika Mpango wa Maendeleo ambapo utakamilika 2015. Sioni kama tunawatendea haki wananchi wa kanda husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 133 wa Mpango, pesa inayokisiwa kugharimu kukamilisha mradi huu ni Shilingi 43,000 milioni. Binafsi naamini kwamba pesa hizi zinaweza kutafutwa na kutumika ili kukamilisha mradi huu muhimu mapema kabla ya mwaka 2015. Naomba kuwasilisha.

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kuwepo hapa salama, lakini pia nimshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira kwa kuwasilisha Bungeni Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/2016).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Miaka Mitano uliozinduliwa na Rais tarehe 7 Juni, 2011 haukizingatiwa katika kuunda bajeti katika mwaka 2011/2012. Utekelezaji wa Mpango ulikadirwa kugharimu shilingi *trillion* 8.277 ukilinganisha na bajeti ya maendeleo ya shilingi trilioni 4.295, uchambuzi wa utekelezaji wa mpango haumo kabisa katika bajeti ya Waziri. Inaonyesha hakuna utaratibu kati ya Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango, katika hali hii Mpango wa Miaka Mitano uliozinduliwa na Rais hauwezi kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi kama haitoshi wasiwasi wangu bado upo pale pale kwenye utekelezaji wa Mpango huu. Ni kweli kwamba hakuna ambaye halitakii Taifa la Watanzania maendeleo ya kweli, hivyo basi, naomba Serikali ijitahidi kutekeleza Mpango huu kama ilivyoupanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote, naunga mkono mpango huu. Ahsante.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nimpongeze Waziri, Mhe. Stephen Wasira kwa kuwasilisha vizuri Mpango huu katika Bunge lako Tukufu. Pili, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuona kuna haja ya kuingilia kati mpango wa muda mrefu wenyewe malengo ya *millennia* ya kukuza uchumi na kuondoa umasikini tufikapo mwaka 2025. Mheshimiwa Rais aliwaza vyema kuwa tutafanya vizuri zaidi tukiugawa sehemu iliyobakia ya miaka 15 kwa vipindi vitatu vya miaka mitano mitano ili tuweze kujipima kidira kama tunaendelea vipi na kama kuna eneo tunasuasua tujirekebishe. Hivyo, naunga mkono mpango mzima na Tume ya Mipango chini ya Katibu Mtendaji na wataalam wake waliouandaa mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wangu kutokana na viashiria vilivyoonekana kuwa uchumi wetu unakuwa kwa asilimia saba tu. Umaskini una upungufu usioridhisha na Mpango huu umeona lazima uanze katika vipaumbele vitakavyojibu. Kipaumbele cha pili cha kilimo nashauri, kwa kuwa kilimo ndicho kinachoajiri zaidi ya asilimia 74, sasa katika vipaumbele chini ya kilimo. Tushirikishe kwa nguvu wawekezaji katika kilimo na viwanda vinavyotumia malighafi ya kilimo lakini pia tuvifufue viwanda vilivyo simama kwa mfano, Kiwanda cha Kusindika Tumbaku cha Songea ambacho kilisimama kwa sababu aliyeomba ubia hakuwekeza chochote wakati kiwanda hicho kilikua kinaajiri watu zaidi ya 3,000. Huu ni mfano wa kiwanda kimoja knachotegemea malighafi ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Waziri wa Fedha alivyosema katika Hotuba yake aya ya 92 (iv) wakati anawasilisha Bungeni Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa, 2010 na malengo ya uchumi katika kipindi cha muda wa kati 2011/12 – 2015/16. Nanukuu aya 92: “(vi)... Rasilimali zitaelekezwa kwenye maeneo yanayochochea ukuaji wa uchumi kwa haraka zaidi”. Mwisho wa kunukuu...

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ndogo ya Tumbaku ni eneo linalochochea katika ukuaji wa uchumi kwa haraka. Kwa mfano hai, zao hili limekuwa likikua kimapato kwa mkulima na Taifa.

Msimu Sh.(Billion)	Tani za Tumbaku	Thamani ya Kilo
2009/2010	94,244	317,099,000,000/=
2008/2009	60,741	170,393,000,000/=
2007/2008	55,357	75,619,000,000/=
2006/2007	50,784	63,979,000,000/=

PATO LA WASTANI KWA MKULIMA WA TUMBAKU

Aina ya Tumbaku

Msimu	Mvuke	Moshi	Hewa
2009/2010	4,105,600	982,200	949,000
2008/2009	3,146,100	873,800	1,189,100
2007/2008	1,794,300	548,600	738,200
2006/2007	1,047,400	149,100	249,900

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushuru wa Halmashauri 2009/2010 umefikia bilioni 15,855. Kodi iliyokusanywa na Serikali Kuu.

Mwaka 2006	Shilingi bilioni 65.1
Mwaka 2007	Shilingi bilioni 80.4
Mwaka 2008	Shilingi bilioni 93.4
Mwaka 2009	Shilingi bilioni 98.8
Mwaka 2010	Shilingi bilioni 110.769

Mauzo soko la nje (*USD*)

Tumbaku

2006	2007	2008	2009	2010
65.1	87.8	176.4	127.4	232.4

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010 tumbaku imeuzwa nje zaidi ya mara mbili, zao la pili kwa thamani ya mauzo ya nje ya *Traditional Cash Crop* ambalo ni Kahawa lililouza dola 101.6 kati ya mauzo ya Jumla ya (USD 559.0 Million) ya mazao kama vile pamba, Korosho, Tumbaku, Chai, Katani, Kahawa na Karafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa takwimu hizo ili kuonyesha eneo hili la sekta ndogo ya Tumbaku linavyochochea ukuaji wa uchumi katika sekta hiyo na kwa pato la Taifa kwa ujumla wake. Hivyo, kama ilivyosema aya 92(vi) katika Hotuba ya Waziri wa Fedha, naomba eneo hili liwe katika kuongeza ukuaji wa uchumi. Litakuza ajira na uchumi wa watu wetu wanaoishi katika maeneo ya vijijini na kupunguza vijana wanaokimbilia mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha kupata nafasi ya kutoa mchango wangu kwa niaba ya Watanzania hususan wananchi wa Wilaya ya Kilombero. Mpango uliowasilishwa pamoja na vipaumbele vyake uko umuhimu wa kuboreshwa kwa kuzingatia michango ya Kambi Rasmi ya Upinzani na ya Wabunge na wadau nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mpango huo ni wa Taifa, utakuwa na tija iwapo utatekelezwa kwa kushirikisha wadau katika kada zote na hasa ngazi ya Halmashauri, hivyo hauna budi utafsiriwe kwa Lugha ya Kiswahili kabla ya kuufikisha kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele vilivyopo ni muhimu kwa maendeleo ya nchi. Ili vipaumbele hivi vileté tija ni ukweli kwamba katika kupata wataalam wa kufanya kazi na kuhamia. Hivyo basi, kipaumbele cha rasilimali watu; ambapo kinazungumzia kuboresha Elimu ya Sayansi na ugunduzi ni muhimu kikawekwa cha kwanza kwa kuwa elimu ni ufunguo wa maisha katika kupata wataalam watakaotekeliza na wanaotekeleza katika Idara zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi mpaka leo imekuwa tegemezi kwa miradi inayotekelawa na inayotarajiwa kutekelezwa kutokana na kutegemea wafadhili. Pia ukosefu wa usimamizi wa kutosha. Ili nchi iendelee inahitaji watu, ardhi na uongozi bora. Hivyo watu tulionao ni wengi na wanatosha kwa maendeleo, ardhi yenye rutuba na rasilimali zilizopo zinatosha zikitumiwa vizuri hata kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa na hasa kwa miaka ya kuanzia 80 hadi sasa tumeshuhudia ubadhirifu mkubwa katika sekta mbalimbali kuanzia Taifa hadi vijiji, pia unyanyasaji wa raia unaofanywa na vyombo vya dola na baadhi ya wawekezaji. Hivyo, kinachokosekana katika kufanya nchi iendelee kwa kazi ni Uongozi Bora. Hilo ni kikwazo kikubwa, watu wanaoaminiwa na wananchi baadhi yao hawana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kilombero wananchi wake wanaendelea kuwa maskini kwa kushindwa kusafirisha mazao yao kutokana na ubovu wa barabara na kufanya nauli iwe kubwa na hivyo kushusha thamani ya mazao ya mpunga na kadhalika, Mpango uone haya ya kuwezesha barabara hiyo iwe kwa kiwango cha lami. Pia Mpango utambue barabara inayounganisha Wilaya ya Kilombero na Wilaya ya Njombe, Mkoa wa Iringa ambayo inaanzia Ifakara-Mlimba-Taweta-Madeke ambapo mpakani Njombe ni kilometra 242. Ifunguliwe na iwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Wilaya ya Kilombero wamechoka kusikiliza na kuona maeneo mengine ya nchi yakiendelezwa kwa barabara za lami na wao wakikosa barabara za kiwango cha lami tangu Uhuru hadi leo hii ni miaka hamsini ya Uhuru na kuachwa kwenye lindi la umaskini. Kilombero ni Wilaya ambayo inatoa mchango mkubwa katika Taifa hili ambapo inazalisha umeme wa Kidatu, Kihansi, Kiwanda cha Sukari, Vyura wa Kihansi, Magogo (mitiki) mlima wa Udzungwa na mazao ya chakula. Hivyo ni muhimu rasilimali hizo ziwanufaishe pia wakazi wa Kilombero. Dhamira njema, uaminifu na nafasi walizopewa iko haja ya kuboresha sheria za kazi katika utumishi wa umma, ambazo zitakuwa na uwezo wa kuwajibisha kwa muda mfupi mara watakobainika kushindwa kutimiza wajibu walopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu pia umeweka kipaumbele katika miundombinu. Kipaumbele cha miundombinu, nizungumzie eneo la barabara. Pamoja na matarajio ya uboreshaji wa barabara zilizopo katika Mpango katika ukurasa wa 127 ambapo umeonyesha barabara ambazo zitafanyiwa matengenezo, katika kipengele hicho napenda kuzungumzia barabara ya Ifakara-Kidatu ambapo katika kitabu cha Mpango wa 2011/2012, ukurasa wa 90, barabara hiyo imetengewa Sh. 210,830,000 tu ambapo kiasi hicho ni kidogo sana, kwa kuwa barabara hiyo ni ya kilomita zisizopungua 80, hivyo itabaki katika kiwango cha udongo na changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kilombero ni Wilaya yenye bonde lenye rutuba na wananchi wanategemea kilimo cha mpunga, mahindi, miwa na mazao mengine ya mboga na matunda, mfano kilimo cha machungwa, Tanganyika masagati. Naunga mkono hoja.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza mchango wangu kwa kukiri na kusema kwamba, naunga mkono kwa asilimia mia moja. Naunga mkono kwa sababu kwanza umeletwa mbele ya Bunge wakati muafaka lakini pia umeandaliwa kwa umakini mkubwa ukizingatia hali halisi ya maisha na uchumi wa wananchi wetu na maendeleo ya uchumi duniani. Aidha, naunga mkono kwa sababu vipaumbele vilivyotajwa katika mpango huu ni sehemu tu ya vipaumbele vilivyomo katika *MDG* ambayo kwa kweli ndio vitakuwa msingi wa kuleta maendeleo ya kweli kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo muhimu la kuzingatia ni utekelezaji wa yale yote yaliyoanishwa katika Mpango huu. Hili litawezekana tu kama kila mhusika katika kusimamia utekelezaji atatimiza wajibu wake. Hapa namaanisha, Serikali kwa upande wake ijithahidi kama ni fedha basi iwepo tayari kwa wakati muafaka. Kwa pamoja wadau wote husika yaani Serikali, watendaji na wananchi tuweke uzalendo mbele kwa maslahi ya nchi yetu. Mpango huu ni dawa kwa matatizo mengi ambayo yalioneckana kwamba hayawezi kutatuliwa. Naunga mkono hoja.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, sinabudi kumpongeza Mheshimiwa Rais Dokta Jakaya Kikwete jinsi ya uzinduzi wa Mpango huo na pia jinsi alivyoueleza kwa walengwa na Tanzania ambao ndio watakaofaidika na Mpango huo. Vile vile nawapongeza Mawaziri pamoja na Bwana Mpango jinsi walivyouandaa Mpango huu na kuwasilisha kwetu, ukweli umeeleweka na ndio michango ikawa mingi yenye kuboresha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele vikuu vyta Mpango ni nishati ya umeme, usalama wa chakula (kilimo), miundombinu; ajira na mfumko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie usalama wa chakula (kilimo). Kilimo ndio uti wa mgongo, Serikali ikitaka kufanikiwa lazima ikinyanyue kilimo na bado wakulima hawajahamasika bado wanaendelea na kilimo duni cha kizamani. Tatizo wakulima wengi maskini hawana uwezo wa kununua nyenzo za kilimo. Vile vile waliomo ambao wanajishughulisha na kilimo ni watu wazima tena wamechoka. Vijana, wasomi ambao ndio wataalam wetu, wengi wanakimbilia mjini au kuijiingiza katika siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Serikali izidishe nguvu kwa vijana na kilimo, kwani wao ndio nguvu kazi. Vile vile na wanasiasa lazima wawe pia wakulima walime mwenyewe au watoe ajira hasa ukizingatia kuwa Tanzania kuna pori kubwa, kwa hiyo tunahitaji kutoa ajira ya kilimo ili vigezo vyetu vyta kilimo na ajira vifanikiwe. Hivi sasa Serikali ingehamasisha wafadhili kuja Tanzania kwa ajili ya kilimo, wawekeze katika kilimo ili Sera yetu ya kilimo kwanza ndio tutaitekeleza na kuweza kuwagombua Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mfumuko wa bei, hili ni tatizo ambalo linachangia njaa, kilimo ndio mkombozi na mfumko wa bei. Lazima tutambue kwanza bila ya kilimo na kuwa na chakula, vipi ajira zitafanyika na mipango yetu haitafuzu, kwa

bei za bidhaa zote kuwa juu lini zitashuka ili jamii ipate afueni ya maisha? Hivi sasa tunategemea kununua chakula nje ya nchi na Mtanzania wakati ananunua anakutana na kodi tofauti, hivyo lazima anunue kwa bei ya juu. Inakuwa haina uwiano baina ya muuzaji na mnunuzi. Mkombozi wa suala hilo ni kilimo na ndio kipewe kipaumbele, pasi na hilo usalama wa chakula haupo nchini na Mpango utasua sua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira, ukweli vijana wamejaa mitaani, tatizo ni ajira duni, kumbe ajira tunazo lakini Serikali haijatilia mkazo, bado tupo nyuma kwa kukipa nguvu kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu haukujikita katika afya, katika vipaumbele vitano afya haimo. Je, vipi tutaweza kufanya kazi bila ya kuwa na afya bora? Tukubali kwamba Watanzania wengi wana matatizo ya afya na bila ya afya hawataweza kufanya kazi yoyote, hivyo basi, suala la afya lipewe kipaumbele. Hata hivyo, tujue kwamba bila ya afya bora uchumi hauwezi kukua, kwani nguvukazi itakosekena. Pia wataalam tutawakosa na hata huo Mpango hautafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba, Mpango huu ni mzuri na umewagusa Watanzania wote na umegusa sehemu zote za jamii. Tunategemea utekelezaji mwema. Naunga mkono hoja.

MHE. ASHA MSHIMBA JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Dhana ya Mpango ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kufungua fursa za ukuaji wa uchumi wa Taifa ili Mpango uweze kufanikiwa haraka, lazima uwazi na uwajibikaji kuanzia ngazi ya chini mpaka juu tuwe tunazungumza na kutetea jambo moja. Mfano, katika kilimo, kila mwenye uwezo wa kulima lazima alime, ashibe na ndio asafirishe au auze na sekta nyingine vivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nchi hii ni ya kidemokrasia, hivyo kila mtu ni lazima aheshimu na kutii sheria mbalimbali zilizopo. Uhuru usio na mpaka ni fujo na hauendi sanjali na dhana ya mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni kuhusu fursa katika kutumia masoko mbalimbali. Juhudi za makusudi zichukuliwe kuelimisha wananchi kuweza kuyatumia masoko ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa elimu uliopo uweze kumwandaan kijana kukabiliana na mazingira magumu ya kuweza kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukuaji wa uchumi, ni kweli uchumi wetu unakua na kipato cha Mtanzania mmoja mmoja kinaongezeka, kuna kundi kubwa la

vijana ambao ndio nguvu kazi hawataki kujituma na kuzalisha, badala yake wanakimbilia mijini na kuzurura, sheria ya kuwashughulikia wazembe na wazururaji ifanye kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwe na dhamira ya dhati ya kuwawezesha wananchi wake kumiliki rasilimali ili iwawezeshe wananchi nao kushiriki katika ubia wa miradi mbalimbali. Naunga mkono hoja.

MHE. ANGELAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua fursa hii, kuipongeza Serikali kwa kuleta Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo ya Tanzania kwa Mwaka 2011/2012 – 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo utatekelezwa kama inavyoelekezwa, ni imani yangu kwamba, utasaidia kuinua uchumi na kuwaondoa Wananchi kwenye umaskini unaowakabili. Kila MWananchi anao wajibu wa kuchangia katika utekelezaji wa Mpango huo ili ulete mafanikio yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo kweli kuna nia ya dhati ya kuhakikisha Mpango huu unatekelezeka; ni vyema fedha za kutosha zikatengwa katika Sekta ya Kilimo, Ufugaji, Uvuvi, Nishati, Maji pamoja Uwezeshaji wa Kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Mpango huu utekelezeke ni lazima niliyoyataja hapo juu yapewe msukumo. Mfano, Wananchi wetu wasipowezeshwa kiuchumi ili nao waweze kuwekeza, tutakuwa hatujafanya lolote na tusipokuwa makini, tutakuwa na Wawekezaji kutoka nje tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kwamba, ipo Mipango mbalimbali ya kuwasaidia wawekezaji wa ndani. Hata hivyo, ni vyema Serikali iangalie namna gani riba ya mikopo kwa ajili ya uwekezaji inapunguzwa hususan msamaha wa kutolipa mkopo (*Grace Period*) ya miaka miwili au zaidi, endapo uwekezaji utachukua muda mrefu kukamilika, ndipo mkopaji aanze kurejesha mkopo aliouchukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ningependa kuishauri Serikali kuunda Chombo Maalum kitakachohakikisha kila Mradi unaotarajiwa kutekelezwa, unatekelezwa kama ilivyokusudiwa. Vilevile Chombo au Tume ya Mipango, iwasilishe Taarifa ya Utekelezaji au Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, angalau mara mbili kwa mwaka ili Waheshimiwa Wabunge, ambao ndiyo wawakilishi wa Wananchi, waweze kufahamu utekelezaji wa Mpango unaendelea vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kushauri kuwa, Bajeti ya Tume ya Mipango iongezwe endapo kweli Mpango huu unahitajika kutekelezwa. Bajeti waliyotengewa katika kipindi cha fedha cha 2011/2012 ni kiwango kidogo mno. Hivyo basi, ni vyema hili liangaliwe kwa umuhimu wa pekee. Naomba kuwasilisha.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ningependa kuipongeza Wizara kwa kuainisha Mpango wa Maendeleo; hongera sana. Huu ni mwanzo mzuri, kuwa na Mipango katika kuendeleza nchi ni jambo la busara sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niseme kwamba, kuwa na Mipango ya muda wa miaka mitano ni wazo la busara, kuliko kuwa na Mipango ya miaka mingi zaidi. Kwa mfano, Mpango wa Serikali wa miaka iliyopita wa miaka 20, haikuzaa matunda. Mipango inabidi iwe ya muda mwafaka kama miaka mitano halafu iwe hivi: Ipangwe kama mlivyopanga; tuone utekelezaji wake; ifuatiliwe; ifanyiwe tathmini kama inafaa; na mwisho Mpango uonekane kama unaleta tija kwa Wananchi; Serikali iseme kwa Wananchi Mpango umeleta tija gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa na Mipango bila utekelezaji, ufuatiliaji na bila kutathmini kama unafaa na kadhalika. Twende na wakati.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, katika kipengele Na. 1.1.2 – *Manufacturing*, kilichopo ukurasa wa 12, kiwango kilichotengwa kwa ajili ya *Benjamin Mkapa Special Economic Zone – Construction of Sewerage Line from BWM – SE 2 to Mabibo Oxidation Pond*; kinapaswa kuongezwa ili kuhusisha pia ukarabati wa *Mabibo Oxidation Ponds*. Ongezeko la uchafu toka *BWM-SE2* katika mabwawa hayo, ambayo kwa sasa yana hali mbaya sana, kutaleta janga la kibinadamu katika eneo husika. Kwa sasa kuna tatizo la uchafu toka Mabibo Hosteli, kutiririshwa mtoni kutokana na ubovu wa miundombinu. Hali itakuwa mbaya zaidi *BWM-SE2* ikielekeza *sewerage* bila *oxidation ponds* kujengwa vizuri na kuwekewa *cover* na dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kipengele A.1.2.1 – *Road Transport Addressing Traffic Congestion Dar es Salaam*, kilichopo ukurasa wa 127, iongezwe Barabara ya Kimara - Mavuruza - Bonyokwa – Segerea, ambapo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Kikwete ya tarehe 24 Mei, 2010 kama sehemu ya mkakati wa kupunguza foleni Dar es Salaam. Pia, zoezi la kupandisha hadhi ya barabara zilizotajwa kwenye *Road Schedule No. 1*, ukurasa wa 127 kufanyike kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Kipengele A.1.1.4 – *Water and Sanitation*, ukurasa wa 117, Miradi ya *Upper Rum, Lower Ruvu and Drilling of Wells* – Kigamboni (Kimbiji) na Mkuranga (Mpera), marekeb isho yafanyike katika mgawanyo wa fedha ili mafungu makubwa zaidi yawekwe katika miaka ya fedha 2011/2012; 2012/2013 ili kutumiza lengo la kufanikisha upatikanaji wa maji Dar es Salaam kwa mwaka 2013. Kwa jinsi Mpango ulivyo sasa, inaonesha utekelezaji utakamilika 2014/2015, kinyume na maamuzi ya Baraza la Mawaziri uliotangazwa kwa Umma na Rais pamoja na Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ongeza *Stieggler's Gorge* kwenye Miradi ya Umeme (ukurasa wa 135); Ongeza Chuo Kikuu cha Kilimo Butiama (ukurasa wa 146) na hakikisha fidia ya Wananchi kupisha MUHAS – Mloganzila imelipwa, kama ilivyotajwa pia kwenye Hotuba ukurasa wa 16. Naomba kuwasilisha.

MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, mpangilio wa Mpango ni mzuri, umegusa maeneo muhimu ili kufungua fursa za uchumi wa nchi kukua. Changamoto iliyopo ni utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa huduma za jamii, suala la watu wenye ulemavu halikupewa uzito. Watakapofanya mapitio ya ufuatiliaji wa Mpango ni vyema masuala ya walemavu yaangaliwe kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia ukurasa wa 148 – 160, yanazungumziwa masuala ya Afya na Ustawi wa Jamii. Kwenye Mpango huu hakuna mahali popote (*strategic intervention*), yoyote inayozungumzia suala la walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninamalizia kwa kusema ninaunga mkono hoja.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninapenda nikupongeze wewe kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa mwanzo Mwanamke katika Bunge hili na Afrika Mashariki kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutuletea Mpango huu wa miaka mitano, unaohusu maendeleo ya kiuchumi nchini, akiwa na maana ya kufikia maendeleo makubwa nchini Tanzania. Hivyo, jukumu letu ni kuuchangia kwa kuuelezea na kuingiza yale ambayo yameachwa ndani ya Mpango ili ubora wa Mpango uweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wake hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi walio wengi siyo rahisi kuelewa na kuufahamu Mpango huu au lengo la Mpango huu, hasa wale waishio vijijini; hivyo ni vyema Serikali kuufikisha Mpango huu katika Halmashauri, Vikao vya Madiwani nao waweze kupendekeza na kutoa maoni yao kuhusu Mpango huu. Rasilimali zinaohitajika haizotoshelezi; ni vyema Mpango huu ungeainisha vipaumbele vichache kwanza vikaendelezwa kufuatana na fedha iliyopo, kuliko kuweka vipaumbele vingi, fedha iliyopo ikashindwa kuviendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango ungejikita zaidi katika Kilimo Kwanza, kwa kutenga fedha ya kutosha kwa kupatiwa mikopo wakulima wakubwa na wadogo, ruzuku ya mbolea na zana za kilimo na kuimarisha zaidi umwagiliaji wa hali ya juu katika maeneo yote yaliyo na mito na maziwa na kuimarisha kwa kiwango kikubwa Kilimo cha Umwagiliaji. Hii itasaidia kwa asilimia kubwa kukuza kilimo chenye tija na kujitosheleza kwa chakula na biashara ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufahamu kwamba, katika mazingira ya umaskini, mahitaji ni mengi zaidi ili kufikia maisha yaliyo bora na kwa haraka ni lazima kuvitekeleza vipaumbele vichache na kiMpango kwa manufaa ya mazingira ya sasa na vizazi vijavyo; kuimarisha miundombinu ya barabara, umeme ambaao hautoshelezi, reli na kadhalika; kuendelea kuimarisha uwekezaji na kutenga maeneo kwa ajili ya Wawekezaji; Sekta ya Viwanda bado ni ndogo mno, Serikali katika juhudzi za kuimarisha

Kilimo iwe na Mipango madhubuti ya kuimarisha viwanda kwa kiwango kikubwa. Hii itawasaidia Wananchi wa kipato cha chini na kati hata wakubwa kuendelea kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri tukuze elimu nchini. Vilevile Sekta ya Afya iimarishwe kwa kupigana na adui maradhi. Katika Sekta ya Madini, tupunguze na kuondoa misamaha ya kodi katika Makampuni ya Madini, fedha inayopatikana isaidie kuongeza barabara zetu na mengineyo. Pia ninashauri madini yawe rasilimali ya Watanzania na siyo kuwa kikwazo, badala yake ni urithi wa kubakiwa na mashimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa kuendelea kudhibiti matumizi ya Serikali kwa ufuatiliaji wa kweli katika nyanja mbalimbali. Watendaji wa Serikali katika Sekta mbalimbali wafanye kazi kwa bidii na ufanisi zaidi. Nyenzo na rasilimali zinazotolewa na Serikali zitumike ipasavyo na siyo kuwa mikononi mwa wachache; kuwe na ushirikiano kati ya Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha; tuondoe ubinafsi katika maeneo na Sekta mbalimbali; tumalize tatizo la Rushwa; na Wananchi wa kawaida nao watekeleze wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ni haki ya raia wote, lazima sote tufanye kazi kwa bidii na ufanisi ili maisha bora yaweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo machache, ninaomba kuwasilisha. Ninaunga mkono hoja.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Mheshimiwa Rais, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu na Tume ya Mipango, kwa kuandaa Mpango wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16) kwa ufasha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita katika Sekta ya Kilimo, kwa sababu ndiyo inayoajiri Wananchi wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kilimo chetu kikue kwa kasi inayoridhisha, lazima tuwekeze katika Kilimo na Viwanda vya kusindika mazao ya kilimo kama vile vya uzalishaji wa pembejeo ikiwemo mbolea. Kikwazo kikubwa ni urasimu katika upatikanaji wa ardhi na vivutio.

Wakati tukiendelea kuwekeza ni muhimu kujenga uwezo wa wakulima wetu kujinunulia pembejeo za kilimo. Mpango wa kutoa pembejeo za kilimo ni mzuri, tumekuwa tukiongeza fedha kila mwaka (2 bilioni – 7 bilioni – 21 bilioni - 143 bilioni (2010/2011). Lazima tufike mahali vyombo vya kukiwezesha kilimo kifedha (*Financing Agriculture*), viongezeke kwa kasi. Kuanzishwa haraka kwa Benki ya Kilimo (*TADB*), utakuwa mchango mzuri na muhimu. Hatua hii itatuondelea dhana ya kumjengea uwezo mkulima kuitegemea Serikali ili ajenge uwezo endelevu wa kujinunulia pembejeo za kilimo.

Tumejiwekea Malengo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwamba, ifikapo mwaka 2015, eneo linalomwagiliwa lionezeke kutoka 330000 ha. (2010/11) – 1,000,000 ha. Asilimia 25 ya chakula chote kitokane na kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri yafuatayo:-

(a) Tunahitaji kuongeza tija katika uzalishaji ili eneo linalomwagiliwa kwanza; litoe mazao mengi katika eneo moja; pili; eneo hilo lilimwe zaidi ya mara moja kwa mwaka (*Increasing Cropping Intensity*), inawezekana na ushahidi upo. Mfano, mpunga unaweza kufikia taninane kwa heka. Hii imedhihirika katika Mradi wa Kilombero (Mugeta).

(b) Mipango/Miradi ya umwagiliaji itoe kipaumbele katika maeneo na mazao machache (*Selective Approach*). Ninaipongeza Serikali kwa kuliona jambo hili.

(c) Kujenga uwezo (*Capacity Building*), tuongeze wataalam. Kwa mfano, mahitaji ya Wahandisi wa Umwagiliaji ni 350 yakilinganishwa na waliopo 140 tu; hivyo, tuendelee kusomesha (*Long Term*), kuajiri na kutumia fursa zilizopo katika ushirikiano wetu na wenzetu kama vile Afrika Kusini, Afrika Mashariki na kadhalika, kuongeza wataalam.

(d) Pamoja na kuimarisha Idara ya Umwagiliaji, iundwe Tume ya Umwagiliaji itakayosimamia Sera, Mipango na Maendeleo ya Umwagiliaji. Aidha, baada ya kuwa na chombo imara (Tume ya Umwagiliaji), Serikali sasa itekeleze uamuzi wake wa mwaka 2000 wa kuanzisha Wakala wa Umwagiliaji (*National Irrigation Agency*). *Agency set up process* ilikwishakamilika, lakini Wakala haujaanza. Wakala ukiundwa, kitakuwa chombo kitakachowenza kutumia fedha zilizopangwa katika Mpango huu wa Miaka Mitano kwa ajili ya kutengeneza vifaa vyta ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji (*See page 97 of Plan, last row, bottom for 5.222 billion/=*).

(e) Pamoja na mazao ya chakula, tuelekeze umwagiliaji katika mazao ya biashara hususan pamba na miwa ili tuongeze uzalishaji wa mazao hayo kwa ajili ya viwanda vyta ndani vyta pamba inayomwagiliwa, inawezekana kuongezeka kutoka 300 kg/eka – 1200 kg/eka, mfano hai ni India, Misri, Sudan na kadhalika.

Bei ya sukari bado ni kubwa kwa sababu uzalishaji ni mdogo kuliko mahitaji. Tupanue mabonde ya kilimo cha miwa na tusaidie uanzishaji wa viwanda vyta sukari vyta ndani na vile vidogo vidogo. Mabonde yapo, kwa mfano, Malagarasi, Ngoni, Ruhuhu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

MHE. CELINA O. KOMBANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa Mpango wake kukamilika. Yapo masahihisho kidogo; katika ukurasa wa 122, *item 31* ni Barabara ya Kidatu – Ifakara – Mahenge; *item 32* ni Ifakara – Lupilo – Malinyi – Namtumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii ili nami niweze kuchangia japo kwa maandishi, kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu wa Maendeleo unaotoa vipaumbele muhimu kama ilivyoainishwa ni vizuri sana ikiwa utatekelezeka. Kitu kinachonitia wasiwasi ni kwamba, mapato ni madogo kuliko matumizi na sehemu kubwa inayotegemewa ni mkopo. Hii inatia wasiwasi na tusipoangalia tutazidi kuiweka nchi kwenye madeni zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na kipaumbele cha kwanza, Miundombinu – Umeme. Tanzania tukitaka kujidesha tunaweza lakini tunapenda kutegemea misaada. Tuna Maporomoko mazuri ya Karambo Sumbawanga, Serikali ikiamua kuboresha maporomoko hayo, tunaweza kupunguza tatizo la umeme Sumbawanga na kwingineko. Mpaka sasa maporomoko hayo yamekuwa ni sehemu ya kutalii kama maonesho kwa nchi jirani ya Zambia.

Reli; Serikali itumie mafundi wetu wa ndani kutengeneza injini na ikiwezekana wapelekwe kusoma kuliko kuagiza injini chakavu kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kilimo, nchi yetu imejaliwa rutuba ya kilimo, kinachokwamisha ni pembejeo; Wananchi wengi hawapati pembejeo, kwani zinatolewa kwa uchache sana; hivyo, Mwananchi wa chini hawezি kumudu na hata kuweka akiba ya chakula. Serikali iangalie utoaji wa pembejeo, kwani haziwafikii walengwa wote. Pia elimu itolewe kwa Wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Ufundu izingatie sana VETA. Elimu hii itasaidia sana kumaliza tatizo la ukosefu wa ajira, kwani kundi la vijana wanaomaliza Kidato cha Nne na Darasa la Saba, wanazagaa vijijini na ni wengi sana kuliko kundi lolote na hii inatokana na shule za sasa hivi hazina stadi za kazi (ufundi); hivyo, wanapomaliza wanatoka kapa hawana ujuzi wowote na kuishia kuhangaiwa wasijue la kufanya. Ninashauri ufundu urudishwe kuanzia Shule ya Msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipaumbele cha rasilimali watu, Mpango unatilia mkazo wa sayansi, teknolojia na ugunduzi. Ili kutimiza lengo hili na kuhakikisha utendaji kazi unaendana na uwiano wa nguvukazi ya wataalam katika ngazi zote, ni vizuri mkakati wa utekelezaji uangalie ufufuaji/uboreshaji wa vyuo vilivyopo kama vile Uyole, Kilosa, Mlingano, Ukiriguru na kadhalika, kwa eneo la kilimo na ufugaji. Kwa eneo la afya na vyuo vya waganga wasaidizi na wakunga, vitiliwe mkazo ili kuhakikisha tunapata Waganga Wasaidizi katika Zahanati zetu za Vijiji na Vituo vya Afya.

Katika eneo la ufundu, kwa kuwa vyuo vingi vya ufundu vimegeuzwa kuwa taasisi za elimu ya juu kama *OIT*, *MIST* na kadhalika, tuone uwezekano wa kuvigeuza Vyuo vya *VETA* vya Kanda kuwa vyuo vya ufundu wakati kila Wilaya au Wilaya nyingi katika eneo husika au Kanda husika itakapokuwa na Vyuo vya *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uimarishaji wa vitendea kazi/maabara ili kuendana na mahitaji ya sasa ni jambo ambalo inabidi litiliwe mkazo ili kuvutia wawekezaji katika maeneo tuliyoyawekea kipaumbele. Kwa kuwa na maabara ya kisasa, wataalam wanaohitimu katika vyuo hivyo wataweza kufanya kazi katika viwanda au maeneo ya kazi yatakayowekezwa na wawekezaji na tutakuwa tumeongeza tija katika uzalishaji au utoaji huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza sana Serikali, maana Mpango huu ni mzuri sana na unatekelezeka.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchangia Mpango huu katika masuala mazima ya ardhi, nyumba na makazi. Kwa kuwa ifikapo mwaka 2030 inategemewa kuwa nusu ya Watanzania watahamia mjini, jambo ambalo litafanya kuwa na upungufu mkubwa wa huduma za jamii hasa makazi, elimu na afya, kwa maana ya hospitali na hata uchafuzi wa mazingira. Hivyo basi, Serikali ina haja ya kuongeza idadi ya majengo ya kuishi maeneo ya mjini kupitia Shirika la Nyumba la Taifa; ni vyema Serikali itafakari mambo gani yanababisha uhamiaji huo wa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mionganoni mwa changamoto zinazosababisha uhamiaji huo ni kuwa karibu na huduma za jamii, ambazo nyingi kati ya hizo hazipatikani vijijini, ikiwemo shule nzuri, hospitali zenye tija na miundombinu imara. Hivyo; ni vyema Serikali isogeze huduma hizo vijijini ili kuepusha uhamiaji huo wa kundi la watu mijini, jambo ambalo linaweza kusababisha amani na ustaaarabu wa jamii kupotea na kusababisha ujambazi na hata biashara ya ukahaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu, nchi yetu ina upungufu au ukosefu mkubwa wa wasomi wa elimu ya juu hasa katika Vitivo vya Sayansi na Teknolojia ikiwemo Madaktari, Wahandisi na kadhalika. Hivyo, kwa kuwa nchi yetu inategemea kilimo, madini, uvuvi, utalii na vyanzo vingine; ni vyema tukawa na wataalam wa kutoka kwenye sekta hizo. Hivyo; ni busara Mpango ukizingatia kuongeza wataalam wa kutosha katika maeneo ya rasilimali hizo kwa Taifa ili kuweza kukuza uchumi wenyewe tija na kupunguza bajeti tegemezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua fursa hii, kutoa maoni yangu kwa maandishi, ila nitachangia katika sehemu mbili; miundo mbinu, yaani nishati na huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishati bado imekuwa ni tatizo katika nchi yetu ambayo inafanya kuwa kikwazo cha maendeleo ya nchi. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, kwenye Kamati yetu tuliongea na Wadau mbalimbali na tukaishauri Serikali kwa kipeleka maoni kama Kamati kuhusu tatizo la umeme kwa hatua ya sasa ya muda wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia ya sasa ni kutafuta mbadala wa kutegemea umeme kutokana na maji ya Mtera, kwa sababu mwisho wa siku lile bwawa litakauka, kwani miongo ya mvua inabadilika siku hadi siku. Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano haukuelezea njia mbadala ya kuiokoa nchi yetu katika suala hili ambalo ni kubwa sana, ambalo linashusha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusitumie njia mbadala ya kutumia nishati ya umeme wa mawimbi ya bahari, pamoja na gharama kubwa, lakini faida yake ni kubwa na wataalam wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za jamii, suala la kumkomboa mwanamke ambaye ni mhimili mkubwa sana kwa Taifa, Mpango haukuonesha unamsaidia vipi mwanamke na haki zake. Wanawake wa vijijini wanapata manyanyaso wanapofiya na waume zao na kwa sababu sheria hawaifahamu, ndiyo maana wanakosa haki zao. Mpango ulipaswa uchambue kila kipengele cha sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango pia ultakiwa uelezee jinsi ya kumsogezea mwanamke huduma muhimu kama vile hospitali, shule, Vikundi vya *SACCOS* na kumpunguzia masafa marefu ya kutafuta maji. Mpango haukuonesha ni jinsi gani tatizo la maji katika vijiji litatatuliwa kwa kuchimba visima, kwani hali za wanawake zinatia huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Mpango ni mzuri kwa Maendeleo ya Taifa, ila pamoja na mambo mazuri hayataki haraka, lakini pia chelewa chelewa utakuta mtoto si wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwa na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Daima bila Mipango thabiti, hakuna utekelezaji na kama hakuna utekelezaji hakuna ufanisi wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwe na maendeleo na mafanikio ya Mpango, huu lazima kuwepo na Mipango thabiti ya kuwa na miundombinu safi. Leo hii kuna tatizo la barabara vijijini ambako Wananchi wengi wanaishi, leo hii ni asilimia 25 tu ya wakazi vijijini wanaishi kilomita mbili toka eneo la barabara inayopitika muda wote. Sasa hawa wengine ambao hawajatengewa Mradi wa Barabara Vijijini, watachangiaje Mpango huu wa Maendeleo Vijijini. Hii ni sambamba na huduma ya maji safi na umeme ili waweze kuwa na uzalishaji mdogomdogo wa shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la afya limepewa nafasi lakini kwa umuhimu wa chini. Mpango unataja kuandaa Madakrati, Wauguzi na Wataalam wa Maabara, Mionzi na kadhalika, lakini Mpango huu hauoneshi dhahiri mbinu sahihi za kuwafanya wabaki sehemu zao za kazi. Takwimu zinaonesha kuwa, wafamasia wanaongoza kuacha vituo vyao vya kazi na kuhamia mijini kwa asilimia 18. Hawa wataalam ni wengi mno, ninaishauri Serikali itafute mbinu za kuwafanya wakae katika vituo vyao (*retention schemes*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupunguza idadi ya vifo vya akina mama na watoto chini ya miaka mitano na vifo chini ya mwaka mmoja, Mipango iliyopo haitoshelezi. Hii ni pamoja na kuyaangalia maeneo haya kwa ukaribu sana. Serikali itumie fedha nyingi kununua pikipiki wakati sehemu nyingine pikipiki hizo haziwezi kwenda kwa sababu ya milima, barabara mbovu na kadhalika. Nimeishauri Serikali ifanye Mpango Mkakati wa kupeleka magari ya wagonjwa yenyе vifaa kazi. Pikipiki haiwezi kukidhi haja hii; ni bora Serikali iijipange hata kama ni kupeleka gari moja kila mwaka kwa kila wilaya, hii itasaidia kuliko hizo pikipiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini na ninatambua kuwa, haya yote yakipewa usimamizi thabiti, utekelezaji wa kina wa Mpango huu utafanikiwa, lakini kubwa zaidi ni ushirikishwaji wa jamii husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Rais na Serikali yake katika kuandaa na kuuleta Mpango huu ili tuweze kuujadili na kuupokea, kwa lengo la kuutekeleza kwa ufanisi ili kuliletea maendeleo Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maendeleo linagusa maeneo mengi ikiwemo na Wananchi wa jinsia zote. Hivyo basi; ni vyema Serikali ikaangalia suala la uwiano wa maendeleo katika mikoa yetu nchini ambapo itainua kipato cha Wananchi wake hasa wanawake amba ni wazalishaji wakuu katika nyanja zote, iwe kilimo au miradi midogo midogo, kwa kuweka uwiano unaolingana; na hivyo Serikali itakuwa imeweza kuikwamua jamii kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaupongeza Mpango kwa kutoa kipaumbele katika miundombinu (umeme, bandari, barabara, reli na kadhalika), ikiwemo kilimo ambacho ndiyo nguzo kuu ya uchumi, ufugaji na uvuvi; vyote hivi vitaongeza tija. Jambo kuu hapa ni utekelezaji na ufuatiliaji uwe wa karibu sana na pia kushirikisha jamii hasa vijana amba ndiyo kundi kubwa ambalo ni nguvu kazi tunayoihitaji kuishirikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kwamba, kwa kuwa Serikali imeleta Mpango huu wa aina yake itakuwa imeweza mkakati madhubuti wa ufuatiliaji ili kujiwekea sifa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, ninaomba nitoe tena pongoezi zangu za dhati kabisa na ninaunga mkono hoja.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kipaumbele cha upatikanaji wa nishati ya umeme toshelevu na ya uhakika kwa mahitaji ya ndani na kuuza nchi jirani, ninaishauri Serikali iangalie Mpango wa upatikanaji wa nishati hiyo katika maporomoko ya RUSUMO Ngara – Kagera, ambapo upatikanaji toshelevu uende sambamba kwa kupunguza gharama za upatikanaji wa nishati hiyo kwa watumiaji ili Watanzania walio wengi, waweze kupata huduma hiyo muhimu kama ni alama moja na chanzo cha maendeleo katika maeneo ya Kagera (Tanzania) na Rwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango unagusia Kilimo cha Biashara na ongezeko la thamani kama Mpango; ni lazima Serikali iangalie upatikanaji wa soko la uhakika la wakulima pamoja na mkakati wa kufufua viwanda vilivyokufa ambavyo vitajumuisha na vile vipyta vitakavyojengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa upatikanaji wa maji kwa mpango wa uvunaji wa maji ya mvua, ulizungumzwa miaka mingi iliyopita, lakini hakuna ufumbuzi uliopatikana. Serikali ni vyema itoe ufanuzi ni sababu gani za msingi zilizopelekea mkakati wa awali kushindwa na sasa Serikali ina mbinu gani za vitendo za kuhakikisha mpango wa uvunaji maji ya mvua utafanikiwa na utatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu kama kawaida utapelekwa Wizarani katika Idara na Halmashauri za Mitaa, lakini wasiwasi wangu fedha hizo hazitaleta tija inayotakiwa, kwani nidhamu ya matumizi ya fedha za umma imepotea na udhibiti ni mdogo na wanaobainika na ubadhirifu, adhabu wanayopewa ni ndogo hailingani na kosa lenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali iangalie kero hii ya matumizi ya fedha kwa ukamilifu katika dhana nzima ya *value for money*. Naomba kuwasilisha.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Ninapenda kusema wazi kuwa, Mpango huu yawezekana usifanikiwe kwa kuwa unaendelezwa na watu ambao hawakupewa nafasi ya kushiriki kuuandaa bali wanapelekewa kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu wote unatakiwa kutekelezwa ardhini, huku bado ardhi ya Tanzania katika maeneo ya utekelezaji, imejaa migogoro ambayo pia huleta machafuko na mapigano katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na utekelezaji wa Mpango, ningependa uendane pia katika utatuvi wa migogoro ya ardhi. Ardhi kubwa ipo vijijini na kwa hali halisi ya Vijiji vya Tanzania, vinakiimbiwa na vijana ambao hukimbilia mijini kunusuru maisha yao kwani huko vijijini hali ya maisha ni ngumu. Ikumbukwe kuwa, Mpango huu utatekelezeka maeneo ya mijini tu kama nguvu kazi ya vijana inaondoka vijijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na kawaida ya kutaja takwimu ya idadi na siyo ubora. Mpango umojiandaa kwa idadi ya wataalam kitakwimu, inayozingatia wingi lakini siyo ubora. Ninapenda kusema kuwa, Mpango huu hautokuwa na mafanikio ya moja kwa moja kama ilivyokuwa katika Mpango wa Shule zetu za Kata, tusipozingatia ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na Mpango wa Kujenga Shule za Kata, ambao unafanikiwa kimajengo na siyo kitaaluma, kwani sasa Serikali inajivuna kwa idadi kubwa ya wanafunzi wanaojiunga na Shule zetu za Kata na siyo kujivunia matokeo mazuri ya Shule za Kata kitaaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeufananisha Mpango huu na Shule za Kata kwa kuwa Serikali yetu ina Mipango mingi ambayo utekelezaji wake una tija ndogo. Hii imetokana na kutowashirikisha moja kwa moja Watanzania wote kutokea chini hasa wakati wa maandalizi ya awali. Pia ni vizuri ijulikane kuwa, Mpango wa Maendeleo yawezekana ukakwama kwa kuwa mahitaji ya maendeleo yanatofautiana kutoka mahali fulani, ukilinganisha na maeneo mengine. Ni vizuri sasa Mpango huu uende chini kwa kuwahusisha Wananchi waliopo maeneo yanayotekeliza hasa maeneo ya vijiji na vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizopo katika Mpango ni nidhamu na uadilifu wa watekelezaji wenyewe na wasimamizi wa Mpango wenyewe. Uadilifu na uwajibikaji ni jambo muhimu sana hasa katika utekelezaji wa Mpango unaohusisha fedha moja moja. Kama nidhamu itazingatiwa, basi yawezekana Mpango huu ukatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwaomba Watanzania wenzangu walione jambo hili ni letu sote, siyo la watu fulani, hapo tutapiga hatua katika Mpango.

Mungu ibariki Tanzania.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono Mpango kama ulivyoelezwa na Waziri mwenye dhamana, lakini ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa maeleo mazuri sana siku ya uzinduzi. Maeleo mazuri hayo yenye ufanuzi yalinogeshwa na Katibu Mtendaji wa Mpango, Dkt. Mpango siku ya semina katika Ukumbi wa Msekwa.

Mpango nimeupokea vizuri na nimeuelewa vizuri sana. Mpango huu tukiutekeleza vizuri, kila Mtanzania akishiriki kwa kile awezacho, pahali alipo, kwa nguvu na akili zake zote, tutaufikisha pazuri. Lazima tuazimie kuutekeleza kwa dhati kwa vitendo siyo maneno na tupimane, kila mwaka tupewe taarifa kwa hivi vipaumbele tulivyoanza navyo kwa kila mwaka ili tujue na tujipime kama kasi ni ndogo basi tuongeze bidii. Wale tutakaosimamia tuhakikishe unafanikiwa, hatuna sababu ya kushindwa kufanikiwa kwani rasilimali zilizopo zinatosha kabisa kutekeleza Mpango huu kwa vipaumbele vilivyoanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *motto* wangu wa Mpango ni “Tupunguze Maneno Vitendo Zaidi.” Sisi sote ni Watanzania, tunaitakia mema nchi yetu na hata ukifika wakati wa kung’atuka kwa sisi Viongozi, basi wajukuu zetu waikute Tanzania yenye neema, kwani kila kitu Mwenyezi Mungu ametujalia, tukishindwa tunashindwa kwa uzembe wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninautakia kila la kheri Mpango mzima na wasimamizi wote wa Mpango. Naunga mkono hoja.

MHE. MARYAM S. MSABAHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninaomba nichangie kwa maandishi Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2011/2012 – 2015/16. Kwa kuwa asilimia 75 ya Watanzania wanaoishi kwa kutegemea kilimo nusu yao ni wanawake, Serikali katika Mpango huu haioni kuna umuhimu wa kuwapelekea wanawake semina elekezi kuhakikisha nao wanaondokana na kilimo cha mkono. Serikali ihakikishe katika Mpango huu inawajali wakulima wadogo wadogo na akinamama wa vijijini wapatiwe pembejeo za bei nafuu ili kuboresha kilimo na waondokane na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mpango huu ihakikishe pesa ambazo zinatolewa na wafadhili, zinawafikia walengwa wa vijijini na kusimamiwa katika Halmashauri mbalimbali. Serikali pia ihakikishe Benki ya Wanawake inapatiwa hisa za kutosha na kufungua matawi mpaka vijijini, ambapo Mpango huu utawanufaisha wakulima wadogo wadogo vijijini, wataweza kukopeshwa na benki na wakishauza mazao yao wataweka pesa zao. Kutokana na Mpango huu wa Maendeleo, wanawake wengi vijijini hawana elimu ya kukopa benki na kuweka pesa zao benki; kwa hiyo, Serikali kupitia Benki ya Wanawake, ihakikishe wanapata elimu ya kufungua akaunti Benki ya Wanawake. Endapo Mpango huu utaweka mfumo mzuri wa mgawanyo wa rasilimali za maendeleo kati ya Halmashauri na Serikali Kuu, tutaondokana na umaskini uliokithiri vijijini. Mpango huu uhakikishe vijana wote wa vijijini wa jinsia zote wanapatiwa elimu endelevu za kujajiri wenyewe. Katika Mpango huu fedha za utekelezaji wa vipaumbele kadhaa zigawanywe mpaka vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali yetu kwa Mpango huu. Pia ninaipongeza Serikali kwa kutafsiri kwa vitendo Dira ya Taifa kupitia Mpango huu wa 2011/12 – 2015/16. Mpango huu unapaswa kuungwa mkono wa Watanzania wote; Viongozi wa Siasa, Dini, Wafanyabiashara, Wakulima, Vijana, Wafugaji na Wananchi wote kwa ujumla wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoa hoja ametwambia kwamba, Mpango umezingatia Malengo ya Dira ya Taifa, Sera mbalimbali za nchi ikiwa ni pamoja na MKUKUTA II; ninapenda kuishauri Serikali kwamba; ili utekelezaji wa Mpango uwe rahisi, Wananchi lazima washirikishwe ipasavyo katika kuainisha kero zinazoathiri ustawi wa maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya mapitio ya utekelezaji wa Dira 2025 yaongeze juhudzi za Serikali katika kuwalettea maendeleo Wananchi. Matokeo ya mapitio yameonesha kuwa, ukuaji wa uchumi bado haujawanufaisha Wananchi wa kawaida. Ninaomba Serikali iliambie Bunge lako Tukufu kwa nini hali za Wananchi bado zinaendelea kuwa mbaya kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo 2011/12 – 2015/16, Serikali imepanga kutumia shilingi trilioni 8.6 kwa mwaka, ambapo shilingi trilioni 2.7 zitatolewa na Serikali, zilizobaki zitatoka kwa Wahisani. Hali hii inatia wasiwasi; hivyo, ninaishauri Serikali yetu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi chini ya Kiongozi wetu Mpandwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, iongeze Bajeti ya Serikali kwa kupunguza matumizi ya kawaida. Maendeleo hayapatikani kwa urahisi ni lazima tujinyime kama Taifa.

Serikali ipitie upya Mikataba ya Uchimbaji Madini ili madini hayo yachangie katika kupatikana kwa fedha za kutosha kwa ajili ya Mpango huu. Vilevile ninaishauri Serikali yetu ipitie upya Mikataba ya Ukodishaji Vitalu vya Uwindaji ili Sekta hii ichangie fedha kwenye utekelezaji wa Mpango huu. Wahenga walisema; “Mtegemea cha ndugu hufa maskini.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ni Sera ya Chama chetu cha CCM, Mpango ungeainisha mikakati madhubuti, namna ambavyo tutafanikisha kuhamishia Serikali yetu hapa Dodoma. Kama hatuna nia au tumebadili uamuzi wa kuhamia Dodoma, ninaiomba Serikali kuitia mtoa hoja, iliambie Bunge lako Tukufu ni lini Serikali yote itahamia Dodoma au hatuhamii tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali yetu kwenye eneo la vipaumbele vilivyoanishwa katika Mpango. Hata hivyo, ninapenda kushauri yafuatayo:-

(a) Taifa letu limekuwa likikabiliwa na hali mbaya ya chakula katika mikoa mingi hasa kutokana na ukame. Ninashauri nguvu zielekezwe katika utafiti wa aina ya mazao yanayoweza kulimwa katika kila mkoa kulingana na hali ya hewa, aina ya udongo na kadhalika. Mikoa ielekezwe na Wakuu wa Mikoa kuitia TAMISEMI, watoe taarifa ya hali ya kilimo cha mazao ya chakula na biashara kila baada ya mwaka.

(b) Vyuo vya Utafiti wa Masuala ya Kilimo viimarishwe. Pia Maafisa Ugani wasomeshwe wa kutosha na wapelekwe vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme Serikali itafute vyanzo mbadala ili kulihiakikishia Taifa letu kuwa na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, atuambie mkakati utakaotumiwa kupima mafanikio ya utekelezaji wa Mpango huu ili kurekebisha kasoro zitakazojitokeza kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pongezi kwa Waziri Wasira, Tume ya Mipango na Serikali, kwa kazi nzuri ya kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango ulivyo ni mzuri sana, kama *framework*, lakini bado kuna haja ya Mpango mzima kuhusishwa katika ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na Kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kila ngazi ya Mpango, timu au watu watakaotekeleza wabainishwe.

Planning, Monitoring Evaluation and Reporting Units zibainishwe katika ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya, Kata na Kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kufanya *Planning, Monitoring Evaluation and Reporting Units*; kuna haja ya kufanya *Baseline Surveys* na kuwa na *Data* ya kutuwezesha kupima afya ya Mpango na utekelezaji wake; ni muhimu kujua *base tunavyoanza* nao ni wapi katika kila Sekta. Pia ni muhimu kubainisha *sources of information, frequency of informantion collection, kukubaliana juu ya objectively verifiable indicators and means of evaluation*.

Vilevile ni muhimu kuandaa *log frames* kwa ajili ya kila Sekta. Pia ni vyema *Plan* ikawa na *Annex* ya *4 x 4 log frame matrix* ili kurahisisha uelewa wa watumiaji wa Mpango huu.

The Plan needs to be more focused and the emphasis should be on outcomes per sector and per every specified period.

The Plan should specify assumptions and develop alternatives per each strategy in case of killer assumption(s).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kuwa na *Tanzania Five Years Strategic Plan (2011 – 2015/16)*. *Strategic Plan* itakuwa na *function* ya kuwa *link* kati ya *Vision 2025, MKUKUTA and 2010 Election Manifesto*; pamoja na *Plan* hii; hivyo, *flow* itakuwa *Vision 2025, Strategic Plan, Operational Plans*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuipongeza Serikali kwa hatua hii. Kweli mara tu baada ya Uhuru, tulikuwa na Mpango huu, 1965 – 1970 na 1970 – 1975, baada ya hapo hatukuwa tena na Mpango bila sababu yoyote. Leo tumeona athari zake baada ya Uhuru kwa miaka 50. Tumechelewa sana, lakini tumejitambua kama Taifa tulikosea wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba, kama upo utashi wa dhamira ya kweli tutafanikiwa lakini ni lazima tuwe na utayari wa kupanga vyema na kuthubutu kuchukua maamuzi magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ni maskini na nchi maskini daima zinakuwa na vipaumbele vingi ambavyo vyote ni muhimu kwa maendeleo ya nchi. Lazima pia tuangalie uwezo wa nchi, kwa maana ya kuwa na uwezo wa kuwekeza katika kila kipaumbele. Vinginevyo, tutaendelea kuwekeza na kutawanya rasilimali chache tulizonazo na kusiwepo na tija. Hivyo basi; ni lazima tuwe na vipaumbele vichache zaidi ambavyo tukiwekeza inakuwa ni kichocheo cha kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele vyote vilivyomo katika Mpango ni muhimu, lakini bado ninasisitiza kuwa ni lazima tuamue kwa makusudi kwamba, katika Mpango tutaendeleza maeneo yepi. Kwa uzoefu tulionao, tumekuwa hatuwekezi ipasavyo katika Mpango ambayo tunaiibua; kwa mfano, tuna Kilimo Kwanza; je ni kweli malengo yake ni lazima Wananchi wayajue? Kama tunataka kuongeza uzalishaji wa chakula au mazao ya biashara; je, masoko yapo na yameandaliwa?

Kama tunataka kuongeza pesa za kigeni basi ni lazima tuweke mkazo katika mazao ya biashara, yaainishwe, tuwekeze ili tuongeze usafirishaji wa mazao hayo; lakini kama mwaka huu wa fedha wa 2011/12, kilimo kimeongezewa asilimia 2.5 kutoka bilioni 903.8 hadi bilioni 926.2; kwa ongezeko hilo hakuna mabadiliko ya msingi yatakayoonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, elimu hapo awali ilipewa msukumo wa aina yake na mafanikio yake yameonekana pamoja na ongezeko la shule au vyuo na idadi ya wanafunzi au wanachuo, lakini pamoja na ongezeko hilo, tumetenga kiasi kidogo sana kama asilimia 12 toka bilioni 2.045.4 hadi bilioni 2.283.0.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya mawili yalikuwa ni vipaumbele vyetu namba moja katika vipindi tofauti, leo ni kipaumbele namba nne na tano katika Bajeti ya 2011/2012. Maswali ya msingi ni:-

- (a) Tumefanikiwa kwa kiwango gani na je inaridhisha?
- (b) Je, fedha tuliyowekeza itaendelea kuleta ufanisi tulokusudia au Sekta hizi tunazirudisha nyuma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu bado inajikita katika kuwa na Mpango Endelevu kwa kuwekeza, badala ya kila mwaka kuwa na kipaumbele kipy. Nimesema ni vyema tukafanya maamuzi sasa, kwa mfano, katika rasilimali zetu za asili; tuna Mpango gani kama Taifa. Kutafuta wawekezaji na kutegemea kodi na mrabaha hatuwezi kuendelea kama Taifa, ni vyema sasa gesi asilia iwe ni kichocheo cha kuleta mabadiliko katika Taifa letu kwa kuwekeza katika nchi na kujenga kiwanda; mfano, viwanda vyaa mbolea au saruji na tuvimiliki kwa asilimia 100 au kama hatujafikia hapo, viwanda hivi

viwe na ubia wa asilimia 51 – 49 na tuachane kabisa na kuachia rasilimali zetu holela na kutegemea kodi na mrabaha; hatutafika ni lazima tupange na kuamua sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii, kumpongeza Waziri na Timu yote ya Tume ya Mipango, kwa kuunda Mpango huu na hatimaye kuuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwa ujumla, Mpango ni mzuri na kama ungetekelezwa au kama utatekelezwa kama ulivyoandaliwa, basi tutegemee kuona nchi yetu ikitoka kwenye dimbwi la umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, ningependa kuchangia katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Kwanza, kama kuna tatizo kubwa katika Serikali yetu basi tatizo hilo ni kushindwa kutekeleza mambo mengi tunayoyaweka kwenye Mipango yetu, ninaomba nitoe mifano michache kama ifuatavyo:-

(a) Mpango wa Serikali kuhamia Dodoma ni wa zaidi ya miaka 35 sasa na bado hakuna hatua yoyote ya maana iliyofikiwa! Kila mwaka Serikali imekuwa inakumbushwa kupitia Bunge hili juu ya kutekeleza Mpango huo, lakini majibu ya Serikali yamekuwa tunatafuta pesa. Inashangaza zaidi kuona Wizara za Serikali na Taasisi muhimu za Serikali ambazo hazina ofisi, zikiendelea kujenga ofisi zake Dar es Salaam. *The government is not serious at all.*

(b) Mpango ulioachwa na Baba wa Taifa, Mwlalimu Julius K. Nyerere ni wa kukijenga Chuo cha Ufundji Mbeya na sasa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia (*MIST*) – Mbeya katika hadhi ya Chuo Kikuu; hadi leo kinachofanyika ni utekelezaji wa azma hiyo usioridhisha. Ukiifutilia Serikali utaambiwa tatizo ni pesa.

(c) Mpango wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Songwe – Mbeya ni wa muda mrefu tangu miaka ya 2000. Kweli ujenzi ulishaanza, awali uwanja huo ungekamilika mwaka 2005 hivi, mara zikaanza hadithi zisizoisha. Mpaka hivi sasa ninapoaandika, kwa hakika haujalikani Uwanja huo utakamilika lini, ingawa kwenye vitabu tunaambiwa mwaka huu wa 2011 (mwezi Agosti), lakini ukitembelea Uwanja huo, busara zinakwambia hata mwaka huu hautakamilika. Tatizo Serikali haina pesa za kutosha.

(d) Miradi ya Chuma Liganga na Mchuchuma ni ya siku nyingi sana na imekuwa kwenye Mpango wa Serikali kwa miaka mingi sana, utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua sana; tatizo, Serikali haina pesa za kutosha.

(e) Mpango wa Ujenzi wa Reli ya Tanga – Arusha – Musoma na Uimarishaji wa Reli ya Kati, bado Mipango hiyo kwa sehemu iko kwenye vitabu, ninaamini bado hazijafanyika jitihada za kutosha katika kuitekeleza. Bado Serikali ikiulizwa tatizo ni pesa!

Pili, kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu hasa ukizingatia kwamba, karibu asilimia 75 ya Watanzania hujihusisha na Sekta hiyo.

Hata hivyo, Mipango yetu mingi hajjaweza kuwafanya wakulima wetu waondokane na kilimo duni. Kwa mfano, dhana ya Kilimo Kwanza bado siyo jibu sahihi kwa mkulima; mkulima huyu anakabiliana na riba kubwa za mabenki, Mfuko wa Pembejeo haupewi pesa za kutosha, bado bei za mbolea na mbegu ziko juu sana, mbolea, mbegu na dawa za ruzuku ya Serikali zinawafikia wakulima wachache sana. Tatizo ni pesa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali sasa inakuja na Mpango wa Kuendeleza Kilimo Kikanda na kutoa msukumo kwa mazao maalum na kwamba, Ukanda Maalum chini ya *SAGCOT* utaanzishwa. Mpango ni mzuri, lakini tena hofu yangu ni upatikanaji wa pesa, ambao kwa sehemu kubwa umekuwa ukiathiri utekelezaji wa Miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kupanga ni kuchagua kama Waziri alivyoeleza katika ukurasa wa 13 wa Kitabu cha Hotuba na kwa mantiki hiyo, ndiyo sababu tumekwenda na vipaumbele vichache, lakini swali langu na ambalo ningependa Waziri alipatie Bunge lako ni kwa namna gani sasa Mpango huu utatekelezwa na kufanikiwa vizuri? Je, sababu ambazo zinasababisha tushindwe kutekeleza Mipango mingi kama ule wa kuhamia Dodoma sasa hazipo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaomba kuishauri Serikali iwe makini (*serious*) katika kufanya kile ambacho inaanua kufanya, kama tunapanga kufanya hayo ambayo yameainishwa kwenye Mpango basi yafanywe kwa umakini. Serikali ihakikishe pesa za kutekeleza Mpango zinapatikana na kupelekwa kwenye Miradi hiyo. Itakuwa ni aibu kwa Serikali ya CCM kama baadae tutarudi na hadithi zile zile za pesa hazikupatikana na majibu kama hayo wakati huu wa Siasa ya Vyama Vingi ni hatari kwa Serikali iliyoko madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutamka kuwa, ninaunga mkono hoja hii. Ninaipongeza Serikali kwa kurejea kuwa na Mpango wa Miaka Mitano ndani ya Mpango Elekezi wa Miaka Kumi Tano kwa kipindi kilichobakia cha Dira ya Taifa ya 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi huu umeendana na kuundwa kwa Tume ya Mipango, chini ya Ofisi ya Rais, Tume ambayo Mwenyekiti wake ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa Tume ya Mipango kunaziba pengo lililokuwepo la kuwa na Dira isiyokuwa na msimamizi wa karibu. Ninashauri Serikali ione umuhimu wa kuiwezesha Tume ya Mipango kwa kuipatia wataalam wenye uwezo

katika fani mbalimbali na kuitengea rasilimali fedha za kutosha kila mwaka ili iweze kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu wa Maendeleo ni mzuri na vipaumbele vilivyoainishwa iwapo vitatekelezwa na kusimamiwa vizuri, utaweza kuzaa matunda yaliyokusudiwa. Hata hivyo, ninapenda kutoa angalizo katika maeneo machache yafuatayo:-

Kwanza, tutambue kuwa Mpango huu ni Mpango wetu wa Taifa na kwa maana hiyo, lazima tuumiliki sisi wenyewe. Kila jitihada zifanyike ili kuhakikisha kuwa, gharama za utekelezaji wa Mpango unatokana na nguvu zetu sisi wenyewe, kwa kupanua wigo wa mapato (mapato yanayotokana na kodi na siyo kikodi), tujielekeze zaidi kutafuta mapato yasiyo ya kodi. Tuboreshe mazingira ya uwekezaji na biashara na maboresho haya tuyafanye kuwa ya kudumu.

Mikakati ya utekelezaji wa Mpango huu ilenge katika kuwanufaisha watu wengi hasa wakulima, wafugaji wa wavuvi ambao hali yao ni duni. Kilimo, ufugaji na uvuvi ndiyo Sekta zinazobeba watu wengi waishio vijijini, ndiyo Sekta za Wananchi. Sekta hizi hasa ile ya Kilimo, ukuaji wake umekuwa ukikua kwa kasi ndogo ikilinganishwa na ongezeko la idadi ya watu vijijini. Pamoja na uchumi jumla kukua kwa asilimia saba, ukuaji huo haujanufaisha Wananchi waishio vijijini (zaidi ya asilimia 70). Pamoja na Sekta kama Mawasiliano, Ujenzi na Uchukuzi kuwa zinakua kwa kasi, lakini mchango wake katika kupunguza umaskini wa kipato ni mdogo kwa vile Sekta hizi zinanufaisha sehemu ndogo ya Wananchi. Sekta ya Kilimo kwa tafsiri pana ndiyo itakayowanyanya Wananchi wengi kutoka kwenye umaskini. Hivyo, ipo haja ya kusisitiza maendeleo vijijini kwa uboreshaji wa miundombinu ya maji, umeme, barabara, pamoja na huduma za kifedha, kwa maana ya wakulima kupata mikopo ya masharti nafuu, matumizi ya pembejeo hasa mbolea (kilo tisa kwa hekta ni matumizi kidogo ukilinganisha na kilo 27 kwa hekta Malawi; kilo 53 kwa hekta Afrika Kusini na kilo 276 kwa hekta kwa nchi ya China).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninashauri tuangalie uwezekano wa kuwa na makakati maalum wa kujikwamua na utegemezi wa Wahisani. Mfano, *Donor Dependency Exit Strategy*, ambao utakuwa unapimwa kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia kama nilivyoanza kwa kusema ninaunga mkono hoja.

MHE. SALEH A. PAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninatoa pongezi kwa Serikali, kwa kuleta Mpango huu. Mpango ni mzuri na ninaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza, Serikali imeleta Mpango wa Miaka Mitano ili kufikia Malengo ya Dira ya Maendeleo 2025. Nimeridhishwa sana na vipaumbele vilivyoomo ndani ya Mpango, yaani miundombinu, maji, nishati na huduma za jamii kama maji na elimu. Kwa kuweka mkazo katika miundombinu; barabara, reli na

bandari, umeme na maji hayo ni maeneo matatu yatakayo-*stimulate growth* na *linkage* katika Sekta nyingine ambazo ni Kilimo Uvuvi, Madini na Biashara.

Kwanza, Malengo ya kutumia 8.0 trillioni katika maendeleo ni mazuri, lakini uwekezaji huu usiwe wa Serikali pekee, Sekta Binafsi lazima ishirikishwe kikamilifu, maana huko ndiko ambako kuna *abundant resources*. Ili kufanikisha haya, tunahitaji kutekeleza haraka yafuatayo:-

(i) Kupunguza urasimu usio wa lazima katika kufanya mambo yetu; njoo kesho njoo kesho, iondoke. Tuwe tunatoa maamuzi ya haraka katika miradi/maombi ya uwekezaji.

(ii) Kuinua uwezo wa kitaaluma (*Human Resources Development*) ili waweze kumudu *challenges* za uwekezaji na kuwapa *skills development*. Maana *middle income economy* ni pamoja na jamii yenyе uelewa na weledi katika kutenda kazi.

(iii) Usimamizi wa karibu wa utekelezaji. Rasilimali fedha na nyinginezo ni vizuri zikasimamiwa vizuri ili kuleta maendeleo tarajiwा.

(iv) Kutoa rasilimali fedha kwa wakati. Miradi ya Miundombinu; Reli, Barabara, Bandari, Maji na Umeme huhitaji fedha nyingi na inabidi zitolewe haraka ili Miradi itekelezwe kwa wakati ili kuepuka na *escalating costs*, kutokana kuchelewa chelewa kutolewa fedha. Miradi isimamiwe vizuri ili iweze kumudu *value for money*.

Pili, kukuza uuza jje. Nchi hii imebarikiwa kuwa na ardhi nzuri na hali ya hewa nzuri. Tuongeze *quality* ya mazao yetu; pamba, kahawa, korosho. Tuongeze ubora wa mazao ili yapate bei nzuri katika soko la dunia. Lazima kuimarisha *extension services* ili wakulima waweze kuinua wingi wa mazao na viwango (*quality*) sasa twende kwenye mazao mengine kama *spices et cetera*, ambazo zina masoko makubwa.

Tatu, wakati umefika wa kuiimarisha Sekta ya Uvuvi ili kuongeza wavuvi vyanzo bora kama nyavu, boti na elimu ya uvuvi ili kuongeza mazao ya samaki. Bahari Kuu ina zaidi ya tani 700,000 za samaki, ambao bado *untapped*, inabidi pia kuimarisha ufugaji wa samaki ili kuiimarisha Sekta hii.

Sekta ya Mifugo inabidi iimarishe, tupate ng'ombe, kuku na mbuzi ili tuweze kuuza nyama jje ya nchi. Nchi kama Botswana, inao ng'ombe wachache na wazuri ambao huuza nyama katika Soko la Jumuia ya Ulaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Mipango yote hii ifanikiwe, nchi yetu inahitaji kuweka fedha za kutosha katika kutunza na kulinda mazingira. Kuna uhusiano mkubwa wa misitu, maji na mvua. Tupande miti ya kutosha ili kuongeza mvua ambayo ni chanzo kikubwa cha maji, ambayo ni nyenzo kubwa katika kilimo, nishati ya umeme na kadhalika. Ni vizuri Serikali ikasaidia Wananchi katika kutumia *alternative energy, gas* na majiko banifu ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa.

Utengamano wa Kikanda: Nchi yetu itumie kuwemo kwenye *Regional Groupings* mfano, *SADC, EAC*, ili kupata fedha, uwekezaji toka kwa *investors* wanaotoka katika nchi hizo. *Cross border na Transboundary Investment Flows* ziruhusiwe ili kukuza uwekezaji ndani ya nchi yetu.

Sheria na mapambano dhidi ya rushwa: ni lazima kuimarisha utawala wa sheria na kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa. Rushwa ni adui mkubwa wa Utawala Bora na uwekezaji. Kesi za kibiashara ziamuliwe haraka ili kujenga *confidence* ya uwekezaji na wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatanguliza kuchangia kwa kuunga mkono hoja hii. Pia ninaungana na mtoa hoja kwamba, kupanga ni kuchagua na ni lazima unapopanga kuwe na vipau mbele. Mpango huu ni wa Taifa zima, bila Watanzania wote kushiriki kwenye Mpango huu, Serikali haiwezi kufanya kitu. Kila mtu kwa wakati wake na kwa nguvu zake, ashiriki kufanya kazi. Serikali haiwezi kuondoa njaa bila watu kufanya kazi na kupata chakula bila kutegemea mtu yeoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba, Umma wa Watanzania unaishi vijiji katika mitaa. Kama mgao wa bajeti ambao tunasema ni kasungura, tatizo la mgao ni tatizo kubwa kwani kuna maeneo mengi bado wako nyuma kielimu. Elimu ni ufunguo wa maendeleo na kwa kuwa kuna wilaya nyingi bado wako nyuma, basi ni vigumu kwenda pamoja na wilaya zingine.

Napenda kunukuu maneno ya Baba wa Taifa, aliwahi kusema: “Tusipoangalia baadhi ya makabila yaliyoko nyuma kielimu, tunaweza kujenga Taifa ambalo kuna watawala na watawaliwa, kwani kutakuwa na watu ambao watakuwa kwenye nafasi ya utawala kwa ajili ya elimu yao.”

Nataka kutahadharisha hapa kwamba, kuna makabila yameachwa nyuma hata kwenye nafasi za Uongozi wa Serikali Kuu, Mikoani na kwenye Halmashauri kutokana na elimu. Serikali sasa ichukue jukumu la kuangalia maeneo hayo na kuweka Mpango wa Kuendeleza sehemu hizo ili nao waweze kupata ajira kwenye Taifa hili. Kwa nini tukae kimya huku watu wengine wabaki kuwa walinzi wa watu mijini?

Kama Serikali inataka kuwasaidia Wananchi hawa ni afadhali sasa kuanzisha Vyuo vyta VETA katika maneo hayo. Inashangaza kuongeza vyuo kwenye maeneo yenye vyuo na kuacha maeneo ambayo hayana Vyuo vyta VETA. Tukijenga Vyuo vyta Ufundu kwenye Halmashauri hizo, wanafunzi ambao hawakuweza kuendelea wasoma kwenye vyuo hivyo na kuweza kujiajiri. Ninaomba hili lianzishwe haraka sana.

Tatizo lingine ambalo limesaulika ni Mpango kuhusu Mifugo. Kwa muda mrefu Sekta hii inasaulika kabisa hasa kwa kuwekwa kila mara kwenye Sekta zingine; mara kwenye Kilimo, mara kwenye Maji; bayaa zaidi, kwenye Uvuvi, Sekta ambayo

haiendani kabisa. Kama tunataka Zao la Mifugo lisaidie Taifa hili, Sekta ya Mifugo ibaki yenye we kwenye Mpango huu ili tuangalie kilio cha muda mrefu cha wafugaji kama kitakwisha.

Suala la kuzungumzia mikopo ni muhimu ili kuwasaidia Wananchi kufanya biashara na kunyanya uchumi wao. Lazima kuwe na utaratibu wa kuwawezesha Wananchi waandaliwe kupata mikopo. Wananchi wapewe Hati za Ardhi, Mashamba na Viwanja ili waweze kupata mikopo. SACCOS za Vijana na Vikundi vingine ziimarishwe ili Wananchi wote wafaidike kwa ajili ya kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu umelenga kufufua kilimo. Ninaishukuru Serikali kuwaletea Wananchi pembejeo na kuongeza kilimo cha chakula na kuuza chakula nje kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali iangalie suala la wakulima kuuza mazao nje ya nchi, jambo ambalo wakulima wanapata shida wanapokamatwa wasiuze mazao nje. Kama tumewawezesha Wananchi walime mazao ya kuuza, lakini bado wananyimwa ni hatari sana, kwani tuko kwenye Biashara ya Jumuia ya Afrika Mashariki huku wakulima tunawakataza waziuze mazao nje; je, watauza wapi? Ninaomba jambo hili liangaliwe, kwani kule Kaskazini kuzuia mazao imekuwa mradi wa watu wanaojifanya wanazuia nafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza kwa dhati Tume ya Mipango kwa mpango mkakati ulioandaliwa kwa kuwa na mawanda mapana na kugusa kila eneo ili kuhakikisha jamii kwa ujumla wake imeguswa. Nashauri Mpango huu mzuri uelekezwe kwa kiasi kikubwa zaidi katika maeneo ambayo kwa muda mrefu kumekuwa na mvua za kutosha na ardhi yenye rutuba ya kutosha kama Mikoa ya nyanda za juu kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya, pamoja na uzalishaji wa mazao ya chakula, Mpango huu haujaeleza mipango ya makusudi ya kuwawezesha wakulima kuondokana na matumizi ya jembe la mkono na wanyamakazi na kuanza kutumia matrekta ili Taifa liwe na uhakika wa chakula na ziada kuuzwa nje ya nchi na hivyo kuongeza kipato kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo dhambi kwa Mpango kutamka namna utakavyokuwa bora kuhakikisha kwamba wananchi wanaelimishwa juu ya uanzishaji wa vikundi. Mpango usije uka-take for granted kama vile wananchi wanaelewa manufaa yatokanayo na uanzishaji wa vikundi, ni vizuri Mpango ukazingatia utoaji wa elimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uzuri wa Mpango huu, kwa bahati mbaya Mpango huu haujataja baadhi ya maeneo yenye fursa kubwa sana na rahisi kwa ufuaji wa

umeme. Eneo ambalo lina maporomoko ya pili kwa ukubwa kwa Afrika ni maporomoko ya Kalambo ambayo ni kivutio kizuri na chanzo rahisi cha kufufua nishati ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashindwa kuelewa kwamba: Je, Tume haiyajui maporomoko haya maarufu au ni kwamba kama nchi tumekuwa na raslimali nyingi mno mpaka nyingine tumeamua kutozitumia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango hautaji jitihada za kutafuta mafuta katika Jimbo la Kalambo, maeneo ya Kasanga, sehemu ya Bismack, eneo linaloaminika kuwa na mafuta mengi sana. Ndio maana Wajerumani walikuwa tayari kuita jina la kwao ili machimbo hayo yatakapoanza jina la kwao liweze kusifika. Napendekeza maboresho yafanyike na mapendekezo haya yaingizwe katika mpango huu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu mzuri umejikita katika kuhakikisha kwamba tumekuwa na miundombinu ya barabara. Kwa bahati mbaya, Mpango haukukumbuka barabara fupi (*Critical part*) kutoka Tunduma, Mbeya kwenda bandari ya Kasanga maarufu kama barabara ya zamani ya Mjerumani ambayo lengo lake la msingi ni kiunganishi cha Mkoa wa Rukwa na nchi za Zambia, Burundi na Demokrasia ya Congo. Barabara hii itakuwa kichocheo kikubwa sana katika kuuletea maendeleo ya haraka kwa Mkoa wa Rukwa na nchi kwa ujumla. Pia barabara hii itasaidia kupunguza msongamano wa malori katika mpaka wa Tunduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2011/2016. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uamuza thabiti wa kuunda Idara ya Mipango na kuja na mipango thabiti. Naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Napenda kuchangia kuhusiana na suala la miundombinu. Umeme ni jambo litakalotukomboa. Kufikisha umeme katika maeneo ya majimbo yetu, kwa mfano, Jimbo la Manyovu kwani ni kikwazo kinachofanya fursa kutokuwepo za kuijendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Manyovu – Kasulu yenye kilometra 45 ambazo ni barabara muhimu inayounganisha barabara toka Kigoma na Burudi ambayo itapita Wilaya mpya ya Bihigwe mpaka Kasulu, ili iweze kuelekea Wilaya ya Kagera (Nyakanazi). Ninaomba Tume iiwekee umuhimu ili tusafirishe mazao yetu na biashara zote za eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mpango utusaidie masoko ya mipakani ili tuweze kuwanufaisha katika biashara zao. Ndani ya Mpango sioni wapi pamewekwa mikakati ili kupata kodi inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, VETA ni muhimu katika kutoa fursa kwa vijana. Naomba Wilaya mpya ya Bihigwe nayo isisaha unlike wakati wa kuweka mipango ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nafurahia mipango hii, ila usimamizi lazima uwe imara, fedha za kuwezesha Mpango huu ni muhimu kutafutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba elimu iweze kuwakomboa na iwe inahamasisha vinaja wetu kujajiri. Hivyo, mitaala iweze kuoanishwa na lengo letu jipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la maji, mipango ya maeneo tofauti itofautiane kwani sehemu nyingine inahitaji visima virefu ili maji yaweze kupatikana, lakini kama umeme utakuwepo utahamasisha maji salama kwa wananchi. Mwisho, naunga mkono hoja.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri iliyotoa dira na mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano. Vile vile ninawapongeza Mheshimiwa Stephen Wasira - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Sera na Utawala Bora, Katibu Mkuu Kiongozi na Watendaji wote walioshiriki kuandaa Mpango huu mzuri ambao una lengo zima la kuwaondoa Watanzania kwenye umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi, sasa nianze kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali kwamba inapogawa bajeti kwenye Mikoa, Halmashauri iangalie hali ya uchumi na wingi wa watu kwa kila Mkoa na Halmashauri ili kuleta maendeleo yanayolingana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwani katika kipindi cha kampeni alitoa ahadi nyingi akizingatia mahitaji ya wananchi walio wengi kwa lengo la kuwaleta maendeleo. Hivyo basi, naishauri Serikali kuhakikisha ahadi hizi zinaingizwa kwenye bajeti za kila mwaka kwa kuangalia kipaumbele. Hii itajenga imani kubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kukiri kuwa utaratibu wa kutenga fedha za kukopesha Watanzania wakiwemo wanawake na vijana ni mzuri sana. Hivyo, napenda kuishauri Serikali kuwa bado elimu hajatolewa vyta kutosha kwa wananchi ndiyo sababu urejeshaji ni wa kusuasua. Ni vyema Mpango mzuri ukaandaliwa kutoa elimu kuhusiana na namna ya kuibua miradi, uendeshaji wa biashara, utunzaji wa fedha na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ukweli imebarikiwa sana kuwa na kila aina ya vyanzo vyta uchumi wa nchi bali bado ukusanyaji wa fedha kupitia vyanzo hivyo, bado hauna tija sana, kwani bado ubadhirifu upo. Ninaishauri Serikali kuweka mikakati madhubuti na usimamizi makini. Nina hakika uwezekano wa kupunguza utegemezi upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa jinsi inavyojitahidi kusogeza huduma kwa Watanzania kama vile shule, zahanati, maji, barabara na kadhalika. Ni ukweli usiopingika kuwa mafanikio ni makubwa sana. Mapungufu ninayoyaona eneo la Mahakama, hospitali na kadhalika, bado kuna harufu ya rushwa. Ninaishauri Serikali kuangalia namna ya kuondoa rushwa ikiwa ni pamoja na kuboresha maslahi ya watumishi na ufuatiliaji wa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza vyanzo vya mapato kwenye halmashauri na kata: naipongeza Serikali kwa mikakati yake mizuri ya kuibua vyanzo mbalimbali kwenye Halmashauri kwa lengo lwa kuongeza pato la Halmashauri ili waweze kujiendesha. Ukweli ni kwamba, Mpango huu ni mzuri na una malengo mazuri. Hivyo basi, naomba nishauri kwamba vyanzo hivyo viainishwe ili isije ikawasumbua wauza nyanya, chumvi, kuni na kadhalika kwani biashara hizi ni za wananchi masikini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda nimalizie kwa kupongeza Mpango mzima ulioainishwa kwa vipaumbele. Ili tuweze kutekeleza vizuri, lazima tudumishe amani na mshikamano. Hivyo, Serikali iwe macho kudhibiti wale wanaopotosha wananchi na kusababisha maandamano na fujo na wakati mwingine kuleta maafa. Vile vile kwa takwimu, wako Watendaji wanakusanya mezani na kutoa *data* ambao zio sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii mia kwa mia, nami nitakuwa mstari wa mbele kushirikiana na Serikali kutekeleza Mpango huu.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza wote waliohusika katika kuwasilisha Mpango huu akiwemo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Ndugu Mpango wa Tume ya Mipango na Mawaziri wote waliohusika na kusimamia uwasilishaji wa Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango kwa ujumla umekidhi mahitaji yote ya kuzindua upya maendeleo ya nchi yetu. Vipaumbele vilivyowekwa ni sahihi, lakini naomba kushauri mambo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dhamira ya kweli iwepo kwa Watendaji wetu kitaifa na katika ngazi zote. Siasa isiruhusiwe katika utekelezaji wa mipango yote. Sheria zitumike kudhibiti wanaohujumu utekelezaji wa Mpango huu kwa maslahi yoyote yale ambayo ni kikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Mpango huu uweze kutekelezeka, ni budi kuwe na utaratibu wa wazi wa kupata fedha za kutekeleza azma ya Mpango huu. Nashauri kuwepo na Mfuko maalum wa utekelezaji malengo ya Mpango. Mfuko huo uchangiwe kwa hali na mali kutoka taasisi, mashirika, wakala, nchi rafiki na kadhalika. Utaratibu huo uwe wa mpito, baadaye iundwe Benki ya Maendeleo tofauti na benki ya raslimali. Benki hiyo itahusika na uratibu na utafutaji wa fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni budi zitungwe sheria mbalimbali mapema kama hatua ya mwanzo/maandalizi ya utekelezaji wa Mpango huu. Bila sheria na usimamizi thabiti wa sheria hizo Mpango huu utekelezaji wake utakuwa ni mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri kuwepo na uwasilishaji wa taarifa ya utekelezaji wa Mpango huu kwa Bunge, yaani kila Bunge la mwezi wa Februari, kwa mujibu wa Katiba bila kukosa. Wahusika wote wawajibishwe kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kabisa na nampongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuwa na wazo la kurudisha tena utaratibu wa kuwa na mpango wa maendeleo wa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili naupongeza na kuunga mkono Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano, yaani 2011/2011 – 2015/2016. Naunga mkono Mpango huu kwa sababu umewajali wananchi wote, umewajali vijana (uk 49 na 69) toleo la Kiingereza, umewajali wafanyabiashara, wadogo na wa kati, umewajali wafanyakazi, umeyajali makundi tete (*vulnerable*), yaani walemovu, wajawazito na watoto walio chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango umewajali wananchi kwa ujumla kwani umegusa vipaumbele vikuu vitano vivilvyoorodheshwa kuanzia ukurasa 51 – 70 (toleo la Kiingereza), nazo ni Miundombinu kwa maana ya umeme, bandari, reli, barabara, uchukuzi na usafiri wa anga, sayansi na teknolojia; kilimo; viwanda; maji na uendelezaji wa raslimali watu kwa ajili ya huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mpango huu ni wa kitaifa, kwani umeandaliwa kwa dhana ya ushirikishwaji jamii kuititia Wizara, Idara na *Agencies* mbalimbali, Halmashauri za Wilaya na wadau mbalimbali na wananchi katika ngazi ya Kata na Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Mpango ni wa kitaifa, kwani umeshirikisha jamii kuititia *O & OD*, Mipango Shirikishi ya Vijiji – Kata – Halmashauri – Wizara na hatimaye Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga ni jambo moja, lakini utekelezaji ni jambo lingine. Ningeomba Watendaji na kila anayetakiwa kuutekeleza Mpango huu afanye hivyo kwa uwajibikaji na uadilifu wa hali ya juu, lakini uwazi wa fedha zinazopelekwa kwenye Wizara, Idara mbalimbali na Halmashauri zote ziwekwe wazi kwenye mbaao za matangazo ngazi zote bila kusahau ngazi za Kata na Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo zitumike kama zilivyopangiwa na kulingana na *interventions* zilizoko kwenye Mpango. Wananchi katika ngazi zote hasa vijijini, vitongojini na mitaa washirikishwe katika utekelezaji, ufuatiliaji tathmini na kujua kiasi licha fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mipango yao ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ombi langu kuwa nayo Serikali isaidiane na Watendaji/watekelezaji wa Mpango kwa kupeleka mafungu ya fedha kwenye Wizara, Idara na Halmashauri za Wilaya ili utekelezaji uende/ufanyike kwa wakati uliopangwa kwenye Mpango (*time frame*) na siyo kama ilivyo sasa ambapo fedha robo ya kwanza angalau robo ya pili mara nyingine hutolewa kwenye robo ya tatu au ya nne. Hii hupelekea utekelezaji zimamoto, hafifu na usio na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono na kuupongeza Mpango huu wa miaka mitano (2011/2012 – 2015/2016).

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kuipongeza Serikali kwa namna ambavyo imedhamiria kuiondoa nchi hii na wananchi wake katika dimbwi la umasikini ambalo kwa kiasi kikubwa kinachangiwa na mitikisiko ya kiuchumi duniani na kupanda kwa bei ya mafuta kiholela, yamkini na ukuaji wa kasi wa sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina kila sababu ya kupiga hatua katika kipindi hiki cha *programme* ya 2025, ila kinachohitajika hapa ni ukweli, uaminifu, kujituma na kuwa na dhamira ya kweli hususan Serikali kuwa na utayari wa kusimamia Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu umeelekeza kutumika kwa nguvu kazi, hususan ya vijana. Ninachoshauri kwa Serikali ni kuanza kuwajengea mazingira mazuri ili waandalike, kukubalika na wawe na uwezo katika kutekeleza. Kwa hiyo, Serikali ikubali kutenga fedha za maandalizi. Vile vile Serikali ishajihishe kutumia raslimali tulizonazo kwa kutumia utamaduni wa kimila ambao bado una nafasi nzuri kuleta maendeleo kwa kushirikisha kila mtu kwa nafasi yake.

Vile vile nashauri Serikali itengeneze mpango mahususi wa kuwa na mawasiliano ya karibu na Taasisi za Kifedha, kwa minajili ya kuleta msukumo, hususan vijijini kwa kuwapatia mikopo nafuu wakulima wetu na wazalishaji wengine wadogo wadogo.

Pia nashauri kuwepo na mipango madhubuti ya kurahisisha sekta za mawasiliano na miundombinu ili Mpango huu uwe endelevu na miundombinu na uanzie chini (*grass root*) na kuja ngazi za juu ambapo hii itairahisishia Serikali kuona wapi kuna mapungufu na kuweza kutafuta ufumbuzi wa haraka na kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Mpango huu, Serikali sasa haina budi kuandaa mjadala wa kitaifa kuhusu upatikanaji wa Dira ya Taifa ili kila Mtanzania aelewe jukumu lake na awe na uwezo wa kujipima ye ye mwenyewe ni kwa namna gani anasaidia kukuza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na mtoa hoja wa Kamati ya kwamba ni lazima tukubali uchumi sasa utumikie siasa, kwani katika dunia ya leo uchumi ndiyo siasa. Ili kuhakikisha Mpango huu unafanikiwa na unatekelezeka, ni lazima Serikali iwe

na utayari wa maamuzi na yafanyike kwa haraka na kwa wakati unaofaa kulingana na mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina budi kuangalia upya upatikanaji wa vyanzo vipyta vya mapato na kuzidisha udhibiti wa ukusanyaji kodi hususan kwa wawekezaji, sekta ya madini na uingizaji wa vifaa nchini, hususan kwa wale wafanyabiashara wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kutumia wataalamu wetu kuangalia upya mpango mkakati wa upatikanaji wa nishati ya umeme ambayo imekuwa ni sugu kwa kutumia raslimali asili tulizonazo kama vile gesi inayotokana na maeneo yenye *volcano*, mpango ambao wenzetu wa nchi jirani (Kenya) sasa hivi wanauendezea. Naunga mkono Mpango huu.

MHE. SALIM HEMEDI KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Mpango wa Maendeleo ya miaka mitano toka mwaka 2011/2012 – 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane na wale wanaosema kuwa kosa la kikatiba lililofanywa na viongozi wa Serikali kuruhusu Mpango huu kuzinduliwa na Mheshimiwa Rais kabla ya kupitishwa na Bunge kama ilivyolekezwa kwenye Katiba ibara ya 36. Hivyo sielewi mawazo ya Waheshimiwa Wabunge yataingizwaje katika mpango wakati vitabu vimeshatolewa na kugaiwa kwa wadau. Labda tuseme, kujadili mpango huu ni namna moja ya kuuhalisha kama inavyotaka Katiba yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na mipango mingi baada ya uhuru, mipango ya muda wa kati na ya muda mfupi, lakini haikutekelezwa kama ilivyokusudiwa. Inawezekana sababu mojawapo ni kutokuwa na nia ya mipango yetu kusimamia uchumi au hatukuwa na uwezo wa kusimamia uchumi kwa maana ya raslimali watu. Sababu zinazotolewa kwa kushindwa utekelezaji wa mipango, ni vita dhidi ya Nduli Iddi Amin au kuvunjika kwa Shirikisho la Afrika Mashariki. Lakini jambo la msingi ni pale tulipokataa masharti ya Shirika la Fedha duniani (*IMF*) tukasusiwa na wadau wote wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya majukumu ya Mpango juu ni kuzalisha kwa wingi mazao ya chakula hasa mahindi na mpunga katika ukanda wa kusini (*SAGCOT*). Ni kweli kuwa ukanda huu ni muhimu kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo, lakini tuisisahau au kuwa Tanzania inazalisha matunda kwa wingi kiasi kwamba yanaiza wakati wa msimu, kwa nini tusianzie hapa kwa kujenga viwanda vya kusindika mazao hayo? Lakini hata yale maeneo yenye mazao mengi ya kilimo, tatizo ni miundombinu ya barabara. Ili kuwa na barabara zinazopitika kwa mwaka mzima, tunahitaji pesa za kutosha. Bajeti ya Mpango ni trillioni nane kwa mwaka. Serikali itatumia mbinu gani kupata pesa ya kukidhi haja ikiwa leo bajeti nzima ya Serikali ni shilingi trillioni 13.525 tu. Hivyo, ni lazima Serikali itafute vyanzo vyingine vya kuongeza mapato badala ya kutegemea wahisani kufadhili Mpango wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kufungu cha 27 kinachosomeka: "Serikali sekta ya umma ambapo kuwepo kwa utawala bora utawala wa sheria, demokrasia, haki za binadamu, kuzuia rushwa, uwazi na uwajibikaji ndiyo nguzo ya kufanikiwa kwa Mpango huu wa Maendeleo." Lakini hivi vyote katika nchi yetu ni kikwazo, bado vinakosekana kwa sababu utawala bora haujafikiwa, kwani demokrasia ya kweli haijakuwepo, haki za binadamu zinakiukwa, rushwa inazidi kukua kila siku na uwazi na uwajibikaji haupo. Kwa hiyo, vyote hivi vinasababishwa na Katiba iliyopo ili kufanikiwa Mpango huu wa Maendeleo wa miaka mitano. Kwanza ni vyema kuwepo na Katiba mpya kwa sababu Katiba ndiyo inayosimamia Mpango huu wote wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu 28 ukurasa wa 21 unazungumzia umuhimu wa sekta binafsi katika maendeleo ya nchi. Sekta binafsi ndiyo inachangia kukua kwa uchumi, lakini Serikali haiipi umuhimu sekta binafsi, badala yake inawapa umuhimu wawekezaji kutoka nje. Ushauri wangu ni kwamba, kipaumbele kikubwa kipelekwe kwenye sekta binafsi na wawekezaji kutoka nje washirikiane na wazalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 23 kifungu cha 29 kinazungumzia kwamba, ili Mpango wa Maendekeo ufanikiwe, Serikali inatakiwa iwe na sera maalum ya fedha, kwa mfano, sasa hivi Taasisi zake kama Benki Kuu na mabenki mengine, fedha za kigeni kama *dollar rate* yake ni kubwa kuliko wanavyouza sekta binafsi. Kutokana na hali hiyo, watu wote hukimbilia kununua dola mitaani. Kwa hiyo, hakuwezi kuwa na sera bora ya kodi na fedha, na kwa hali hii, Mpango huu wa Maendeleo hauwezi kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 25 kifungu cha 30 (d) kinazungumzia kwamba asilimia 60 ya nguvu kazi ya Taifa ni vijana. Lakini vijana wote wamehamza vijijini na wako mjini, wanazurura mitaani na kufanya mambo maovu, kuvuta bangi, kujihusisha na madawa ya kulevyaa na wengine kuwa vibaka na wezi. Lakini tukirudi nyuma, chama chochote hakiwezi kupata ushindi ikiwa haijaungwa mkono na asilimia 60 ya vijana. Hawa vijana siyo kama tunakaa tukasema asiimia 60 ni vijana, bali tunawashawishi, tunawahamasisha, ndiyo hutuunga mkono na wakatupa kura. Kwa hiyo, sasa umefika wakati vyama vyaa siasa, CCM, CUF na CHADEMA na vyama vyote ambavyo vinashiriki kwenye uchaguzi, tuwahamasisha hawa vijana warudi vijijini na Serikali watengeneze mazingira mazuri ya kilimo kwa mfano, kuwakopesha pembejeo na zana za kisasa za kilimo na chama chochote kikishindwa kuwahamasisha hawa vijana kurudi vijijini wasiruhusiwe kushiriki kwenye uchaguzi wa mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwapa pole wananchi wa Tarime wote hususan Wananyamongo na Watanzania kwa ujumla kwa dhuluma wanayofanyiwa wazawa na Polisi wetu.

Napenda kukuchukua fursa hii kuitaka Serikali kuchukua hatua mbadala ya kutafuta suluhisho la muda mrefu ambalo litatoa fursa kwa Serikali kuu kupata mapato (*revenue*), wawekezaji kupata *profit (return on investment)* na wazawa kufaidika na uwekezaji kwa maana ya kupata ajira, maendeleo au uboreshaji kwenye huduma za jamii kwa shule, hospitali, barabara, maji na kadhalika ili kuweka mazingira bora kati ya wawekezaji na wazawa na kuepusha vifo vya Watanzania wasiokuwa na hatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, napenda kutoa angalizo au ushauri katika kuchangia maboresho ya Mpango wa Maendeleo 2011/ 2012 – 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja, ila baada ya marekebisho ya pendekezo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tangu nazaliwa nimekuta shida ya maji, siyo mijini siyo vijijini. Tumeshuhudia vijijini akinamama wanatembea zaidi ya kilomita mbili hadi tano kutafuta maji kitu ambacho kinapelekea mfarakano katika familia za Watanzania. Vile vile mijini hasa katika majiji kama Dar es Salaam, maji safi na salama imeendelea kuwa ndoto, kitu ambacho ni fedheha kwa Serikali. Hivyo basi, kufuatana na Mpango huu, naishauri Serikali kutenda yote kama ilivyoandikwa na kuwasilishwa katika Bunge lako Tukufu. Serikali ihakikishe kuwa sehemu zote za miji zinapata maji safi na salama kwa muda wote na masaa 28 bila kikomo, kwani maji ni uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali ihakikishe kuwa kila kijiji au kitongoji ndani ya kijiji wapate maji safi na salama kwa kuchimbiwa visima vyenye hadhi mbadala ndani ya miaka ya Mpango huu nchi nzima hususan Mkoa wa Mara hasa Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kuchangia kwenye kipaumbele cha elimu kwenye Mpango huu. Ili tuweze kuwa na elimu bora na sio bora elimu (*quality education that produce quality graduate with the right knowledge for the development of our country*) Serikali inahitaji kuboresha na kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kujenga msingi ulio imara kwa watoto wetu kuanzia Shule ya Msingi na Sekondari, na hili limetimia kwa kuwa na *right facilitator*. Watu mbadala wanaotoa elimu, wajue *the subject matter*. Pili, tujenge maabara na kuweka vifaa vya maabara na wataalam. Pia *computer ziwekewe syllabus* tangu Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo. Ni fedheha kuona Vyuo vyetu havina hata *computer* za kutosha. Sasa katika hali hii hatuwezi kusonga mbele. Vile vile kwa kipindi hiki, Serikali ipeleke Watanzania nje waweze kupata utaalam mbadala ili waweze kutekeleza Mpango huo kikamilifu. Inabidi Serikali iweke sheria kali juu ya uwajibikaji wa wafanyakazi ili kuweza kuleta ufanisi kazini, kwani utendaji kazi kwenye sekta za umma ni dhaifu kulingana na ule wa sekta binafsi. *Production rate ratio is 5:1 comperably*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni kuhusu utekelezaji wa kuboresha barabara za vijijini ambazo ndiyo msingi wa utekelezaji wa Kilimo Kwanza, kwani wakulima wanapata urahisi wa kusafirisha mazao yao. Vile vile katika kuenzi Kilimo Kwanza,

nashauri utoaji wa trekta katika vijiji ili Watanzania waweze kukodi na kuyafanya shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa mwendelezo wa mchango au angalizo kwenye Mpango wa Maendeleo kwenye kipaumbele cha raslimali watu. Mpango umeainisha kufanya *rehabilitation* na *expansion* kwenye *higher learning institution*. Ni jambo zuri, kwani majengo ya Vyuo ni ya zamani na yanahitaji kufanyiwa ukarabati na kuonyesha *theatre* zao kwani enzi hizo usajili wa wanafunzi ulikuwa kidogo ukilinganisha na sasa. Hivyo namba imeongezeka na majengo lazima yaongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napendekeza kuboreshwa kwa *thearte* za kufundishia na kufanya ziwe za kisasa zaidi kwani hadi leo kwenye vyuo vyetu tunatumia *blackboard* and *chalks*, badala ya *projector* au *clip board*. *Theatre* zipewe *teaching facility* kama *microphone*, na vitu vingine. Pia nyumba za wahadhiri hususan Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Na-declare interest kwamba mimi ni mwajiriwa wa *UDSM*. Tangu naajiriwa mwaka 2005 niliahidiwa nyuma kuwa kuna *one of the package*, lakini sikuweza kupewa. Hii inapelekea wahadhiri kuhangaika na kuishi mbali na Chuo kitu ambacho kinaathiri utendaji kazi wao, hasa ukizingatia foleni za Dar es Salaam. Pia Tume izingatie ujenzi wa *hostel* kwa ajili ya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni kuhusu mto hoja (Waziri) kulidanganya Bunge, kwani kwenye ukurasa wa 16 Waziri kaainisha kuwa Chuo Kikuu cha Butiama cha Kilimo kwenye Mpango wa miaka mitano hadi 2015. Ukiangalia page 146 na 147 ya Mpango, Chuo hiki cha Butiama hakipo. Hivyo, Waziri unaweza kuainisha kipi kitekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Mara naitaka Serikali kuingiza ujenzi huu wa Chuo cha Butiama kwenye Mpango kama ilivyotajwa na Mto hoja (Waziri husika).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsante.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa kupendekeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Serikali itafute wawekezaji wa ndani na nje watakaoweza kufufua miundombinu ya reli nchini kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kwa nchi kubwa sana kama Tanzania kutokuwa na Shirika lolote la ndege. Serikali ikaribishe wawekezaji wa ndani waendeshe shirika hili muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza pia Serikali ikaribishe wawekezaji wa usafiri wa majini kutoa huduma kwenye jiji la Dar es Salaam ili kupunguza msongamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tuhimize kuendeleza utalii wa utamaduni badala ya kuwa na utalii wa kuona wanyama tu. Hii itasaidia watalii kutembelea vijiji vyetu na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri wakulima wapewe uhuru wa kuuza mazao yao popote kulingana na mahitaji ya soko; wafugaji na wakulima wapewe ruzuku na pembejeo na madawa ya mifugo na kujengwa mabwawa na malambo kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji pamoja na maji kwa ajili ya ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuupongeza mpango mzima wa maendeleo unayotokana na dira ya mwaka 2000 – 2025. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuanzisha Tume ya Mpango na ilioandaliwa pamoja na wadau wa maendeleo, Mpango wa miaka mitano ya kwanza. Pia nawapongeza wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine.

Mpango umelenga kuleta maendeleo kwa Watanzania wote kwa ujumla. Mpango umeainisha vipaumbele ambavyo vikitekelezwa ipasavyo, patakuwa na hatua kubwa kwa uchumi wa nchi na maendeleo kwa ujumla kwa wananchi wote.

Napenda kuchangia katika maeneo machache ambayo naamini yakiboresha pataleta mabadiliko katika uchumi wa nchi na wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, katika Sekta ya Nishati na Miundombinu, napenda uongezwe mfumo wa usambazaji wa umeme kwa wananchi waliokuwa wengi. Maeneo ambayo umeme unapita haina budi nayo yapatiwe umeme. Kama Serikali haina bajeti ya kutosha sekta binafsi au wadau waweze kuchangia (*TANESCO*) Serikali kwa kukopesha na baadaye warudishiwe kwa kupunguza kwenye bili. Pili, katika sekta hiyo tuanze kutengeneza nguzo za umeme za sementi ambazo zitakuwa bei nafuu na kupunguza kutegemea nguzo za mbao na kuboresha mazingira yetu. Pia tutafute wawekezaji ambao watazalisha malighafi, mfano nyaya na *insulator* hapa hapa nchini.

Pia katika miundombinu, Mpango ni mzuri sana. Ningependa kuboresha pale katika reli ya Tanga – Moshi – Arusha, kwamba mpango ni kuandaa ujenzi wa reli mpya kutoka Arusha – Musoma. Katika mpango wa bajeti hakuna fungu la kuiendeleza reli ya Arusha – Moshi – Tanga. Ni muhimu kama ilivyo na itasaida uchumi wa kanda hiyo pamoja na wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napendekeza kuwekwa katika mpango wa miaka mitano barabara muhimu kwa maendeleo ya wananchi wa Manyara, Singida, Shinyanga na za kanda ya ziwa. Barabara ya Babati – Mbulu – Mwanhuizi - (Mlatu) Mwandoya (Kisesa) – Bariadi – Lamadi kwa kiwango cha lami; barabara muhimu katika sekta ya madini, ufugaji, kilimo na mpango wa *EPZ* Mererani.

Sekta ya Kilimo, iwekwe katika Mpango huo wa miaka mitano, mazao yenye thamani kubwa yazalishwe nchini ambayo kwa sasa tunaagiza kwa gharama kubwa na kunufaisha wakulima wa nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna maeneo mengi nchini ambako kunafaa kupanda matunda ya *apple* tunayo-*import* na tunaweza kuwa muda mfupi tuka-*export* nchi za jirani pamoja na matunda mengine, mfano zabibu, *plums, pears* na kadhalika. Pia mikopo inayotolewa na *TIB* asilimia 60 zipelekwe vijijini katika vikundi vya *saccos* na vikoba. Kwa sasa ni asilimia kidogo tu ambayo inapelekwa huko na sehemu kubwa kwenda kwa wakulima wakubwa binafsi na viwanda vya kilimo. Nashauri kwamba pawe na azma na lengo la kuwawezesha wakulima wadogo waliokuwa wengi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vituo vya *VETA* vitoe mitaala na mafunzo katika vituo vyote vitakavyofundisha kilimo na usindikaji wa mazao ya kilimo. Halafu tuwe na mpango madhubuti wa kuanzisha vituo vya kupima udongo kwa Mkoa na baadaye kila Wilaya (*Soil testing centers*). Hiyo itaboresha utumiaji wa mbolea sahihi na uzalishaji utakua na zaidi vituo hivyo pia inaweza kuwa vituo vya hali ya hewa (*weather stations*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mifugo nashauri tuwe na mpango ndani ya miaka hii mitano wa kuweka vituo vya maabara kila Mkoa na baadaye Wilaya. Pia mikopo itolewe kwa wafugaji ili waweze kuboresha mifugo na kuijendeleza wenye. Pia *breeding stations* ya mifugo uanzishwe ile mbegu bora ipatikane hapa nchini.

Pia iwekwe katika mpango huu, kipindi cha bajeti kila mwaka sehemu kubwa ielekezwе vijijini ambapo Watanzania wengi wapo na ndiyo wenye hali ngumu ya kimaisha. Kwa sasa fedha nyingi ya maendeleo inaelekezwе katika miji, miji midogo, na *centers* katika Kata. Kama ni barabara, umeme, maji bajeti kwa sehemu kubwa inalengwa pale vijijini. Hali ya miundombinu inabaki kuwa duni na sababu kubwa ya wananchi hao kukimbilia mijini au miji midogo ambako hawana kazi.

Pia pawe katika mpango huu, mafunzo ya uraia na utawala bora. *Mind set* ya viongozi wetu katika ngazi mbalimbali pia iangaliwe namna ya kubadilisha kwa kupata mafunzo ili twende na wakati. Hii itasaidia pia kuondoa migogoro ya miaka mingi iliyopo hasa katika sekta ya ardhi na migogoro ya miaka mingi haijatatuliwa na ndipo vurugu inatokea na wananchi kupoteza maisha (mfano: katika Wilaya ya Babati Bonde la Kiru, Mamire na Galapo) hapo pia viongozi wanaopotosha wananchi na kuhubiri umwagaji wa damu wasingepata nafasi kama wananchi wangepata elimu juu ya utawala bora na uraia.

Ni muhimu tukubali *conscrutive criticism* ili kuleta mabadiliko katika uongozi nchini katika ngazi mbalimbali. Ni muhimu kuongeza katika mpango huu wa miaka mitano, kuleta mabadiliko katika Sekta ya Mahakama - “*legal reform*” ili iende na wakati kwa kutumia *ICT* na kuharakisha utoaji wa haki, “*justice delayed is justice denied.*”

Muhimu pia katika Mpango huu pia Tume iwezeshwe kuijendeleza ni iwe na uwezo kufikia hadi ngazi za Wilaya, Kata na Vijiji ili Mpango ujao uwe “*broad based*” na mawazo ya wananchi wote katika Jamhuri ya Muungano yaweze kuchukuliwa elimu juu ya Tume na mfumo wa kuandaa mipango ifikiwe katika ngazo zote.

Katika Sekta ya Madini, uaandaji na mafunzo ya “vito” *jewell's (lapidary)* na Makao Makuu yasiwe Dar es Salaam yapelekwe Arusha, Dodoma na Moshi. Miradi yote leo Dar es Salaam pekee. Tuendeleze nchi kwa kupeleka miradi Mikoani na Wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tungeweka katika mpango, namna ya kutumia wataalam wetu wa kutoka katika majeshi yetu, JWTZ, JKT, Magereza na Polisi na nyingine katika kuendeleza nchi yetu na kutoa huduma kwa raia mfano, madaktari, *engineers, technicians* na wengine wengi ambao tuna upungufu katika sekta ya umma (raia). Mara nyingi wataalam hao hawana kazi ya muda wote huko katika sehemu zao za kazi na wanasaidia kutoa mawazo, elimu, kusimamia ili tufaidi kuwepo kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni machache niliyonayo, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali chini ya mpango huu inadhamiria kujenga moja kwa moja barabara nzuri kwenye maeneo yenye fursa kubwa za uzalishaji (*high economic potential*) nje ya korido za usafirishaji za kawaida na kwa kuwa ukiangalia ukurasa wa 122, Mkoa wa Mwanza una eneo kubwa la uzalishaji ambalo halikuhusishwa katika Mpango huu, basi napendekeza na kuitaka Serikali katika jedwali katika ukurasa wa 125 iongeze barabara ya Sengerema – Nyamazugo – Bukokwa – Nyehunge – Nzera – Geita na kuanzia Nyehunge hadi Kahunda kuititia msitu wa Buhindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mwanza kwa ujumla hutegemea sana mazao ya chakula na samaki kutoka maeneo ambayo yanapitwa na barabara hiyo. Naomba kuwasilisha.

MHE. SALOME D. MWAMBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais kwa Mpango mzuri aliotuandalia. Pia, nawapongeza wote walioshiriki katika kutengeneza Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwa upande wa ujenzi wa barabara na miundombinu. Naomba suala la barabara lizingatiwe kwa kufungua hata sehemu za ndani ya nchi ziunganishwe na nchi jirani. Barabara nyingi za kuunga na nchi jirani nyingi ni zile zinazotoka Mikoa ya jirani kama zilizoanza wakati wa ukoloni. Mfano, barabara ya Dar es Salaam – Mwanza, Dar es Salaam – Arusha na kadhalika. Mikoa ya Singida - Shinyanga haina barabara zinazokwenda nchi jirani, mfano Kenya. Hivyo basi, naomba Mpango uhakikishe barabara zinazoanzishwa kupata katika Mikoa ambayo haijapitiwa mfano hii barabara inayojengwa toka (i) Shinyanga – Meatu – daraja la Sibiti – Ibuga – Gumanga – Nduguti – Iguguno. (ii) Kuna barabara inayoanzia Mara – Lamadi – Bariadi – Meatu – Mbulu – Babati – Arusha – Nairobi (Kenya).

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii haijapita jimbo la Iramba Mashariki ambako ndiko mazao ya alizeti na vitunguu vinalimwa kwa wingi. Naomba barabara hii ipitie hata katika baadhi ya Kata kama Ibuga, Mwangeza. Kwa kifupi barabara hii ipitie Mara – Lamadi- Bariadi – Meatu – Ibaga – Mwangeza – Mbulu – Babati – Arusha – Nairobi. Barabara hii itawasaidia sana wananchi wa Iramba Mashariki badala ya kusafirisha mazao hadi Mbulu ili waunganishe kwenda Arusha hadi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana eneo la Iramba Mashariki liunganishwe na barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni huu, sehemu ambazo ziko ndani, Mpango uziingize kwenye utaratibu wa kuunganishwa na barabara kuu moja kwa moja. Kwani unaweza kukuta ni kilomita chache tu za kuunganishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. PHILIPA G. MTURANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata wasaa huu kuweza kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kuzungumzia suala la uchumi, ningombala yale yaliyopewa kipaumbele yafanyike kwa kuwa kimaandishi Mpango ni mzuri, bali tatizo limekuwa ni utekelezaji. Serikali isimamie Watendaji wake katika sekta mbalimbali za uzalishaji na pale itakapobainika kuwa kuna ubadhirusi wa mali ya umma, basi viongozi waliohusika na hujuma hiyo wachukuliwe hatua mara moja. Tumeona viwanda vingi vimefilisika na hivyo kusababisha uchumi wetu kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mujibu wa hoja hii, sehemu kubwa ya pesa ya kuendeshea shughuli mbalimbali zitategemea misaada na mikopo kutoka wa wafadhili. Kwa maoni yangu, hii haipendezi, inashusha hadhi ya nchi yetu, kwani tungeweza kuboresha vyanzo vyetu vyaa kiuchumi/mapato kama vile madini, mbuga za wanyama, bahari na vinginevyo tukisimamia vyema raslimali zetu tungeweza kupunguza utegemezei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika huduma za jamii, pamoja na mafanikio yaliyoelezewa kupatikana, ningombala juhudhi zaidi ziongezwe ili wananchi hata wale walioko pembezoni waweze kufikiwa na huduma hizo, mfano umeme, maji, zahanati na hata shule, bali hata wauguzi na walimu sambamba na upatikanaji wa vifaa vyaa kufanya kazi. Ni imani yangu kama itafanyika hivyo, baadhi ya matatizo yatapungua kama sio kwisha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nishati ya umeme, umeme usambazwe kote tena kwa bei nafuu ili wananchi waweze kuutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema ya kutengeneza ajira ili vijana waweze kuajirika ingelikuwa ni busara pia kuandaa mazingira ya kukopesheka nyenzo au

fedha (mtaji) ili vijana hawa waweze kujajiri zaidi kuliko kuajiriwa Serikalini. Hii ni kwa kuwa ajira Serikalini ni ndogo. Serikali idhibiti riba zinazotolewa na mabenki yetu ili hata wanawake waweze kukopeshwa ikiwemo ulegezwaji wa masharti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu yetu iboreshwe hususan reli, barabara na bandari ili huduma zinazotolewa ziwe bora zaidi kiasi cha kuvutia wawekezaji wengi na hata wale wanaopitisha mizigo yao katika bandari zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwajibikaji ndiyo msingi wa mafanikio wa yote haya niliyoyazungumzia. Serikali isimwonee haya kiongozi au mtu ye yeyote atakayelisababishia hasara Taifa hili. Inawezekana, kama kila mtu atatimiza wajibu wake kikamilifu. Naomba kuwasilisha.

MHE. HAMAD ALI HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu ndani ya kitabu unaposomwa ni mzuri tu, lakini tatizo litatupata katika utekelezaji, kwasababu maeneo mengi yalioguswa katika huu Mpango yanahitaji fedha. Kwa ujumla, unaona kabisa kwamba Mpango huu umetangazwa wakati bajeti imeshasomwa na kwamba unaonekana Idara ya Mipango na Katibu mpango kama hakuwa na mawasiliano na Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu umewazungumzia vijana, lakini katika vipindi vilivyopita pia wahisani au mashirika walitoa misaada aidha, mikopo kwa maendeleo ya vijana na fedha zilipitia Wilayani na kwamba fedha zinarejeshwa zilikotoka ati kwa kisingizio kuwa zimepitiwa na muda na hazikutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kwamba Wabunge, Serikali na kila mmoja wetu anazungumzia tatizo la ajira kwa vijana na tunajiona kama Taifa tuna mzigo wa vijana wasio na kazi, lakini misaada inayofikishwa Wilayani inafanywa siri kabisa kiasi kwamba viongozi wachache wa Wilayani amba wanaelewa na ajabu hata Wabunge wenye majukumu ya kusaidia jamii hawaelewi na hatimaye fedha zinarejeshwa zilikotoka kwa lugha kwamba zimekosa vijana wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ukatili wa viongozi kwa vijana na hii ni kuonesha namna ambavyo baadhi ya viongozi hawako tayari kuona Taifa linajikwamua kiuchumi na kimaendeleo ambo hili linaonesha wazi kwamba usimamizi ni mbovu na kwa mwenendo kama huu pia bado Mpango huu wa maendeleo wa Taifa hautaweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kwamba, kama ni misaada au ni mikopo, miradi itakapoletwa Wilayani basi ni vyema mambo kama haya ya maendeleo yakasimamiwa na Wabunge. Aidha, ni vyema Wabunge nao wakawa wanaelewa kwani nao ndio wenye majukumu kwa wananchi huko majimboni na Wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatia aibu kwamba kila mwaka nchi inazalisha vijana zaidi ya 500,000 wasio na kazi amba wanamaliza masomo yao ya Darasa la Saba na

Kumi na kwamba fursa kama hizo za kuwawezesha na kuwaendeleza vijana zinarejeshwa baada ya muda kwa kukosa vijana wa kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu, tusipokuwa na mkakati wa kuwajibishana kwa watakaokuwa na dhamana ya kusimamia, basi hatutafikia lengo la Mpango huu na tutakutana tena hapa kuja kuzungumzia kufeli kwa Mpango huu na sio mafanikio yaliyopatikana. Hivyo basi, ambaye atakuwa na jukumu la kusimamia na asipofikia lengo awajibike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba kuwasilisha.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Taifa (2011/12 – 2015/16) kama Mpango wa kimaandishi hamna tatizo, lakini una mapungufu mengi pamoja na hofu nyingi katika utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mionganoni mwa changamoto zinazoukabili Mpango huu ni pamoja na:-

(1) Mpango kutegemea zaidi fedha za wahisani ikiwemo mikopo pamoja na misaada, ambayo uhakika wake wa kupatikana ni mdogo. Hivyo basi, fedha hizo zikikosekana, basi mpango wetu hautafanikiwa.

(2) Nadharia ya mwendelezo wa kutokufanikiwa kwa mikakati iliyopita kama vile MKUKUTA, MKURABITA, MKUMBITA na kadhalika. Hivyo basi, kwa kutokuelezwa kwa sababu za kushindwa kwa mikakati iliyopita kutapelekea pia mkakati huu kutokufanikiwa kama ulivyopangwa.

(3) Muda wa utekelezaji mipango ni mdogo na umekaa kinadharia zaidi kuliko kihalisa. Maana ni vigumu sana kufikisha maji safi na salama kwa asilimia 95, maeneo ya mjini katika kipindi cha muda wa kati, wakati tumeshindwa kufanya hivyo kwa miaka 50, tangu tupate uhuru.

(4) Tatizo katika uwajibikaji wa wakati na urasimu ambaو umekwamisha mipango/mikakati mingi iliyopita. Hivyo, Watanzania waelezwe endapo Mpango huu utashindwa, Serikali itawajibikaje? Waziri husika atawajibikaje na Sekretarieti yote inayotekeliza mpango?

(5) Hofu ya mtikisiko wa uchumi ambaو umekuwa ukitumika kama kigezo cha kushindwa, hii inamaanisha kuwa endapo mtikisiko wa uchumi utatokea wakati wowote kuanzia sasa, basi mkakati huu hautafanikiwa.

(6) Kuporomoka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania kunakotokea mara kwa mara, kutapelekea mambo mengi yaliyopangwa kushindwa kufanya kwa wakati.

(7) Mkakati /mpango haukushirikisha wadau wa chini kabisa ili kutambua mahitaji yao halisi na ambayo yanapewa kipaumbele, kuliko kutumia wataalam ambao nao wana mitazamo na maono yao kiundani kama binadamu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nashauri Serikali iangalie mapungufu yote yaliyojitekeza katika awamu zote za mipango/mikakati ya maendelo tangu kupata uhuru mwaka 1961, iyafanyie kazi na kuwaeleza Watanzania ni namna gani sasa wataweza kukabili ana nayo ili wananchi wafaidikie na raslimali za Taifa na hivyo kuondokana na ugumu wa maisha. Naomba kuwasilisha.

MHE. IGNAS ALOYCE MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naipongeza Serikali katika kuwa na wazo la kuwa na Mpango huu. Nawapongeza wote waliyoshiriki kutoa mawazo katika kuandaa Mpango huu ambao ni dira ya kuleta ukombozi katika kuleta unafuu wa maisha kwa Mtanzania. Mpango huu ni mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia Mpango huu, naomba nianze na kilimo. Kilimo ndio uti wa mgongo katika Taifa letu kwa sababu asilimia 75 ya Watanzania wanategemea kilimo. Hivyo, ni wakati muafaka kwa sasa kuondoa dosari mbalimbali zinazofanya kilimo kushindwa kwa uhalisia wa kuwakomboa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, Serikali itambue zipo tabaka katika suala hili la kilimo.

Kwanza wapo wakulima wakubwa; pili, wapo wakulima wa kati; tatu, wapo wakulima wadogo na nne, lipo kundi ambalo halijihuishi na shughuli ya kilimo wala Mpango wa shughuli yoyote (wazururaji).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Serikali ikishayatambua makundi haya, ni rahisi katika kujua inawasaidiaje ili kila kundi liwe na namna ya kutambuliwa matatizo au changamoto zipi, ni kikwazo gani walichonacho na baadaye kukitafutia ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikwazo kikubwa ni ukosefu wa mtaji na kutokuwa na sifa za kuweza kukopa fedha au zana za kilimo kwa sababu hawana kitu kingine cha kusimama kama dhamana zaidi ya ardhi au nyumba na hasa maeneo ya vijijini. Hivyo, Serikali iharakishe Mmpango wake wa kurasimisha ardhi na nyumba walizonazo vijijini ili waweze kuwa na hati za kumiliki mashamba au nyumba ili Taasisi za Fedha ziweze kuwakopesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri pia kwamba Serikali ihakikishe wasio na ardhi wanapatiwa ardhi ya kulima; Serikali ihakikishe wakulima wanapata soko la kuuza mazao yao kwa bei nzuri; wawekezaji kutochukua ardhi yote kabla wananchi hawaajitosheleza; Serikali iwe na dhamana ya makusudi ya utatuzi wa migogoro hiyo ili kuleta amani, usalama na utulivu katika nchi yetu; Mabaraza ya Ardhi na Nyumba yawepo kila Wilaya badala ya kuwa Makao Makuu ya Mkoa ili yawe karibu na

wakulima. Hii itasaidia sana utatuzi wa kisheria juu ya migogoro mingi iliyopo inayohusiana na mashamba; Kilimo cha kibiashara kinaweza kuwa kilimo kinachowenza kuleta tija kubwa ya uchumi kwa mkulima, pia na uchumi wa Taifa letu na kwa namna hiyo umasikini utapungua kwa kasi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata siku moja kilimo kwa ajili ya hifadhi ya chakula hakiwezi katuondolea umasikini. Mfano mzuri, Mkoa wa Rukwa umejaliwa kuwa na ardhi nzuri, hali ya mvua za kutosha karibu takribani miaka kumi umekuwa ukiongoza kwa ununuzi wa mahindi kupitia Shirika la SGR. Lakini wananchi hao hao wanaozalisha bado ni masikini kwa sababu ya bei ndogo wanayouzia mazao yao kwa ajili ya hifadhi ya chakula. Wanaofaidika ni walangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapaswa kuhakikisha barabara za kutoka vijijini (mashambani) zinapitika wakati wote ili mkulima aweze kusafirisha mazao yake kwa gharama ndogo ya kumwezesha kupata faida. Aidha, wavuvi wadogo watambulike na Serikali ili wawezeshwe kupata zana za uvuvi pia Serikali kuwatafutia masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwe na mpango wa kuwawezesha Wakulima kuwa na bima ili kujikinga na majanga yanayoweza kutokea, kama vile ukame na mafuriko, vitu ambavyo vikitokea, humfanya mkulima kurudisha uchumi wake nyuma na mara nyingine kukata tamaa kabisa.

Pia, Serikali ianzishe kilimo cha mkataba wa kumpatia mkulima pembejeo za kilimo kwa mkataba ikiwa ni pamoja na kuhakikisha inanunua mazao kwa bei ya makubaliano ya mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Serikali iimarishe kitengo cha Takwimu hadi vijijini ili kuwa na takwimu sahihi na za wakati ili Serikali inapopanga mipango yake, iwe na ufahamu mzuri wa kujua takwimu kwa uhakika. Hivyo, itakuwa ni rahisi kwa Serikali kujipanga kutohana na takwimu sahihi. Naunga mkono mpango huu.

MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na kuniwezesha kuchangia hoja katika Mpango huu wa kitaifa wa maendeleo. Pia napenda kukushukuru wewe kwa kuliongoza Bunge hili la Kumi kwa upeo na uadilifu. Mwenyezi Mungu akusaidie zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuipongeza Kamati ya mipango chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Khalfan Kikwete na Katibu wake Dr. Phillip Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi iliyofanywa katika kutayarisha Mpango huu ni kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Mpango huu ni wa kitaifa, hatuna budi sote kuufanya kuwa wa kitaifa. Wasitokee wasiokuwa na nia nzuri, aidha, kwa ubinafsi wao au kwa utashi wao tu wakaugeuza Mpango huu mzuri kuwa ni wa chama fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi ya Taifa ni jambo la kwanza na la umuhimu wa pekee kabisa. Dira hii ya mpango wa maendeleo itazidi kutujenga katika uitaifa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango huu wa miaka mitano ni vya muhimu sana kwa maendeleo ya haraka ya kukuza uchumi wa nchi yetu na kupunguza umaskini wa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari, reli, usafiri wa anga, elimu, kilimo, uvuvi, ufugaji, nishati na Viwanda ni mambo ya kupewa umuhimu wa kipekee na usimamizi mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina wasiiasi na upangwaji wa vipaumbele vya Mpango huu, lakini nina wasiiasi na utekelezwaji wake, hasa katika suala zima la usimamizi na uwajibikaji (*Supervision and Accountability*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wasiiasi huo kutokana na uzoefu ulivyo wa mambo yanavyoendeshwa katika Idara zetu na Taasisi za Umma, kuangalia maslahi binafsi badala ya maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Mpango huu ulete matunda tunayotarajia, hatuna budi kuungana kama watu wa Taifa moja bila kujali itikadi binafsi au za vyama vyetu. Tuungane kuweka sheria, kanuni na taratibu za kumwajibisha yeoyote ambaye atafanya uzembe, ubadhirifu au ujisadi ili kuuharibu utekelezaji wa Mpango huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Mungu ibariki Tanzania na watu wake. Amin.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima nawasilisha mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu una mwelekeo mzuri, lakini jambo kubwa na la kusikitisha, Serikali haijaeleza kinaga ubaga mgawanyo wa madaraka na mamlaka ya Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha na Uchumi. Mwenyekiti wa Tume ya Mipango, kwa kawaida Tume ya Mipango husimamia mkakati wa maendeleo ya Taifa na Bajeti ya Maendeleo, kutokana na hali hii, Tume ya Mipango ina mamlaka gani? Mpaka sasa Tume ya mipango haina meno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu kimantiki unatakiwa ufuatwe na bajeti, lakini inaonekana Mpango ndio unafuata bajeti. Nasema hivi, ili kusimamia sera za uchumi mpana, Serikali lazima itekeleze Mpango wa Uchumi (*PSI*) *Policy Support Instrument* ambayo imekubaliana na *IMF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu pamoja na mambo mengine, una malengo yanayopimika ikiwa ni pamoja na fedha ambayo Serikali itakopa kutoka mabenki. Hii ni kusema, Mpango huu unaburuzwa na Shirika la *IMF*. Pia bajeti inakuwa makini katika matumizi kuona kwamba inafuata Shirika la *IMF*. Kutokana na hali hii, Mpango hauonyeshi dira kwa utekelezaji hasa katika Wizara ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala muhimu ni kwamba, mipango ya Tanzania kimaelezo ni mizuri, lakini tatizo kubwa ni la utekelezaji. Kama kutakuwa na usimamizi na utekelezaji, basi hatua za maendeleo zitakuwa zinapanda. La msingi, lazima kuundwe Tume ya Bunge ya kuratibu na kufuatilia mipango hii ambayo tutaipitisha punde. Kinyume na hivi, basi Serikali haitofikia hata kidogo malengo iliyojipangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kwamba Tume ya Bunge iundwe kusimamia Mpango huu. Naomba kuwasilisha.

MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli Mpango huu utatekelezwa, Tanzania itakuwa ni nchi nzuri kwa maendeleo ya wananchi wake. Mpango umejikita katika nyanja mbalimbali ambazo ni chimbuko la maendeleo ya Taifa. Kwa kuzingatia hayo, ni vyema nikajikita katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni msingi wa maendeleo, lakini ikiwa tutaangalia sana wasomi waliopo vyuoni hivi sasa na kuwaacha wale ambao wamemaliza Chuo na kuwepo mitaani, mpango huu utakuwa umeshaweka matabaka. Ni vyema Mpango ukawahudumia waliokwishamaliza Chuo hivi sasa ili kuonekana kwamba Serikali ipo makini na Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili elimu itolewe vizuri kama malengo yalivyosemwa, kwanza, ni kuangalia kama walimu watakaofundisha vyuoni wapo na wakutosha. Walimu 133,000 watakaochukua Diploma, kila mwaka watafundishwa wangapi ili kukidhi mahitaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katka maeneo ya Elimu ya Sekondari na Msingi itabidi yashughulikiwe kwa kuangalia mitaala yao ambayo itahitaji kujikita zaidi katika elimu ya awali kuliko hii tuliyonayo sasa ya kupasi mitihani tu, lakini haimfunzi mtu kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni afya. Mpango haujajikita sana katika afya, lakini ina umuhimu wake. Malengo ya afya ni mazuri, lakini ni vyema likaangaliwa suala zima la utapiamlo. Tanzania ni nchi ya tatu iliyoathirika vibaya na utapiamlo Barani Afrika na nchi ya kumi duniani. Utapiamlo ni mionganini mwa changamoto kubwa inayoikabili Tanzania. Utapiamlo unadhoofisha uchumi. Kutokana na utapiamlo, wakulima hushindwa kutumia nguvu nyingi, hivyo kupelekea mavuno kidogo na kupungua kwa tija ya wafanyakazi.

Pia utapiamlo hupoteza upotevu wa fursa za kiuchumi. Uwekezaji mkubwa nchini Tanzania kwenye Elimu ya Msingi na Sekondari unazaa matokeo duni, kwa sababu

watoto hawapati lishe ya msingi. Utapiamlo huchangia 56% ya vifo vya utotoni Tanzania na ukosefu wa akili kwa 13%. Ni vyema Mpango huu ukaangalia tena suala hili ili tupate nguvu kazi nzuri na iliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwa na Mpango mzuri, moja ni kuangalia nguvukazi ambayo asilimia kubwa ni vijana na wengi wao hawana kazi za uhakika angalau za kupata mkate wao kwa siku. Ni vyema Serikali ikawa na mkakati madhubuti mbali ya kuwapa vyombo vingine vya umma dhamana hii. Ingawa kuna Wizara ya kazi na moja kati ya shughuli zake ni kutoa maelekezo, lakini ni wangapi wanaojua na wanaokwenda? Ni vyema wizara ikawa na Mpango mzuri wa kutoa elimu kwa njia ya vyombo vya habari kama redio, TV na magazeti au kufanya midahalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa kifedha kwa vijana: Je, kuna tathmini yoyote iliyofanywa katika fedha za mabilioni ya J.K? Wangapi wamefaidika nazo na kuzirejesha? Miradi mingapi imefanyika na kuleta tija? Hata hivyo kunaweza kuwa na mawakala (*Agents*) ambao watakuwa na ushirikiano na sehemu/mashirika yenyewe kazi za aina mbalimbali ili vijana wanapotafuta kazi waende hapo na kupatiwa. Shughuli hii hufanywa na nchi nyingi zilizoendelea. Mawakala hawa hupata asilimia fulani kwa kupeleka wafanyakazi.

Mpango usitegemee sana katika fedha za misaada. Tukiangalia ,bajeti ya mwaka uliopita, miradi mingi haikufanyika ipasavyo kwa kusubiri fedha za wafadhili, na walipowasilisha wakati umesalia mdogo na fedha hurejeshwa. Serikali itafute njia mbadala ili iwe na uhakika wa fedha zake yenyewe. Tuna raslimali nyingi katika nchi, tuzitumie, huu ni wakati wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango siyo matumizi, lakini ni vyema Serikali ikavitaja vyanzo hivyo vya fedha kwa ajili ya utekelezaji. Hii itasaidia maeneo yote ambayo yatafanya shughuli hii ya utekelezaji kuwa nyepesi, kwani kila sehemu itakuwa na wajibu wa kupania kuzitafuta fedha hizo kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Mpango huu ungeweka “*Time Action Plan*” ambao ungeonesha mpangilio wote, dhamana ya kila mhusika mmoja, fedha itakayotumika kwa kila tukio na muda utakaochukua. Hii itaweza kumbana mhusika na kutoa taarifa ikiwa jambo halijatekelezwa. Pia kuwe na uwezekano wa kufanya tathmini ama kila baada ya miezi mitatu au sita kwa mwaka, badala ya kukaa mpaka mwisho wa shughuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mbunge. Haya Katibu.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema tumemaliza kujadili, tukikaa kama Kamati ya Mipango, kwa hiyo sasa tunarejea kwenye kiti kama Bunge na namwomba Mheshimiwa Mtoa Hoja aanze kutoa ufanuzi wa kiujumla halafu baadaye atoe majumuisho. (*Makofii*)

(*Bunge lilirudia*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):

Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa hii tena ili niweze kutoa maelezo katika baadhi ya maeneo kwa kujibu hoja. Maana yake kwa kweli hoja zilizopokelewa hapa zimewahusisha zaidi ya Wabunge 130 yaani ni zaidi ya nusu, karibu zaidi ya nusu ya Bunge Zima. Kwa hiyo, uwezekano wa hoja zenu zote Waheshimiwa Wabunge zipo kwenye hili bunda la karatasi. Sasa uwezekano wa kujibu hoja zote mpaka Bunge hili litaahirishwa tuendelee kesho maana ni nyingi. Kwa hiyo, ninachotaka kuiwaahidi ni kwamba zile ambazo zitazijibu, tutazijibu kwa maandishi kwa kila mmoja ambaye ameitoa ili abaki na *reference*. Kwa sababu ni nyingi sana na hatuwezi kuzijibu zote. Lakini nitajitahidi kwa kadri ninavyoweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, rasimu ya mpango huu Bungeni inaonekana imewagusa Waheshimiwa Wabunge wengi, ndio maana wengi sana wamesema, lakini sisi tuliowasilisha hoja hii tunafurahia sana jinsi Wabunge walivyochangamkia hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunafurahia kwa sababu tulisema katika maelezo yetu kwamba huu ni mpango wa Taifa. Bunge hili linawakilisha wananchi wa Taifa letu. Kwa hiyo, kutoa mawazo mengi yanayosaidia kuboresha mpango huu ni afya nzuri tu kwa kazi ya Bunge hili. Kabla sijatoa maelezo ningependa nitambue wale ambao wamesema au kwa hoja hapa hapa Bungeni au wameandika. Yule ambaye sitamtaja, anaweza akaniandikia akanikumbusha kuwa sikumtaja maana ni wengi hapa.

Sasa kwanza napenda kutambua jina la Mheshimiwa Dkt. Omar Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, Mbunge wa Karatu anawakilisha Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Dokta Binilith Mahenge, Mbunge wa Makete, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mbunge wa Kisesa, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa David Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini, Mheshimiwa Charles Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mbunge wa Rombo, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, Mheshimiwa David Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Agripina Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijijini. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge wengine ni Mheshimiwa Alphaxard Lugola, Mbunge wa Mwibara, Mheshimiwa Augustino Mrema, Mbunge wa Vunjo, Mheshimiwa Mwigulu Madelu, Mbunge wa Iramba Magharibi, Mheshimiwa Pauline Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mbunge wa Mbulu, Mheshimiwa Ramo Makani, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, Mheshimiwa Regia Mtema, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa January Makamba, Mbunge wa Bumbuli, Mheshimiwa Christina Mughwai, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa

Assumpter Mshana, Mbunge wa Nkenge, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Salum Barwany, Mbunge wa Lindi Mjini, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini, Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh, Mbunge wa Magomeni, Mheshimiwa Dokta Mgimwa na Mheshimiwa Henry Shekifu. Hawa wamechangia kwa kuzungumza. Nawashukuru sana kwa mchango wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa vile vile nitambue wale ambao wameandika ili watambue kwamba rekodi zao tunazo ambao ni Mheshimiwa Angella Kairuki, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa John Mnyika, Mbunge wa Ubungo, Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa *Engineer* Christopher Chiza, Mbunge wa Buyungu, Mheshimiwa Celina Kombani, Mbunge wa Ulanga Mashariki, Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Charles Kitwanga, Mbunge wa Misungwi na Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mbunge wa Viti Maalum. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge wengine ni Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Antony Mbassa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, Mheshimiwa Zaynabu Vullu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mbunge wa Mtambile, Mheshimiwa Vincent Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mbunge wa Sumve, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, Mbunge wa Dole, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mbunge wa Kiteto, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Andrew Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi, Mheshimiwa Saleh Pamba, Mbunge wa Pangani, Mheshimiwa Michael Laizer, Mbunge wa Longido, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mbunge wa Kalambo, Mheshimiwa Albert Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Henry Shekifu, Mbunge wa Lushoto aliandika na amesema.

Wengine ni Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mbunge wa Ole, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Philipa Mturano, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mbunge wa Magogoni, Mheshimiwa David Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, aliandika tena.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Ignas Malocha, Mbunge wa Kwela, Mheshimiwa Haroub Muhammed Shams, Mbunge wa Chonga, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mbunge wa Simanjiro, Mheshimiwa Margaret Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mahamoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, Mbunge wa Arumeru Magharibi, Mheshimiwa

Mansoor Sharif Hiran, Mbunge wa Kwimba na Mheshimiwa Mbarouk Salum Ali, Mbunge wa Wete. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Deogratias Ntukamazima, Mbunge wa Ngara, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Mgogoni, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh, Viti Magomeni. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, *sorry*, wameandika viti halafu Magomeni, usahihi ni Mbunge wa Magomeni. Asije akabadilika kuwa Viti Maalum. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge wa Busanda; Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijiji; Mheshimiwa Dokta Maua Abeid Daftari, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Juma Hamisi, Mbunge wa Kondoa Kusini, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, Mheshimiwa Felister Bura, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Agness Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mbunge wa Kisesa, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyangh'wale, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mbunge wa Kirasawe, Mheshimiwa Profesa Kulikoyola Kahigi, Mbunge wa Bukombe, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mbunge wa Mfenesini, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mbunge wa Ziwani, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa James Lembeli, Mbunge wa Kahama, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mbunge wa Kojani, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, Mheshimiwa Naomi Kaihula, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Esther Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijiji na Mheshimiwa Abdallah Haji Ali, Mbunge wa Kiwani. (*Makofi*)

Wabunge wengine ni Mheshimiwa *Engineer* Ramo Makani, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, Mheshimiwa Aliko Kibona, Mbunge wa Ileje, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mbunge wa Kilolo, Mheshimiwa Augustino Masele, Mbunge wa Mbogwe, Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga, Mheshimiwa Freeman Mbewe, Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mheshimiwa Dokta Fenella Mukangara, Naibu Waziri na Mheshimiwa John Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hao ndiyo Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi. Halafu kuna Mheshimiwa Salome Mwambu, Mbunge wa Iramba Mashariki, kuna Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, kuna Mheshimiwa Salome D. Mwambu, nimeshamsoma. Mheshimiwa Jitu Vrajai Soni, Mbunge Jimbo la Babati, kama nimemsahau mtu ataniwia radhi. Lakini nia ni njema kabisa. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Juma Nkamia umemsahau.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, pamoja na Mheshimiwa Juma Nkamia. Kama nilivyoeleza hapo awali natarajia kuwa michango mizuri iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wote nitialeza kwa muhtasari majibu ya hoja mbalimbali zilizotolewa. Hata hivyo kutokana na muda naona nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba sitawezza kujibu kila ambacho kimesemwa, kwa saababu muda hautoshi. (*Makofi*)

Naomba sasa nianze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kuanza na Kamati ya Fedha na Uchumi, nizungumze mambo ya jumla ambayo yamesemwa. Moja kubwa ambalo limesemwa sana hapa ni suala la kukua kwa uchumi, lakini bila kupunguza umaskini. Nalichagua hili kwa sababu nia ya mpango huu ni kukuza uchumi na kupunguza umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukubali ya kwamba kukua kwa uchumi ingawa kunategemeana na kupunguza umaskini lazima hatua zichukuliwe za kuhakikisha ya kwamnba kule ambako kuna sekta inayoajiri maskini wengi, tuipe kipaumbele kwa sababu bila kufanya hivyo ni vigumu sana kupunguza umaskini. Unaweza ukakuza uchumi, lakini uchumi ukawa hauwezeshi umaskini kupungua. Kwa mfano, nitatoa maelezo tu, sasa hivi katika hali ilivyo sasa, mawasiliano yanachangia asilimia 20 ya *GDP*, fedha yaani sekta ya fedha inachangia asilimia 10, ujenzi unachangia asilimia 9.5, biashara inachangia asilimia 9 na sekta ya kilimo inachangia asilimia 4.2.

Lakini sekta ya kilimo inayochangia asilimia 4.2 inaaajiri asilimia 75 ya Watanzania. Hizi zinazochangia kwa kiwango kikubwa sana ajira ya watu wake ni wachache sana. Kwa hiyo, hizi zinaweza zika-*drive* ukuaji wa uchumi, lakini hazitoi ajira na hazipunguzi umaskini, hii ndiyo hali halisi ilivyo. Kwa hiyo, kwa mipango ambayo tumekuwanayo ambayo imewezesha uchumi wa nchi kukua kwa asilimia saba katika kipindi cha miaka kumi, uwekezaji katika sekta ya kilimo inayaoajiri asilimia 75 ya watu wa nchi hii haikutosheleza kuiwezesha sekta hii iweze kupunguza umaskini na hasa ukizingatia kwamba tarakimu hizi za kukua kwa uchumi vile vile zinategemeana na kukua kwa idadi ya watu.

Kwa mfano, ikiwa Watanzania sasa ongezeko la watu ni asilimia 2.9 kwa mwaka na kama sekta ya kilimo inaongezeka au inakua kwa asilimia nne kwa mwaka, ukiondoa asilimia 2.9 ambayo ndiyo ongezeko la watu, utaona kwamba kwa kweli ukuaji halisi wa kilimo ni asilimia 1.2 au 1.5. Hiki ni kiwango kidogo sana cha kupunguza umaskini. Kwa hiyo, tunachosema katika mpango huu ni kwamba lazima sasa tuwekeze zaidi katika sekta ya Kilimo. Nataka kukumbuka habari ambayo aliisema, alinikumbusha ndugu

Luhaga Mpina akasema katika zile Benki mbili, moja inaitwa *TIB* na nyingine ambayo itaundwa karibuni inaitwa *Tanzania Agricultural Bank* lazima tuna-channel resources za kutosha ili mikopo inayokwenda kwa wakulima iweze kusaidia kukuza kilimo zaidi ifike kwenye lengo la asilimia sita au zaidi. Tukiweza kufanya hivyo tunaweza kushusha kiwango cha umaskini. Tumekubaliana na hoja ya Ndugu Mpina na katika mpango utakaokuwa *the final budget* utakuta katika kila mwaka tutakuwa tunachangia *TIB* kwa shilingi bilioni 100 kwa mwaka na katika Benki ya Kilimo tutachangia kiwango hicho hicho kwa sababu tunataka kupitia *SACCOS* za wakulima, wakulima waweze kukopa, hakuna namna tunaweza kuwakopesha wakulima. Kama tunaogopa kuwakopesha wakulima ni tunaogopa kupunguza umaskini. Kwa hiyo, ni lazima tukubali kuchukua hatua ili wakulima waweze kukopeshwa kupitia benki hizo na bado Serikali iendelee na wajibu wake, wajibu wa kusimamia yale mambo ambayo ni *investiment* katika kilimo, ambayo ni pamoja na kupeleka pembejeo na kuhakikisha zinafika, ambayo ni pamoja na kupeleka *extension services* ya wataalam ili ile mikopo ikiungana pamoja na utaalamu, utaalamu uongezeka katika kilimo, uzalishaji utaongezeka na ukiongezeka *graph* itaonesha kwamba uzalishaji ukienda juu, umaskini unashuka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hakuna dawa rahisi, lakini tunakubaliana, timesikiliza mashauri ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge, tunayazingatia na ndio maana tunataka kufanya mabadiliko hata katika zile *figures* ili kuhakikisha kwamba kweli wakulima watapewa rasilimali ambayo itaweza kusaidia kubadilisha kilimo chetu. Lakini vilevile kilimo hiki kinaweza kikakua zaidi kama tutaingiza wawekezaji na kitu kimoja ambacho kinatisha kidogo, ukizungumza wawekezaji Tanzania hapa, watu wanafikiria wazungu; lakini sisi tunasema wawekezaji hata hapa Tanzania wapo!

Mheshimiwa Spika, wapo watu wana mitaji, waiingize basi mitaji yao katika kilimo. Kwa sababu, kwa kufanya hivyo na kwa kushirikisha wakulima wadogo wanaozunguka eneo linalolimwa na mkulima mkubwa na kufanya mfumo kama ule wa Kilombero wa *contract family*; ukienda Kilombero leo, huwezi kuona umaskini unaozunguka Kiwanda cha Sukari, kwa sababu wakulima wa nje wanapata soko la moja kwa moja kwenye Kiwanda cha Sukari na vilevile wanapata huduma na wanakopesheka. Kwa hiyo, hali ya wakulima wa Kilombero pale ni nzuri na sasa hivi Kiwanda cha Sukari kile cha Kagera na chenyewe kimeanza mfumo ule, pamoja na kile kingine cha Morogoro cha Mtibwa, ingawa pale kulikuwa na matatizo mengi kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haya ndio mambo ambayo kwa kweli inabidi tuyazingatie vizuri katika mpango huu ili tuweze kujibu hoja ambayo inasema ni kwa nini uchumi unakuwa lakini umaskini au unabaki pale pale au unaendelea kukua na wenyewe! Ni lazima tu-*address* hii *problem* kwa sababu mpango huu mafanikio yake ni kukua kwa uchumi lakini mafanikio yake makubwa zaidi ni kupunguza umaskini. Lakini ushauri wake tuliuopata kutokana na jambo hili, tunauzingatia.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengine yamesemwa lakini nitayajibu vizuri kidogo na kwa ufupi. Bunge hili tuna vijana na mimi ningependa tuwape fursa tu ya kuendelea kujifunza, maana sisi kwa kweli hatuwezi ku-supress vijana, kazi yetu ni

kuwaongoza na kuwasaidia ili mwisho wa yote wawze kuingia katika mazingira ambayo yatawapa.

Sasa kuna baadhi yao, wala siwalaumu kabisa *actually* napenda niseme haya kwa sababu ningependa wajue na wala siwalaumu kabisa kwa sababu *ku-demand* maendeleo zaidi ni suala la kizazi tu. Nalo unaweza kuwa kama Mrema hivi, anakumbuka mambo ya zamani, lakini hataki kujua mambo ya sasa, lakini watu wa sasa nao wana matatizo yao, nao wana mahitaji yao ambayo inatubidi kuya-*address*. Sasa lakini kwa kuwasaidia vilevile maana wako wachache wamesema mambo hapa, kwanza wanasema mpango huu haukushirikisha watu! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sisi hapa Tanzania tuna vijiji 11,000; kwamba utembee vijiji vyote 11,000 ndio uje upange, utamaliza miaka yote ya mpango hujapanga. Maana hata sisi Waheshimiwa Wabunge ni Wabunge, tumechaguliwa leo ni miezi sita, hatujamaliza vijiji vyote vya Majimbo yetu. Sasa uje utembelee vijiji vyote, ndio uje ukae sasa na Tume upange, hapana! Lakini Tume hii ilitembelea mikoa tisa kwa kutumia kitu kinaitwa *ESRF*, ambao walikuwa ndio wataalamu elekezi wa Tume. Wametembelea Pwani yaani Dar es Salaam kwanza, halafu wametembelea Kigoma, wameenda Singida, wameenda Lindi na walichukua mkoaa mmoja mmoja kutoka katika kila Kanda. Wameenda Morogoro, wameenda Arusha, wameenda Rukwa, wameenda Mara na walikwenda Mwanza. Kwa hiyo, kama ni *sample* ya Tanzania hii ni *representative sample* ya kutosha kukuonesha kwamba matatizo yanayozungumzwa hapa katika mikoa hii yatakuwa yanawakilisha matatizo ya kweli ya wananchi wote wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia mfumo huu na Bunge hili lina wasomi kwa hiyo, wanajua mambo ya *statistics* na namna unavyoweza kufanya *sample* ili iweze kukupa jibu ambalo linawakilisha eneo kubwa zaidi. Kwa hiyo, hivi ndivyo Tume ilivyofanya na imepata habari. Halafu mkitazama vipaumbele, utapata taabu sana kubisha kama vipaumbele hivi kweli haviwahu Watanzania! Miundombinu, hivi wapi Tanzania unaweza kwenda wakakwambia hawataki barabara, wapi? Uende wapi ambako watasema kilimo sio *problem* yao? Utaenda wapi ambako watasema maji hawataki tena? Utaenda wapi ambapo hawatasema elimu bado ni shida kubwa? Umeme na kadhalika. Kwa hiyo, kwa kweli tumezingatia jambo hili na wenzetu wamefanya kazi yao vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna mwenzeti mmoja alisema kwamba unajua watu wakifanya vizuri tena ni watu wenu, ni vizuri vile vile kuwapongeza, maana mnawapa moyo. Sasa hiki kikundi kilichofanya hii kazi ni kikundi cha wataalamu wa Tanzania. Huyu Dokta Mpango huyu anatoka Kasulu; wewe unajua Kasulu hata ukisema hatujafanya lolote, lakini mpaka Kasulu itoe mtaalamu anaitwa Dokta Mpango, ujue kuna mambo yamefanyika Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kazi hiyo imefanyika, lakini kuna jambo lingine nataka kulisema kwa haraka. Kuna vijana wanasema tangu Uhuru hamna kitu! Aah, jamani, watu wazima sisi tumekuwepo miaka 50, iwe hamna kitu kweli? Labda tatizo ni kwamba wale waliopo ndio hawakuwepo wakati wa ukoloni, kwa hiyo, hawajui kilichokuwepo!

Mheshimiwa Spika, eeh, watuulize wenzao tuliuonja. Viwanda vyote ambavyo mnavisikia viko Tanzania, vinavyoendeshwa na vilivyoshindikana kuendeshwa, vyote vimejengwa na Serikali ya Tanzania katika mpango wake mrefu wa mwaka 1964 – 1975. Ningeweza hata nikavitaja, maana viko hapa. Umeme tunaouzungumza humu, *infrastructure* zote za umeme pamoja na mabwawa yale yanayotoa umeme yale ya Mtera, yote yamejengwa na Serikali hii. Wakoloni hawakutuchia umeme, waliacha umeme wa dizeli pale Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam pale mradi mkubwa wa Waingereza ulikuwa ni *Drive-in Cinema*, ndio walioituachia. Tumeuvunja, tumeweka pale Ubalozi wa Marekani. Tanzania ilikuwa ni shamba la Waingereza, tunawalimia pamba wanatengeneza nguo Uingereza; Manchester, wanasema hali ya hewa ya hapa haifai kwa viwanda vya nguo! Tanzania hii tulikuwa tunalima chai inakuwa *processed* Uingereza na Waingereza ni wanywaji wakubwa wa chai na ugomvi wao na Marekani ule wa pale *Masechusets*, unatokana na kunywa chai tu maana waliwalazimisha Wamarekani wanywe chai yao wanayolima kwenye makoloni yao, walipokataa wakawapiga na ukoloni wa pale ukakoma. *Let us face it*, tuache kujikatisha tamaa, tukubali historia yetu! Ndio! Tukatae kujikatisha tamaa bila sababu nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yako mambo mengi tunaweza, hata *University of Dar es Salaam*. Mimi nilikuwa bado mtoto wakati *University of Dar es Salaam* inajengwa kwa kuchanga thumni, thumni ndani ya kikopo. Kinaendeshwa na muandishi wa Rais wa *TANU*, mama mmoja wa Kiingereza. Walitembeza hivi wanaweka senti hamsini, mpaka tukajenga pale Lumumba, halafu baadaye Chuo Kikuu kikahamia Dar es Salaam; kimejengwa, hatukuachiwa Chuo Kikuu Tanzania na Waingereza! Waingereza wametoka hapa wametuachia *graduates* wawili wa *Masters*, mmoja ni Julius Nyerere na mwingine, wote wameshakuwa Marehemu, wawili tu! Mainjia watatu, katika miaka 40 ya utawala wao! Unasema hatujafanya kitu! Aah bwana! Hatutendei haki. Ni vizuri tuambiane hapa bila kulaumiana, lakini tupeane semina kidogo ili tunaposema tuwe tunajua tunachokisema. Hatuwezi kusema tumetosheka, tuna uchu wa maendeleo, tunataka kwenda *speed* zaidi, ndio msingi wa maendeleo haya ya mpango, *we want to speed up*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumze kidogo na niwashukuru sana Kamati ya Fedha na Uchumi, Kamati ile imetupa ushauri mwingi na ile Kamati kwa kweli sisi ni wateja wao, katika muda mfupi sana tumekutana na Kamati ile mara tatu, tumebadilishana na *leader* wa *opposition* ni *member* wa ile Kamati, anajua. Ila kikao kimoja hukuhudhuria lakini vingine ulikuwepo, eeh! Kwa hiyo, kwa kweli yale uliyoyasema wala hatuna mgogoro nayo hata kidogo na nisingependa nitumie muda mrefu sana kuyazungumza kwa sababu tutaendelea kushauriana nao na tutajua ni kitu gani tunaendelea kurekebisha ili kufanikiwa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni la rafiki yangu Mchungaji, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. Na yeze wala sina tatizo nae kubwa, ila kwa kweli nilimtegemea yale mema aseme, halafu mabaya nayo ayaseme; na yeze kasema, akakosoa tu mpaka

akakaa! Aah, lakini Mchungaji na wewe bwana, uwe unasoma maneno haya tunaelewana. (*Makofi/Kicheko*)

Mhweshimiwa Spika, Mchungaji anasema ni kwa nini ile rasimu imetiwa saini na Rais? Hili sio jambo kubwa, Rais ameweka saini ile kwa sababu ile Tume ni ya kwake, ye ye ni sehemu ya Tume. Mimi hapa nakuja kufanya kazi ya Yohana, lakini mwenye Tume ni Rais; hukuona saini yangu mimi mle! Ipo ya mwenye Tume, Rais, ambaye ndiye Mwenyekiti wa Tume na alikuwa anafurahia kazi iliyofanywa na *think tank* ambayo ameiunda mwenyewe, akasaini, akitaka sasa ile kazi itoke kwake iende Bungeni. Na ye ye mwenyewe akaona hiyo haijatosha akaja kueleza, kusaidia kuwaeleza Taifa ili liweze. Na ninamnukuu alisema, “Nimewaiteni siku ya leo kutoa taarifa rasmi kwamba Tume ya Mipango imekamilisha kazi mbili, kupitia Dira ya Maendeleo 2025 na wamekamilisha maandalizi ya Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016). Mpango huo umeshapitishwa na Baraza la Mawziri na kazi yangu siku ya leo ni kuutangaza rasmi kwa Watanzania na hata kwa marafiki zetu duniani. Kama ilivyo ada, mpango huo utafikishwa Bungeni kwa hatua zipasazo.” (*Makofi*)

Kwa hiyo, Rais huyu, alisaini *with conscious* kwamba bado kazi inaendelea. Nadhani hili sio kubwa, hili ni dogo. Nadhani, unajua mambo madogo hayachukui muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lugha ya mpango kwamba imeandikwa Kiingereza! Ni kweli, ule mpango umeandikwa Kiingereza, lakini ni kwa sababu tulijua watu wa Bunge humu mnasema tu Kiingereza na kukisoma, wote tunasoma Kiingereza. Lakini utakapotoka humu umeidhinishwa na sisi tunaojua Kiingereza, unatafsiriwa Kiswahili kwenda kwa wananchi. Kwa hiyo, tumeshawaambia na hili nalo sio tatizo kubwa, tutalifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Israel Natse, alikuwa anaeleza mapendekezo, anazungumza juu ya kupunguza umaskini; wala hatuna *problem*, hiyo ndio shabaha yenye. Anazungumza juu ya kumaliza tatizo la umeme; ndio liko kwenye mpango kabisa. Anazungumzia juu ya Taifa letu kuongeza uzalishaji wa gesi; na sisi tunaendelea na hii kazi kwa sababu, gesi inaonekana iko nyingi na kwa kweli tuna *encourage* makampuni kuja kutusaidia kuchimba hii gesi ili na sisi tuweze kupambana na nchi nyingine zinazozalisha gesi duniani. Hata hatuna ubishi juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, amezungumzia juu ya barabara za vijijini; na sisi tunataka kwa kweli katika mpango huu unapozungumza miundombinu, imegawanyika sehemu tatu. Ipo ile ya *TANROAD*, ipo ya Taifa zima tu ya lami inayounganisha mkoa kwa mkoa ambayo iko humu na maelezo yake, lakini vile vile barabara za vijijini, ni muhimu kwa sababu huwezi kuzungumza juu ya ukuzaji wa kilimo bila kuzungumza barabara za vijijini. Barabara za vijijini ni sehemu ya kilimo. Suala la kukua kwa uchumi na umaskini unabaki; nimeshalizungumzia.

Mheshimiwa Spika, Mchungaji alikuwa amezungumzia juu ya mgawanyo wa rasilimali. Nadhani alikuwa anazungumza juu ya *ratio*, kati ya fedha zinazokwenda

Halmashauri na fedha zinazobaki Serikali Kuu. Kwa kweli jambo hili linategemea tu uzito wa utekelezaji wa vipaumbele. Kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya haiwezi kujenga reli! Reli itajengwa na Serikali. Serikali itajenga bandari, Serikali ndio yene kazi ya kuhakikisha inawekeza umeme. Kwa sababu hiyo *ratio* ni lazima itakuwa tofauti kwa sababu fedha nyingi zaidi zinahitajika katika kuondoa vikwazo hivyo vya reli, vya bandari, vya umeme, lakini fedha nyingine nyingi zaidi zitakazobakia zitakwenda kwenye Halmashauri ili zielekezwe kwenye kilimo, kwenye uvuvi na kwenye ufugaji na vile vile kwenye elimu ambayo ni ya msingi na ya sekondari inatekelezwa katika Halmashauri, lakini elimu ya juu na elimu ya ufundi inasimamiwa na Wizara ya Elimu. Kwa hiyo, mgawanyo utafuata uzito tu wa majukumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Upinzani alikuwa anazzungumzia trilioni 8.2 kwamba ndio fedha inayokusudiwa kutumika katika mpango huu na alikuwa anashangaa, hii itatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, lakini nadhani niseme tu kwamba unajua iko tofauti kubwa kati ya *budget*, *budgeting* na *planning*. Kwenye *budgeting*, Waziri Mkulo, kwanza anakaa anasema tumtoze nani kodi na kwa kiasi gani? Anaanza na *revenue*, halafu akimaliza anasema sasa tugawe mapato kwa maana *revenue* amepata. Sasa anasema kuna *recurrent*, na kadhalika, kwa hiyo, anagawa; *recurrent* kiasi gani, *development*, zinazobaki zinakuwa ni za *development*. Tofauti yake na mpango huu, ni kwamba mpango huu unamwambia Mheshimiwa Mkulo, kusanya kodi kwa sababu kuna mpango yaani unapanga kabla hujajua ni nani unamtoza, halafu unaanza kumtoza sasa ili kutekeleza mpango.

Mheshimiwa Spika, nadhani ninaelewaka hapo yaani kule unakuwa na pesa halafu unafanya *shopping* ya vitu unavyotaka; hapa unakuwa na mpango, halafu unatafuta fedha na mpango unaku-guide katika kutafuta fedha na mpango huu, umeeleza kwamba tutapata wapi fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumesema kwanza kuna kodi ile inaitwa ya kuongeza thamani. Ile kodi bado Waswahili wanaikwepa, mpaka Waheshimiwa wa Hazina pale wameleta mpaka mashine. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, naomba ulekee kwenye *microphone*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):
Mheshimiwa Spika, samahani, imenoga hapo. Wanaweka mashine kwa ajili ya kutaka kuboresha ukusanyaji wa kodi, hilo ni eneo moja. Kuna maeneo mengine ambayo tunadhani itabidi yaye *explored* kujua ni nani analipa kiasi gani.

Kuna mambo ya kukopa kutoka kunakoitwa *seven bonds* ambayo nayo huwezi kuyaogopa kwa sababu unapotaka kujenga bandari ni lazima ujiulize kwanza ni hela ngapi? Utatoza kodi mwaka mmoja ukajenga bandari? Ni vigumu na watu wengine wanasema ooh, Deni la Taifa limekuwa kubwa sana! Kumbe lifanyeje? Jambo la maana

ni kuhakikisha kwamba halivuki kiwango ambacho mmekubaliana. Kwa hiyo, likitaka kuvuka mnalipa, linapungua, mnaendelea. Kukopa utakopa tu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekani wanadaaiwa na China, China imenunua *bonds* za Marekani, na China ikisema *bonds* za Marekani zote zilipwe, Obama na Serikali yake watatafutana maana wamekopa sana kutoka China, sasa kama Marekani wanakopa itakuwa sisi? Hakuna, huwezi kukwepa hiki kitu kama Marekani wanakopa China sisi hatuwezi kuogopa kukopa na hasa kama tuna *good will* halafu tupo *bankable*, siku hizi tuko *bankable* siyo zamani sasa tunaweza kukopesheka hiyo nayo ni kasifa kazuri kwamba unaweza kwenda ukakopa, ukajenga bandari, unaweza kukopa ukaimarisha reli, unaweza kukopa ukaongeza umeme na kadhalika. (*Makofi*)

Lakini vilevile unaweza ukashirikiana na watu wengine *private* mkawa na *private public partnership*, kwa hiyo, sisi katika mpango huu tunasema Serikali itakuwa ina *raise* trilioni 2.7 kwa mwaka lakini zingine ambazo hazimo katika trilioni 2.7 zitatokana na aina nyingine ya mashirikiano yetu pamoja na ku-*encourage investors* kuingia kwetu na kuwekeza.

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbwe alipokuwa anasema lazima tufanye, tusiende na *business as usual*, lazima tuhakikishe kwamba sasa tunasisitiza juu ya kuweka mazingira ambayo wawekezaji wataona hapa mahali ni salama. Tena nafurahi kwamba maneno haya yanasmwa na Mheshimiwa Mbwe, ni Kiongozi wa Upinzani kwa sababu kuweka mazingira salama ni pamoja na kuhakikisha amani ipo eeh! Lazima kuhakikisha amani lakini kama mnaandamana usiku kama alivyosema pengine amani inaweza... maana hawawaoni, lakini mchana kila siku kwa kweli itakuwa *problem* kwa hili Mrema atakubaliana na mimi kwamba *what he was saying was right.* (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, nilitaka kumuueleza Msemaji wa Upinzani kwamba wala hatuzungumzi habari ya muujiza wa kupata fedha hizi haaah! Ni *planning* halafu tunatazama hali ya uchumi wetu, tunatazama walipa kodi, tunaona wewe hujalipa kuna watu hapa wengine hawalipi pesa za kutosha tu inabidi na wao tuwaingize katika mkondo wa kodi ili tuweze kujenga nchi hakuna namna. Wananchi wameshirikishwaje nimeshaeleza kwangu hauna ufanuzi juu ya wadau wa maendeleo, wadau wa maendeleo ni wengi wadau ni wananchi wote, ni vijana nimeeleza katika hotuba yangu, ni wanawake, watu wenye mahitaji maalum, wawekezaji, Serikali, Serikali za Mitaa wote kwa ujumla ndiyo wanaitwa wadau ambao wanatakiwa washiriki katika mpango huo.

Suala la kushuka kwa thamani ya shilingi na lenyewe limezungumzwa lakini nataka kusema unajua suala la kushuka kwa thamani ya shilingi ni suala la *supply and demand* kama kuna dola nyingi hapa thamani ya shilingi haishuki, tena *actually* inaweza ikajirekebisha kwa sababu dola zipo na dawa yake hapo moja ni kuhakikisha kweli tunauza zaidi nje na kupunguza nakisi iliyopo kati ya uagizaji na uuzaaji na vilevile kuna hii habari ya kusema wachimbaji wa madini badala ya kupeleka fedha nje waziwekeze hapa zinaweza zikasaidia vilevile ku-*stabilize currency* hapa nyumbani. Kwa hiyo, ni

mambo ya uchumi haya wachumi wanayajua vizuri zaidi, mimi ni mchumi wa kufundishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Wananchi mbona halikuwekwa kwenye mpango, baba Mchungaji huwa hatuweki mambo haya kwenye mipango, sasa tuandike nini tuseme tutanunua mizinga kumi wee, watu watakimbia hapa, kwa hiyo, haya mambo yako kwenye mpango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya Kamati na rafiki zangu wa *opposition* sasa narudi kwa wachangiaji. Uchangiaji wa jumla wengi sana wamezungumza juu ya usimamizi wa miradi walikuwa wengi Mheshimiwa Rosesweeter Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Pindi Chana, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Ramo Makani na wengine wengi kabisa Mheshimiwa Christina Mughwai wote wamezungumza na kusisitiza kwamba mpango usimamiwe na kwamba bila kuusimamia tutakuwa hatuna mpango na hautatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, sina maneno ya kutosha kukubaliana nao ndiyo maana tumesema lazima tuunde utaratibu wa kusimamia. Yapo maelezo yametolewa humu ya kusema tubadili sheria, tuwape mamlaka zaidi Tume, tutayatazama tukishirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali tuone namna ya kutimiza azma hiyo lakini ukweli usimamizi hauwezi kufanya na Tume peke yake, kwa mfano kule kwenye Serikali za Mitaa, Tume ambayo iko Dar es Salaam ina watu 21 haiwezi kusimamia mipango yote nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukubali kwamba katika ngazi nyingine hasa mkoani tuna kitu kinaitwa sekretarieti, tuna wataalam pale, wataalam wale tuwa-*commission* kazi ya kufanya ya ku-*liaison* na Tume kusimamia na kuona utekelezaji kweli unafanyika ama sivyo kwa kweli tukitegemea Tume peke yake kama alivyosema rafiki yangu mmoja anasema sasa itabidi Waziri ajiuzuru, Waziri anaweza tu kujiuzuru, unajua kujiuzuru nayo vilevile ni kupumzika haina tatizo unaweza ukaweka kila Waziri hapa akajiuzuru kila wiki lakini bado hakuna kitu hiyo siyo *issue* ya maana sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mpango ujikite kwenye kuendeleza kilimo, mazao, mifugo ndivyo mpango unavyosema na wasemaji hawa walikuwa akina ndugu Mheshimiwa Luhaga Mpina na nimeshajibu habari zake, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Nyambani Nyangwine, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Agripina Buyogera, wote hao wamezungumza jambo hilo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Augustino Mrema, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Assumper Mshana wa Nkenge, Mheshimiwa Mendrad Kigola wa Mufindi, wote wamezungumza kwa nguvu kabisa juu ya kuhakikisha kwamba kilimo kitoe kipaumbele cha kweli kwa kilimo, mifugo na uvuvi na sisi tunakubali mpango huu lazima usimamie jambo hilo. (*Makofi*)

Kuhusu madini, tuweke mkazo katika kusimamia na kufanya wachimbaji madini wadogo wadogo waweze kupewa fursa ya kuchimba, hili lilitsemwa vilevile na Mheshimiwa Nyambari Nyangwine kwa mazingira ya pale, nasi tunakubali kusema ukweli hili lazima niseme, ukishaweka mwekezaji, halafu amezungukwa na watu maskini halafu yeye peke yake ndiyo tajiri ndiyo ana umeme pale Nyamongo, pale wenyeji wale wanajenga nyumba ya mviringo halafu haina dirisha lakini ina mlango unafanana na dirisha kwa sababu ya usalama wao, halafu wanaishi humo wanaona *mine* kule na pesa unawapa muhemko wa bure, lazima tuwasaidie wachimbaji wadogo wapate vifaa vyta kuchimbia, lazima Wizara ya Nishati na Madini ikubaliane na hili kwa sababu hawa ni wadau pale kwenye mgodi kwa hiyo, tuwasaidie na wao wachimbe kwao kama wanavyofanya wakulima wadogo wanaolima miwa, wanaiza kiwandani, tusipofanya hivyo tunatafuta tatizo. (*Makofi*)

Suala la nishati, kumekuwa na mpango uliokwishapitishwa na Bunge ambao baadhi ya miradi yake haimo katika mpango, miradi yote imo katika mpango, tunachosema hapa ni kwamba miradi ipo ambayo itatekelezwa kati ya sasa na mwaka 2015/2016 na itakapofika wakati huo sisi mpango huo tunazungumzia *megawatt* 2780 lakini hilo ni lengo la chini, wapo watu ambao wapo tayari kuwekeza zaidi.

Kuna mmoja ametuuliza juu ya *Stigler's Gorge*. *Stigler's Gorge*, wapo watu wanaitafuta kuwekeza, juzi nilimwambia *Prime Minister* kuna watu wengine wanasesma *we want to come there for Stigler's Gorge*, wapo duniani hapa watu wanataka kuwekeza. Kwa hiyo, mimi nadhani tusipate matatizo, mimi naona kama mpango huu tutausimamia vizuri na hizi *megawatt* zitapatikana na hii *problem* itaisha lakini matumaini yetu ni kwamba tuki-exploit resources zetu kwa ajili ya umeme siku zijazo Tanzania itakuwa *exporter* wa umeme na siyo *importer* na siyo ya mgao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uchumi unakua kwa kiwango cha asilimia saba, lakini umaskini umebacki pale pale nimeshalijibu na wale wote waliosisemea ndiyo hayo majibu niliyatoa.

Mheshimiwa January Makamba, Mbunge wa Bumbuli alikuwa ameuliza specifically, nilimzoea Yusuf Makamba, lakini nilitaka kusema tu kwamba tunayo orodha tu ya miradi na yeye kwa kweli tunaweza tukampa tu inayoonyesha kila mwaka kiasi gani cha *megawatt* kitazalishwa mpaka kufikia lengo la *megawatt* 2780.

Mheshimiwa Spika, rasilimali fedha kwamba fedha zimetengwa kwa ajili ya wawekezaji ni kidogo, napendekeza fedha iliyotengwa kwa ajili ya maendeleo iongezwe toka 35% mpaka 40% nadhani tunganeza hapo kwanza maana tukiwa na malengo makubwa sana tunaweza kufika mahali tukashindwa lakini tukiweza 35 percent ya revenue yetu inakwenda kwenye *development* na tutapunguza utegemezi ukabaki asilimia 10 mwaka 2015/2016. Mimi nadhani tunaweza ku-move, let try this, tukienda speed sana tunaweza kupata matatizo.

Mheshimiwa Spika, kiasi gani cha maji safi na salama, malengo ya asilimia 95 mjini na vijiji, kuna wengine walikuwa wana-query kwamba hii kitu haiwezi kufikiwa,

lakini nitumie uzoefu wangu wa Waziri ya Maji wa mwaka 2006. Mimi najua miradi ya maji ya mijini, miji mikubwa hii mji ambao una matatizo kuliko yote ni Dar es Salaam, Dar es Salaam ndiyo nitaizungumzia baadaye wakati nazungumza masuala ya Mheshimiwa John Mnyika, lakini miji mingine hii kwa suala la maji ipo *taken care of*. Ukienda Tanga kwanza maji sio tu kwamba yanatosha lakini na *quality* ya maji ni nzuri pale Tanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukienda Moshi kuna kiwango kikubwa sana cha *supply* ya maji katika mji wa Moshi, hata Arusha. Ukienda Mwanza kuna mipango mikubwa pale ya kusambaza maji, ukienda Mbeya ipo mipango, ukienda Iringa ipo na mingine pale Iringa sijui nani walisema ametoboa bomba, mambo haya mwingine anataka maji, mwingine anatoboa bomba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Mbunge wa Iramba Magharibi pamoja na Mheshimiwa Mariam Kisanga, wote walikuwa wamezungumzia suala la wanawake, vijana na makundi maalum. Mimi nasema hatutaweza kutekeleza mpango huu na tukaondoa umaskini kama hatukuwaingiza vijana wa Tanzania katika programu ya kuwaondolea umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani, kwanza nimesema katika hotuba yangu wanafika 60%, sasa kama ni 60% na umaskini ndiyo una 60% sasa mpango utakuwa umetekeleza nini? Kwa hiyo, kwa kweli tutatazama hesabu katika vile vitabu kwenye *final draft* ili tuone *resources* kiasi gani tunazi-channel kwenda katika makundi hayo ili kuhakikisha vijana, wanawake na kundi la watu wenye ulemavu ambao Mheshimiwa Mbunge wa Viti maalum alivyokuwa amesema mimi sina hata takwimu, lakini mimi ninazo takwimu, labda hizo zangu ni nyingi kuliko idadi ya walemavu, mimi nadhani zipo karibu na sawa tu.

Suala la ardhi, limeongelewa na Mheshimiwa Alphaxard Lugola, Mheshimiwa Mwigulu Madelu na Mheshimiwa Pauline Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, wamezungumzia sana ardhi na mimi nataka kusema katika mpango huu tumeweka *provision* ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na *resources* ambazo zitapima ardhi, lazima tupime ardhi. Tupime ardhi tujue ya kijiji ni ipi, tujue ardhi isiyokuwa ya kijiji ni ipi. Sasa ipo *problem* ya wawekezaji wanakuja kuwekeza kwenye ardhi ya kijiji na wengine wanasema rafiki yangu nitakuja kumjibu baadaye, rafiki yangu kweli kweli Mbunge wa Mbulu, ye ye anasema kwamba Katiba mpya ndiyo itaondoa hii *problem*, hii *problem* haiwezi kuondolewa na Katiba, hii inaondolewa na kupima na kupima unaweza ukapima na Katiba hii iliyopo ukapima tu ukasema wewe ardhi yako ni hii hapa, mifugo yako inachunga huku unalima huku na unajenga huku. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Katiba mpya nitaisemea, tunaitaka wote sasa siku hizi wala haina chama, lakini hili ni la ardhi, ardhi itapimwa na mpango huu unataka ardhi ipimwe. Mazingira ya kufanya biashara nimeshasema, miundombinu ya barabara tumekwishaizungumza.

Hoja nyingine ni usimamizi wa utekelezaji wa miradi katika mpango huu na wenyewe umerudiwa lakini tumeshasema, mpango ujikite kwenye kuendeleza kilimo, mazao, mifugo na uvuvi tumekwishayasema, madini yaangaliwe upya tunakubali, masuala ya nishati yanaendelea, viwanda; viwanda hatuwezi kuingia kwenye nchi ya uchumi wa kati bila viwanda haiwezekani, kwa hiyo, kwa kweli katika kujaribu kuboresha mazingira ya uwekezaji katika nchi yetu lazima tuelekeze nguvu yetu na wawekezaji kuingiza mitaji ili kuhakikisha kwamba mazao ya kilimo yanaongezewa thamani. Miaka 50 unalima pamba unauba roba yaani wewe kiwanda chako ni cha kutoa nyuzi, basi halafu wanaenda wanatengeneza shati unarudi unasema *Made in Hong Kong*, pamba yenewe ya Bunda, eeh, mambo ya ajabu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tuna matunda hapo ukienda *Southern Highlands* tunawenza ku-produce matunda, *horticulture* na ipo kwenye mpango tumeitilia mkazo na viwanja vile vya Songwe vile tutengeneze ili ndege zitoke kule na mazao ya *horticulture* ziende moja kwa moja *Europe*. Haya mambo yanawezekana ndiyo maana humu tumeandika yes we can, ni vitu vinawezekana tu. Kwa hiyo, utilie mkazo suala la viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakaribia sana kumaliza maana mambo haya yamejirudia rudia. Rasilimali watu; rasilimali watu tunaipa mkazo kwa sababu huwezi kutekeleza mpango huu bila kuboresha elimu, bila kuhakikisha ya kwamba elimu unayoitoa inawafanya wanaopata wawe *competitive* kama alivyosema Mheshimiwa Freeman Mbobe, wawe *competitive* katika *East Africa*, wawe *competitive* katika ushirikiano wote ule ulioungana juzi kule *South Africa*, wawe *competitive* duniani. Haya mambo yote yanawezekana kwa hiyo, haya masuala yote tumeyaandika katika huu mpango na yamezungumziwa sana na Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Martha Umbulla na Mheshimiwa Charles Kitwanga, wote wengine wameandika, wengine wamesema na Mheshimiwa Michael Laizer, wote wamazungumzia suala hili la elimu ya ufundi na elimu ya juu ili tuweze kuboresha zaidi na kuhakikisha ya kwamba tunakuwa na kada ya wasomi ambao ni *competitive* na ambao watasaidia katika kutekeleza mpango wenyewe. Kwa hiyo, kwa kweli wala hatuna ubishi mkubwa katika hili.

Mheshimiwa Spika, rasilimali fedha nimeshalizungumzia, nimeshazungumzia rasilimali afya na yenewe imepewa nafasi maalum katika mpango, maji tunesema tutaongeza zaidi, ongezeko la maji, kuna mmoja alikuwa amesema yeye huu mpango haoni kama una faida sana na akasema yeye haendi huko kwao kwenda kueleza huu mpango, ataenda tu kusema CCM wamesema, nilikuwa nasema eeh, huyu bwana huyu hata mpango tena anahutubia kesi tena? Huu mpango wa Taifa siyo wa kwenda kusema CCM imesema hivi, watakuuliza wewe unasemaje? Maana CCM yenewe inasema vipaumbele ni hivi, wewe vyako ni vipi? Wanasema kuna kilimo, kuna miundombinu, kuna umeme na yeye mwenyewe sitaki kutaja jina lake, maana sitaki kuharibu mambo sana hapa, lakini alisema kwao kule hata umeme uko kijiji kimoja tu, sasa ndiyo tunasema tuongeze *megawatt* ili ufikie na vijiji vingine. Sasa utaenda kusema, nenda useme kwamba CCM wamesema, halafu tutakuja kusema ni sisi ndiyo tuliosema na umeme utakuwa umefika, mambo yako yatakuharibikia kweli. Kwa hiyo, angalia sana lakini ni mambo ya kujifunza humu ndani ya Bunge, ufuatiliaji nimeshausema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nadhani sasa nijikite katika hoja maalum ambazo zimewasilishwa na nianze na hoja ya Mheshimiwa Freeman Mbewe. (*Makofi*)

Kwanza ni suala alilolisema na *section aliyo-i-quote* Mheshimiwa Freeman Mbewe siyo inayohusiana na jambo hilo. Hiyo *section* anayosema kwamba ni 234 kwa kweli yenyewe inafanya tathmini ya hali ilivyo, lakini haizungumzii juu ya mpango wenyewe. Lakini pamoja na kwamba ni tathmini nataka niseme kwamba mimi nakubaliana na yeche pamoja na hoja yake, nakubaliana nayo. Kwa sababu hii ni dunia ya utandawazi kama kuna *knowledge* inapatikana nje na sisi tuna watu ambao wakienda huko watakuwa *more competent why not?* Tena siyo hiyo tu, tunaweza kuwaleta wataalamu wa nje wafanye kazi na wataalamu wetu hapa Tanzania. Kwa mfano, kwenye sekta ya kilimo na umwagiliaji tuna Wahandisi 130 lakini matakwa halisi ni Wahandisi 350, hakuna ubaya wowote wa kutumia *South-South Cooperation* kuleta Wahandisi wa Vietman kufanya kazi na Wahandisi wetu pamoja na *graduates* wanaoingia mwaka huu wakafanya kazi pamoja wata-gain experience, hakuna ubaya wowote.

Kwa hiyo, kupata *experience* kutoka nje na kufanya kazi na Mashirika ya Kimataifa ili tuweze kupata *competent people* ambao wanaweza kuja kusaidia nchi yetu hakuna ubaya wowote. Kwa hiyo, mimi nasema mawazo ya Mheshimiwa Freeman Mbewe yanakuwa *accommodated* na hakuna tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukikataa na hilo nalo itakuwa hakuna unalokubali maana wewe unakataa vyote tu sasa sijui utakuwa unakataa nini. Hatuwezi kupingana na *ideas, if the idea is good, you don't look at Mbewe's face, you attest what he says.* Lakini ukitoka ukaenda kwa Mheshimiwa John Mnyika una *deal* naye tofauti kidogo kwa sababu hoja ya Mheshimiwa John Mnyika ni tofauti kabisa.

Mheshimiwa Spika, ameomba pia maji, lakini nataka nimueleze ukweli Mheshimiwa John Mnyika kwamba ule mpango wa miaka mitatu wa Serikali wa kumaliza tatizo la maji Dar es Salaam ni *taken care of* na huu mpango pamoja na Bajeti ya mwaka huu. Ule mpango umepitishwa na Serikali na hizi *figures* anazozisema zipo na nyingine kwa ajili ya huu mpango kwa ajili ya Bajeti itakayojadiliwa kuanzia kesho, zipo pia pesa na nyingine zitakuja kwenye mpango huu mwaka unaofuata halafu na mwaka wa tatu. Shabaha ni kufanya Dar es Salaam iwe *free from problems* ya maji ifikapo mwaka 2013/2014, mpango ule ni *covered*. Kwa hiyo, kwa kweli kuingiza hii miradi kwa jina haisaidii kwa sababu tunaitazama Dar es Salaam *as a unit* na fedha zipo na nataka uni-quote itakapofika mwaka 2014 kwamba ulisema zipo na *problem* ya maji itaisha, mimi nitasema sawa sawa! Maana zipo and the plan are there.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kusema tunaingiza namba hii na hii, haiwezekani iwe ni *problem* ya Ubungo tu, lakini tunazungumzia *problem* ya Dar es Salaam na utekelezaji unaanza mwaka huu na fedha zipo kwenye Bajeti. Nadhani utaona jinsi tunavyohukumu kesi kutegemeana na mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara anayoisema Mheshimiwa John Mnyika inasimamiwa na *Municipal Council*, ni kweli kwamba Rais alisisitiza ifanye nini?

Itengenezwe, hilo ni kweli. Kwa hiyo, mimi nataka Mheshimiwa John Mnyika tuonane naye na tuzungumze namna tutakavyosaidia utekelezaji wa barabara ile maana ni ahadi ya Rais na sisi kazi yetu ni kusimamia. Kwa hiyo, tutazungumza tuone *how to go through* na ni kilomita tisa tu yaani *it is only nine kilometres*, siyo barabara ndefu kama ya kutoka hapa Dodoma kwenda Rarya. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hata hiyo ya mtaro nayo ni jambo ambalo tunaweza kulitazama kwa sababu mpango upo na fedha zipo, kinachotakiwa sasa ni kila mwaka unaweka mradi lakini tukianza mpango huu tunau-*ammend* kwa kuweka mradi *specific* na Mbunge wa Mbozi, Mheshimiwa David Silinde naye aseme wa kwake nao uingizwe, tutapata *problem* wala hatutatoka. Kwa hiyo, kwa kweli mimi nadhani hii miradi itatekelezwa lakini tuzungumze kuona namna ya kuishughulikia.

Mwisho ni mradi wa *Stigler's Gorge*, huu ni mradi ambao tumekubaliana miaka mitano tufanye *study* na tunadhani tunaweza kuupa *priority* katika mpango wa maendeleo unaokuja. Lakini tukipata mwekezaji ambaye yuko *serious* tunaweza kumruhusu akaanza kutekeleza mpango huu kama anatumia fedha zake mwenyewe. Kwenye Bajeti pengine tutakuwa hatuna fedha maana mradi wenyewe ni mkubwa, ukiutekeleza wote kwanza una *combination* ya kilimo, maji pamoja na umeme, ni mradi mkubwa. Halafu vilevile una-*encroach* kule kwenye *Selous Game Reserve* ambayo kuitumia ni mpaka tuzungumze na *UNESCO*. Kwa hiyo, tukiweka humu tunaweza tukamaliza *five years* bila kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ya Mheshimiwa John Mnyika ilikuwa inauhusu vyuo. Aliingiza vyuo vitatu kimoja ni Chuo cha Madini, alikuwa anapendekeza kiwe Chuo Kikuu. Tumezungumza na wenyewe chuo hiki, wanassema Chuo Kikuu cha Dodoma kina masomo ya *degree program* kwa hiyo, hiki kinatakiwa kibaki, kinatoa *technicians* na kwamba soko la sasa kwenye migodi linawahitaji *technicians*, wale ni *more practical* kuliko waliosoma *degree*. Kwa hiyo, mimi nadhani lazima tu-*balance* kati ya *technicians* na wale wasomi wa nadharia wa Chuo Kikuu. (*Makof*)

Lakini lile la Chuo cha Mafuta kilichopo Mtwara, hili ni jambo zuri lakini halijafanyiwa *study* kwa hiyo hili tunalichukua ili tuone jinsi tunavyoweza kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini kuona inavyowezekana. Chuo cha mwisho alichokuwa amekiandika nilishangaa hata hiki amekitoa wapi kilikuwa ni cha Butiama ambacho kimeandikwa kwenye hotuba yangu. Lakini nilitaka nikieleze vizuri Bunge lako Tukufu lijue na chenyewe kimetoka wapi maana hakipo.

Mheshimiwa Spika, Chuo kile kimeombwa na Kanisa la Mennonite wanataka kushirikiana na Serikali kujenga Chuo cha Kilimo Butiama kwa ajili ya kumbukumbu ya Baba wa Taifa pale nyumbani kwao. Lakini majengo yaliyopo pale tulipewa msaada na Cuba tena kwa maelekezo ya Mzee ya Fidel Castro kwa sababu ya uhusiano wake na Marehemu Baba wa Taifa. Alijenga majengo kwa ajili ya *artificial insemination* lakini haifanyi kazi na haitumiki. Kwa hiyo, kwa kweli tunachoomba pale ni ku-up grade yale majengo halafu yatumike kuanzisha Chuo Kikuu cha Kilimo cha Butiama na itakuwa ni *joint effort* kati ya Kanisa la Mennonite na Serikali ya Tanzania. (*Makof*)

Mimi nadhani Bunge hili halitakuwa na tatizo la kukubaliana na kukubali kujengwa kwa chuo hicho ili kufanya mahali pale alipozaliwa Baba wa Taifa pasiwe Mwitongo. *In the real sense*, Mwitongo ni mahame lakini ukiweka *institutions* za namna ile zinasaidia kupafanya pawe *live*. Mimi nadhani hili Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana na mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji*)

SPIKA: Bado hoja ya Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):
Aaaah! Mustapha Boay Akunaay!

Mheshimiwa Spika, kengele ndiyo imenisumbua!

SPIKA: Hiyo kengele isikusumbue, endelea tu!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):
Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay sina tatizo naye, lakini Katiba hata kwa mwaka huu wa fedha imekuwa *taken care off* katika Bajeti ya *recurrent*. Huu mpango ambao kwa kweli tunataka *u-turn around* uchumi, lakini tunaugharamia katika *Recurrent Budget*. Huu mpango hauchukui fedha zote za Serikali ila ni kwa ajili ya mipango ya maendeleo ndiyo maana tunazungumza 35%. Lakini suala la Katiba litashughulikiwa na Serikali imekubali ila tunachotakiwa kwa kweli ni Bunge lipitishe ule Muswada baada ya Bajeti kuisha ili tuanze kupata Tume na tuanze kutafuta maoni ya wananchi. Hili jambo halina mgogoro sasa hivi na itagharamiwa na Serikali kuititia *recurrent*. Kwa hiyo, namuomba rafiki yangu aelete we kwamba hakuna matatizo makubwa ya ajabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuwashukuru wote kwa kutoa mchango mkubwa katika mpango huu, tutawaandikia yale ambayo hatukuyajibu kwa ukamilifu na tutatoa maelezo lakini naomba kutoa hoja sasa kwamba Bunge lako liukubali mpango.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, naafiki!

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Spika, kazi tunayoifanya hapa...

SPIKA: Tafadhali isome!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Kanuni ya 68(7) inatamka kwamba, naomba kunukuu; “Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote wakati hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema, ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo kwa hapo au baadaye, kadri atakavyoona inafaa.”

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 5(1) Bunge hili linaongozwa kwa mujibu wa Katiba kwa maana ya majukumu ya Spika yanaongozwa kwa Katiba, Kanuni na inaendelea kutamka kwamba mila na desturi na kadhalika pale ambapo Kanuni hazitamki bayana. Nitaomba kwa sababu ya muda nisisome kifungu chote.

Mheshimiwa Spika, jambo tunalolifanya hapa lililotokea muda mfupi uliopita ni jambo la Kikatiba, kwa sababu Katiba Ibara ya 63(3)(c) inasema kwamba Bunge lenye mamlaka ya; “kujadili na kupitisha mpango...”

Sasa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 94 ambayo tumeitengua jana kabla ya kuanza mjadala huu, naomba niisome pamoja na kuwa tumeitengeua inasema kwamba; “Ili kutekeleza majukumu yilioainishwa katika Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba, Bunge litakaa kama Kamati ya Mipango katika Mkutano wake wa Februari ili kujadili na kushauri kuhusu mapendekezo ya mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha unaofuta.”

Kanuni hii tumeitengua kwa hiyo *hai-apply* hapa, lakini *spirit* ya hii Kanuni inaonyesha kwamba Kanuni zetu zina *vacuum* yaani zina ombwe, hakukuwa na Kanuni *specific* inayoeleza utaratibu wa kujadili mpango wa miaka mitano. Sasa kama Kanuni hazipo tunarudi kwenye Katiba na tunarudi kwenye desturi za Kibunge. Kwa mujibu wa desturi za Kibunge hoja za michango ya ujumla huwa zinajibiwa kiujuropa ujumla, lakini hoja ambazo mtoa hoja amepeleka mabadiliko kimaandishi zinajibiwa kwa kadri ya mabadiliko yake aliyoyawasilisha. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, pale ambapo mtoa hoja anakuwa hakubaliani na yale mapendekeza, amependekeza mabadiliko baada ya maelezo yake, yule aliywasilisha mabadiliko anapewa haki na yeze ya kusema kabla ya Bunge kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako katika hili ili tupewe fursa kwa kuwa mtoa hoja amesema na sisi watoa mabadiliko tupewe nafasi hata kama ni dakika tatu au tano ya kusema ili Bunge liweze kuamua baada ya kusikia upande wa pili kwa mujibu wa desturi za Kibunge katika hoja kama hii ambayo Kanuni hazijaeleza bayana.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa John Mnyika. Anachosema Mheshimiwa Mnyika ni sahihi kwamba Kanuni hasa ya 94, ukweli ni kwamba ilikuwa inazingatia ule mpango wa mwaka hadi mwaka. Lakini mpango kwa maana ya mpango wa miaka mitano hata kama Katiba imeeleza hivyo, Katiba imesema Bunge litafanya kazi ya kujadili na kuidhinisha mpango wa muda mfupi, wa kati na wa muda mrefu, ndiyo Ibara ya 63(3)(c).

Lakini Kanuni hii ilizingatia zaidi ule mpango wa kimwaka ndiyo maana kwanza tulisimamisha, lakini sisi tumeichukulia ile Katiba yenyewe, sasa inatutaka sisi tufanye hiyo kazi. Sasa tumezungumza kwa kadri siku zinavyokwenda na nashukuru kwamba mabadiliko ya Kanuni zetu tulizotaka kuyafanya tumeyachelewesha ili kusudi uzoefu upatikane kwa Wabunge wengi katika kufanya kazi kwenye Kamati, humu ndani na mambo mengine ambayo sasa yanajitokeza.

Huu mpango wa Tume ni mara ya kwanza umewasilishwa, ni mara ya kwanza kwa maana ya Bunge hili, kwa hiyo, linakosa Kanuni zinazofuata. Hii ya marekebisho unakuta ni Kanuni za hoja za kubadilisha Miswada. Kwa hiyo, unawenza kukuta Muswada kifungu fulani kidogo tu mnapishana maneno lakini hapa mpango ni taabu, lote hili na linaangalia nchi hii kwa miaka mitano ikitokana na dira ya miaka 15. (*Makofi*)

Sasa tukisema tuanze kubisha tuweke Ruvu Chini au Ruvu Juu humu ndani tutabishana mpaka asubuhi, halafu hiyo inakuwa ya Mheshimiwa John Mnyika lakini na mwingine angependa mahali pengine afanye hivyo. Basi hatutamaliza na ndiyo maana nilimueleza kwamba kwa hili umeweka maelezo yako vizuri yamekuwa *captured* na niliyasambaza mapema kabisa ili kusudi Serikali yenyewe iangalie maneno aliyoyasema Mheshimiwa John Mnyika yanavyowiana na mpango huu mzima. Hivyo hivyo hata ndugu yangu Mheshimiwa Mustapha Akunaay alileta nikasambaza ili kusudi Serikali na wanaoangalia mipango huko waone hayo mambo hayapingani lakini yanaingia. Hivyo hivyo, Mheshimiwa Freeman Mbowe maelezo yake nayo yamesambazwa kwa makusudi ili kusudi tuone namna gani inavyoingia katika mpango mzima.

Sasa haya mliyoyazungumza mengi mmewafunua macho, mmewasaidia au mmeboresha namna ya kuandika. Kwa maana hiyo, tunapitisha sasa hivi kwa sauti moja halafu baadaye tunaangalia Kanuni zetu, kuna mambo mengi sana ya kuangalia kwenye Kanuni na lakini nadhani nilikuwa kwenye Kamati yao ya Nishati nikawaambia kuna vitu vingi humu unaona kidogo vimeacha *loophole*. Lakini hii ni kwa sababu ya wakati, wakati daima unafanya mambo yasiwe hivi, Kanuni tulioanza nayo ilikuwa na *page* mbili sasa inazidi ku-grow in size kwa sababu na sisi tuna grow na mambo yanabadilika.

Kwa hiyo, Mheshimiwa John Mnyika ni kweli kwamba Kanuni zetu zina nafasi sana ya kuangaliwa na tutatoa yale yaliyopendekezwa ili kusudi muyaangalie na muongeze mengine. Kwa hiyo, tutafanya kazi nzuri zaidi kwa sababu na ninyi mtakuwa na uzoefu na Kanuni hizi. (*Makofi*)

(*Hoja Ilitolewa iamuliwe*)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Bunge liliafiki na Kupitisha Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 – 2015/2016)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. CHRISTOPHER O. OLE SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuomba Mwongozo, nimeomba Mwongozo sielewe kama itakuwa na nafasi baada ya uamuvi uliofanyika lakini utanisaidia kuniongoza chini ya Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Spika, nia yangu ilikuwa ni kuzingatia yote tuliyokuwa tumeyajadili kwa maana moja tu kwamba iliyokuwa mbele yetu ilikuwa ni rasimu ya mpango na kwamba kila Mbunge aliyepata nafasi ya kuzungumza au kuandika aliweza kuweka *input* yake na mionganoni mwa michango iliyotolewa imani yangu ni kwamba inaweza kuboresha zaidi mpango tulionao. (*Makofi*)

Sasa nilichotaka kuomba Mwongozo na hasa ukizingatia kwamba hatupitii ukurasa hadi ukurasa na jambo hili lilikuwa ni geni hata tu kwa ufahamu ni kwa namna gani sasa mawazo ya maana ambayo yametolewa na Wabunge yatakavyoweza kuwa *accommodated* katika mpango huu au utaendelea kubaki kwa neno kwa neno kama lilivyo maana hofu yangu iliyokuwepo ni kwamba tulijaribu sana katika maandishi tuliyoyatoa kuzingatia kwamba mpango mzima ni lazima uitazame Tanzania kwa mapana yake na kiwango cha maendeleo cha jamii ili tuweze kwenda katika maendeleo yenye uwiano na ili tuweze kukimbia pamoja hata katika mbio za mashindano ya ridhaa, lazima kuna mstari unachorwa na watu wote wanapiga magoti na kuondoka kwa pamoja na kwa kuwa, kuna jamii zilizopo nyuma na zilizopo pembezoni tulishauri kwamba ni vizuri kuwepo na mpango mahususi au *affirmative plan* ambayo inaweza kuwafanya waweze kunyanyuka na kuweza kukimbia kwa pamoja ili kuleta maendeleo yenye uwiano.

Mheshimiwa Spika, sasa hoja yangu hapo ni kuomba ushauri kwamba je, mawazo yaliyotolewa kwa siku hizi mbili yatakuwa na nafasi katika mpango huu au ndiyo basi rasimu hii imepita kama ilivyo na hakuna masahihisho yoyote yatakayofanyika?

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama mmemsikiliza aliyejewa anatoa hoja kwamba baada ya maneno haya na hasa mpango wenye ni kuongeza *growth* na kupunguza umaskini hata hayo maeneo mnayosema ni rasmi si ni umaskini umezidi? Ndiyo hilo tu. Sasa kama mpango huu lengo ndiyo hilo maana yake watakwenda kuuangalia upya kwa maana ya michango yenu na iko kwenye *Hansard*. Hamuwezi kuandika mpango kila mtu, mwingine anaweza akasema neno lile lile lakini kwa lugha nyingine lakini ni lile lile. Sasa mkisema wote mtaandika *page* kwa *page* hamtawezza, mimi nadhani tumezingatia yote yanayostahili na hasa maana ya mpango huu ni kuongeza ukuaji wa uchumi ili kupunguza umaskini, na maeneo yote hayo mnayosema ni umaskini ndiyo uliozidi kuliko wengine na huu mpango ndiyo kazi yake.

Mheshimiwa Mbunge, kwa hiyo, mimi nakuhakikishia kwamba utabertilishwa lakini siyo neno kwa neno kama ulivyosema lazima kwa sababu wataalamu wako pale na ni Watanzania na wengine wanatoka Kasulu kwa hiyo, mambo yatakwenda vizuri tu. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naomba nitangaze machache, moja ni kwamba Katibu wa Kamati ya Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM Mheshimiwa Jenista Mhagama anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM kwamba leo tarehe 14 Juni, 2011 kutakuwa na kikao cha kamati hiyo katika ukumbi wa Pius Msekwa mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge jioni hii. Kwa hiyo, Wajumbe wa Kamati ya CCM mnaombwa kukutana.

Halafu kesho tutakuwa na kipindi cha Maswali na Majibu halafu Mwenyekiti wa Kamati iliyosughulikia Bajeti atapewa muda wa kutoa maoni ya Kamati yake kwa muda wa saa moja kwa sababu kuna suala la Mpango na Hali ya Uchumi. Kwa hiyo, ni nusu saa na kwa hiyo, itakuwa ni saa moja.

Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani naye atakuwa na saa moja kwa sababu kuna huu Mpango na Hali ya Uchumi halafu na Bajeti, kwa hiyo kutakuwa na saa moja. Hii itatifikisha kwenye saa sita baada ya saa sita nitasitisha shughuli za Bunge ili twende kwenye ukumbi wa Pius Msekwa sisi wote tukajifunze namna ya kuingia kwenye masuala mazima ya kuitisha Bajeti kwa sababu hili tumelisoma lakini hatujaingia vizuri kwa sababu tusipofanya hapa ni eneo mojawapo ambalo litaleta kidogo ghasia kwa sababu wengi watasema wanajua kumbe hawajui. Kwa hiyo, tutakwenda kuangalia makosa tuliyofanya toka tulipoanza mpaka tulipofika pale tulikuwa tunatunga Miswada ndiyo tumefika hapa sasa tunaingia kwenye Bajeti.

Kwa hiyo, kesho baada ya kupata maoni ya Kambi ya Upinzani na ya Mwenyekiti tutaahirisha shughuli kisha tutakwenda kwenye ukumbi wa Pius Msekwa na tatarudi tena hapa jioni.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naomba msiache kwenda kwa sababu baadaye tunaanza kutumia *measures* zote za Kanuni hizi na kutoa adhabu kwa wale ambao wanaanza kufanya vitu visivyoeleweka. Mpaka sasa inabidi kuvumiliana, kama ukiwa na mtoto mchanga analia hovyo hovyo huwezi kumfungia kwa kuona kwamba anasumbua, itabidi tuvumiliane kwa sababu tunajifunza kwa pamoja. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, sina matangazo mengine naomba kuahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho.

(*Saa 1.41 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatano,
Tarehe 15 Juni, 2011 saa tatu asubuhi*)

